
# KUMBUKIZI ZA OLIMPIKI

# OLYMPIC MEMOIRS

## PIERRE DE COUBERTIN



# YALIYOMO


Baron Pierre de Coubertin ........ 1

Dibaji ........ 1

I. Mkutano wa Paris na Ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki ........ 4

II. Ushindi wa Wagiriki (1882 – 1896) ........ 14

III. Michezo ya Kwanza ya Olimpiki (Athene, 1896) 20

IV. Mkutano wa Michezo ya Olimpiki huko Le Havre (1897) ........ 31

v. Mashindano ya Pili ya Michezo ya Olimpiki (Paris, Mwaka 1900) ........ 36

VI. Michezo ya Tatu ya Olimpiki Nchini Marekani na Mkutano wa IOC Jijini London ........ 47

VII Mkutano Uliofana na Wenye Mafanikio (1905) ........ 54

VIII. Ujumuishaji wa Fasihi na Sanaa (1906) ........ 59

IX. Michezo ya Nne ya Olimpiki (London, 1908) ........ 64

X. IOC Jijini Berlin (1909) ........ 71

XI. Michezo ya Ridhaa (1909) ........ 77

XII. Jijini Budapesti (1911) ........ 83

XIII. Michezo ya Tano ya Olimpiki (Stockholm, 1912) ........ 90

XIV. Mkutano wa Saikolojia ya Michezo (Lausanne, 1913) ........ 98

XV. Maadhimisho ya 20 ya Ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki (Paris 1914) ........ 105

XVI. Miaka Minne ya Vita ........ 112

XVII. Michezo ya Saba ya Olimpiki (Antwerp 1920) ........ 119

XVIII. Mbinu za mwaka 1921 ........ 125

XIX. Idara Sita za Serikali kwenye Uwanja Mmoja (1922) ........ 132


XX. Ikulu ya Roma (1923) ........ 136

XXI. Michezo ya Nane ya Olimpiki (Paris – 1924) ........ 142

XXII. Jiji la Prague (1925) ........ 148

XXIII. Mji wa Olimpia (1927) ........ 152

XXIV. Wanamichezo Maarufu ........ 156



**Baron Pierre de Coubertin**

## Dibaji

Kwa sasa, historia ya Michezo ya Olimpiki ya kisasa imekuwa ikisimuliwa na waandishi mbalimbali wenye vipaji.

Hata hivyo, kitabu cha Kumbukumbu za Michezo ya Olimpiki kilichoandikwa na mtu aliyefufua Michezo ya Olimpiki ya Kale, kinajumuisha taarifa muhimu na nyaraka halisi zenye thamani kubwa kwa wanaohitaji kuelewa maana ya kuanzishwa kwake.

Pierre de Coubertin alikuwa na umri wa miaka 69 alipochapisha kitabu chake cha Kumbukumbu za Michezo ya Olimpiki mwaka 1931. Kipindi hicho, baada ya kufanya utafiti wa kazi zilizopita za waandishi mbalimbali kwa kipindi kirefu huku akijilinganisha na wengine, alianza kuandika kazi yake.

Kama anavyoonesha mwishoni mwa kitabu chake, alijaribu kujikita katika ukweli, akiheshimu uhusiano na utaratibu wao wa asili. Katika kufanya hivyo, aliamua kutumia nafsi ya kwanza, ambayo ni "mbinu pekee, sahihi na mtindo wa wazi zaidi".

Masimulizi ya harakati zake za muda mrefu yamejitokeza katika muktadha wa kipindi hicho, masimulizi ambayo yameoneshwa kwenye kila ukurasa. Fikra, njia, desturi, matukio ya kisiasa na ya kihistoria, ni mambo ya kale yaliyoendelezwa ambayo kwayo taasisi ilianzishwa ikiwa na "changamoto tatanishi za kidiplomasia, watu wachache wenye fitina, wenye majivuno na wenye hila za chinichini."

Hizi ni changamoto za kudumu ambazo zinatokana na hulka za kibinadamu.

Vilevile, alikumbuka kwamba tayari kulikuwa na matatizo kama vile uwakilishi wa kitaifa, jumuiya zilizounganishwa katika himaya, ushindani kati ya miji inayotaka kuandaa michezo ya ridhaa: "ukijitokeza tena mara chache mchezo kama polomaji."

Mnamo 1925, "mambo ya siri yaliwekwa wazi na wanamichezo wa ridhaa pamoja na wafuasi wao ambao waliondolewa na baadaye kuchunguzwa upya."

Hata hivyo, haikuwa mara ya mwisho.

Wapo walioshindwa na kiwango cha ufanisi wa mtu huyu, hasa pale mtu alipozingatia kuwa, kwa wakati ule, hakukuwa na sekretarieti, kiasi kwamba watu waliposafiri, hawakusafiri kwa ndege.

Katika uhalisia, ni kweli kuwa, kwa wadhifa wake katika jamii, aliweza kufungua fursa nyingi: alipata msaada kutoka kwa watu wengi wenye nia njema na wenye wadhifa ambao walifikika kirahisi, ambao walikuwa wengi na wenye ushawishi kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Msomaji wa kazi hii, bila shaka atashangazwa na uwezo wa juu wa kuhudumu kidiplomasia. Wala hakudharau njia iliyotumika. Mbinu bora ilikuwa kuitisha mkutano mwaka 1891, ambao ulitangaza kwa mshangao, mtu angeweza kusema, kuhusiana na uhuishaji wa michezo au makubaliano ya Rais wa Baraza la Mawaziri la Ufaransa ya kusimamia maadhimisho ya awamu ya 20 ya michezo ya mwaka 1914 kwa njia ya barua ambayo iliandaliwa na Pierre de Coubertin na kuiwasilisha mbele ya Katibu wa Waziri, kitu ambacho hakikuwa kawaida kufanyika kwa wakati ule!

Katika kitabu chake, Pierre de Coubertin mara nyingi anasisitiza hulka ya kifikra na kifalsafa ya kazi na matakwa yake "kuweka majukumu ya Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki (IOC) kuwa ya juu, zaidi ya yale ya chama kidogo cha michezo tangu kuanzishwa kwake". Jambo hili liliibuliwa katika mkutano wa kwanza aliouandaa mnamo mwaka 1897 huko Le Havre, katika mji wa Nomandi, mwaka mmoja baada ya Michezo ya kwanza huko Athene.

Maombi yake ya kuwaunganisha tena "washirika wa zamani", "Mamlaka na Fikra", yalikuwa yakijirudia mara kwa mara. Je, hakumpongeza Rais wa Jumuiya ya Kifasihi katika Mkutano wa mwaka 1905 ambaye alikuwa amekuja kutoka Paris kuzungumzia "Fikra katika shule ya Michezo"?

Wakati huo, uhusiano kati ya Sanaa na Michezo ya Olimpiki haukuwa wazi sana na Coubertin alisisitiza kwamba, "kuendelea hatua kwa hatua" kulionekana kwake kama ndiyo mbinu bora kwa shughuli yoyote kubwa ambayo ingedumu. Mkutano wa Ushauri wa Sanaa wa 1906, Fasihi na Michezo vilionekana kuwa vya muda mfupi.

Kwa sasa, Michezo ni "tukio la Sanaa" na Coubertin angefurahishwa na maendeleo yaliyopatikana.

Msomaji anapofikia kurasa za mwisho za kitabu cha Kumbukumbu, atasoma maneno haya ambayo yanamwakisi vizuri mwandishi wake: "... ingawa nina mtazamo chanya na naona fahari kubwa katika kazi ambayo nimepewa kuikamilisha. Sihitaji maslahi binafsi", nikihisi kuungwa mkono mara kwa mara "na aina ya msukumo wa ndani".

Miaka mitano baada ya kukamilika kwa kitabu cha Kumbukumbu za Michezo ya Olimpiki, Pierre de Coubertin alianza sura ya mwisho ya kitabu hicho ambayo alikuwa ameiandika kwa umakini katika madaftari ya shule.

Sura inayoitwa *Simfoni Isiyoisha* (*La Symphonie inachevée*), haijakamilika na haijachapishwa, ina maneno yafuatayo ambayo yanafichua mawanda ya kazi ambayo anayatamani: lakini Michezo ya Olimpiki inawakilisha nusu ya sehemu ya utekelezaji wangu" na huyu mzee mwenye miaka 74 alitamka kuwa atajitolea "kikamilifu" kuimalizia sehemu ya pili.

Mwaka uliofuata, kifo chake kilikatisha kazi hiyo.

Iwapo usomaji wa kitabu cha Kumbukumbu za Michezo ya Olimpiki utatoa uelewa mzuri zaidi kuhusiana na mtu aliyefufua Michezo, pia unatoa mwanga mpya kwa taasisi ya kipekee na ya aina yake, ya Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki.

Kwa kusoma kwa uangalifu mkubwa na uvumilivu kazi za wafasiri wake, zingeweza kumtia mtu katika hatari ya kupoteza kuona kusudi zuri la mwandishi kama lilivyowasilishwa katika matini zake halisi ambazo maudhui yake yameendelea kuwa muhimu hadi leo.

Na Geoffroy de Navacelle

Mpwa mkubwa wa Pierre de Coubertin

Paris, 1997

# I

## Mkutano wa Paris na Ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki



*1 Baron Pierre de Cubertin*

Ilikuwa jioni siku ya Ijumaa ya tarehe 25 Novemba 1892. Mandhari: eneo la ukumbi maarufu uliopo Sorbonne ya zamani uliokuwa umetiwa nakshi, kama kumbukumbu zangu ziko sahihi, kulikuwa na maua ya zambarau isiyoiva, ambayo yalikuwa yametandazwa eneo la urefu wa nchi mbili lililokuwa limetiwa kitani nzuri likiwa na sehemu mbili maalumu zilizokuwa chini ya usimamizi wa maaskofu wawili, Bossuet na Fenelon. Katika ukumbi huu wenye mwanga hafifu, nilichukua moja ya karatasi zilizokuwa zimeandikwa katika kikasha (*bachot*) changu na kutafuta kwa bidii sana jambo la kuzungumzia kuhusiana na "Wazo Bunifu". Lakini wanafunzi wengi waliokuwa wamehudhuria katika ukumbi wa Sorbonne jioni ile ya majira ya vuli mwaka 1892, walikuwa wakifikiria mambo tofautitofauti. Walikuwa wakiangalia kwa mshangao jukwaa la ukumbi, ambalo lilikuwa na mtu maarufu Bw. Viscount Léon de Janzé aliyekuwa amevaa shati na koti nadhifu, mavazi ambayo kwa wakati huo yalikuwa yakivaliwa na watu mashuhuri, ambaye nilikuwa naye muda mfupi uliopita kabla hajawa Rais wa Chama cha Wanamichezo wa Riadha na ambaye nilimfahamu vyema kuwa, hakuwa tu mtu mashuhuri wa jamii hiyo, bali mtu mwerevu na mwenye tabia njema. Upande wake wa kulia na kushoto walikuwa wamekaa Mkuu wa Chuo Kikuu, Bw. Octave Gréard na

Bw. Prince Obolensky, kiongozi wa mahakama ya Grand-Duke Vladimir, ambaye alikuwa amekubali kuwa msimamizi wa "Jubilei" hii na alipaswa kuja mwenyewe katika eneo la Bois de Boulogne siku mbili baadaye ili kukabidhi tuzo kwa wanamichezo wachanga. Kwa heshima ya uwanja duara (wenye safu za viti kwa watazamaji) uliokuwa umepambwa kwa bendera za Urusi na Ufaransa zilizokuwa zinapepea kwa pamoja; mkutano ulifanyika kati ya nchi hizo miezi kumi kabla ya wakati.

Jubilei ya nini?... Tulikuwa tukisherehekea maadhimisho ya miaka mitano mfululizo ya Chama cha Wanamichezo (USFSA): tamasha lililofanyika huko *Ville d'Avray*; ambako kulikuwa na mashindano ya michezo ya kupigana kwa panga, mbio za masafa marefu za nchi nzima za huko Meudon, ambazo kwa pamoja ziliishia na kiburudisho murua kilichotolewa na mwanaastronomia maarufu Janssen... kwa wakati huo tulikuwa na wasaidizi kadhaa waliokuwa wameandaliwa vizuri katika nyuga za fasihi, sayansi na siasa: ambao ni Victor Duruy, Jules Simon, Georges Picot na watu wengine ambao walikuwa wa kwanza kwa mwaka 1888, kunisaidia katika kampeni yangu ya awali... Je, tunaweza kusema kuwa yalikuwa ni maadhimisho ya tano ya USFSA tuliyokuwa tukisherehekea?... Sivyo. Jambo hili lilifanyika kwa siri. Ni kweli kwamba katika tarehe hiyohiyo, miaka mitano iliyopita, baada ya tafrija, vilabu viwili vidogo vya Paris viliungana kuunda Umoja wa Wanamichezo wa Ufaransa (Union des Sociétés françaises de Courses à pied). Na huu wenyewe ulikuwa mzuri sana na ishara ya ujasiri kwa upande wa Georges de Saint-Clair, kwa wanachama wa Stade Frances, walishinikizwa tu kukimbia kwenye miinuko ya Orangerie huko Tuileries siku ya Jumapili asubuhi na ukodishaji wa Klabu ya Wanariadha huko Croix-Catelan usingeweza kuwa wa hatari zaidi. Baadaye kidogo, ilinibidi kuingilia kati mamlaka ya manispaa kwenye Hotel de Ville ili kujaribu kurekebisha hali hiyo. Unaweza kuhisi mshangao wetu mimi na Saint-Clair, wakati tulipopokea barua siku moja ikitutaarifu kuwa, klabu kitaruhusiwa kuandaa njia za kukimbilia katika uwanja huu mzuri, lakini baada ya michezo kilabu kiliamuriwa kuzikunja na kuziondoa njia hizo. Huo ndio uliokuwa utaratibu wa serikali kwa siku ile. Wajumbe wa IOC ambao walisimamia shughuli zetu kwa hakika walikuwa wamechoka sana.

Ilikuwa kwa namna hii, mwandishi wa habari msumbufu aliendelea kunihoji kwa nia mbaya kuhusiana na matumizi ya nakala ya cheti cha kuzaliwa kilichorekebishwa - tulipopata fursa ya kufanya sherehe hizi nzuri kwa bajeti ambazo zilikuwa ni ndogo sana. Mkutano wa huko Sorbonne, ambao ulihusisha uwasilishaji wa mada za kitaaluma za sherehe hizo, ulijumuisha wimbo wa taifa wa Ufaransa, wimbo wa taifa wa Urusi na utungo ulioimbwa kwenye hafla hiyo, uwasilishaji wa mada tatu kuhusiana na historia ya mazoezi ya viungo: Georges Bourdon alizungumzia kuhusu Mambo ya Kale.: J. J. Jusserand, Balozi mteule wa Ufaransa huko Washington, alizungumzia Zama za Kati: na mimi niliwasilisha kuhusiana na Zama Mpya.

Kwa kipindi hiki niliamua kumalizia mazungumzo yangu kwa mtindo wa kuvutia na tangazo la azimio la mapema la kufufua Michezo ya Olimpiki. Wakati ulikuwa umefika wa kuchukua hatua! Kwa kawaida, nilikuwa nimeona kila tukio, isipokuwa kile kilichotokea. Upinzani? Pingamizi, kejeli? Au hata kutojali? Hapana kabisa. Kila mtu alipiga makofi, kila mtu aliridhia, kila mtu alinitakia mafanikio makubwa lakini hakuna aliyekuwa ameelewa. Kilikuwa ni kipindi cha ukosefu kamili wa ufahamu ambacho kilikuwa karibu kuanza. Na kilidumu kwa muda mrefu.

Miaka minne baadaye huko Athene, kwenye hafla ya Michezo ya Kwanza ya Olimpiki, namkumbuka vizuri mwanamke wa Kimarekani ambaye, baada ya kunipongeza, alisema, huku akitabasamu: "Tayari nimetazama Michezo ya Olimpiki." "Kweli!" Nikamwuliza, "na hiyo ilifanyika wapi?" "Katika mji wa San Francisco". Alipoona mshangao wangu, aliongeza: "Mashindano yalikuwa mazuri sana. Kaisari alikuwapo". Ufufuaji wa michezo, mashindano na maonesho ya aina ya mbio za Farasi katika uwanja wa de l'Alma au wa Michezo ya Olimpiki ya London ilikuwa ikifanyika katika siku hizo; michezo ambayo ilitupatia changamoto mimi na hadhira mwaka 1892. Nikiwa na nia njema –lakini bila kujua - hawakuweza kuelewa mawazo yangu, kulielewa jambo hili lililosahaulika: Michezo ya Olimpiki na kutofautisha kiini, asili na misingi yake ya kale iliyokuwa haitumiki na ambayo katika kipindi cha miaka elfu moja na mia tano iliyopita, ilikuwa imesahaulika.

Jambo hilo lilinifanya niwe mpweke na lilikuwa gumu sana kuvumilika. Kama ningekuwa milionea, ningeweza kupata suluhu, lakini nilikuwa na kipato kidogo ambacho hadi wakati huo kiliniwezesha kutoa msaada mdogo kwenye vyama vya michezo shuleni, ambavyo vilikuwa vikiundwa katika shule za sekondari za Ufaransa na kuniwezesha kusafiri hapa na pale ili kuandaa mikutano mbalimbali muhimu. Je, ningewezaje kutekeleza majukumu ya kimataifa kwa kipindi hiki? Na bila kuwa na kipato cha kutosha, majukumu haya yangetekelezwaje?

Jambo lingine la kutokuelewana miongoni mwa wanamichezo lilikuwa ni kukosekana kwa ushirikiano baina ya wanamichezo. Kizazi cha sasa hakiwezi kuelewa kamwe jinsi mambo yalivyokuwa kwa kipindi hicho. Kwa kweli, unapolifikiria jambo hili, ukosefu wa uelewa miongoni mwa wanamichezo ni vigumu kuuelezea kwa kuwa wote hutegemea msingi sawa wa ubora wa afya na mafunzo awali ya viungo vya mwili. Msingi wao wa saikolojia ya mwili ni sawa. Lakini katika karne ya 19 wanamichezo walisadiki kabisa kwamba mazoezi ya mchezo mmoja yalitofautiana na yale ya mchezo mwingine; michezo hiyo miwili ilikuwa haiingiliani. Mchezaji wa michezo ya kutumia upanga, angeshuka kiwango endapo angeshiriki mchezo wa masumbwi. Mpiga makasia alipaswa kujihadhari na mchezo wa sarakasi. Mchezaji wa mbio za farasi, wazo la kushiriki mchezo wa mpira wa mguu lisingekuwa na tija kwake. Kulikuwa na mchezo wa tenisi katika hatua zake za awali na mchezo wa uogeleaji ambao haukujitokeza wala kuaminiwa: Mchezo wa tenisi ulikuwa ni kwa ajili ya burudani na pia kupitisha muda,

wakati uogeleaji ulikuwa ni kwa sababu za kiafya na usalama katika matukio ya ajali au kuokoa maisha.

Nijuavyo mimi, wawakilishi wa michezo mbalimbali hawakuwahi kukutana pamoja kwa madhumuni yaleyale kabla ya kuwaalika wakutane kwa ajili ya kuunda Kamati ya Uenezi wa Michezo Shuleni: mwaka mmoja baadaye, Kamati ya Maandalizi ya Mashindano kwenye Mkutano wa mwaka 1889, idadi ya wajumbe niliyokuwa nimewaalika kwa wakati huu walikutana pamoja rasmi katika Wizara ya Elimu ya Umma. Lilikuwa ni jambo la kufurahisha kuwaona jinsi walivyokuwa wakitazamana kwa shaka. Lakini wote walikuwa ni wanafunzi, kwani wakati huo tulikuwa tukishughulika na duru za elimu pekee. Hali ilikuwa tofauti kabisa kwenye Michezo ya Olimpiki. Hapa tulikuwa tunashughulika na watu wazima pekee...

Wakati wa majira ya baridi ya 1892-93 yalipita bila wazo hilo kusababisha mtafaruku wowote miongoni mwa umma kwa ujumla. Pale ambapo pendekezo lolote lilipotolewa kuhusiana na wazo hilo, daima lilikuwa wazo la tamasha la aina ya mbio za farasi ambapo mshindi alikuwa tayari kwenye fikra za watazamaji. Jambo la kuchekesha miongoni mwa watu "waliostaarabika" walikuwa wakihoji ikiwa wanawake wataruhusiwa kuhudhuria kwenye Michezo mipya kama watazamaji na ikiwa, michezo ya kutovaa nguo ingefanyika kwa wanamichezo, kama ilivyokuwa katika vipindi fulani vya zamani, ambapo kwa ujumla iliwazuia kabisa wanawake kuhudhuria michezo kwenye viwanja vya mashindano hayo.

Mipango yangu kabla ya mkutano wa mwezi Novemba mwaka 1892, ilitokana na wazo kwamba, matokeo yaliyosababishwa na mradi huo yangekuwa makubwa kiasi cha kuwezesha kuwapo kwa mkutano wa kimataifa, ambao kwa kutokuelewa kwangu nilifikiria kuwa serikali na vyuo vikuu vingepata nafasi ya kushiriki kama wajumbe rasmi. Baada ya hapo niligundua kuwa, nilikuwa na matumaini makubwa. Nini kifanyike basi? Haraka sana, niliamua kuweka wazo la kuwa na Mkutano, lakini kwa kutumia udanganyifu kidogo. Katika mafaili ya USFSA (mara tu kulipokucha, niliyapata mafaili kwa uaminifu) kulikuwa na mradi wa Baraza la Kimataifa la kutatua changamoto za michezo ya ridhaa, zilizopendekezwa na Ad. de Pallissaux, mmoja wa waanzilishi waaminifu na wenye shauku zaidi wa zamani. Ninakumbuka vizuri washirika wakarimu wa wakati huo, bila kusahau changamoto ambazo wakati mwingine tulizipitia.

Michezo ya ridhaa ilikuwa ni aina ya michezo ambayo ingeendelea kubaki kwenye majengo mazuri ya kihistoria kama yale ya Bulaq kama maiti za wanawake wazuri zilivyohifadhiwa! Nusu karne imepita bila kuonekana kwa athari za namna yoyote ile kutokana na uendeshaji mbovu uliokuwa ukifanyika. Ilionekana kuwa imara. Hakuna hata mmoja wetu aliyetarajia kuwa ingedumu. Katika kukabiliana na tatizo hili, tulijiona kuwa tungefanikiwa katika muda usiozidi miaka mitano. Lakini kwa upande wangu, Mkutano uliopangwa ulikuwa na umuhimu mkubwa wa kunipatia kinga muhimu. Kwa

hiyo, niliandaa programu ya awali na ikaidhinishwa na Mkutano wa USFSA, ambayo ilikuwa imebadilishwa mwanzoni mwa 1890. Kuanzia wakati huo, programu hiyo ilikuwa na Bodi na Kamati, kila kimoja kikiunganishwa na kutofautishwa na kingine kwa urahisi. Kwa njia hii, ilikuwa ni aina ya kinyago chenye uso mmoja unaotazama mbio za farasi, kutokana na utaratibu tuliotumia kuajiri wajumbe wa heshima kwa faranga ishirini kwa mwaka, na nyingine kwenye madaraja ya kati ambayo, kwa uanzishwaji na uendeshwaji wa bidii (ari na nguvu), tulipewa wasaidizi tuliowahitaji na tulikabidhiwa kwa furaha nguvukazi. Huu mwingiliano wa matabaka ya watu, ambao haukuwa rahisi kudumisha muda wote, ulinifurahisha.

Ninapoandika haya, nina programu ya mkutano wa mwaka 1894, katika matoleo mawili yanayotofautiana kwa kipindi cha miezi kumi. Kwenye ngazi ya juu, kulikuwa na washirika watatu ambao kwa: Uingereza alikuwa C. Herbert, Katibu wa Chama cha Wanamichezo wa Ridhaa (AAA) (London), kwa Bara la Amerika alikuwa ni Profesa wa Chuo Kikuu cha Princeton, W. M. Sloane, na mimi nikiwakilisha Ufaransa na Bara la Ulaya. Mazingira haya yasiyokuwa ya kawaida, yalilenga kunirahisishia shughuli zangu za uenezi. Wenzangu wawili walikuwa wamekubaliana nayo mazingira hayo ili kuniridhisha. Herbert, aliyekuwa mkimya, mwenye uelewa zaidi kuliko alivyoonekana mwanzoni na kiongozi mkuu wa AAA, aliipangilia vizuri timu nzima ya uenezi. Sloane, kwa sababu ya wadhifa na sifa yake kubwa, alipata fursa ya kuzifikia duru za vyuo vikuu vya Atlantiki ambavyo tayari nilikuwa nimepata taariza zake tangu mwaka 1889 kuwa ni maeneo maalumu ya wanamichezo wa Amerika na bila ya sehemu hizo kusingeweza kufanyika chochote.

Baada ya majina ya wajumbe watatu wa Bodi zilifuatia vifungu vinane vifuatavyo ambavyo, ninaamini, havijawahi kuchapishwa tangu kipindi hicho:

I- Ufafanuzi wa Mwanamichezo wa ridhaa: Msingi wa ufafanuzi huu, - Uwezekano na manufaa ya ufafanuzi wa kimataifa.

II- Kusimamisha, kuondolewa hadhi na kurejeshewa hadhi – Mazingira yanayosababisha hali hiyo na njia zinazotumika kushughulikia masuala hayo.

III- Je, ni sahihi kuweka tofauti kati ya michezo mbalimbali kwa mtazamo wa michezo ya ridhaa, hususani mbio za farasi na ulengaji shabaha? -Je, mtu anaweza kuwa mwanamichezo wa kulipwa katika mchezo mmoja na akawa mwanamichezp wa ridhaa katika mchezo mwingine?

IV- Kuhusiana na vito vya thamani vya kisanaa vinavyotolewa kama tuzo, je, kunapaswa kuwa na kikomo cha thamani zake? Je, ni hatua gani zichukuliwe kwa yeyote anayeuza vito vya kisanaa alivyotunukiwa kama tuzo?

V- Uhalali wa fedha zinazozalishwa kutokana na viingilio kwenye viwanja vya michezo. Je, fedha hizo zigawanywe kwa vilabu au kwa washindani? Je, zinaweza

kutumika kama fidia ya gharama za usafiri? Je, ni kwa kiwango gani wanachama wa timu wanaweza kupokea fidia kutoka kwa kilabu pinzani au kilabu chao wenyewe?

VI- Je, dhana ya jumla ya mchezaji wa ridhaa inaweza kutumika kwenye michezo yote? Je, inaweza kujumuisha vikwazo maalumu vinavyohusiana na mbio za baiskeli, upigaji makasia, riadha na michezo mingine?

VII- Kamari, Je, inakubalika katika michezo ya ridhaa? Namna ya kuzuia kuchezwa.

VIII- Namna ya kufufua Michezo ya Olimpiki. Ni katika mazingira gani inaweza kufufuliwa?

Programu ya mwisho iliyochapishwa mwanzoni mwa mwaka 1894, ilikamilishwa kwa usahihi. Ilikuwa na tarehe: 16 hadi 24 Juni 1894, tangazo lililotolewa kuwa kikao kingefanyika Sorbonne na kuwa na sherehe ya ufunguzi ya Juni 16 ingesimamiwa na Baron de Courcel, Seneta na Balozi wa zamani wa Berlin (kwa hakika alikuwa Bw. Casimir-Périer, Waziri wa Mambo ya Nje kwa wakati huo, ambaye awali alikubali wadhifa huu na baadaye alikataa, alipendekeza niwasiliane na Bw. de Courcel. Aidha, kulikuwa na Makamu wa Rais wanane, akiwamo Mwingereza, Mmarekani, Mbelgiji, Mswedeni na Mhungaria; maofisa wasaidizi wachache, ikiwa ni pamoja na Frantz Reichel, "kwa ajili ya vyombo vya habari”, na tangazo la sherehe kadhaa ambazo hazikuwa zinafahamika. Programu ilikuwa imeongezewa aya mbili mpya. Aya hizo zilikuwa zimegawanywa katika sehemu mbili: Ya kwanza yenye kichwa cha habari "Michezo ya Ridhaa na Michezo ya Kulipwa" ilijumuisha vipengele saba vya mwanzo vilivyoelezwa hapo juu; ya pili, yenye kichwa cha habari "Michezo ya Olimpiki", ikijumuisha Kipengele cha 8 hapo juu na vipengele viwili vinavyofuata:

IX. Masharti yaliyotumika kama mwongozo kwa washiriki wa mashindano, – michezo iliyowasilishwa, – taasisi, – idadi ya mashindano na masharti mengine.

X. Uteuzi wa Kamati ya Kimataifa inayohusika na maandalizi ya ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki.

Hatimaye, kanuni zilitungwa, nilitamani ziendelee kuwa na uhalisia wake kadiri ilivyowezekana, hasa kwa kueleza kwamba "Vyama na Vilabu vilivyoshiriki havikulazimika kukubaliana na maazimio yaliyopitishwa". Kwa mantiki hiyo, kanuni hizi zilionekana kuwa za uhakika japo hazikuwa na uhalisia. Nilijiingiza kwenye jambo ambalo sikuwa na uhakika wa mafanikio yake ya haraka.

Wakati wa Majira ya Vuli mwaka 1893, nilirejea Marekani ambako nilikaa kwa miezi minne. Nilitumia muda mwingi kutembelea maonesho ya Chicago, nilikaa California, na kurejea Washington na New York kupitia Texas na Louisiana. Huko Chicago, niliishi katika sehemu za kifahari kwenye Vilabu vya wanamichezo na kutembelea Kilabu cha Michezo ya Olimpiki kilichopo katika mji wa San Francisco. Katika vyuo vikuu

nilivyokuwa nikivitembelea kwa mara ya kwanza au nilivyokuwa nimeshatembelea mwaka 1889, nilipata mapokezi mazuri, licha ya ukweli kwamba kitabu changu kinachohusu Vyuo Vikuu vya Mwambao wa Bahari ya Atlantiki, kilichochapishwa mwaka 1890, hakikukubaliwa vyema na maprofesa, ambao waligundua kuwa fani na maudhui havikuwa na muunganiko mzuri. Kwa vyovyote vile, hakuna mahali ambapo wazo la kufufua Michezo ya Olimpiki liliendana na shauku iliyokuwa inastahili. Rafiki yangu William Sloane peke yake alikuwa na shauku kubwa kuhusu mradi. Siku moja kabla ya kuondoka New York kurejea Ulaya, aliandaa chakula cha jioni katika Kilabu cha Chuo Kikuu jijini New York, alialika wageni ambao aliamini wanaunga mkono mawazo ya michezo na historia. Kulikuwa na mazungumzo mazuri yaliyokuwa na nia ya dhati, lakini yenye hisia za kushindwa kusikoepukika.

Kulikuwa na mawazo yaleyale yenye nguvu zaidi, huko London mnamo mwezi Februari mwaka 1891. Bw. John Astley aliwaalika marafiki kadhaa kwenye Kilabu cha Michezo ili wazungumzie mipango yangu lakini idadi ya waliokuwa wamekubali ilipungua na kubaki wageni wachache. Wakati huohuo, Majira ya Masika yalikuwa yakisonga bila kuonesha matumaini yoyote. Hata hivyo sikufikiria kukata tamaa. Ingekuwa ni vigumu kuomba kujiunga bila ya kuwa na idadi na uimara wa kutosha wa watu, waliokuwa wakitokea pande zote za Dunia, kuanzia New Zealand na Jamaica hadi kwenye miji ya Amiens na Bordeaux.

Hata hivyo Kulikuwa na vyanzo viwili vyenye kutia shaka: vyuo vikuu havikuonesha kuvutiwa. Nilitarajia ushiriki wao mkubwa ili kuongeza "utaalamu" wa wanazuoni. Ujerumani haikuitikia kama ilivyotarajiwa. Kipindi hicho, sikufahamiana na yeyote katika hiyo nchi lakini nilitegemea ni muhimu sana kuungwa mkono na Ujerumani pamoja na Uingereza na "Walatini", neno nililoendelea kulitumia hadi pale nilipogundua kwamba sio neno sahihi. Nikiwa nimeandaa utangulizi nilitembelea tawi la jeshi la Ujerumani la Paris ambapo Kanali maarufu Schwartzkoppen, baadaye alihusika kwenye sakata la Kashfa ya kisiasa (*Dreyfus*). Kutokana na ushauri wake, niliamwandikia barua Waziri wa Prussia, Bw. de Podbielski, ambaye alitambulishwa kwangu kama kiongozi mkubwa wa michezo, lakini sikujibiwa.

Suala la kuingiza Ujerumani kwenye jambo hili lilisababisha hatari ya kujiondoa kwenye Chama Cha Sarakasi cha Ufaransa. Mnamo tarehe 15 Mei Mwaka 1891, Bw. Cuperus alikataa kwa ghadhabu kuruhusu Chama Cha Sarakasi cha Ubelgiji kujiunga: Alisema, "Shirikisho langu liliamini na linaendelea kuamini kwamba Sarakasi na michezo ni vitu visivyohusiana na muda wote vinakinzana. Mimi nilikubaliana na suala hili. Niliona mawazo kama hayo ni ya kipuuzi, lakini ningefanyaje? *Chama cha Wanasarakasi wa Ufaransa (Union des Sociétés Français de Gymnastique*) kilijiunga. Hata hivyo Bw. Sansboeuf alinishauri kwamba wanachama wangu watajiuzulu ikiwa Wajerumani watajiunga. Jambo hili lilikuwa la kuudhi na kudhalilisha. Mwendelezo huu wa upinzani dhidi ya washindi wa Mwaka 1870 ulinighadhabisha. Ni kitu gani kingekuwa cha

Ufaransa pekee, Ubeligi au Austria, zaidi ya kupigana ngumi kwa hasira ukiwa umeketi? Je, hii ndiyo namna ambayo mababu zetu walielewa "nafasi kati ya mapigano?" Nisingeweza kusema ni kwa namna gani, wakati wangu wa balehe, niliteswa na mtazamo huu, ambao dhana hasi ya uzalendo ilipandikizwa kwenye kizazi changu. Ingawa nilikuwa kwenye upinzani mkubwa, sikujihisi nimeshindwa. Mwamko wa 1878 ulinihamasisha na kilele cha mafanikio cha mwaka 1889 kilinikomboa kwa kunipa wazo la nguvu za Taifa na matumaini ya wakati ujao ulio tofauti na wakati muhimu uliopita. Tarehe ya mkutano ilipokaribia kila kitu kilibaki kama kilivyo, mwanga kwenye mandharinyuma ya kijivu. Ni kana kwamba nilikuwa nina bendi ndogo ya okestra ambayo ilikuwa ikiniangalia huku ikisubiri ishara ya kuanza bila kujua ni mdundo gani utakaopigwa. Nilielekeza nguvu zangu zote kwenye ufunguzi wa kikao na utumbuizaji wa awali wa wimbo wa "*Hymn to Apollo*" uliotungwa katika magofu ya Delphi. Gabriel Fauré aliipongeza kwa furaha.

Ghafla jina la mkutano lilibadilika. Maneno, "Mkutano wa kufufua Michezo ya Olimpiki" yalionekana kwenye barua za mwaliko, moja ya barua inaweza kuonekana katika Makumbusho ya Olimpiki huko Lausanne. Kwenye mandhari nzuri ya uwanja wa maonesho ya Sorbone (Sorbonne mpya wakati huu), uliopambwa na mchoraji maarufu Puvis de Chavannes "*Sacred copse*", baada ya hotuba ya kitaaluma ya Baron de Courcel na wimbo mzuri ulioimbwa na Jean Aicard na maelezo mazuri ya Théodore Reinach, upigaji wa mziki huu mzuri uliamsha ari ya watazamaji wengi. Hisia zisizoweza kuelezewa zilienea kwa watu waliokuwapo jukwaani wakicheza kwa miondoko iliyowafanya wakumbuke zamani. Kwa jinsi hii mziki wa Ugiriki ya zamani ulipenya kwenye ukumbi wote. Nilifahamu kwamba iwe kwa kujua au kwa kutojua hakuna atakayepinga ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki.

Kwa hakika ilitangazwa kwa kauli moja kwenye kikao cha mwisho tarehe 23 Juni. Wajumbe wa mkutano walitekeleza majukumu yao vizuri. Wakiwa wamegawanywa katika kamisheni mbili, moja ya Michezo ya Ridhaa na nyingine ya Michezo ya Olimpiki. Waliongozwa kwa upande mmoja na Michel Gondinet, Rais wa Kilabu cha Mashindano ya mbio za Ufaransa, na upande mwingine D. Vikelas, mwanachama wa chama cha wanasarakasi. Makamu wa Rais walikuwa Profesa W. M. Sloane na R. Todd, wanachama wa umoja wa waendesha baiskeli wa Taifa wa kundi la kwanza, na Baron de Carayon la Tour, mwanachama wa Société Hippique Française, kwa kundi lingine.

Vikao vilikwenda vizuri. Kulikuwa na mijadala kadhaa ya kuvutia kuhusu masuala ya kiufundi na masuala ya kimichezo ya ridhaa, ambapo Mkuu wa Chuo Kikuu alikuja kutoka nyumbani kwake ili kuhudhuria vikao kadhaa.

Kuhusu Michezo ya Olimpiki, kila mtu alikubali mapendekezo yangu bila mjadala. Mkutano ulipitisha kanuni kuu moja baada ya nyingine ambazo awali nilikuwa nimezifanyia uamuzi; kila baada ya miaka minne, mhusika wa kisasa wa matukio ya

kuondoa michezo shuleni (Vikelas na Swede Bergh wangependa kuingiza mashindano ya watoto, jambo ambalo niliona halitekelezeki na ni la hatari), na hatimaye uteuzi wa Kamati ya Kimataifa - ya kudumu ikiwa na misingi ya kudumu na muundo imara - ambao wajumbe wake watakuwa wawakilishi wa mashindano ya Michezo ya Olimpiki katika nchi zao.

Uchaguzi wa Athene wa Mwaka 1896, haukuendana na mipango yangu ya awali kwa sababu Ugiriki haikuwa na sifa ya kufanyika kwa mashindano hayo pia sikufikiri kwamba inaweza kuhimili uzinduzi wa mashindano ya michezo ya kimataifa.



**2.** Mkutano wa mwaka 1894; Mwenyekiti wa Mkutano Baron de Courcel



**3.** Mkutano wa mwaka 1894; Mwenyekiti wa kwanza wa IOC Demetrius Vikelas



***4.*** *Mkutano wa mwaka 1894 Kamishna Charles Herbert*



***5.*** *Mkutano wa mwaka 1894 Kamishna Charles M. Sloane*


Kipindi fulani nilifikiria kuzindua michezo huko Paris katika mwaka wa kwanza wa karne ya 20, kama nilivyoelezea katika jarida la Revue de Paris la tarehe 15 Mwezi Juni Mwaka 1894, nilifanya kila linalowezekana "kuiinua Ugiriki ya zamani", kwenye sherehe za michezo. Mazungumzo mbalimbali na D. Vikelas, ambaye ucheshi wake ulinivutia kuanzia mwanzo, ulinifanya nibadili maoni yangu. Kwa upande wake, alitaka yafanyike Ugiriki lakini wakati huohuo alisita kwenye jukumu la kuihusisha nchi yake kwenye jambo kama hilo. Tulitiana moyo na Athene ilichaguliwa kwa shangwe kubwa.

Wazo la kuendesha Michezo hiyo katika nchi tofauti lilikubaliwa bila mapingamizi mengi. Vinginevyo hakuna nchi ambayo ingekubali gharama ya uendeshaji. Kwa namna yoyote Ugiriki, isingeweza kumudu maandalizi ya kiufundi na kifedha.

Niliruhusiwa kuteuwa wajumbe wa IOC. Wafuatao walipendekezwa na walichaguliwa bila mabadiliko yoyote: Vikelas kwa Ugiriki: Callot na mimi kwa Ufaransa; Jenerali de Boutowsky kwa Urusi; Kanali Balck kwa Swideni; Profesa Sloane wa Marekani; Jiri Guth (wa Bohemia); Fr. Kemény (wa Hungaria); C. Herbert na Lord Ampthill kwa Uingereza; Profesa Zubiaur kwa Argentina na L.A. Cuff kwa New Zealand; Count Lucchesi Palli, ambaye alikubali kuwa mjumbe wa Italia kwa muda; na, hatimaye Max de Bousies kwa Ubelgiji. Hakuna aliyeonekana kugundua kuwa nilikuwa nimechagua karibu wajumbe wasiokuwapo. Kama majina yao yalivyoonekana kwenye orodha ya "wajumbe wa heshima wa Mkutano", watu walikuwa wamezoea kuona majina yao na walidhani kwa urahisi kuwa walikuwa wanachama waaminifu kila wakati kwenye majukumu yao. Nilihitaji nafasi ya kutosha kuanzia mwanzo, kwa sababu migogoro mingi ingeibuka. Baadhi yao kwa gharama yoyote wangetaka kuzuia au kufaidika kutokana na mradi au kubadili uelekeo. Hiyo ndio asili ya binadamu.

# II

## Ushindi wa Wagiriki (1882 – 1896)



**06**. *Wanaounga mkono na wanaopinga Michezo ya Olimpiki huko Athene: Mvutano kati ya waziri Derlyannis na Trooupis*

Siku chache baada ya mkutano kumalizika, Sloane, E. Callot na mimi tulikutana na Bw. Vikelas kwa ajili ya mkutano katika nyumba ndogo aliyoiandaa huko Rue de Babylone, Paris. Hapo ndipo jengo la IOC lilipojengwa. Vikelas alisita kuukubali Urais. Niliunga mkono wazo la Urais wa zamu kwenye kila taifa katika michezo ya Olimpiki inayofuata. Kila kitu ambacho kingeweza kusaidia kuimarisha utaratibu wa mzunguko wa kimataifa uliokuwa karibu kuanza ulionekana kuwa ni muhimu sana. Vikelas angeendelea kubaki kwenye wadhifa huo hadi mwisho wa mwaka 1896 nami ningeshika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne inayofuata. Wakati huohuo ningeshika cheo cha "Katibu Mkuu", wadhifa wenye maslahi makubwa kuliko wa marais, kwa kuwa katibu mkuu ni mhimili wa utawala uliopo madarakani.

Hivi ndivyo nilivyofanya na USFSA ili kuibadilisha na kuifanya kuwa msingi wa ufufuaji imara wa huko Ufaransa. Nilimteua Ernest Callot kuwa Mweka Hazina, mmoja wa wazee ambaye aliunganisha hali ya kupenda fasihi na michezo na kufungamana pamoja nasi kwenye matarajio yetu: kisha nikaelezea mpango wangu ambao nilipaswa kuukamilisha bila kusita na bila kuchelewa, mbele ya IOC na kuwapa wanachama wake ngao ya uhuru kamili kwa kukataa kuingizwa kwa "uwakilishi" wa mtu au kitu chochote pamoja na ruzuku inayotoka katika chanzo chochote. "Ngao ya mtu masikini" Vikelas alinung'unika lakini wote walielewa hitaji la kutenda kwa njia hii ikiwa tungetaka kuhakikisha mustakabali wa taasisi yenye jina maarufu, lakini isiyo na misingi ya kiutendaji na ambayo bado haijaeleweka kwa umma. Katika hadhira ya watu elfu mbili

waliosikiliza wimbo wa Apollo, kulikuwa na wasanii wengi kuliko wanamichezo na mwisho wa mkutano ulizuka mshangao uliosababishwa na mauaji ya Rais Carnot.

Aidha, tulifikia makubaliano kuhusu kanuni ya usawa wa michezo. Wakati wa mkutano, kwenye mkutano wa tarehe 19 na 22 Mwezi Juni, ilibidi niingilie kati ili kuzuia ile "michezo midogo" isichukuliwe tu kama nyongeza ya michezo ya "riadha", kama ilivyokuwa ikitokea mara nyingi na kwa muda mrefu.

Baadhi ya maazimio haya muhimu yameandikwa kwenye jarida Na. 2 la kila robo mwaka ambalo nilianza kulichapisha mara moja. Vifungu vifuatavyo vimenukuliwa kutoka katika kurasa za jarida hilo: "Tumeombwa kutoa ufafanuzi wa namna ya utekelezaji wetu. Kwa maelezo mafupi haya ndio majibu yetu…. Yafuatayo ni madhumuni yetu katika ufufuaji wa taasisi ambayo ilisahaulika kwa karne nyingi; kwa ajili ya umuhimu wa wanamichezo wanaoongezeka kila mwaka. Mchango wanaotoa ni muhimu na unaodumu katika wakati huu kama ilivyokuwa zamani; wamejitokeza tena wakiwa na sifa mpya ni wa kimataifa na kidemokrasia, jambo linalofanya wafae kwa mawazo na mahitaji ya sasa. Kadri siku zinavyokwenda, matokeo yao yatakuwa na faida au hasara kutegemeana na matumizi na mwelekeo waliochukua.

Wanamichezo wanaweza kuwa na faida au hasara; wanaweza kuleta umoja, heshima au ubinafsi, kujenga heshima au ufisadi, kujenga ujasiri au ukatili; hatimaye, wanaweza kuimarisha amani au kuleta vita. Mwisho, wanaweza kutumika kuimarisha amani au kusababisha vita. Kwa sasa, heshima, wema, fadhila, uungwana na amani ni mahitaji ya msingi kwenye demokrasia ya kisasa, iwe ya mfumo wa jamhuri au wa kifalme.

Katikati ya Majira ya Kiangazi, hatimaye IOC iliundwa kwa makubaliano ya wale ambao walikuwa wameteuliwa bila mimi kuwa na taarifa zao kabla. Mnamo tarehe 4 Septemba, hati ya kukubaliwa kwa Bw. Cuff iliwasili kutoka Christchurch na tarehe 15, ya kiongozi wa Andria's kutoka Naples. Kwa hivyo, mataifa kumi na mawili yaliwakilishwa wakati wa ufunguzi na moja ya shughuli ya kamati ilikuwa kukamilisha idadi yake. Ilikuwa "ni chombo pekee cha kuajiri", kama chombo cha maandalizi ya michuano ya mashindano ya mbio za mashua huko Henley. Hata hivyo, ilikuwa imeshafikia malengo ya miaka thelathini ijayo, na ndivyo ilivyo hadi sasa- kamati iliundwa na mihimili mitatu: mhimili wa ndani wa wanachama hai; "wanachama wa hiari" wanachama waliotayari kuelimishwa kwa njia sahihi; na hatimaye kundi la watu wenye viwango tofautitofauti ambao uwapo wao ungedhihirisha uwakilishi wa kitaifa.

Wakati wa Majira ya Vuli, Bwana Vikelas aliondoka kuelekea Athene, baada ya barua zake zilizokuwa zimeambatishwa kwenye majarida ya mwanzo kuwasilishwa huko. Tarehe 4 Mwezi Oktoba baada ya kuwasili, alinijulisha: "Kuanzia mji wa Prindisi, wenzangu walizungumza nami kwa shauku na furaha kuhusu Michezo ya Olimpiki." Jambo hili liliungwa mkono na mwandishi wa jarida la "*Le Temps*" huko Ugiriki. Siku iliyofuatia barua ya pili ya Bw. Vikelas ilimfikia Waziri mkuu, Bw. Tricoupis na ilimkuta

"akiwa na furaha", licha ya kwamba angekuwa na furaha zaidi ikiwa jambo zima lisingetokea. Vikelas alipendekeza kuitishwa kwa mkutano wa kamisheni ya Zappeion, ambao kwa mujibu wa sheria na kanuni zake, sio kwa kumbukumbu za jina hilo, bali mahame ya uwanja yaliyokuwa karibu.

Wakati huohuo, nilikusanya nyaraka kwa lengo la kuandaa maelezo ya kina kuhusu programu. Tarehe 26 Julai, Bw. G. Strehly, mwalimu wa sekondari ya Montaigne huko Paris, na mwanasarakasi maarufu, alinitumia mapendekezo binafsi kuhusu michezo ya "sarakasi" (mchezo pekee uliokuwa maarufu kwa kipindi kile). Maelezo ya "michezo ya sarakasi" yana maana ya michezo ya sarakasi pamoja na vifaa vingine vyote. Ni neno sahihi. Leo, baada ya miaka thelathini na mitano, ninafanya kila linalowezekana kufanya ukubalike. Baadaye, Bw. Herbert akiwa London alituma taarifa za kupokea masafa ya mashindano ya riadha.

Baadaye yakaletwa mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya UVF kwa ajili ya mashindano ya mbio za baiskeli: kimsingi yalikuwa mashindano ya kilomita 2, bila washiriki kuachiana nafasi na mbio za kilomita 100 ambapo washiriki wanaachiana nafasi. Bila kutafakari kwa kina, Chama cha Waendesha Baiskeli wa Uingereza waliomba nyongeza ya maili, mbio za kilometa 10 na 100, kwa muda usiozidi saa kumi na mbili.

Hatimaye, Klabu ya Kuhamasisha Mapigano ya Kutumia Panga (Societe d'Encouragement de Escrime) ilianzishwa, kwa maombi yangu, mradi uliojumuisha mashindano ya wanamichezo wa ridhaa na walimu (mchezo unaotumia sime nyembamba pekee).

Nikiwa na nyaraka hizi zilizojazwa kwenye sanduku langu, nilichukua usafiri wa haraka kwenda Marseilles na baadaye nilikwenda Ortegal kupitia Piraeus, nikiwa na wasiwasi na furaha – lakini furaha zaidi kuliko wasiwasi kadiri nilivyokuwa nikikaribia kufika. Wakati nikiwa kwenye bahari, niliisoma barua ndefu ambayo Bw. Stephan Dragoumis, Mbunge na Raisi wa Kamisheni ya Zappeion, alinieleza, baada ya Vikelas kuondoka kwenda Athene, hitimisho la kukatisha tamaa ambalo yeye na wenzake walilifikia. Kwakweli, alinishauri niache kutekeleza mradi wangu wa Olimpiki.

Baada ya kuwasili Piraeus usiku, kulikuwa na mkesha mtulivu, meli ilipotia nanga asubuhi, tulikaribishwa na vijana wenye shauku ambao muda mfupi baadaye walikuwa marafiki wazuri, ambao walienda uwanjani bila ya kutambulika kwa idadi kubwa kiasi cha kuharibu baadhi ya vito vya thamani ambavyo vilikuwa vivutio vikubwa kwenye njia ambayo wanariadha walikuwa wakiitumia kuingia uwanjani… Zilikuwa ni nyakati nzuri na zisizosahaulika. Muda mfupi kabla ya kuingia kwenye chumba changu cha hoteli, nilipokea ugeni wa naibu balozi wa Ufaransa Bw. Maurouard na wakati akiwa hapo kiongozi huyo wa Serikali, Bw. Tricoupis, ambaye ukitoa itifaki zote, alionekana kuwa na haraka ya kujenga ukaribu nami ili kupinga jitihada zangu kadri nilivyogundua baadaye alikuwa amedhamiria kufanya kila lililowezekana kuusitisha mradi wa Olimpiki. Alijidai

kupinga kwa kutumia hoja ya ufinyu wa bajeti, japo kwa mtazamo wangu, hiyo haikuwa sababu yake ya msingi pekee.

Ni kweli kwamba, kwa wakati huo Ugiriki ilikuwa katika hali ngumu sana kiuchumi. Waziri Mkuu alihofia kuwa, Serikali zilizokuwa zikiidai zingeweza kupinga "matumizi yasiyofaa" ya fedha kwa Ugiriki ambayo uchumi wake mdogo ungeifanya kuheshimu madeni yake. Nilieleza kuwa, matumizi yaliyokuwa yamependekezwa, hayakuwa makubwa. "Litazame kwa umakini, litathmini jambo lenyewe" Bw. Tricoupis alisema huku akiondoka. "Nina uhakika kwamba utakuja kugundua kwamba Ugiriki haina fedha za kutosha kulitekeleza suala lako".

Hazikupita siku nyingi, nilipata fursa ya kutembelea Acropolis, au sehemu nyingine yoyote ya Athene. Nilikuwa kama mpira uliokuwa ukirushwa huku na huko dhidi ya timu mbili pinzani. Upande wa upinzani ukiongozwa na Bw. Th. Delyannis, uliunga mkono kwa shauku kubwa wazo la kuwa na Michezo ya Olimpiki. Vyombo vya habari vilikuwa vimegawanyika katika kambi mbili na kusababisha vurugu. Nilitumia muda wangu nikiwatembelea wanasiasa na waandishi wa habari, chini ya uangalizi wa marafiki wangu wapya, George Melas, mtoto wa Meya wa Athene, Alexander Mercati mtoto wa Mkurugenzi wa Benki na rafiki wa utotoni wa Mwanamfalme.

Kocha alishuka kwenye gari linalokokotwa na farasi na kumwambia George Melas kwa ukaribu na mazoea ya ucheshi waliokuwa nao kwa wakati huo: "Bw. mdogo George, nitakwambia kile ambacho rafiki yako ni lazima akifanye ili kumshawishi Bw. Tricoupis". Nilikereka kuwa Kigiriki nilichojifunza shuleni hakikuwa na faida yoyote kwangu, hasusani kwenye matamshi tuliyokuwa tukifundishwa. Lakini kwa upande mwingine, kila mtu alikuwa akizungumza Kifaransa. Nilishangaa sana kuiona Ugiriki ambayo ilikuwa na uhalisia wake na wakati huohuo, ikiwa ya kale na ya kisasa. Kuanzia sasa, nilikuwa na imani na wakati ujao wa nchi ya Ugiriki. Ningeendelea kuwa na imani kubwa kama ningeiona Ugiriki ikiendelea kama ilivyokuwa hapo awali.

Hata hivyo sikufanikiwa kuonana na mtu niliyekuwa namhitaji, ambaye alikuwa ni kiongozi mkuu. Muda wote wa kuwapo kwake, Vikelas alikuwa ametumia ushawishi wake wote na shauku, lakini aliniachia jukumu la kuandaa mipangokazi… Mfalme alipokuwa Urusi, Mwanamfalme alikaimu nafasi hiyo kama mtawala na jambo hili lilimfanya awe mwoga katika kushughulika na baraza la mawaziri hasimu. Hata hivyo, baada ya vikao viwili vya majadiliano marefu pamoja naye, nilijiridhisha kuwa, kwa hakika alikuwa upande wetu. Baada ya kuhoji kuhusiana na rasilimali za michezo ya Athene, viwanja na wafanyakazi waliokuwapo, niliandaa rasimu ya mradi na kupanga bajeti ambayo kwa kiasi fulani ilionekana kuniridhisha. Kwa jinsi ninavyokumbuka, sikuwa na tawimu sahihi, niliamini kuwa zingekuwa zinakaribia drakimas 250,000. Kwa upande wa uwanja masharti yalitolewa kwamba, yajengwe majukwaa ya mbao pekee.

Baadaye nilimwita tena Bw. Tricoupis ili kumwambia kuhusu wazo langu zuri. Alikuwa amejiandaa kwa ajili ya jambo hili. Hakuleta pingamizi lolote lakini alikataa ushiriki wowote wa serikali. Nilimwuliza endapo angeweza "kutopendelea upande wowote" aliniambia angeweza… lakini baada ya kuridhishwa. Kisha nikaomba kutumia ukumbi wa Zappein, ambapo wasingekataa.



7. *Athene: upande wa uwanja wa michezo ya Olimpiki 1894*

Nikiwa na marafiki wangu ambao idadi yao ilikuwa ikiongezeka, niliandaa barua za mialiko kwa ajili ya mkutano, ambao ulifanyika tarehe 12 mwezi Novemba na kuhudhuriwa na watu wengi. Kwa ilivyo bahati, nilikuwa nimezoea aina hii ya mkusanyiko ambao upo katika hali ya utulivu na mshtuko. Kamati iliundwa chini ya usimamizi wa Mwanamfalme – kukubali kwake kuwa mlezi kulinyamazisha kila upinzani. Kanali Mano, Bw. E. Scouloudis, Mbunge wa Bunge na Waziri wa zamani, Kamanda Soutzo, anayeongoza kikosi cha wapanda farasi, na Bw. Retzinas, Meya wa Piraeus, walichaguliwa kuwa Makamu wa Rais; Bw. Paul Skouses, Mweka Hazina: Bw. A Mercat na Bw. G. Melas, Makatibu. Tarehe ya Michezo ilipangwa kuanzia tarehe 5 hadi 15 Mwezi Aprili Mwaka 1896. Mwaka huo, tungekuwa na bahati ya kushuhudia tarehe za sherehe za Pasaka za kanisa la Ugiriki na Magharibi zikigongana. Programu niliyokuja nayo kutoka Paris ilipitishwa.

Siku nne baadaye, tarehe 16 Mwezi Novemba, nilitoa mhadhara kwenye chama cha wanafasihi wa Athene, Parnassus. Ukumbi ulikuwa umejaa. Ikiwa chama cha Bw. Tricoupis kisingejiondoa hata cha upinzani kisingejiondoa. Bado nina nakala ya Romos, jarida la dhihaka lililoandikwa kwa muundo wa shairi, lenye katuni za kufurahisha likiwaonesha Bw. Tricoupis na Bw. Delyannis, mikono yao ikiwa imefichwa kwenye glavu kubwa za masumbwi, wakipigania Michezo ya Olympiki. Nikiwa na shaka baada ya kukaa kwa mwezi mmoja ilibidi niondoke Athene kupitia nchi kavu wakati huu. Klabu ya sarakasi ya Panachaic ilinikaribisha kwa kishindo huko Patras. Mmoja wa wajumbe wa kamati aliteuliwa kunisindikiza kwenda Olimpia. Ilikuwa jioni tulipofika pale. Ilinibidi

nisubiri hadi asubuhi ili kuona kwa mara ya kwanza mandhari nzuri, ambayo nilikuwa nikiiwaza. Nilitumia muda wote wa asubuhi nikizuru mahame. Nisingeuona tena mji wa Olimpia kwa kipindi cha miaka thelathini na mmoja. Wakati wa tukio maalumu la kumbukizi ya ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki. Kutoka Patras, baada ya kusimama kwa muda mfupi huko Curfu, nilifika Brindisi na baadaye Naples ambako nilikaribishwa na mwenzangu mpya Mtawala wa Andria. Nilitoa mhadhara terehe 7 Mwezi Desemba kwenye kikao cha Filolojia kilichoongozwa na Mbunge maarufu, Bw. Borghi – mhadhara ambao ulinikatisha tamaa. Mbali na nyimbo za Apollo na kuhahakishia picha za michoro ya magofu ya zamani, zenye kukumbusha Michezo ya Olimpiki, ulikosa imani.



# III

## Michezo ya Kwanza ya Olimpiki (Athene, 1896)



***8**. Watazamaji wakiwa juu ya mapaa ya nyumba wakiangalia mwanzo wa mbio za Marathoni*

Mara tu nilipoondoka Ugiriki, Bw. Scouloudis alifanya kila linalowezekana kuharibu misingi iliyokuwa imewekwa. Aliwaalika Makamu wa Rais wengine watatu waje kumwona, akawashawishi kwamba, bajeti niliyoipanga haikuwa halisi, kwa maana kwamba gharama zingekuwa kubwa na hakungekuwa na faida... Baada ya kuwakatisha tamaa vya kutosha, aliwatangazia wanakamati kuwa, suala zima lisitishwe na wasubiri uamuzi wa mwisho kutoka kwa Mtukufu Mfalme.

Alikuwa na uhakika kuwa, uamuzi huo ungekuwa hivyo, lakini mambo yalikuwa tofauti na alivyotarajia. Mwanamfalme aliwapokea wajumbe wenye ripoti na baada ya kuipokea aliiweka mezani, akisema kwamba ataisoma na baada ya mazungumzo mafupi akaagana na wajumbe hao wakaenda zao. Sikuona kama alikuwa na shaka hata kidogo. Alikuwa tayari ameshafanya uamuzi. Ingawa alikuwa akitunza siri kwa kila kitu

kilichokuwa kinaendelea, sikuwa na maelezo kamili ya kile kilichotokea kati ya Mwanamfalme na Mfalme, baada ya kurudi kwa Mfalme, japo kwa hakika Mfalme ni lazima angeunga mkono kuwa mrithi wa kiti cha ufalme alikuwa kiongozi mkuu wa Ugiriki, kwa muda wa miezi sita baadaye nilipowasiliana naye alipokuwa kwenye ziara fupi huko Paris, Mfalme aliniambia kwa weledi ambao Mwanamfalme aliuonesha kwenye maandalizi ya Michezo.

Sifa hizi zilikuwa za kweli kabisa. Nilivutiwa na werevu na mbinu alizozitumia kudhibiti na kuweka mambo sawa katika hali tete; lakini hata hivyo, hali hiyo haikudumu. Bw. Tricoupis hakuridhishwa na kupuuzwa kwa matakwa yake kiasi hicho. Alitumia kisingizo cha tukio hilo lililotokea wakati wa mgomo na kumweka Mfalme kwenye nafasi ya "kuchagua" kati ya mtoto wake na Waziri wake. Kwa utulivu lakini kwa uthabiti, Mfalme alionesha masikitiko yake kwa kitendo cha kujiuzulu kwa Bw. Tricoupis. Tricoupis aliondoka kwa hasira. Michezo ya Olimpiki iliendelea kumtia uchungu kiasi kwamba, kadri michezo ilivyokaribia, alikwenda Nice. Akiwa huko, alipatwa na kifo cha ghafla, taarifa hizo zilifika Athene wakati wa Michezo, jioni moja ya sherehe iliyokuwa na taa nzuri zenye mwanga mkali na muziki mkubwa.

Kabla ya kusubiri kumalizika kwa sherehe hiyo, Mwanamfalme aliunda upya Kamati ambayo awali iliundwa tarehe 12 Novemba, akifanya marekebisho madogo ya kanuni za shirika. Aliongeza idadi ya washirika wapya, miongoni mwao alikuwa Bw. Delyannis ambaye wakati huohuo alikuwa Waziri Mkuu, na Bw. Zaimis ambaye ni Rais wa sasa wa Jamhuri. Aliwaingiza Makatibu hao wawili lakini pia alimchukua Constantin Mano na George Streit, ambaye baadaye angekuwa mwanasiasa mzuri. Aliwaweka ndugu zake kwenye nafasi za juu za kamisheni za kiufundi. Hatimaye, alimteua Bw. T. Philemon, Meya wa zamani wa Athene, kuwa Katibu Mkuu na kumtuma mara moja kwenda huko Alexandria kumtembelea Bw. Averof ili kupata fedha zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Marumaru, kama ilivyokuwa wakati wa Pericles. Muda ulikuwa unaenda. Tangu tarehe 23 Juni 1894 miezi ilikuwa imepotea kutokana na upinzani dhidi ya mradi huo. Wakati huo, Majira ya Vuli ya 1895 yalikuwa yanakaribia.

Ulikuwa umebaki walau mwaka mmoja kukamilisha kila kitu. Ni wanamichezo wachache sana leo wanaofahamu programu halisi ya Michezo ya 1896. Haishangazi, baada ya miaka thelathini na saba! Hii ni taarifa rasmi iliyochapishwa mwanzoni mwa robo mwaka wa IOC:

A. Michezo ya riadha: Mbio meta 100, 400, 800 na 1,500; meta 110 kuruka viunzi (Kanuni za Muungano Française des Sports Athlétiques).

Matukio ya dimbani: kuruka chini, kuruka juu, kuruka kwa upinde: kunyanyua vitu vizito na kurusha kisahani (Kanuni za Waingereza).

Marathoni

B. Michezo ya sarakasi: sarakasi kwa mtu mmoja,upandaji kamba, sarakasi za kuruka nyuma/mbele: sarakasi za kuruka kwa mwimo sawa; pete; baa sambamba, mbio za farasi; kunyanyua vitu vizito.

Timu za Makundi (timu za makumi)

C: Michezo ya mapanga: nyenzo za kitara, seba na upanga mwembamba kwa wanamichezo wa ridhaa na walimu (Kanuni Maalum za Vyama vya Michezo ya Vitara huko Paris).

Mieleka: Kirumi na Kigiriki.

D. Kulenga shabaha kwa kutumia silaha za kijeshi, bunduki (Kanuni zinazotumika katika Usajili)

E. Michezo ya kuendesha mashua: mbio za mashua za zaidi ya maili 10 (Kanuni za Cercle de la Voile, Paris). Uendeshaji wa mashua (Ukadiriaji na Kanuni za Chama cha Mashindano ya Kuendesha Mashua cha Uingereza) kwa mashua za tani tatu, kumi na ishirini na zaidi ya tani ishirini.

Umbali: maili 5 na 10.

Kupiga makasia: kasia moja meta 2,000 bila kupokezana; mashua ndogo: kupiga makasia mara mbili bila kupokezana: mashua ndefu na nyepesi za michezo ya kupiga makasia: (mpiga kasia mmoja) bila kupokezana, (Kanuni za Klabu ya Kupiga Makasia ya Itali).

Kuogelea: kwa kasi kwa kuachiana nafasi ndogo: meta 100 umbali mrefu wa kuachiana nafasi meta 500, umbali mrefu wa mchezo wa majipolo meta 1,000.

F: Mbio fupi za Baiskeli: meta 2,000 bila kuachiana nafasi: meta 10,000 kwa kuachiana nafasi; umbali mrefu: kilometa 100, kwa kuachiana nafasi (Kanuni za Chama cha Kimataifa cha Waendesha Baiskeli).

G: Mbio za farasi: eneo la mafunzo ya mbio za farasi, kuruka viunzi, uendeshaji farasi wa madoido, kubembea.

H: Michezo ya riadha: Tenisi ya sakafuni ya mtu mmoja na watu wawili

Nimeamua kutoa tena nakala nzima ya matini hii. Kila mtu sasa anaweza kushuhudia ni ukweli kiasi gani uliomo katika simulizi iliyorudiwarudiwa ambayo mashindano ya kisasa yalijumuishwa, mwanzoni, hususani mwa michezo, ambayo baadaye iliongezwa

michezo mingine mbalimbali. Je, kuna ukweli kiasi gani ndani yake?... Hakuna hata neno moja.

Programu hii ambayo, hata baada ya kuundwa upya kwa Kamati, bado iliweka tarehe ya awali ya mkutano ambayo ilikuwa ni 12 Novemba 1894 katika ukumbi wa Zappeion ambapo uwasilishwaji tofautitofauti wa kategoria za michezo ya lazima kama iliyoorodheshwa ulifanyika kwa usawa kwa mujibu wa mkataba: riadha, sarakasi, kuendesha mashua na michezo ya ngumi, mbio za farasi... Endapo nitaongezea maelezo kuwa, kama itifaki nyingi kwa ajili ya ufunguzi na ufungaji wa sherehe zingezingatiwa, upandishaji wa bendera za kitaifa kwa kila mshindi, ungefanyika kwa kila tukio la utoaji wa tuzo... muda huohuo kila mtu angekubaliana kuwa, michezo mipya ya Olimpiki iliyokuwa imeanza, ilipaswa kuendelea hivyohivyo. Hizi ndizo harakati dhidi ya vurugu za upinzani ambazo zilitokana na kutokuelewa, kukata tamaa na wivu vilivyodumu kwa kipindi cha miaka zaidi ya ishirini, vikiendelea kwa kila robo lakini vilifanikiwa mara moja tu mwaka 1900 vikiwa na malengo yake mabaya ambayo hapo baadaye hayakufanikiwa kutushinda.

Programu iliyoanzishwa tena ilichapishwa kwa idhini ya Bodi ya IOC, ambayo iliundwa na Bw. Vikelas, Bw. Callot na mimi. Vikelas aliogopa sana kusaini hati "iliyotoka kwa mtawala wake wa baadaye". Hata hivyo nilisisitiza. Ulikuwa uamuzi madhubuti na nilidhamiria kutoikosa fursa yoyote ya kutetea nafasi ya uongozi wa IOC, hata hivyo inaweza kuwa dhaifu na isiyo na maana.

Katika miezi ya Januari na Februari mwaka 1895, Vikelas, ambaye alirejea Athene, aliniandikia ujumbe wastani mara tatu kwa juma. Shauku yake haikuwa na kikomo na alijitoa katika juhudi zake. Alifanya kazi kama ofisa mawasiliano. Siku moja alinitumia tafsiri ya hotuba ya uzinduzi ambayo mwanamfalme angeisoma. "Tafadhali soma na unukuu." Siku nyingine alinitaarifu kuhusu maonesho makubwa ya kwanza. Wale waliokuwa kwenye nafasi za juu, bado hawakuwa na uhakika, walihitaji kuhakikishiwa kuhusu mipango kwa ajili ya mashindano ya mbio za baiskeli, mpangilio wa viti Uwanjani, kadi za mialiko, ushauri kuhusu njia zitakazotumika kukimbia... Wakati huohuo, vipande vya marumaru vilipangwa katika maeneo yenye kuheshimika, na taarifa zilienea ulimwenguni kote. Kamati ziliundwa. Huko Hungaria, licha ya ukweli kwamba kila mtu alikuwa akijiandaa kwa hamu kwa ajili ya sherehe za milenia za Jimbo la Magyar kwa mwaka huohuo wa 1896. Michezo ya Olimpiki haikupuuzwa. Count Czaky na Kemény walinihoji wakati mambo yakiwa hayaendi vizuri huko Athene. Kwa nini hatukufanya ufunguzi wa Michezo ya Olimpiki huko Budapest wakati wa sherehe za milenia? Nilikuwa makini kutokataa ofa hizi, lakini niliridhika kuzitumia ili kujijengea heshima kwa Wagiriki. Balck aliandika kutoka Stockholm kwamba alikuwa "amefanya kazi nzuri", kwamba Mwanamfalme (mwakilishi wa Mfalme) alivutiwa. "Tuna wasiwasi kidogo, lakini tutafanya kila kitu kulingana na uwezo wetu." Wakati huohuo, kutoka Urusi, Jenerali de Boutowsky alielekeza juhudi zake. Alipata "mawazo tofauti". Kwenye

"Vyombo vyetu vya habari," aliandika. (2 Februari 1895), anaona suala la Mafunzo ya mazoezi ya viungo vya mwili kuwa halistahili kutajwa katika gazeti la msimamo fulani.”

Kutoka Uingereza, habari zilitia moyo, Bw. Romanos, mtendaji mkuu wa uhusiano wa Ugiriki kwa wakati huo, na Bw. Constantin Mano, mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Oxford, walichochea hamasa katika ukusanyaji fedha miongoni mwa makoloni ya Kigiriki. Baadhi ya nchi ambazo mifumo yake haikuwa na ulinganifu, zilikuwa na woga na kuongozwa vibaya, japo zilikuwa na matumaini. Haya yalianzishwa kama sheria ya jumla, iliyoanza kabla ya kupelekwa Athene, ambayo ilimkasirisha Bw. Philemoni. Ninaamini alikuwa mtu mzuri, mwerevu, mtawala mzuri, lakini alikuwa mtu mwenye wivu na majivuno. Alijiona hafai na hilo lilimkasirisha. Hatimaye, alinikaribisha kwa kutoridhika bila ya kificho, shida hiyo niliipitia nikiwa huko Ufaransa na hususani katika dhoruba iliyovuma kwa muda kutoka kwenye kingo za Spree.

Huko Paris, bila shaka, serikali ilipuuza harakati hizo ingawa zilikuwa zimeidhinishwa mwaka mmoja kabla. Ruzuku za kuwasaidia wanamichezo wa Ufaransa kwenda Athene!... Ni ujasiri ulioje! Ilitubidi kuunda Kamati ya Ufaransa sisi wenyewe, na Bw. de Courcel kama Rais na Bw. Fabens, Kaimu Katibu. Baada ya kukubali kujiunga, Bw. Mérillon, Rais wa Umoja wa Vilabu vya Walenga Shabaha (Union des Sociétés de Tir), alijiondoa kwa dhamiri yake mwenyewe, "Umoja uliamua kwamba hakuna sababu ya kushiriki katika maandalizi". Kinachoshangaza ni hasira iliyoonyeshwa katika barua zake kuhusu jambo hilo. "Ni ajabu." Aliniandikia ujumbe tarehe 14 Februari 1895, "kwamba waandaaji wa Michezo ya Olimpiki walipaswa kufikiria kwamba *Union Nationale de France* ungekubali kuwa mshirika wa kamati yao na kwamba kulenga shabaha kungekuwa ni tawi lililojumuishwa na kuwekwa kwenye orodha ya michezo." Ninanukuu maneno haya kwa maana yanaonyesha hali ya kutoaminiana ambayo inaendelea kuwapo licha ya misingi ya ushirikiano iliyopo baina ya michezo, hata kwenye duru isiyo rasmi ilipaswa kueleza. Hata hivyo, uelewa wa kawaida ulitawala na wanamichezo wa Ufaransa walijiunga na wengine kupitia Akropolis, ambapo kutokuwapo kwao kungekuwa kashfa.

Walijua kwamba wangelazimika kushindana na Wajerumani lakini hawakukubali kutishwa tena. Kundi lililoundwa mjini Berlin na Dkt. W. Gebhardt, ambaye nilikuwa nawasiliana naye mara kwa mara, alijaribu kuamsha ari za Wajerumani na alionekana kufanikiwa hadi mwishoni mwa mwaka (1895), barua ilipopokelewa huko Athene kutoka kwa kilabu kikubwa cha sarakasi cha Ujerumani kilikataa mwaliko ambao hapo kabla ulikuwa umekubaliwa. Kukataa huko kulitokana na mahojiano ya uongo ambayo yalichapishwa katika gazeti la Ufaransa bila ya kuzingatia taarifa yangu. Maneno yaliyohusishwa kwangu yalikuwa yamepotoshwa sana kiasi kwamba maandamano ya Wajerumani yalionekana kuwa ya wastani katika kukithiri na yenye kuzingatia taratibu. Mara tu nilipoambiwa kuhusiana na suala hilo, niliwasiliana na Gebhardt, lakini wakati huohuo gazeti la *Nationale Zeitung* lilichapisha barua iliyotoka kwa wanasarakasi. Ghafla

kulikuwa na malalamiko ya umma kwenye vyombo vya habari vya Ujerumani. Wakati huohuo nilituma nakala ya kukanusha kwa Bwana Rangaves, Waziri wa Ugiriki huko Berlin, ambaye alinishukuru na kunitaarifu kuhusiana na hatua alizochukua ili "kuutangazia umma" kuhusiana na kukanusha huko. "Alisema, aliweza kupata nakala aliyopewa Kansela, ambaye angeileta kama taarifa kwa Mfalme", kwa kufuata hatua zote muhimu "ambazo kwa chuki ya Ujerumani, ilikuwa imefikia viwango vya kutisha... Ni jana tu, aliongeza "Nilipokea baadhi ya makala hamsini kutoka kwenye himaya yote". Hata hivyo, chuki hiyo iliisha haraka na Gebhardt, ambaye alikuwa ametenda kwa uthabiti, aliitisha mkutano huko Berlin ambao, baada ya kusikia maelezo yake, alimwomba anihakikishie kwa njia ya telegramu "kwa moyo wa dhati na kwa kunuia mafanikio ya ushirikiano wa pamoja". Kwa ukarimu wake alituma nakala ya ujumbe huo kwa Balozi wa Ufaransa, Bw. Jules Herbette.

Hili lilifanyika tarehe 16 Januari (1895). Asty akiwa nchini Ugiriki, aliupokea ukanusho wangu mnamo tarehe 1 Januari na aliuchapisha, Bw. Philemon alijifanya kana kwamba aliamini uhalisia wa mahojiano hayo. Baadaye nilisikia kutoka kwa Gebhardt kwamba alikuwa akijinufaisha na tukio hilo la kujaribu kuiondosha IOC, "taasisi ya muda ambayo haikuwa na sababu zozote za kuwapo". Mwandishi wa jarida la *Le Temps*, katika barua yake kutoka Ugiriki ya tarehe 12 Januari, alisimulia taharuki iliyosababishwa na tukio hilo kwa nchi nzima ya Ugiriki. Kupuuzwa kwa maoni ya umma wa Wajerumani, Philemon alilazimika kuachana na mawazo yake maovu. Hata hivyo haikuwa hivyo hadi tarehe 7 Februari, nilipomkemea, aliamua kujibu kwa kunitumia telegramu ambayo Kamati ya Ugiriki "haikuamini maneno yaliyosemwa kuhisiana na mimi. Sikupata muda mapema wa kujitetea ili kusema ukweli.


Hatimaye siku ya tukio ilifika wakati umati ulipoingia kwenye uwanja huo, ambao ulikuwa umerejeshwa kwenye hadhi yake na wakati huo Mfalme George alipotangaza rasmi ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki na kutamka maneno ya kimila: "Ninafungua Rasmi Michezo ya 1 ya Olimpiki ya Kisasa." Milio ya mizinga ilisikika mara moja, ikifuatiwa na kuachiliwa kwa njiwa ambao waliruka kwa furaha juu ya uwanja; kwaya ziliimba nyimbo za mahadhi ya muziki mzuri zilizotungwa na mwanamuziki wa Ugiriki Samara na mashindano yalianza. Wazo hilo lilikuwa halisi na sasa lilikuwa ni sehemu ya historia. "Hizi zote ni juhudi zako", Gebhardt aliniambia (mara zote tulikuwa tukizungumza Kiingereza pamoja). Kikundi kilichoundwa na IOC na kwa upande mwingine wa Mwanamfalme kiliwakilisha hali ya kudumu ya tukio na tabia ya kimataifa ambayo niliazimia kuitunza kwa gharama yoyote. Kelele zilisikika kote zikionesha shauku ya utaifa wa Wagiriki walivutiwa na wazo la kuuona mji wa Athene ukiwa makao makuu ya kudumu ya Michezo hiyo, ukiwa kama mji mwenyeji kwa kila baada ya miaka minne kwa wingi huu wa watu wa kuvutia na wenye faida kwa wageni.

Mahali pengine nilipoelezea fahari na sherehe za Michezo hii ya kwanza, ugumu na changamoto za kiufundi. Shauku ya watazamaji, hila, kukatishwa tamaa na wenzangu,

na hatimaye mpango wa kifalme unaitaka mamlaka ya Ugiriki kufufua michezo ya Olimpiki... Mimi pia ningeunga mkono kwa hiari kama nisingekuwa ninajua kutotekelezeka kwa mpango huo, ambao usingekuwa na mafanikio. Hakuna mtu ambaye angeamini kwa urahisi kwa kipindi ambacho mji wa Athene ungeendelea kila baada ya miaka minne kuweka juhudi zilizohitajika kwa ajili ya kipindi cha uhuishaji wa taasisi na ufadhili. Pamoja na kujaribu na kufanya taifa liende, watu wote walikabiliwa ghafla na maono hai ya zamani zake tukufu zaidi. Ugiriki yote ilizizima kwa pamoja kwenye tamasha hili. Namna fulani ya uhamasishaji wa maadili ulifanyika. Hata watawa kwenye Mlima Athos, wakati huo walijitenga na nchi mama na mpaka usiokubalika. Ilituma michango kwa ajili ya kusherehekea Michezo hiyo. Wakati huohuo maeneo mengine duniani ufufuaji wa michezo ya Olimpiki ulikuwa umeshika kasi, ulikuwa na taswira nzuri kwenye fikira za Wagiriki na ulikuwa na uwezekano wa kuleta matokeo makubwa. Kwa hiyo, ni kweli kwamba mwaka mmoja baadaye vita vilitokea kati ya Wagiriki na Waturuki kwa ajili ya ukombozi wa mji wa Crete, Michezo ya Olimpiki ililalamikiwa kwa kuwa na majukumu makubwa na kuhudumu kama mratibu wa maandalizi ya michuano hii kwa kuwezesha kukaimisha kutoka kwenye makoloni ya Wagiriki na kuwekwa pamoja huko Athene kwa majadiliano kuhusu vita. Kulikuwa na ukweli kidogo kuhusu madai haya. Zaidi, inaweza kusemwa kwamba sherehe zililenga kuhamasisha harakati ambazo zilikuwa zimeshaandaliwa awali kutokana na msukumo wa mazingira. Haikuwa mara ya kwanza kwa Wakrete kuchukua silaha ili kupata uhuru wao. Jambo lao lilikuwa na nguvu iliyokuwa imetolewa kwa usawa na haki licha ya kushindwa kabisa kutokana na majeshi ya Ugiriki yaliyoongozwa na mchakato wa maboresho ya mazingira ya mji wa Crete na upangaji wa maandalizi ya uongozi ili kukamilisha mamlaka yajayo ya kisiwa cha Ugiriki.

Kwa namna yoyote ile mazingatio haya ya kisiasa hayakulenga kuzifanya serikali za Ulaya kujihusisha hususani na ufufuaji wa michezo ya Olimpiki. Wala haikuwa majukumu ya IOC wala ya kwangu yaliyorahisisha kwa namna yoyote ile. Kwa bahati michezo ya miaka miwili ya Olimpiki haikuzingatia ahadi zote. Washirika wangu waliposhindwa, Maoni ya umma ya Kigiriki kwa mtu aliyepinga kwa uthabiti utekelezaji wa mpango wangu uliokuwa "umeenea"..., nilikuwa peke yangu na mpweke kuliko wakati mwingine wowote, kwa kiwango kikubwa zaidi wakati nikiandaa mikutano ya mwaka 1894, bila kutegemea mtu yeyote. Pamoja na hayo nilitofautiana na Mfalme, ambaye hotuba yake kwenye dhifa ya mwisho iliyohudhuriwa na wanamichezo wote ilinifanya kuwa njiapanda: kukubaliana au kutokukubaliana. Niliamua kutofanya lolote. Lakini, kwa upande mwingine, kulipinga jambo hilo haikuwezekana. Nilijifanya mjinga asiyefahamu chochote. Niliamua kuipuuza hotuba ya Mfalme kwa kisingizio cha utata; akizungumza Kigiriki na Kifaransa kwa uwiano sawa, hakutumia maneno yanayofanana wakati wa kurudia pendekezo lake la kuimarisha makao makuu ya kudumu ya michezo

huko Athens. Pia nilipuuza taarifa za wanamichezo wa Marekani iliyotakiwa kusainiwa ili kuunga mkono wazo lao.



*9. nyuma ya Mwanamfalme Konstantino wa Ugiriki waliosimama ni wajumbe wa IOC wanaowakilisha katika Michezo ya kwanza ya Olimpiki, kutoka kulia kuelekea kushoto ni Dkt. Wilhem Gebhardt, mjumbe wa Ujerumani, Jenerali de Boutowski, mjumbe wa Urusi, Pierre de Coubertin mjumbe wa Ufaransa na mfufuaji wa Michezo ya Olimpiki, Franz Kemeny mjumbe kutoka Hungaria, Dimetrius Vikelas, mjumbe wa Ugiriki na rais wa kwanza wa IOC, Jiri Guth-Jarkoveky mjumbe wa Bohemia na wajumbe wawili wa Kamati ya Ugiriki.*

Vyombo vya habari vililitangaza jambo hili, lakini nilijifanya kama sijui kinachoendelea, kama mtu ambaye hajawahi na hatasikia chochote. Na jioni ileile Michezo ilifungwa. Nilimtumia Mfalme barua ya kumshukuru, pamoja na watu wa mji wa Athene na Ugiriki, kwa juhudi na weledi nishati ambao, kwa msaada na jitihada zao, na ujumbe uliotumwa kwao mwaka 1894 ulikuwa umejibiwa. Ndani yake, nilibainisha mwendelezo wa mpango na kamati ya Kimataifa kwa kuzungumzia suala la Michezo ya pili ya Olimpiki ambayo ingefanyika Paris... Barua ilikuwa fupi na ya kueleweka. Matoleo ya Kijerumani na Kiingereza yalitoka pamoja na lile la Kifaransa, haikuwa na umuhimu sana endapo toleo la Kigiriki lingechapishwa ama la mwonekano wa nje ulikuwa mzuri kulingana na mahitaji ya itifaki, lakini maudhui yalikuwa mabaya. Wajumbe wa Kamati hiyo, ambao kwa sehemu kubwa walikuwa ni wa nafasi za juu walionesha tahadhari kwa kuwa sikuwashirikisha wenzangu au kuwasilisha chochote kabla. Philemoni alificha uso wake kwa wasiwasi. Nini kingetokea kwake?... Sikujipa moyo sana. Hata hivyo hakuna kilichotokea. IOC ilihimili jaribio bila kujiuzulu au mpasuko kwenye muundo wake wa uongozi. Mwanamfalme, ambaye kwa hakika alielewa ugumu wa kujaribu kuhodhi Michezo kwa niaba ya Athene, hakumsaidia Mfalme, ambaye Philemoni alimsaidia, kwa hakika alichukua hatua ya haraka ambayo haikuwa na maana yoyote. Hivyo mzozo uliisha na Michezo ya pili ya Olimpiki ilianza kuonekana huko Paris. Isivyo bahati kama kungekuwa na sehemu moja ulimwenguni ambayo kila mtu angekuwa haungi mkono kabisa wazo hili ingekuwa ni Paris...

Kwa mtazamo wa kiufundi, Michezo hii ya kwanza ya Olimpiki haikuwa na chochote cha kuwavutia. Utendaji wao kwa kawaida haukuwa na kumbukumbu wala hawakuongeza matarajio yoyote. Yote hayo yalihitimisha uvumbuzi mkubwa kwa wakati huo ulikuwa ushirikiano kati ya michezo tofautitofauti, lakini hii ilikuwa hatua kubwa, ya kusonga mbele ikiwa imeweka misingi kwa ajili ya siku zijazo. Ninaposema kwamba hakukua na jambo lolote zuri lililotokea, upekee ulipaswa ufanyike kwenye Marathoni. Wazo la wajumbe mashuhuri wa Taasisi ya Ufaransa Bw. Maurice Bréal - ambaye, kwa shauku yake, aliniandikia ujumbe mara baada ya kufufua Michezo ya Olimpiki kusema kwamba atatoa Kombe kwa mbio hizi, Marathoni haikuvutia tena. Zilikuwa na umbali mkubwa kati ya kilometa 42 na 44 na wataalamu hawakuona kama kuna sababu ya msingi. Hatukutaka kuanzisha mbio hizo hata kama tulikuwa na uwezo mkubwa wa kuanzisha hata kabla hazijazinduliwa rasmi, lakini haikuwa rahisi kwa tamko la mara moja kuzuia kufanya hivyo. Wagiriki walikuwa na wanariadha wachache. Miongoni mwetu hakuna aliyetarajia kwamba mshindi atakuwa miongoni mwao na hususani mshindani "kinara". Spiridion Louys alikuwa mkulima mzuri aliyevalia sketi inayopendwa na ilikuwa ya kipekee na alionekana maridadi kwenye muktadha wa sasa wa mafunzo yote ya mbio. Alijitayarisha kwa ajili ya tukio hilo kwa kufunga na kuomba, na alikuwa na kauli mbiu iliyosema kesha ukiomba kwa kuwasha mishumaa kabla ya kuanza mashindano. Ushindi wake ulikuwa mkubwa kwa uzuri na rahisi. Kwenye lango la kuingilia uwanjani walifurika watazamaji zaidi ya 60,000, aliwasili bila kuonesha dalili zozote za uchovu, na wakati mwanamfalme Constantine na George, walimwonesha ishara ya kumkumbatia na kumpeleka mbele ya mfalme aliyekuwa amekaa kwenye kiti cha enzi cha ufalme, ilikuwa kana kwamba mizimu ya kale ya kigiriki iliingia naye uwanjani. Ushangiliaji wa nguvu ulimpa hamasa ya kuweza kushinda, halikuwa jambo la kawaida kulishuhudia. Sitasahau kamwe tukio hilo ambalo liliniacha nikiwa nimeamini nguvu za maono kuwa na mchango mkubwa kwenye michezo kuliko nilivyokuwa najua; uzoefu mwingine nilioupata baada ya mwaka 1896 umethibitisha imani hii lakini pamoja na msaada wa kitabibu ukweli ungebaki kama ulivyo na matokeo ya kiutendaji yasingekuwa ya kubashiri.

Hii haimaanishi kwamba upande wa kisayansi wa mafunzo unapaswa kupuuzwa, na huko Athene pia uthibitisho huu ulitolewa kwa tukio la pili. Chuo Kikuu cha Princeton cha Marekani, ambapo rafiki yangu W. Sloane alifundisha, aliwatuma wanamichezo watano bora. Mmoja wao, Robert Garrett, ambaye hakuwahi kurusha kisahani maishani mwake, shauku yake iliongezeka katika mchezo huu na alifanikiwa vizuri tangu alipoanza na aliniambia angetamani kuingia kwenye matukio ya michezo ya Olimpiki. Hata hivyo, aliogopa kwamba inaweza kuonekana kuwa "majivuno na mzaha" kwake. Nilimtia moyo, na alifanya vizuri na hata kupewa tuzo! Alistahili kupata tuzo kwa sababu ya mazoezi ya viungo aliyoyafanya. Miaka michache kabla, nilimwona kijana wa kikanada, ambaye hakuwa mwendesha farasi, akiwa katika mtindo sawa na mmoja wa washindi katika shindano la kuendesha farasi. Kwa hivyo, pamoja na umuhimu wa fikra,

tuna ushahidi mzuri wa mbinu za mafunzo ya jumla: taarifa zenye manufaa yenye lengo la kuonesha njia za mafanikio ya baadaye.

Hata hivyo, katika majimbo na visiwa vyote vya Ugiriki, vijana walipotoka shuleni, walikuwa wanajifurahisha "kucheza kwenye Michezo ya Olimpiki". Baada ya kukimbia,



*10. Panagotis paraskevpoulos, mshindi wa medali ya fedha katika nchezo wa kurusha kisahani huko athene mwaka 1896*

kuruka na kurusha mawe machache kwa ajili ya kujifurahisha tu, waliunda misururu ya maandamano na mkubwa zaidi ya huo, ulikuwa makini uliwapa wengine tawi la mzeituni. Ishara hii ilifanyika tena huko Athene baada ya karne nyingi kupita, iliwapa mguso wa fahamu ya maisha yao ya zamani ambayo waliyahisi. Mchezo huu wa ishara uliojaa mashairi katika maeneo ya pembezoni mwa Corfu ulikuwa maono yangu ya mwisho ya Michezo ya kwanza ya Olimpiki. Sasa inanipasa kufanya kazi kuhakikisha ninafanikiwa.

# IV

## Mkutano wa Michezo ya Olimpiki huko Le Havre (1897)



11. *Mchungaji Count Laffane*



12. *Padre Didon*

Kwa nini Le Havre? Watu hawakukubaliana. Ni kwa vipi bandari hii ya Normandy inahusika na Michezo ya Olimpiki?

Aliporejea kutoka Athens, Dkt. Gebhardt alielezea matamanio yake kwamba mkutano ujao wa IOC ufanyike Berlin. Messrs, Vikelas, Kemény na Guth walikubali, alisema. Lakini, nilijihadhari nisiwasikilize, na kabla ya majira ya kiangazi nilifika kwenye mamlaka ya Manispaa ya Le Havre. Lingekuwa jambo la kijinga kwa wakati huu kuitisha mkutano wa IOC, peke yake, mchana katika Mji mkubwa. Ninakumbuka vizuri jibu la binti mdogo, ambaye leo ni mke wa mwandishi mashuhuri, alipoulizwa ikiwa "amecheza sana msimu huu." Alijibu kwa bashasha: "Wazazi wangu hawaoni kwamba niko tayari. Wanakataa kuniruhusu nitoke nje hadi mwaka ujao."

Niliizingatia IOC kama iko hivyohivyo. Niliwaza haikuwa tayari kutoka nje. Udogo wake, ukosefu wake wa rasilimali na hususani ukosefu wa misingi imara, na kufanya itegemee ama utawala wa kudumu au bado kunaifanya kushindwa kutegemea uongozi wa kudumu au kuanzishwa kwa utaratibu na nguvu za kiufundi zilinifanya nikatae wazo kama hilo lisilo la busara. Kwa upande mwingine, niliona ni muhimu zaidi kujilinda kwa kuchukua tahadhari za kuepuka lawama juu yangu kutoka mamlaka yoyote. Ilikuwa muhimu kutodharau ushindi uliopatikana huko Athene na kwa upande mwingine kukuza umuhimu wake.

Nikiwa Normandi nilitumia muda wangu vizuri; kwenye Uhusiano, nyumbani, kwenye masuala ya kisiasa niliyokuwa nayo, na mambo mengine, kwa kweli, yalinifanya nipende kuwapo mahali ilipozaliwa familia yangu. Kwa hiyo, Ilikuwa rahisi kwangu kupata msaada huko kuliko mahali pengine popote. Rais wa Ufaransa, aliyechaguliwa mwaka uliopita baada ya kujiuzulu kwa Casimir-Périer bila kutarajiwa, alikuwa mzaliwa wa Le Havre na wakati wa majira ya Kiangazi alipenda kupumzika kwenye mji wake. Nilikuwa na uhakika ningemvutia katika wazo hilo.

Huko Athens, juhudi zote zilielekezwa upande wa michezo katika muktadha wa kihistoria; Hapakuwa na mkutano, hakuna kongamano, hakuna dalili ya kusudi lolote la maadili au elimu. Kuchukua mwelekeo huo haraka baada ya Michezo ilikuwa kuwakumbusha watu fikira kuhusu tabia za kifikira na kifalsafa ya mawazo yangu na kuyapanga majukumu ya IOC, tangu awali, zaidi ya hayo ya vyama vidogo vya michezo. Hata hivyo, bila kusikiliza mapingamizi yoyote yaliyotolewa, niliendelea na mradi wangu wa Le Havre na nilihakikisha kwamba, kwanza natumia ukumbi wa mjini na baadaye nitaangalia ushirikiano wa marafiki wawili wa karibu: ambao ni Padri Didon,mwanzilishi wa Chuo cha Arcueil na Gabriel Bonvalot, maarufu kwa safari yake kupitia Asia ya Kati. Walikuwa wazungumzaji wawili maarufu wa siku hiyo. Programu inayoweza kunyumbulika ilitayarishwa, ikituacha huru kushughulikia mambo kama tulivyotaka, ikiwa tunayakubali au tunayakataa. Hizi ndizo programu:

**Elimu**
Saikolojia ya mazoezi ya viungo vya mwili: sifa za kila aina. Tofauti kati ya michezo ya ridhaa na mazoezi ya lazima; faida na hasara ya kila moja. Athari za kimaadili za mazoezi ya viungo vya mwili kwa watoto, vijana; Ushawishi kuhusu juhudi za malezi ya tabia na ukuaji.

Maandalizi ya mafunzo ya viungo vya mwili katika shule za sekondari na vyuo;

Je, wanafunzi wanaweza kufanya maandalizi na kuyaendesha wenyewe, na kwa namna gani?

Matokeo ya kuwaacha wanafunzi huru kufanya wanavyotaka. Jukumu la mamlaka.

**Usafi**
Fiziolojia ya mafunzo ya viungo vya mwili; kanuni za kipekee kwa kila aina ya mazoezi.

Kufundisha usafi katika shule za sekondari na vyuo; Programu ya ufundishaji huo.

**Mavazi.**

Haidrotherapia inachukuliwa kama kikamilishi cha mazoezi ya viungo vya mwili.

Kwa namna gani inapaswa kutumika.

**Michezo**
Suala la tuzo za pesa taslimu na ufafanuzi wa mwanamichezo wa ridhaa. Maandalizi ya mashindano ya kimataifa; idadi na masharti ya jumla.

Kuanzishwa kwa chama cha Michezo ya Olimpiki na Habari duniani.

Ufufuaji na maendeleo ya mafunzo ya viungo vya mwili katika karne ya 19; historia ya harakati hii kwenye nchi tofautitofauti duniani.

Baadhi ya programu za michezo hazikuguswa kabisa; zilikuwapo kwa utaratibu tu. Uanzishaji wa Chama cha Michezo ya Olimpiki na Habari Duniani kwa lugha mbalimbali ulijumuishwa kwa lengo la kuwaridhisha wenzetu wa Hungaria, F. Kemény, ambaye alikuwa na matamanio makubwa. Ushiriki wa Mkuu wa Chuo cha Akademia ya Caen, mkuu wa idara ya Seine-Inférieure, msaidizi wake wa huko Le Havre na idadi kubwa ya viongozi mashuhuri kutoka nchi za kigeni iliboresha majadiliano na kuyafanya yawe na tija. Kwa siku mbili katika hoteli yake iliyopo kando ya bahari Mkuu wa Nchi alipokea wajumbe wa mkutano, Mkuu wa Nchi alipokea wanachama wa mkutano, kwa heshima waliokuwa nayo iliwezesha idadi kubwa ya sherehe zilizopangwa kufanikiwa.


Ilikuwa wakati wa vikao vya hadhara, ambapo Padre Didon, alikuwa kwenye chumba cha mkutano mkuu katika Ukumbi wa Mji, alichochea shauku ya watazamaji wengi kwa moja ya hotuba ya kusisimua aliyoiwasilisha, ndipo, nilipokabidhiwa kadi ya aliyechelewa kufika, Mchungaji Courcy Laffan, Mwalimu Mkuu wa Chuo cha Cheltenham

na mwakilishi wa Kongamano la Walimu Wakuu wa Uingereza. Baada ya kumsalimia, nilimkaribisha kuja kuketi kwenye safu ya mbele inayotizamana nami. Bado alikuwa ameanza maisha, mwonekano mwembamba na mtanashati. Alitoa mawazo ya uwiano mzuri kati ya fikira, nguvu na hisia. Alikuwa amerejea kutoka Southampton. Wakati Padri Didon alipomaliza kutoa hotuba yake, watazamaji waliipenda, mjadala ulifunguliwa, lakini hakuna mtu aliyeonekana na shauku ya kuzungumza baada ya yeye kumaliza kuhutubia. Kwa hiyo, nilidhani kwamba, hotuba fupi ya Kiingereza ingewapumzisha na kuomba radhi kwa kutokuwa na busara, nilimwomba Mwalimu Mkuu wa Shule ya Cheltenham aongee maneno machache. Alisita, kwa majivuno na kwa kujiamini, Bw. Laffan alisimama na aliweza kujieleza kwa Kifaransa kizuri kabisa jambo ambalo halikutarajiwa kabisa, aliwasilisha mawazo yake kuhusu misingi ya maadili ya mchezo. Mawazo yake yaliendana na ya Padri Didon, lakini aliyaweka mawazo yake kwa namna tofauti, yakidhihirisha utulivu lakini wakati huohuo, yakionesha uungwana ambayo yalipinga uhalisia wa shauku kutoka kwa watazamaji na kufanya kikao hiki kuwa sherehe halisi ya Kifaransa. Kwa upande wangu, nilishawishika kwamba washirika wapya wenye umuhimu sana waliletwa ili kutusaidia. Laffan, ambaye misingi yake ilikuwa ni lugha aliyoirithi kutoka kwa mababu wa Irish waliompa mwelekeo wa kuishi kulingana na imani zao, hatimaye aliniambia kwamba, kwa siku hii ya kwanza, alisikia "akiitwa" kusimamia michezo ya Olimpiki kwa nguvu zake zote. Kimsingi, alipaswa kubaki mwaminifu hadi mwisho, na urafiki kati yetu ulibaki wa karibu na thabiti.

Mkutano wa Le Havre ulilazimika bila msaada wowote kutoka Ugiriki. Wagiriki walikuwa wanapambania uhuru wa Crete na kurejesha upya mipaka yao halali, lakini hatma yake ilileta uadui. Urafiki na uadui wa kupambania mahitaji ya nchi zao na hawakuwa na muda wa kugeuza macho kwenda Normandy. Hata hivyo, utamaduni wa kigiriki ambao ulipenya kwenye anga ya mkutano wa kwanza wa mwaka 1894 ulioanza kufifia kabla ya ushawishi wa Uingereza, ambao ulikuwa karibu. Ilikuwa kwa Arnold kwamba tulirejea, tukiwa na ufahamu zaidi au kidogo, kwa lengo la kuhamasisha.

Hata baada ya miaka kumi kupita nilikuwa najaribu kupandikiza mafundisho yake huko Ufaransa; kimsingi yalijikita kwenye kugundua ukweli huo na nguvu hizo ambazo nilishangazwa kugundua dunia ya kisasa isiyokuwa na uelewa. Hata sasa hakukuwa na mafanikio makubwa, licha ya kupata msaada kwa watu watatu ambao ni Padre Didon, Laffan na Bonvalot. Hata ndani ya Kamati yenyewe, hakuna aliyeridhika. Balck alidhani kuwa tunapoteza muda na jambo lililojadiliwa "halikuwa na uhusiano wowote na kazi zetu". Kwa wakati huo, alifikiria kujiuzulu. Jambo hili liliyumbisha uaminifu wake kwa muda, wengine walihisi kama yeye, kwamba kwa jitihada wangeona kila kitu. Tulihatarisha kutawanya majeshi yetu. Nilifikiria kinyume na kwamba mawazo yangu yalikuwa yakibadilika kama kinyonga, IOC ingeweza kuwa na ufanisi zaidi na kuepuka, mashambulizi madogomadogo. Hapakuwa na namna ya kukwepa kwa sababu vita

ilikuwa imekaribia, nilihisi ingekuwa hatari zaidi kuliko iliyopita, bila kutarajia zaidi werevu na kuwa na hakika ya matokeo yake.



# V

## Mashindano ya Pili ya Michezo ya Olimpiki (Paris, Mwaka 1900)



**13.** *Urushaji wa kisahani huko Paris mwaka 1900, mshindi wa medali ya shaba Frantisek Janda-Suk (meta 35. 25)*

Mapema miaka kumi na mmoja iliyopita nilipata uelewa wa haraka kama huo na wenye mantiki nzuri kiutendaji na nilipata hamasa kutoka kwa wakurugenzi watatu wa Maonesho ya Dunia ya mwaka 1889, hususani Bw. George Berger na Bw. Alphand na kwamba nilitegemea kupata msaada uleule kwa mwaka 1900. Kwa kukubali wazo jipya la kuhamasisha michezo katika shule za Ufaransa, ni kwa vipi mtu katika mwaka 1900 angekataa hasa linapokuja suala la kufufua Michezo ya Olimpiki baada ya kufanikiwa huko Athene na manufaa yaliyopatikana katika vyombo vya habari? Lakini udikteta wa mmoja wao umebadilisha uongozi wa

watawala watatu na kama ilivyo kwa wanaume maarufu, Kamishna Mkuu Bw. Alfred Picard mwaka 1900, hakuwa tayari "kutekeleza" wazo la mtu mwingine. Mazungumzo yetu ya pekee yalifanyika miaka mingi iliyopita hadi kufikia tarehe 30 Mwezi Januari,1894, hasa siku kadhaa kabla ya kufufua Michezo ya Olimpiki. Kuanzia awali alikuwa hapendi wazo la kujumuisha Olimpiki ya Pili katika Maonesho ya Dunia ya Paris, wala hakupenda wazo lolote linaloendana na hilo la kutenganisha michezo ya sasa na ya zamani ambalo niliwasilisha kwake siku hiyohiyo kwa mtindo wa mradi niliousaini pamoja na Bw. G. Strehly, mwalimu wa sekondari ya Montaigne na mtaalamu wa michezo ya kale ya Kigiriki na sarakasi. Mradi ulijumuisha ujenzi wa uzio eneo la Maonesho au eneo linalozunguka eneo la Olimpia ya Altisi. Ndani ya majengo ya makumbusho kulipaswa kuwekwa vitu na nyaraka zote zinazohusiana na michezo kuanzia zama za kale, zama za Kati na zama za Sasa. Huku akituhakikishia namna alivyovutiwa na rafiki yake, Bw. Picard alikuwa ameshaamua mpango wake na alikuwa anasubiria fursa ya kuutekeleza. Hatukuwahi kupokea uamuzi ulioahidiwa, miaka mitatu baadaye, Katalogi rasmi ya Maonesho ilitolewa, wanamichezo walikasirika kuona kwamba mchezo wa kuteleza kwenye barafu umewekwa katika kipengele cha vifaa vya kulia chakula, mchezo wa kupiga makasia umewekwa kwenye kipengele cha kuokoa maisha, vyama vya michezo katika ustawi wa jamii na mingineyo. Nilishatambua muda mrefu kabla ya hapo kwamba, kuhusiana na michezo ya Olimpiki hakukuwa na chochote kilichotarajiwa kutoka kwa Bw. Alfred Picard ambaye alikuwa ameombwa na Bw. Ribot aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu lakini hakukuwa na mafanikio yoyote.

Kwa mantiki hiyo, mwaka 1900 niliamua kuandaa michezo ambayo haiingiliwi na kikwazo chochote kutoka nje kwa kutumia kamati binafsi ambayo Viomite de la Rochefoucauld alikubali kuwa Rais. Pia alikubali kuruhusu ofisi zake kuanzishwa katika jumba kubwa la *La Rouchefoucauld* lililopo *Rue de Varennes* huko Paris. Mpango ulionekana kuwa na nguvu kubwa kwa mara ya kwanza; kwa kweli, ilikuwa ni kidogo sana. Hoja yangu ilikuwa kama ifuatavyo: Waandaji wa Maonesho walikuwa wanapanga kulingana na upendeleo wa watumishi wa umma uliopendekezwa, kushikilia idadi ya "mazoezi ya mwili na mashindano ya michezo". Wazo lote lilishindikana tangu mwanzoni na kwa namna yoyote kulingana na eneo lililochaguliwa (Vincennes), kamati kuu na kamati ndogo, ukubwa uliopitiliza wa programu (walikuwa wanapanga kujumuisha mpira wa

mezani, uvuvi na chesi), isingekuwa chochote zaidi ya haki ya watu wa kawaida iliyotukuzwa; jambo ambalo ni tofauti na tulivyotaka Michezo ya Olimpiki iwe. Kwa hakika, kwa wanamichezo tulitaka kuwawezesha kupata vitu ambavyo wasingeweza kuvipata popote.  Katika Mji wa Athene wangeshiriki michezo ya kale ambayo bado haijaathiriwa na usasa. Mashindano ya Paris yalipaswa kuwaonesha washiriki Ufaransa ya kale Pamoja na mila na desturi zake. Washiriki wangekuwa na mashindano na matamasha ya Maonesho wakati ambapo tungeandaa Michezo  kwa ajili ya wasomi- wasomi miongoni mwa wanamichezo ambao wangekuwa wachache kwa idadi lakini wakijumuisha wachezaji mashuhuri duniani;  wasomi miongoni mwa watazamaji, wake kwa waume katika jamii, wanadiplomasia, maprofesa, majenerali na wafanyakazi wa taasisi. Kwa mambo haya, ni jambo gani lingekuwa jema zaidi ya sherehe ya bustani ya *Dampierre*, mapokezi katika mtaa wa Varennes, safari za kitalii kwenda *Esclimot au Bonnelles?*


Hata hivyo, mawazo yetu hayakuishia hapo. Tulitaka Kamishna Mkuu awe msimamizi mkuu wa suala hili. Nilifanikiwa kumshawishi Robert Fournier-Sarloveze kuikubali kazi, kuzingatia uwezo na werevu wake wa kukubali mabadiliko na uelewa wake wa kiwango cha juu. Kuteuliwa kwake kukaibua Kilabu ya Michezo ya Compiegne yenye viwanja vizuri vya michezo, wachezaji mahiri na watazamaji. Michezo ya riadha, mbio za miguu, na mashindano yakabakia katika Vilabu vya Riadha kutokana na jitihada zilizofanywa katika kuendeleza michezo shuleni. Kwa sababu hiyohiyo, mpira wa miguu ulikuwa chimbuko la kilabu cha mpira wa mkono. Kwa namna hii waasisi wawili wa Kilabu cha USFSA wataheshimika baada ya maumivu yao yote. Chama cha Societe d’encouragement a’ l’Escrime kiliahidi kutoa msaada na vyama vingine vikatoa ya kwao …

Ili kuelewa kikamilifu dhamira ya mpango huo, msomaji anapaswa kufanya jitihada ya kutafakari na kuiona hali ya masuala haya kwa miaka thelathini iliyopita. Wakati huo hakukuwa na jambo gumu kama kujaribu kuwashawishi mashabiki wengi kuhudhuria katika mkutano wa michezo. Mikutano hiyo haikuwa na hamasa. Ni mchezo wa mbio za baiskeli uliokuwa na mashabiki wengi. Miaka michache iliyopita, wakati Kilabu ya riadha ilipotembelewa na Timu bora ya Kilabu ya Michezo ya Manhattan ya New York, viingilio vilitosha kulipia kiasi

kinachokaribia mbili ya tatu ya gharama zote. Mwaka uliofuata, mechi ya kwanza ya Anglo-French ya mpira wa miguu ilichezwa Ufaransa na kumalizika kukiwa na upungufu mkubwa wa fedha, pamoja na kwamba ilisimamiwa na Balozi mpya wa Ufaransa Bw. Dufferin. Na kipindi kifupi baadaye, mechi nane za kwanza za kupiga makasia zilifanyika Andresy dhidi ya klabu ya kupiga makasia ya London na ilimalizika kwa ushindi kwa Ufaransa. Hata hivyo kwa mshangao mkubwa, umma haukuupa mchezo huo umuhimu unaostahili. Ungewezaje kutarajia vinginevyo? Michezo, kulingana na profesa wa chuo kikuu, ilikuwa ni burudani tu na haikupaswa kutarajiwa kuwa kitu kingine chochote, maoni ya umma yalikuwa katika mtindo uleule.

Mkutano wa kwanza wa Kamati ya Maandalizi ya Michezo ya Olimpiki wa mwaka 1900 ulifanyika katika jengo la Rochefoucauld. Ulikuwa na mafanikio makubwa. Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe arobaini, kumi na wanane kati yao waliteuliwa kama wasimamizi na wakapewa wadhifa wa kusimamia michezo mbalimbali. Wajumbe hao walikuwa ni pamoja na Marius Dubonnet na Ed. Caillat kwa ajili ya mchezo wa kupiga makasia, Bruneau de Laborie kwa ajili ya masumbwi, Hebrard de Villeneuve na Count Potocki kwa ajili ya mchezo wa kupigana kwa mapanga, Jacques de Poutales kwa ajili ya mchezo wa gofu, Jean de Bellet kwa ajili ya mchezo wa tenesi na mingineyo. Programu hii ilifanana na ile ya huko Athene, ikirejeshwa kwenye uasilia wake na kuongezwa kwa mchezo wa masumbwi na mchezo wa polomaji na kuongezwa kwa vitu vidogovidogo kwenye michezo mingine. Mchezo wa kulenga shabaha uliachwa, wakati mchezo wa upigaji mishale ukiongezwa. Tuzo ya kupanda Mlima ilitolewa kwa upandaji wa kustaajabisha zaidi uliofanywa popote duniani tangu michezo ya mwaka 1896.

Vyombo vya habari hasa vya mrengo wa kulia na mrengo wa kushoto viliunga mkono hoja. Wanamichezo binafsi walionekana kuridhika. Mnamo tarehe 16 Juni, 1898 Henri Desgrange alitukabidhi Uwanja w*a Parc des Princes Velodrome* chini ya usimamizi wetu;



***14-*** *Mchezo wa kupigana kwa mapanga: Roman Fonat (Mkyuba) dhidi ya Albert Ayat (Mfaransa)*



***15*** *(Mwanamke mshindani katika mashindano ya gofu)*

Kisha Giffard akachukua jukumu la kuandaa shindano la kuogelea na Pierre Laffite alitupatia *Vie* au *Grand Air* tuitumie kama chapisho rasmi. Bw. Molier

alizungumzia kuhusu tamasha kubwa katika uwanja wake maarufu na Count Potocki wa Jimukana itakayotolewa na Kilabu ya Wapanda Farasi wa Etrier. Nje ya nchi watu walikuwa wakisubiri kwa muda mrefu kusikia mipango rasmi. Imani ilirejeshwa haraka sana. Kila mtu alianza kufanya kazi kwa hiari. Barua kutoka kwa Bw. De Bousies na Jenerali de Boutowski zilitangaza kuundwa kwa kamati nchini Ubelgiji na Urusi; na kutoka Australia. L. A. Cuff aliahidi kutumia maneno yake mwenyewe "timu yenye nguvu".

Tulikuwa karibu kuanza kupanga malazi ya Wanamichezo hasahasa kwa kuwawekea vifaa vya kutosha, kambi zilikuwa nzuri (Wanamichezo hawakuwa watu wa pekee sana siku hizo), wakati kila kitu kilionekana kwenda kombo. Ningeonekana kukosa uzoefu kama nisingetarajia hali ile. Kwa ujinga nilifikiri kwamba mashirikisho ambayo kanuni zake tungekuwa tunazitumia na ambayo tungeyaachia kazi ya upangaji wa majopo na uendeshaji wa mashindano, yangeona majukumu haya yanawaridhisha vya kutosha kwenye mradi huo. Na mapambo je? Mungu wangu, niliyasahau mapambo! Nchini Ufaransa, nilionekana mjinga kiasi gani! Kama tusingeunda "Utaratibu wetu wenyewe wa Kimataifa" tusingekuwa na utepe hata mmoja wa kijani, njano au zambarau wa kumvika mtu yeyote. Zaidi ya hayo, isingewezekana kutarajia "Washindi" wowote wa Olimpiki kupata tuzo zinazotolewa na Mashindano ya Maonesho.

Wasiwasi ulipoongezeka, Ed. Caillat alikuwa tayari amenionya kwamba "Shirikisho la Ufaransa la Kupiga makasia lilikuwa likifanya fujo sana". Katika ukumbi wa Jiji, walikuwa wakipinga mkutano wa Counts na Marquesses uliofanyika katika ukumbi wa *Rue de Verennes*. Tarehe 9 Novemba, 1898 USFSA ilipitisha hoja ya kujitenga na sisi, licha ya juhudi za mwezetu wa IOC, Ernest Callot, ambaye alikuwa ametuonya siku moja kabla ya machafuko kuongezeka. USFSA ilikuwa ikipitia mgogoro wa ndani uliosababishwa na matamanio fulani ambayo hayanihusu. Hata hivyo, madhara ya hatua hii yalikuwa madogo sana. Shirika rasmi la mashindano ya Maonesho haya halikuwa endelevu na hakuna mtu yeyote ambaye alikuwa na imani yoyote na Kamisaa Mkuu wa suala hili. Changamoto zetu ziliongezeka, lakini zilikuwa zinatatulika. Nje ya nchi, kamati hiyo ilijulikana kama "Kamati ya La Rochefoucald". Tatizo liliibuka likiwa ni matokeo ya kitendo kisichotarajiwa kabisa nchini Marekani. Kanali H... alikuwa

amewasili Paris, akiwa na mpango wa kuandaa maonesho ya michezo chini ya Kamisheni ya Marekani; hapo kungekuwa na viwanja vya michezo, mashindano... ili "kufundisha nchi zingine jinsi mchezo halisi ulivyokuwa". Hakuna kitu ambacho kingekuwa kimepotoshwa zaidi kuliko kitendo kama hicho. Kwa isivyo bahati, Tume ya Marekani ilionekana kuhimiza wazo hilo na Bw. Picard (bila kutarajia) alionekana kuunga mkono. Nilijihadhari nisioneshe uadui wowote. Hata hivyo, niliendeleza uhusiano wa karibu sana na Kanali kwa kipindi cha karibia mwaka mmoja. Nilikuwa na uhakika kuwa mradi wake hautekelezeki. Hapakuwa na haja ya kuupinga mradi huo, lakini uliongeza mkanganyiko. Kwa upande wa maonesho, ilionekana hakuna maendeleo. Niliambiwa kwa siri kuwa, mamlaka zingine zote zilikuwa ni za kutiliwa shaka mbele ya macho ya Kamishna Mkuu pekee ambaye alikuwa na sifa zinazohitajika. Waandishi wa Kamisaa walikuwa na sifa za kuandaa michezo kama inavyotakiwa. Hatimaye, tarehe 19 Februari, 1899, Daniel Merillon aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa mashindano haya. Hakuwa hasa mtu aliyehitajika, lakini aliwasaidia kwa kiasi fulani. Migororo iliyorejelewa hapo juu, haikuvunja uhusiano wetu. Ilionekana kwangu kuwa tungefikia makubaliano naye na, bila kuunganisha vikundi viwili, kuunda aina fulani ya ushirika ili kufanikisha sherehe nzuri ya Michezo ya Pili ya Olimpiki. Bw. Ribot alimwendea Bw. Alfred Picard tena lakini kwa mara nyingine akaja na upinzani wake mkali dhidi ya Michezo ya Olimpiki, ambayo aliipuza na kusema kuwa haziendani na uhalisia.

Wakati huohuo, Charles de La Rochefoucauld akawa mhusika wa kampeni za chinichini, ambazo sikujaribu kujihusisha nazo kwa sababu niliogopa ningegundua kitu kuhusu rafiki yangu ambacho kingevunja uhusiano wetu. Uadui mwingine wa kijamii unasameheka, ingawa hauna matokeo mazuri. Hata hivyo, tarehe 22 Aprili, kikao kiliisha kwa purukushani na kumalizika kwa kujiuzulu. Tulifanikiwa kupata rais mwingine; kwa urahisi. Kama ilivyokuwa kwa Katibu Mkuu wetu, Fournier Sarloveze, hakuwa mtu wa kutengwa kwa urahisi. Lakini nilipima hatari ambazo zilikuwa zinakaribia kujitokeza muda mfupi uliobaki, hasara ya kuonekana kwa mpasuko wa kitaifa katika muktadha wa kimataifa. Tulipaswa kushauriana na IOC, lakini muda ulikuwa hautoshi, kwa hiyo niliiruhusu Kamati ya Maandalizi ipitishe azimio la kuvunjwa kwake. Niliidhinishwa kumtaarifu Bw. Merillon kama nilivyoona inafaa. Nilimfahamisha rais mpya kwa faragha na akanishukuru kwa

furaha. Tulikubaliana na masharti ya barua rasmi ambayo nilimtumia tarehe 15 Mei. Miezi kadhaa ilikuwa imepita tangu uteuzi wake, lakini hii ilionekana kuwa muda wote wa kazi ya Ukamisaa. Alipendekeza idadi fulani ya hatua muhimu na zisizoepukika. Hata hivyo, hakuna jibu lililotolewa, nilikuwa na barua yake ambayo ilionesha masikitiko yake na kusema kuwa alitishia kujiuzulu endapo mapendekezo yake hayatatekelezwa mara moja – baadaye jambo la kufurahisha; kila kitu kilitiwa saini. Hatimaye, tulifanikiwa kuwezesha kila kitu kufanya kazi; hatimaye, kusema kweli tumekwishachelewa.

Tarehe 5 Juni, 1899, Bw. Vikelas, Count Brunetta d'Usseaux ambaye alikuwa amejiunga na IOC mwaka mmoja kabla na mimi, sote tulikutana nyumbani kwa Merillon. Mwenyeji wetu alikuwa na wasiwasi hasa kuhusu nchi nyingine, ambazo kamati zao zilizoundwa kwa ajili ya maonesho hayo hazingekuwa na msaada wowote na tuliona ni mwenzetu pekee ndiye angeweza kuokoa jahazi. Alikuwa ameniomba nimtumie waraka, jambo ambalo nilifanya mara moja. Nilipendekeza hata kutumia fursa ya kusafiri kwenye nchi za Ulaya ya Kati na Kaskazini ili kuharakisha juhudi za wanajumbe wa IOC. Madhumuni ya safari hii yalikuwa kukusanya taarifa kwa nia ya kuandika mfululizo wa ripoti kuhusu Ulaya ya Baadaye ("*The Future Europe")*, ambayo nilikuwa nimeahidi kwa *L'Independance Beji* ambayo kwa kweli hutoka wakati wa Majira ya Vuli. Merillon angependa niongeze safari yangu kujumuisha nchi nyingi iwezekanavyo, kwa nia ya kusaidia kwa kiwango cha juu zaidi ahadi ambayo aliwajibika kwayo, lakini Bw. Picard alikataa kumpa fedha zinazohitajika. Nilimhakikishia Merillon kwamba popote nilipokwenda nitatekeleza malengo yetu kwa bidii, kwa kuzingatia ukweli tulilazimika kufanya "Mashindano ya Maonesho", badala ya Michezo ya Olimpiki; japo halikuwa tarajio letu, lakini ilibidi tukubali kwa wakati.

Kituo changu cha kwanza kilikuwa Berlini. Wakati wa ziara yangu ya muda mrefu, bila kukengeuka utafiti mkuu niliokuwa nafanya wa kuangalia fikra za maofisa wa michezo sikufanikiwa sana. Hata hivyo, Serikali ya Kifalme ilionesha dhamira ya dhati ya maonesho ya Paris na ilikuwa imetoa uthibitisho wa kuonekana. Kwa hakika mwaka uliofuata sehemu ya Ujerumani ilikuwa moja ya vivutio vikuu vya maonesho haya katika *Bustani ya Paris Ufaransa* na kutoa mchango mkubwa katika kuboresha uhusiano kati ya nchi hizo mbili. Mnamo mwaka 1899, tukio

kama hilo lilionekana kuchelewa kufanyika. Mkutano ulifanyika kwenye kasri la Kifalme ambao uliitishwa na Kamishna Mkuu wa Ujerumani, ambaye alinialika kwa ajili ya chakula cha mchana baadaye. Kikao hakikwenda vizuri kiasi kwamba chakula kilionekana kutokuwa na ladha. Si kwamba kulikuwa na nia mbaya ya makusudi, lakini hofu ilikuwa imeoneshwa kuhusu usalama wa kimaadili wa wanariadha wa Ujerumani ambao wangekuja Paris na "huenda wakawa hatarini kutukanwa". Haya maneno yaliyokuwa kwenye barua yalitumiwa na Mjerumani huko Paris ambayo isivyo bahati mjumbe mmoja wa mkutano aliyasoma kwa sauti. Mwanamfalme Aribert d'Anahalt alikuwa mwenyekiti alifanya kosa zaidi la kushindwa kuingilia kati. Bila ya kutarajia niliamua kupinga. Hata hivyo, hakuna mtu yeyote aliyependekeza kutolewa kwa Wajerumani, lakini ilikuwa dhahiri kwamba ushiriki wao utakosa hamasa. Wakati mtu anapokumbuka mambo yaliyopita na kulinganisha na wakati wa mvutano kati ya Ujerumani na Ufaransa kwa miaka ya hivi karibuni, hata hivyo haikufikia hatua ya matukio ya vita na umwagaji damu - mtu anaweza kuona mabadiliko makubwa yaliyosababishwa na ari ya Kimichezo.


Mnamo mwaka 1900, ari hii ilikuwa imebaki kwa baadhi ya wanamichezo wa kweli na umma kwa ujumla na watumishi wa umma hawakujua kabisa nini kinachoendelea. Kadhalika, wasimamizi wa bustani ya *Shamp de Mars* walikosa ari ya kimichezo na ufanisi. Nyaraka zisizoeleweka zilitumiwa mara kwa mara, bila taarifa yoyote muhimu. Kwa udadisi wa kina wa kamati ya *La Rochefiucauld*, ambayo iliendelea kuzingatiwa kwa kujiamini katika nchi zingine; na bila kupata jibu chanya lolote ilikuwa kwa Rais wa IOC kwamba watu wamemgeuka. Malalamiko yaliendelea kutolewa. Tarehe 11 Oktoba, miezi sita kabla ya tarehe ya ufunguzi, Casper Whitney alionesha kutoridhika kwa Wamarekani. Tarehe 23, Jiri Guth alitangaza kwamba kila mtu katika Mji wa Praha alikuwa amevunjika moyo kabisa, kwa sababu hawakujua kinachoendelea au nini cha kufanya. Muda mfupi baadaye, ziliwasilishwa lawama zilezile kutoka mji wa Copenhagen. Pande zote yalisikika maneno ya kutoaminiana kuhusu michezo "iliyoandaliwa na kundi la watu wasio na ujuzi huko Paris", kama Sloane alivyosema. Kila wakati niliombwa kuingilia kati. Whitney bila kutafakari aliuomba ubalozi wake huko Paris kushawishi kuacha Mpango Rasmi wa Mashindano ya Maonesho na kurejesha "fedha na uhuru wa kutenda" kwa wale waliochaguliwa na IOC. Na tarehe 14

Aprili, 1900, Count Thun Valessian, Franz Joseph’s Chamberlain, walidai kwamba kuwe na mjumbe wa Austria wa IOC “kwa ajili ya michezo ya Paris”, Wakanada nao walitoa maombi yaleyale.

Wakati huo siku zilipita. Hakuna jambo lolote la maana lililofanyika... hata upatikanaji wa ofisi yoyote isipokuwa zile za kamati ndogondogo na bila shaka utungaji endelevu wa kanuni. Vincennes aliachwa; hakuna pesa; hakuna uwanja, hakuna viwanja. Wakati tu wajumbe wa IOC walipokuwa wakiombwa kuunda majopo, vilabu viliombwa kutoa usaidizi na kutuazima viwanja hususani Kilabu ya Mbio kwa siku ya Michezo ya Riadha. Na kufikiria kuwa mnamo 1898, mpango wangu ulikataliwa kwa kuwa ulionekana kuwa “mbaya na usiofaa kwa taifa”.

Mashindano ya mbio za miguu, kuruka na kurusha... yalifanyika pia katika Bois de Boulogne tarehe 19 Julai, 1900, chini ya uongozi wangu na uongozi wa heshima wa Waziri wa Biashara, Bw. Alexandre Millerand, ambaye alikuwa pamoja na sisi mchana na alionesha kupendezwa sana na ushujaa wa wanamichezo; hata hivyo, nilijizuia kumfahamisha hali halisi, kwani alionekana kutofahamu kabisa suala zima. Wanasiasa wengi wa wakati huo walishirikishana maoni ya profesa wa chuo kikuu niliyemnukuu hapo juu; kwao michezo haikuwa muhimu sana, lakini ilithaminiwa kwa kiwango kidogo kama burudani nyingine yoyote ya kiafya. Katika suala hili mchezo wa kurusha tufe haukuonekana kuwa tofauti kwa njia yoyote na mpira wa miguu. Kuhusu Olimpiki, waliona kuwa ni umamboleo usio wa kawaida kabisa. Miaka sita baadaye, kwenye hafla, neno “Olimpiki” bado lilipokewa kwa kejeli na waziri..., ambaye hata hivyo baadaye alibadili mawazo yake.

Kuhusiana na matukio mengine ya mwaka 1900, sikuyasimulia humu. Nia njema ilioneshwa. Wanamichezo walijitahidi sana. Matokeo ya kufurahisha yalipatikana, lakini bila Olimpiki yoyote kutambuliwa na wao. Kwa mujibu wa maneno ya mwenzetu mmoja, “wazo letu lilikuwa limetumika, lakini lilikuwa limetupiliwa mbali”, jambo alilosema lilikuwa ni sahihi. Inaakisi kile kilichotokea mwaka 1900. Ilithibitisha kwa vyovyote vile kwamba tunapaswa kuwa waangalifu kutoruhusu kamwe michezo kuwa tegemezi au kuchukuliwa na





16. *Waogeleaji wakisubiri kuanza mashindano ya kuogelea meta 200*

matamasha makubwa ambayo malengo yake hayaonekani na umuhimu wake wa kitaaluma haupo. Kwa isivyo bahati, muungano tuliokuwa tumehitimisha haukuweza kutenganishwa tofauti na tulivyotarajia. Katika mashindano mengine mawili ya mwaka 1904 na 1908, kwa sababu za kibajeti, hatukuweza kuendeleza mashindano bila ya utegemezi. Haikuwa hivyo hadi mwaka 1912 ambapo utatuzi wa changamoto ya kifedha ulipatikana huko Swideni. Hata hivyo, katika huu "muungano usio na nguvu", Mashindano ya Olimpiki angalau yangefanyika kwa uhuru zaidi na yasingeshushwa hadhi kama ilivyokuwa huko Paris.


66

# VI Michezo ya Tatu ya Olimpiki Nchini Marekani na Mkutano wa IOC Jijini London



17. *1904 - Uwanja wa St. Louis*

Kwa bahati, IOC haikuathirika kwa namna yoyote katika michezo ya mwaka 1900. Makundi makuu matatu yaliyotajwa hapo kabla: *nucleus -nursery- façade*, yaliimarishwa na idadi ya waajiriwa wapya: Godefroy de Blonay (Uswisi), Kanali Holbeck (Denimaki), Clarence de Rosen (Swideni) na Bw. Howard Vincent (Uingereza), walikuwa tayari washiriki madhubuti. Mwanamfalme Georges Bibesco (Romania), Messrs Reyntiens (Ubelgiji), de Beistegui (Mexico), de Ribeaupierre (Urusi) na Hébrard de Villeneuve (Ufaransa) waliunga mkono lakini hawakuwa na cha zaidi. Hatimaye, Mwanamfalme Salm-Hortsmar (Ujerumani) na Mwanamfalme Sergei Beliosselski (Urusi) waliunda kikundi cha "wavurugaji wa mipango".

Wazo la Michezo ya Olimpiki lilikuwa limepata umaarufu kwa sababu kabla mwaka 1900 haujaisha, watu walikuwa wakijadili ni wapi Michezo ya 3 ya Olimpiki itafanyika. Kimsingi, mnamo 1894, tayari ilikuwa imeazimiwa chinichini kuwa, michezo hiyo

ingefanyika huko Marekani, Ugiriki, Ufaransa: mihimili hii mitatu ilichaguliwa ili kuimarisha hadhi ya Michezo ya Olimpiki.

Mara moja mji wa Chicago ulichaguliwa. Rais wa Chuo Kikuu, Dkt. Harper, aliunga mkono hoja hiyo na wananchi wachache waliokuwa wamemzingira walipata uungwaji mkono kutoka kwa Balozi wa Ufaransa Bw. Mérou. Bw. Mérou alimwagiza Bw. Henri Bréal, mtoto wa professa ambaye niliendelea kushirikiana naye kwa karibu. Nakumbuka vizuri mazungumzo yangu ya mwaka 1889 na Bw. Pullman, mtu ambaye alikuwa ni mhisani tajiri ambaye ujuzi wake ulikuwa wa pekee kwa kipindi hicho nchini Marekani na kwa upande Harper ambaye hakuweka msisitizo, alisema ubora wa chuo kikuu chake ulisababishwa na kuendeshwa kama kampuni ya reli. Awali jiji hili lilikuwa na kelele, moshi na machinjio, lakini likaboreshwa na kuwa na mandhari nzuri ya tofauti kabisa. Karibu jiji lote lilikuwa ni zuri. Nilivutiwa na fahari na uzuri halisi wa Maonesho ya Dunia ya mwaka 1893. Nilijihisi nikijawa na mshangao wa ghafula wa kuishiwa na nguvu.

Wazo la kufanya Michezo huko Chicago lilinivutia. Na ulianza kupokea vyombo vya habari maarufu kutoka sehemu zingine nchini Marekani, wakati barua yenye ujumbe mkali iliyoandikwa na James E. Sullivan ilipochapishwa. Ndani yake, alionesha kuwa, bado tatizo halijatatuliwa kwa kuzingatia ukweli kuwa, Kamati ya Olimpiki na Rais wake walikuwa wakipuuzwa na kupendekezwa kwa "Chama cha Kimataifa" kilichoanzishwa hivi karibuni huko Parisi; na aliwataja baadhi ya "waanzilishi", Count Brunetta d'U'sseaux wa Italia. Profesa Bergh- Petre wa Uswidi, Bw. G. de Saint-Clair na Pierre Roy wa Ufaransa na yeye mwenyewe wa Marekani. Brunetta, ambaye shauku yake ilikuwa ikiongezeka kuhusu IOC na Profesa Bergh mara moja walituma barua ya kupinga. Pierre Roy aliamua kufanya vivyohivyo.

Baada ya jibu la kwanza la haraka, Sullivan aliandika barua ya pili ya usuluhishi mnamo tarehe 21 Machi, 1901 ambapo, alisema: *"Muda wote niko tayari kuomba radhi ikiwa nitaonekana nimefanya makosa"*. Kwa namna yoyote, si kila mtu nchini Marekani alimuunga mkono. Mwishoni mwa mwaka 1900, gazeti la *Morning Telegraph* liliandika "hii yote ilikuwa kampeni dhidi ya Chicago", likihitimisha kwa maneno ya kuumiza: "*jambo la kusikitisha linaweza kufahamika tu kuwa, James Sullivan hakuwa mjumbe wa IOC wa Kimarekani"*, mgogoro ulikuwa unaendelea! Sawa! Hakukuwa na jambo zuri zaidi ya kuunda kamati ambayo wajumbe wake wangekuja kuingia kwenye matatizo. Haya yalinikumbusha maneno makali ya Jules Simon wakati watu walipolalamika wakidai mpango wa uanzishwaji wa michezo shuleni nchini Ufaransa: "Kukubalika kwa hoja hiyo, kulitegemea kuungwa mkono na idadi kubwa ya watu waliokuwa wanadai suala hilo".

Mnamo tarehe 21 Mei, 1901, katika mkutano uliofanyika kwenye majengo ya Klabu ya Magari huko Paris, IOC ilikubali kwa kauli moja kuwa Chicago utakuwa mwenyeji wa

Michezo ya Olimpiki ya mwaka 1904; wakati wa kupokea taarifa kuhusiana na matokeo ya kura kupitia chombo cha habari (cable), wanafunzi walishangilia taarifa hiyo kwa furaha kubwa. Baada ya historia fupi ya kufufuliwa kwa Michezo hiyo, nilimwandikia barua Rais wa Marekani nikieleza jinsi ilivyokuwa muhimu kwake kuwa msimamizi wa Michezo hiyo na pia akawatangazia rasmi kipindi ambacho Rais McKinley alipouawa. Mauaji hayo yalimfanya Makamu wa Rais, Theodore Roosevelt kuwa Rais wa Marekani. Alikuwa mpenda michezo, rafiki yetu wa karibu na kurithi kwake madaraka ya urais, matarajio yetu ya Michezo ya Tatu ya Olimpiki yangefikiwa kwa ufanisi mkubwa.

Kila kitu kilianza vizuri. Programu iliyoundwa, kwenye michezo iliongeza michezo ya kifasihi na kisanaa. Machapisho makubwa yalitolewa kwa lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani. Wakati wa Majira ya kiangazi mwaka 1901, Bw. Furher, Rais wa Kamati ya Maandalizi, nilikaa naye kwangu na tukafikia maazimio ya masuala mbalimbali. Hata hivyo, kuelekea mwishoni wa mwaka, niligundua changamoto ndogondogo kwenye barua zake ambazo nilikuwa nazo. Baada ya muda mfupi, niligundua sababu ya changamoto hizo. Sherehe za miaka mia moja ya kukabidhi Louisiana kwa Balozi wa kwanza Bonaparte wa Jamhuri ya Marekani, ingeadhimishwa kwenye maonesho makubwa huko St Louis, Missouri, mnamo 1903, kwa maonesho makubwa. Lakini kabla ya miaka kumi na mmoja, maonesho ambayo yalitakiwa kufanyika huko jijini Chicago, yaliyoandaliwa na kamati ili kuadhimisha karne nne baada ya kugunduliwa kwa bara la Marekani na Christopher Columbus, yaliahirishwa. Kwa hiyo, maonesho ya St. Louis hayakufanikiwa kwa kipindi kilichopangwa. Kwa hiyo, yangefanyika mwaka 1904. Kuahirishwa huko kulitazamiwa kuwa, kungeboresha Michezo ya Chicago, kwa kuwa na idadi kubwa ya watazamaji. Kwa isivyo bahati, kulikuwa na mvutano wa muda mrefu kati ya miji hiyo miwili. St. Louis iling'ang'ania kuandaa Michezo hiyo. Pale ambapo ingelazimu, mji huo ulikuwa tayari kuandaa wenyewe. Kuelekea mwaka 1902, mgogoro huu ambao hapo awali haukuonekana kutiliwa maanani, taratibu ulianza kushika kasi. Mkutano wa hadhara ulifanyika Chicago kwa lengo la kupinga uhamishaji wa michezo kama hiyo, lakini hali ya kutoaminiana iliibuka miongoni mwa waandaaji. Rais wa Chuo Kikuu Harper aliandika kwamba, wangetuachia uamuzi huo na kwamba ikiwa tungeamua kuwaunga mkono "wangefikia mwafaka mzuri". Hali ya wasiwasi ingeweza kubainika kwenye barua yake. Kabla hata sijaipokea, tayari nilikuwa nimeshamwandikia barua Mkuu wa nchi ambaye alikuwa kwenye nafasi nzuri kuliko mtu yeyote kufahamu hali ilivyokuwa. Mnamo tarehe 23, Desemba 1902, baada ya kupokea ujumbe wa kuunga mkono kutoka kwa wenzangu – (14 waliunga mkono, 2 walikataa na 5 hawakupiga kura). Niliandika ujumbe kwa njia isiyo rasmi kumwomba Rais Roosevelt atafute ufumbuzi wa suala hilo. Kama nilivyotarajia, aliamua kukubaliana na uhamisho huo. Kulikuwa na kutumiana kwa telegramu zenye maneno makali, mji wa Chicago ulijiondoa na Bw. David R. Francis, Rais wa Maonesho ya St. Louis, alitutumia ujumbe kutoa shukrani za dhati. Kwa upande wa Sullivan, ambaye alikuwa ameunga mkono

jambo letu kwa shauku kubwa, alisema kuwa, huu utakuwa ni "mfululizo wa maadhimisho ya michezo duniani ambayo hayajawahi kutokea".

Lakini, ulimwengu ulifurahishwa?... hapana. Katika majira hayo ya kiangazi, nilisafiri hadi huko Wagner Bayreuth, nilipata muda wa kutafakari na kuchunguza kwa amani masuala ya Olimpiki. Muziki na michezo daima vimekuwa njia yangu bora ya kujifariji na kutulia, vitu vinavyonisaidia kutafakari na kupata utulivu zaidi pamoja na "vitulizo vya akili" vinavyonichochea kuvumilia. Kwa kweli, baada ya kipindi kigumu na hatarishi, wasiwasi wote uliokuwapo uliondolewa ghafla. Michezo ya Tatu ya Olimpiki ingesherehekewa kwa fahari na shamrashamra zote.

Timu yenye uzoefu ilikuwa imewekwa kusimamia mipango hiyo. Bila shaka wangefanya makosa mengi sana, lakini hakukuwa na hofu ya athari yoyote iliyowapata watangulizi wao wa mwaka 1900. Mafanikio ya Michezo ya Olimpiki, yatategemea kuwapo kwa mwongozo wa Olimpiki, Mkuu wa nchi na mamlaka ya IOC. Walitarajia mambo makubwa ya "wana wafalme (walikuwapo watatu kwa wakati huo) pamoja na viongozi wa ngazi za chini. Tulipewa ukumbi mzuri kwa ajili ya vikao vyetu. Niliamua kwa uthabiti kukataa mwaliko bila wao kuhisi chochote. Tungekuwa watu sita au saba kwenye meza iliyoandaliwa kwa ajili ya watu thelathini. Watu wangesema kwa mshangao; "hii si IOC mashuhuri ambayo imejiingiza kwenye gharama zisizo na sababu! Hata hivyo IOC ilifanya mkutano mwaka 1904 ili kujitambulisha; tukio hili la kujitambulisha lilifanyika jijini London katika eneo la kiutamaduni la Meya kwenye jengo la kifahari, chini ya usimamizi wa mfalme Edward VII, likifanyika kwa heshima zote kwenye taasisi changa ambazo ziliongeza sifa kwenye vikao vyetu. Tukiwa London, IOC ilikabidhi majukumu kwenye mji wa Rome (Eternal City) kwa ajili ya kusimamia mashindano ya miaka minne baadaye ya michezo ya nne ya Olimpiki.

Kila kitu kilikwenda kama kilivyopangwa. Kikao kilikuwa na mafanikio makubwa kwa kila namna, isipokuwa ningependa kuwa na ushiriki wa vyuo vya Oxford na Cambridge katika kazi yetu, pamoja na shule maarufu ya umma ya Rugby, ambayo ni kitovu cha elimu ya michezo. Lakini marafiki zangu wapendwa, RS Laffan na Sir Howard Vincent, walipanga mambo vizuri sana, mbali na mikutano yetu, juma zima lilikuwa kwenye ratiba, kuanzia tarehe 19 hadi 27 Juni, kwa hafla mbalimbali, chakula cha mchana kwenye jengo la kifahari, chakula cha jioni kwenye makazi ya mfalme na wafanyabiashara maarufu wa samaki, matembezi ya kitalii kwenda Windsor na Hurlingham na kadhalika. Pia, sio marafiki zangu wote walielewa hoja yangu ya kuhusisha vyuo vikuu kwenye ufufuaji wa michezo ya Olimpiki. Huko Marekani, ambapo vyuo vikuu vilikuwa vimetawala kwenye riadha, jambo hili halikuwa gumu. Kwa ulaya jambo hili halikuwezekana. Sina nia ya kuwakosoa wanafunzi, mitazamo yao na ile ya walimu wao. Isivyo bahati, ni dhahiri kwamba kati ya mwaka 1890 na 1930, ushirikiano kwa upande wa vyuo vikuu haukuwapo katika nyanja nyingi (Olimpiki ikiwa mojawapo). Majaribio ya kushirikisha vyuo vikuu katika masuala yasiyo ya kitaaluma

yalipuuzwa na mara nyingi mijadala iliishia njiani, bila kuonyesha mwendelezo au dhamira ya dhati ya kuyafikia. Baadaye, wanafunzi waliposhiriki kwenye michezo walitaka kuwa na michezo yao maalumu ya Olimpiki. Kwa upande wa wafanyakazi, walitaka kuwa na michezo ya aina hiyohiyo na nilikuwa nimepingwa vikali kwa kuwa na mtazamo kinzani wa pande hizi mbili. Hapo baadaye nitaeleza sababu zangu kwa kina.

Mnamo tarehe 24 Machi 1903 Seneta Todaro , kwa mamlaka yake kama Rais wa Federazione Ginnastica Italiana , alinitangazia rasmi uamuzi wa pamoja uliotolewa siku chache zilizopita na wawakilishi wa vilabu vya sarakasi vya Italia wa kuiomba Roma ichaguliwe kuandaa mashindano ya nne ya Michezo ya Olimpiki. Miaka mitatu ilikuwa imepita bila mafanikio na bila ya kuwa na mikutano yoyote ya IOC, lakini kulikuwa mawasiliano mengi yanayolenga kuimarisha ushirikiano kati ya wajumbe wake na vilabu mbalimbali vya michezo. Mkutano wa London ulilenga kuangazia matokeo ya mafanikio ya juhudi zetu.

Maombi ya Roma ambayo yalisitishwa kwa muda na Rais Todaro, yalipata mtetezi mashuhuri ambaye ni Katibu wa Shirikisho la Italia, Bw. F. Ballerin. Kwa maombi yangu, Count Brunetta d'Usseaux aliweka hadharani uungwaji mkono wake wa shauku. Changamoto pekee ilikuwa mwelekeo wa ukanda, ambao ulikuwa na nguvu zaidi wakati huo kuliko sasa. Mamlaka ya Roma hayakuwa wazi kwa kila mtu. Milan lilijiona kuwa jiji kuu la michezo katika eneo lote la peninsula. Aidha, mji wa Turin nao ulijiona hivyohivyo.

Michezo ya Olimpiki katika mji wa Milan au Turin ingekuwa kawaida sana na isingesaidia kwa namna yoyote kuendeleza lengo letu. Niliutaka mji wa Roma kwa sababu ni sehemu pekee baada ya kufanya mabadiliko ya mtazamo wa kisiasa kwa Wamarekani, ingeweza kuubeba Mchezo wa Olimpiki kama ambavyo nilikuwa nimefikiria tangu mwanzo.

Tulipiga kura kwa uadilifu mkubwa, jambo ambalo lilisababisha marafiki wenzangu wa Ujerumani, waliondoe pendekezo lao la kuuchagua mji wa Berlin. Niliamua upigaji kura uwe wa kiwango cha kimataifa ili kuijengea heshima Roma ya Kale. Upigaji kura huu baadaye ungesaidia pia kuzuia vipingamizi vya mwelekeo wowote unaopunguza ushiriki wa Michezo kwenye miji kadhaa. Hata hivyo, jambo hili lilieleweka vyema. Miji ya Athens, Paris, Chicago na St. Louis iliwasilisha maombi yake kuwa waandaji wa kujitegemea. Wakati huu, baadhi ya magazeti na kamati zilizokuwa zikizungumzia kuchaguliwa kwa Italia kuwa mwandaaji wa Michezo ya Olimpiki ya mwaka 1908, viliibua matamanio ya kificho kutaka miji ya Italia ishirikiane kuandaa mashindano. Hiki kilikuwa kitisho kikubwa ambacho kilipaswa kuepukwa kwa gharama zote. Hii ndiyo sababu, tuliuzungumzia mji wa Roma na ukawa mji wa Roma pekee. Muda mfupi baadaye, zoezi la upigaji kura lilikuwa limekamilika. Matokeo yalipelekwa kwenye

Ubalozi wa Italia. Balozi alituma matokeo ya uchaguzi pamoja na salamu zetu kwenda kwa mamlaka ya juu na kwa Meya wa Roma na Mwanamfalme Colonna.

Mapema mnamo tarehe 27 Februari, Baraza la Kijamii, lililokutana Makao Makuu, kujadili suala hilo na kuamua kuwa wasimamizi endapo watapewa fursa hiyo. Mrejesho wa Mwanamfalme Colonna ulikuwa ni wa kufurahisha. Kiongozi Mkuu wa Kasri la Mfalme alituma taarifa kuwa Mfalme alimwamuru kutuma shukrani zake za dhati kwenye Kamati ya Kimataifa ambayo "kwa kuitangaza Roma kuwa mwenyeji wa mashindano ya nne ya Michezo ya Olimpiki" kuliupa "heshima" mji wa Italia.

Muda mfupi baadaye, wenzetu Gebhart na Kemény walianza safari ya kuelekea Marekani, washiriki wakiwa wamebeba salamu zetu kwa waandaaji wa Michezo hiyo. Ikiwa imeshapata nguvu huko Ulaya, IOC ilitaka kueleza kwa muhtasari kadri ilivyowezekana, udhaifu wa taasisi ya Kimarekani. Hoja muhimu zilipatikana. Lisingekuwa jambo la busara kutarajia zaidi. "Uvumilivu" ulibakia kuwa kaulimbiu yetu.

Kwa hiyo, Michezo ya St. Louis ilikosa kabisa mvuto. Binafsi sikuwa na hamu ya kuhudhuria. Niliweka chuki kubwa na mji huo kwa kukatishwa tamaa kulikosababishwa na kuona mara ya kwanza makutano mito ya Missouri na Mississipi. Baada ya kusoma kitabu cha Fenimore Cooper, mandhari ya makutano niliyotarajia siyo niliyoyakuta. Hakukuwa na uzuri na uasili. Niliwaza kuwa, washiriki wa Olimpiki wasingefurahishwa na mandhari yale. Kwa kadiri uhalisi ulivyoonekana, kitu pekee kilichokuwapo hakikuwa cha kufurahisha. Ninamaanisha "Maonesho ya Zama za Kale (Anthropolojia)", ambayo yaliwahusu watu Weusi, Wahindi, Wafilipino, Wainusi, Waturuki na Wasiria. Hiyo ilikuwa miaka ishirini na sita iliyopita!... Sasa niambie kama ulimwengu haujabadilika tangu kipindi hicho, hakuna maendeleo yoyote yaliyopatikana kwenye uga wa michezo...

# VII

## Mkutano Uliofana na Wenye Mafanikio (1905)



18. *Pierre de Coubertin*

"Katika mfululizo wa miaka ya Michezo ya Olimpiki", mwaka 1905 ndiyo unaokuja kwenye kumbukumbu zangu, si kwa sababu ni mwaka bora lakini ni wenye umuhimu zaidi.

Kwa upande wangu, mwaka huo ulianza nikiwa Roma kwa muda mrefu, ambapo ziara yangu ilikuwa na malengo mawili: kwanza, kuwahakikishia Waroma kuwapo kwa sherehe za Michezo ya Nne ya Olimpiki ambazo zilipaswa kufanyika mwaka 1908 na pili, kuishawishi Vatican kuanzisha mijadala inayohusu elimu ya michezo katika miktadha mbalimbali ya kidini. Lengo la kwanza halikufanikiwa lakini la pili lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Kila kitu kilionekana kuwa ni mbinu inayoweza kuleta mafanikio katika michezo ijayo. Roma ilikuwa na rasilimali zote ambazo hapo awali hazikuwapo huko Athens; kila mmoja alionekana kuunga mkono lengo letu kuanzia Mfalme hadi maofisa wa kawaida. Kimsingi, kuungwa mkono huku hakukuambatana na shauku kubwa, lakini hii haikuwa muhimu kwa Ugiriki. Lakini bado tulihitaji Kamati ya Maandalizi. Kamati iliyokuwa

imeundwa na Count Brunetta d'Usseaux mwaka uliopita haikuwa na kiongozi. Hakuna mtu aliyepatikana kujaza nafasi, matokeo yake ni kwamba hali ya kikanda ambayo niliitaja hapo awali ilijirudia. Ninapoongelea ukanda simaanishi kwamba Italia haikuwa imeungana wakati ule: hakukuwa tena na mwelekeo wa kujitenga wa siku zilizopita miongoni mwa wenyeji wa Piedmont, Venice, Roma, Neaple au Sicily. Hata hivyo, tabia zao, tamaduni na njia ya kuona na kufanya mambo vilibaki kuwa tofauti kiasi kwamba ukiachana na masuala muhimu ya kitaifa, ilikuwa ngumu kushirikiana na kulikuwa na migogoro ya mara kwa mara isiyoisha. Sina lengo la kueleza kwa kina kuhusiana na tofauti zao nyingi. Tayari nimekwishazungumzia baadhi ya migogoro hiyo katika kitabu cha kumbukumbu kilichochapishwa mwaka 1908. Kama ilivyokuwa huko Athene miaka kumi na mmoja iliyopita, ilibidi niamue kufanya kazi mwenyewe ili kurekebisha upungufu wa rasimu iliyokuwa imeandaliwa na wengine na kuandaa mipango na makadirio ya michezo. Mfalme na Malkia walishauri tutumie uwanja wa "Piazza di Siena" uliopo "Villa Borghese", ambao ulikuwa uwanja mzuri wa asili uliofaa kwa michezo ya riadha. Niliuchagua uwanja wa "Piazza dei Armi" kwa ajili ya michezo ya sarakasi na "Caracalla's" kwa michezo ya sanaa ya mapigano.

Ilikuwa ni mandhari nzuri kiasi gani na yenye urahisi wa kuandaa! Uwanja wa "Tor di Quinto" ulikuwa kwa ajili ya michezo ya wapandafarasi, na mto Tiber uliopo kati ya daraja la Ponte Molle na daraja la Ponte Margarita kwa ajili ya mchezo wa kupiga makasia na kuogelea; Jengo la Makao Makuu kwa ajili ya sherehe za ufunguzi na mapokezi... Makadirio ya awali kulingana na taarifa zote zilizokusanywa yaligawanywa katika sehemu kumi na mbili. Jumla ilifikia lira 303,000. Zilikuwa siku zenye furaha iliyoje! Zinakubalika, kama miaka ya 1896 na 1900 na michezo 1908 ilionekana kuwa imeandaliwa mahususi kwa ajili ya wasomi; washindani mia tano na watazamaji kati ya elfu kumi na tano hadi elfu ishirini. Makadirio yalijumuisha tuzo na medali ambazo zingeongeza thamani na kwa vile niliamua kuzivunja kalibu mara tu baada ya michezo kumalizika. (Nimekuwa nikitaka hili lifanyike kila baada ya michezo ya Olimpiki lakini halifanikiwi) na mshahara wa mkurugenzi mkuu, nafasi ambayo nilipanga kumteua Katibu Mkuu wa klabu ya Mbio za Farasi ya Ufaransa, Bw. Gaston Raymond, ila mpaka kwa makubaliano na kilabu.

Majadiliano na Vatican yalikuwa rahisi. Tofauti na wakuu wengi wa mashirika ya kidini, Papa Pius X ambaye alitoa tuzo mara kwa mara katika michuano maarufu ya mashua iliyofanyika huko Venice na Katibu Kiongozi Kadinali Merry, ambaye alisoma huko Elton, walikuwa na mtazamo chanya kuhusiana na mchezo (nazungumzia mchezo halisi na mashindano ya michezo na sio michezo ya ridhaa iliyokuwa ikiruhusiwa kwa muda katika mashirika kama haya). Kutokana na kuvutiwa na wazo la kufanyika kwa michezo ya Olimpiki huko Roma, Papa alizungumza kwa kuunga mkono moja kwa moja, jambo lililoonesha hisia zake. Msimu uliofuata, lilifanyika tamasha la sarakasi wakati wa hija ya Wafaransa, Wabelgiji na wafuasi wengine wa kikatoliki, ambapo Papa ndiye aliyeongoza

ndani ya ukumbi maarufu wa St Damase. Picha za kumbukumbu za tukio hilo zimekuwa zikivutia sana kwenye maonesho ya miaka ya awali ya Michezo ya Olimpiki.

Kipindi IOC ilipokutana Ufaransa katika majira ya vuli mwaka 1901, ililazimika kujadili mapendekezo matatu na kukubaliana kuitisha Mkutano wa kimataifa ulioweka viwango na kanuni za michezo. Pendekezo la kwanza lilifanywa na wenzetu wa Ujerumani, la pili lilifanywa na kikundi cha Waswideni na la tatu lilifanywa na Chama cha Michezo ya Riadha ya Ridhaa cha Marekani. Rasimu ya kwanza ilipendekeza, kuandaa mwongozo ambao utakuwa wa lazima kuufuata katika mashindano yote yajayo. Mwongozo huu ulikuwa wa kidikteta sana. Kwa nini IOC ijisikie kuwa ina mamlaka ya kuanzisha sheria kama hiyo bila kushauriana na vyama na vilabu vya kiufundi vya wataalamu wabobezi? Hapa tulipata taswira ya mkanganyiko utakaojitokeza kati ya michezo ya Olimpiki na michuano ya kawaida ya kimataifa kwa wakati ujao. Wajumbe wa IOC ni waanzilishi wa wazo la Olimpiki na walikuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba mashindano manne ya kila mwaka yanafanyika kulingana na ari hiyo. Hii haikuwafanya wao wakidhi haja kuchukua nafasi ya wataalamu katika uendeshaji wa mashindano haya. Watu waliokuwa nje na ndani ya kamati walipata ugumu wa kuelewa jambo hili.

Pendekezo la pili, kama nilivyosema kuwa liliandaliwa na Waswideni; lilikuwa linashawishi hata hivyo limerahisishwa na linakasirisha kwa namna ya kutazama maswali yaliyochanganywa na mambo yasiyotarajiwa, kwa kawaida hufanya mawazo ya Waskandinavia kuwa magumu kueleweka, hata kwa wale wageni ambao huwa na shauku kubwa na kila kitu cha Skandinavia. Kwenye akili zao, kwa kuwa tulikuwa tunafufua michezo ya Olimpiki, tulitakiwa kufanya kwa uadilifu, kuondoa kila kitu cha kisasa katika programu na kubakiza yaliyokuwa yakifanyika zama za kale. Sina haja ya kubainisha athari zitazojitokeza kwa kupuuza michezo ya kisasa na kuendeleza michezo ya kale. Pendekezo la tatu ndilo pekee lililostahili kubakizwa.

Bw. L. P. Sheldon, aliyetumwa na Chama cha Michezo cha Marekani kwa malengo hayo, aliruhusiwa yeye mwenyewe kuiwasilisha rasimu kwenye IOC. Alifanya hivyo kwa ujuzi na ufanisi mkubwa. Ilishauriwa kuwa, tunapaswa kushawishi mabadiliko ya mitazamo miongoni mwa wote wanaotamani suala la kuunda taratibu za kuandaa kanuni za mashindano ya michezo na kuiunga mkono mamlaka yetu kwa makubaliano yoyote yaliyoafikiwa. Au siyo? Hasa yale yanayoendana na ari na mwelekeo wa IOC.

Suala hili lilitufikisha hadi kwenye Mkutano wa Brussels. Mwezi Desemba ya mwaka huohuo wa 1901, nilitumia fursa ya ziara ya Mfalme Leopold wa Ubelgiji jijini Paris kuomba kwa lengo la kupata ufadhili wake. Mfalme Leopold wa pili ndiye aliyekuwa mfalme anayetisha kuliko wafalme wote waliokuwa wakitawala. Aina ya ugonjwa wake wa maradhi ya mifupa (jongo) ulimfanya kuwa na mazoea ya kubaki akiwa amesimama, akiegemea fimbo yake na alikuwa na kawaida ya kupokea wageni katika mtindo huu hata kama atavutiwa na mazungumzo aliyaruhusu kuendelea kwa muda mrefu. Urefu

wake, kila mara macho yake madogo na maoni yake ya kukera yalimfanya kuwa anatisha kabisa. Kama hatampenda mgeni wake, alionekana kuwa mkali zaidi. Je, alikuwa anapenda michezo? Au, aliwahi kuipenda hapo awali? Sina uhakika sana, lakini kwa malengo ya kuwafunza ukakamavu wanaume na kuwafanya wafae, aliona mazoezi ni muhimu kwa ajili ya makoloni yake. Miaka kadhaa baadaye, aliniomba nitengeneze mipangokazi kwa ajili ya maandalizi ya "chuo cha maandalizi ya ukoloni" ambapo niliifanya kazi hiyo kwa ukamilifu. Kiuhalisia, mafunzo ya michezo yalikuwa na nafasi kubwa. Mradi haukufaulu; niliufanya kuwa wa kidunia na mfalme aliudhinisha lakini ushawishi wa viongozi wa dini uliuharibu.

Mkutano uliopangwa kufanyika mwaka 1904 uliahirishwa hadi mwaka 1905. Tuliungana na mjumbe maalumu kutoka Ubelgiji, Count Henry de Baillet-Latour ambaye kabla ya kuchukua nafasi yangu miaka ishirini baadaye kama kiongozi mkuu wa IOC, angetuongoza na kutoa mchango mkubwa kwenye Michezo ya Olimpiki. Mtangulizi wake aliyekuwa na jukumu la kuandaa mkutano na aliyejiuzulu ghafla kulisababisha matatizo makubwa ambayo tulisaidiwa kuyatatua na mwanadiplomasia wa Ufaransa aliyekuwa akiunga mkono IOC.

Tarehe 7 Oktoba mwaka 1904, Count Smet Waziri Mkuu wa Ubeligiji, ambaye binafsi nilimfahamu, alinijulisha kwamba Waziri wa mambo ya nje amekubali kuruhusu mialiko itumwe na maafisa wa Ubeligiji. Hii ilikuwa hoja muhimu. Hata hivyo, alijutia sana kiongozi wa mji wa Brussels, Bw. de Max, alitunyima kutumia ukumbi wake maarufu wa Town Hall. Lakini Count de Baillet alitupangia kutumia ukumbi wa Palais des Academies ambao kwa kweli ulikuwa katika hali ya kuridhisha na ulitufaa zaidi kwa shughuli yetu.

Sherehe rasmi za ufunguzi wa mkutano ambazo zilifanyika Juni 1905, zilitanguliwa kwa risala ya Bw. Marcel Prevost, Rais wa Chama cha Wanafasihi, ambaye alikuja rasmi kutoka Paris kuzungumzia suala la "*the mind in the school of sport*" mchango mzuri wa vikao vilivyojikita kwenye masuala ya ufundi. Ilikuwa ni zamu ya michezo, kama ilivyokuwa jijini Le Havre ambayo ilikuwa zamu ya elimu. Programu ilikuwa ya kuvutia sana kwa kuwa iligusa maeneo yote yaliyohitajika. Kilikuwa ni kitabu chenye kurasa tano au sita. Kiuhalisia haikuwa rahisi kuyaelezea kiundani, yalikuwa ni bayana. Jambo moja lililovutia na la kukumbukwa katika mjadala lilikuwa ni mchango wa michezo jeshini. Wawakilishi kutoka Ufaransa waliunga mkono hoja. Wawakilishi kutoka Ujerumani na wafuasi wao walipinga hoja hiyo. Kwa mtazamo wao, ilikuwa ni kupoteza muda kwa wanajeshi na ni tukio la ukiukwaji wa nidhamu. Kila mmoja atakumbuka itakavyokuwa miaka kumi baadaye kwa upande wao, upinzani huu ulikomeshwa kwa nguvu kwa namna ambavyo mafunzo ya michezo yalikuwa na thamani kubwa.

Kikao cha IOC, kilifanyika wakati wa mkutano ambacho kilikuwa na matokeo makubwa. Kamati ya Wajerumani ilimteua Rais wao mpya. Jenerali Count von der Asseburg, alichukua nafasi ya Prince Salm-Hordtmar, ambaye alihitaji kustaafu. Hii ilikuwa ni

kinyume na utaratibu wa IOC. Hakukuwa na cha kuhoji. Wakati Jenerali alipowasiliana na wenzangu kama washiriki wa mkutano, alisema kamati yake ndiyo iliyofanya makosa na hivyo alitamani uchaguzi ufanyike. Kimsingi, tulimchagua yeye (Jenerali Count von der Asseburg) kwa furaha kubwa. Alikuwa ni mtu mcheshi ambaye kila mtu alimwamini. Michezo ya Olimpiki ilimhamasisha kutengeneza mazingira mazuri ya michezo huko Brussels. Kwa kweli hali ilikuwa ngumu. Delcasse alijiuzulu baada ya kuwasili kwa Kaiser huko Tangiers pamoja na matukio yaliyofuata. Watu walikuwa wanaongelea uwezekano wa vita. Wabelgiji walikuwa wanatiliwa shaka. Kwa upande wa Waskandinavia walikuwa na mgogoro uliotokana na kujitenga kwa Swideni, kulikosababishwa na Wanorwei. Lakini yote haya yalisahaulika katika mazingira mazuri ya michezo. Mkutano huu wa wajumbe



**19.** *Count Brunnetta*




**20.** *Count Hann de Ballert Letour*

zaidi ya mia mbili wakati mwingine uligawanywa katika kamisheni, wakati mwingine ulifanyika kwa majadiliano ya pamoja yaliyolenga kuwa na masilahi makubwa kwa umma.

Kwa kawaida, mambo yote yalimalizika vyema. Lakini kwa kipindi hicho, wakati mikutano haijamalizika, 'matarajio' bado yalikuwapo. Zaidi ya hayo, idadi hiyohiyo ya wajumbe wa mkutano uliipa hadhi IOC. Uundaji wa hivi karibuni wa Chama cha Michezo ya Olimpiki cha Uingereza ambacho kilisaidia kuleta usawa na *'Deutscher Reichsausschuss fur Olympische Spiele*, ulitupa mambo mawili muhimu. London na Berlin kwa wakati huo walimiliki vituo vya Michezo ya Olimpiki ambavyo vilifanya kazi pamoja nasi chini ya usimamizi wetu. Jambo hili lilituweka kwenye nafasi nzuri ukilinganisha na Athene. Hata hivyo, mwenzetu Mercat alitumia fursa kuimarisha uhusiano wa karibu, ambao Mwanafalme aliuendeleza kwa kadiri alivyoweza. Michezo ya ziada ilitakiwa kufanyika huko Ugiriki mwaka 1906. Ilieleweka kwamba IOC itatoa ushirikiano pamoja na kulinda michezo ya jumuiya ambayo tayari ilishaundwa katika nchi mbalimbali na wanachama wake. Kwa hiyo, ingawa mkutano wa Brussels ulifanyika katika kipindi hatari sana cha mivutano ya kisiasa iliyokuwa ikiendelea huko Ulaya Magharibi tangu mwaka 1887, ulifanikiwa kusimamia Michezo ya Olimpiki kukamilika kwa utulivu na amani ya hali ya juu ambayo hatukuwahi kuitarajia. Hata hivyo, hii haikumanisha kwamba maadui wetu wameisha.

# VIII

## Ujumuishaji wa Fasihi na Sanaa (1906)



Ce mois de May (Jannequin 1550).

Ce moys de May, ma verte cotte
Ce moys de May, je vestiray
De bon matin m'y leveray
Ung sault, deux saulx, trois saulx en nue je
[teray

Pour voir si mon amy verray
Je lui diray qu'il me descrotte
Me descrotant le baiseray...
Ce moys de Mai... etc...

Allez mes premières amours (Costeley 1570).

Allez mes premières amours
Allez je ne vous veux plus suivre
Vous me refusiez le secours
Qui fait l'amant fidelle vivre
Allez j'ay trop cognu vos tours

Approchez, mon amour seconde
N'usez point vers moy de rigueur
Venez ça, ma mignonne blonde
Je n'ayme que vous en ce monde
Baisez moy et prenez mon cœur

Las! je n'yray plus (Costeley).

Las, je n'yray plus jouër au boys
Hier au matin m'y levay
En notre jardin entray
Las, je n'yray plus jouër au boys
En notre jardin entray
Trois fleurs d'amour j'y trouvay
Las, je n'yray plus jouër au boys
Trois fleurs d'amour j'y trouvay

Une en prins, deux en laissay
Las, je n'yrai plus jouër au boys
Une en prins deux en laissay
A mon amy l'envoiray
Las, je n'yray plus jouër au boys
A mon ami l'envoiray
Qui sera joyeux et gay
Las, je n'yray plus jouër au boys

Par les Chœurs de la *Société Chorale d'Amateurs.*

L'enlèvement d'Europe.

de Leconte de Lisle

Poésie dite par Mme BARTET, de la Comédie Française

Quand le berger.

Quand le berger voit la bergère
Dessus la verdure à loysir
vint d'une course légère
Et droit au col la va saisir

O quel desir, o quel plaisir
Il avait d'embrasser sa dame
Ha, je le vy si fort ravy
Que je pensoys qu'il rendit l'âme

Par les Chœurs de la *Société Chorale d'Amateurs.*

Oceano nox.

de Victor-Hugo.

Poésie dite par M. MOUNET-SULLY, de la Comédie Française

Nos pères.

de Bourgault-Ducoudray.

Par les Chœurs de la *Société Chorale d'Amateurs.*

Les Chœurs sous la direction de M. Jules Griset
Directeur de la *Société Chorale d'Amateurs*

COMITÉ INTERNATIONAL OLYMPIQUE

Palais de la Sorbonne

26 MAI 1906

FESTIVAL OLYMPIQUE

Arts, Sciences, Lettres, Sports

CITIUS
FORTIUS
ALTIUS

PROGRAMME

Haikutosha kuwaleta pamoja "washirika wa mwanzo wa Mamlaka na Fikra", mbele ya Msajili (katika tukio hili, Bw. Jules Claretie, ambaye aliongoza hafla hiyo ndani ya ukumbi wa kihistoria wa "*Comedie Francaise",* akiwa na Bi. Bartet na Bw. Montet – Sully pembeni yake); ambaye alikuwa ni muhimu kwa chama hicho kuleta mafanikio. Hata hivyo, mafanikio yalipatikana mwaka 1926, miaka ishirini baadaye. Miongoni mwa waasisi ni wangapi ambao walikuwa na dosari tangu kuzaliwa! Mwaka 1906, jambo la muhimu lilikuwa ni kuleta maelewano baina ya washirika wawili ambao walionekana kumiliki kila kitu kinachowaunganisha. Lazima ieleweke kwamba, kiuhalisia hawakujaliana hata kidogo. Jambo muhimu lilikuwa ni chama kuchukua nafasi na zaidi ya yote ni lazima kuleta mafanikio.

Nimesharudia mara nyingi kwamba nina aibu ya kufanya hivyo tena, lakini watu wengi hawakuelewa kwamba Michezo ya Olimpiki sio tu michuano ya kawaida ya Dunia bali ni tamasha la kila baada ya miaka minne la vijana wa duniani, "asili ya wanadamu", tamasha kubwa, matarajio mengi na aina zote za shughuli za vijana zinazoadhimishwa na kila kizazi kinapofikia hatua fulani ya maisha. Halikuwa jambo la nasibu kwamba, katika nyakati za kale waandishi na wasanii walikusanyika pamoja kwenye Mji wa Olimpia kusherehekea na hivyo kujenga heshima kubwa ya michezo iliyofurahiwa kwa muda mrefu. Nikiwa na nia ya kufufua misingi ya taasisi iliyodumu kwa zaidi ya miaka elfu moja, nilidhani ingeipatia nchi yangu vichocheo vya muhimu vya elimu walivyovihitaji. Nilijaribu kurejesha nguzo imara zilizosaidia jambo hili kipindi kilichopita: nguzo ya kifikra, maadili na kwa kiasi fulani nguzo ya kidini. Dunia ya sasa imeongeza vitu vipya viwili, ambavyo ni maboresho ya kiufundi na demokrasia ya kimataifa.

Katika mji wa Athene, mnamo mwaka 1896 mkutano wa kwanza wa vijana uliofanyika katika uwanja uliojengwa upya wa Pericles, ulizuia utafutaji wa kazi mpya za kisanii na za kifasihi zilizochochewa na wazo la michezo.

Ingekuwa ni ujinga. Hata hivyo, haikuwezekana kufanya kila kitu kwa wakati mmoja. Utendaji kazi wangu wa hatua kwa hatua, daima umeonekana kuwa ndiyo njia bora ya kufanya shughuli yoyote kubwa inayotarajiwa kudumu. Mnamo mwaka 1900 huko jijini Paris, mbali na hali mbaya ambayo nimeshaieleza hapo awali, Maonesho ya Dunia yalikumbwa na wingi wa aina za miundo mipya na mawazo mengi sana kwa kuwa hakukuwa na hatua ya kujaribu kujumuisha juhudi za kina na za asili kama hizo... Lakini tangu mwanzo Chicago ilionekana kuvutiwa na suala hili la Michezo ya Olimpiki. Hata hivyo, programu niliyoitaja hapo juu iliruhusu mvutano usiokuwa na sababu, lakini iliyofanywa kwa uaminifu na shauku, kisanaa na kifikra. Kwa mtazamo huu, kuhamisha Michezo kwenda St. Louis, lilikuwa kama jambo la mkosi. Juhudi zote kwenye mambo haya zililazimika kuahirishwa tena. Roma kwa wakati huo, ilikuwa inaelekea kushindwa kwenye upeo wa fikra. Kuyumba, kupungua kwa lengo na ujasiri vilianza kuwa dhahiri, vikisababishwa na ukanda ambao bado ulikuwa na nguvu sana licha ya kuonekana kuna umoja… Uhamisho mwingine kwa wakati huu ulipangwa kwenda London. Kwa sababu

muda ulikuwa ni mfupi sana, tulipaswa kuwa wabunifu na upande wa Michezo ya kisanaa ungeathirika sana.

Hofu ya kuona uzinduzi wa wazo hili ukicheleweshwa tena ilinifanya niitishe "Mkutano wa Mashauriano kuhusu Sanaa, Fasihi na Michezo" wakati wa Majira ya Vuli ya mwaka 1906. Wakati huohuo, ningeweza kutumia jambo hili kama udhuru wa kutokwenda Athene, safari ambayo nilitamani sana kuikwepa. Kwa sasa tulikuwa na uhusiano mzuri sana na Kamati ya Ugiriki ya Kale. Maridhiano yalikuwa ni matokeo ya juhudi za makusudi kwa pande zote mbili kuliko mabadiliko makubwa ya nafasi zetu. Je, michezo ya ziada ya mwaka 1906 ingepewa jina gani? Ingefanyika mara ngapi? Mpango wa muda wa kila baada ya miaka minne, ambao niliukubali bila kushawishiwa, ulikataliwa. Jijini Athene, walikuwa wakifikiria kipindi cha kila baada ya miaka kumi, jambo ambalo lingefanya matukio mawili kugongana mwaka 1916… Haya yote hayakuwa na uhakika sana; hali ingekuwa tete wakati wote. Katika hali yoyote, msuguano mkubwa na matatizo mengi vingejitokeza wakati wa mashindano, lingekuwa jambo la heri kama nisingekuwapo. Count Brunetta d'Usseaux angechukua nafasi yangu na angeweka pingamizi kila inapowezekana, kwa kulizungumzia suala ambalo nilipaswa nilisemee; kwa kutumia njia hii tulifanikiwa kuchelewesha na kuepuka maswali ambayo yangezuia uamuzi wa haraka.

Nakumbuka vizuri tabasamu la furaha usoni mwa André Beaunier - mwandishi ambaye alitawaliwa na hulka ya wivu. Nilimtembelea katika ofisi yake ya Le Figaro na kumpatia mwaliko wa kuhudhuria Mkutano utakaofanyika huko *Comédie Française*. Mwaliko ulikuwa wa "Kuja na kujifunza ni kwa kiasi gani na kwa namna gani Sanaa na fasihi zinaweza kujumuishwa katika Michezo ya Olimpiki ya sasa na kuhusishwa na shughuli za michezo kwa ujumla ili sio tu kufurahisha bali kutengeneza jina". Alisema, "iliwekwa vizuri sana" "na jinsi inavyoendana na mandhari yaliyochaguliwa!" Bila shaka mandhari yalikuwa siyo ya kawaida na mwanzoni ombi letu hakika lilimshitua Jules Clarite. Lakini aliendelea kutumia wazo hilo akiongoza ufunguzi wa mkutano ambao wasanii wote na waandishi wa kumbukumbu walialikwa. Takribani watu sitini tu ndio waliohudhuria, ambapo wale waliohudhuria siku ya kwanza walirudi siku zilizofuata kwa ajili ya majadiliano na kusaidia kuandaa mpango. Jean Richepin, Bourgault-Ducoudray na Poilpot walivutiwa na mpango mzima. Walipanga kuwe na maandamano, kwaya mbalimbali, maonesho ya kuvutia na mashairi ya ushindi. Wengine waliunga mkono mpango huo kwa shingo upande au waliangalia ugumu pekee. Kikwazo kikuu kinaweza kufupishwa kwa maneno machache: hofu ya jadi. Wasanii wachanga ambao walionekana wa kizamani na walionwa kuwa hawana jipya, ndio hasa walitegemewa kufanikisha mpango huo. Lakini chuki zao ziliwafanya kupuuza wazo hilo. Aidha, katika usanifu hakuna mahitaji mapya ambayo bado yameelezwa; katika upakaji rangi, matukio ya michezo yalihitaji mistari zaidi kuliko rangi, hii ni kinyume cha mambo yaliokuwa yakiendelea, katika muziki, umma ulikuwa umepoteza kabisa ladha ya

nyimbo za hadharani, kwa waandishi wa fasihi hawakuwa na uzoefu na uwezo wa kuandika kuhusu michezo ya kutumia nguvu – hawakuwa na uwezo wa kuielezea hiyo na haikufahamika kwa umma.

Ingekuwa inawezekana kurekebisha haya yote kwa kiasi fulani kwa kutoa wito kwa nchi nyingine kushiriki. Katika hatua hii nilifanya makosa makubwa ya kutojizuia kutuma barua za mialiko, ambazo hazikueleweka vizuri na zilizotuletea telegramu za kutuunga mkono na kututia moyo, ambazo hazikuwa na msaada wala kueleweka. Chuo cha Sanaa cha *Royal Academy* cha London ndicho kiliunga mkono wazo hilo, ambalo lilikuwa ishara nzuri kwa Michezo ijayo (uwezekano wa kuichagua London ulikuwa ukiongezeka). Katika kikao cha ufunguzi, Laffan kwa mara nyingine alitoa hotuba ya kuvutia kwa Kifaransa… Bi. Bartet, aliyevutiwa, alipita nyuma ya Claretie, akanivuta mkono: "Huyu ni nani?" aliuliza kwa udadisi mkubwa uliochanganyika na pongezi…

"Huyu ni nani?"

Mkutano wa 1906 ulitimiza lengo lake kuu kwa kupendekeza kuwa IOC ianzishe "mashindano matano ya usanifu majengo, uchongaji, muziki, uchoraji na fasihi kwa kazi za asili zilizopata msukumo wa michezo, hivyo basi mashindano hayo yawe sehemu muhimu ya sherehe za kipindi cha miaka minne baina ya Michezo ya Olimpiki". IOC ingejifanya kitu cha aibu cha kujaribu kuanzisha mashindano ya aina hii papo hapo kwa kujitegemea. Walialikwa kufanya hivyo na kikundi chenye weledi kilichoundwa na wajumbe wenye hadhi kubwa, IOC iliungwa mkono na umma.

Kwa mantiki hii, Mkutano wa Mashauriano, ambao ulipangwa karibu na tamasha zuri la Michezo na Sanaa ulifanyika huko Sorbonne, haukushindwa kufikia lengo lake kuu. Mkataba wa kufufua Michezo ya Olimpiki ulikuwa umekamilika...

Au ulikuwa karibu kukamilika. Orodha ya hoja zilizotolewa kwenye mkutano mkuu wa mwaka 1894 zilijumisha pendekezo kwenda IOC (ambayo ilikuwa imeanzishwa hivi punde) kuingiza kwenye kanuni zake kifungu kinachoidhinisha kumuondoa mtu yoyote kwenye Michezo, ambaye matendo yake ya awali yaliharibu taswira ya Michezo." Maneno haya yalimkera André Beaunier! Wazo hilo sio tu la kushangaza lakini halikuwa wazi sana.

Hata hivyo, pendekezo lilifanyika ili kutoa nafasi ya kulinda maadili, hatua kwa hatua ikiifanya Michezo ya Olimpiki ya kisasa kuendana na vigezo vya uchujaji wa mshindani anayezingatia misingi muhimu ya Olimpiki ya kale. Kwa njia gani? Sikuwa na uhakika lakini kwa kuwa hatukuweza kutatua changamoto zilizohusisha Michezo ya ridhaa, niliona kwamba tungeanza kwa kuanzisha kiapo cha Michezo ya Olimpiki ambalo lingekuwa ni tukio la sherehe na lingempa heshima mshiriki wakati akijizolea umaarufu.

Katika duru za Michezo, wakati huo, hakuna mtu aliyejiandaa kwa tukio geni kama lile na mazungumzo yetu ya awali hayakuwa na jambo lolote la maana zaidi ya tabasamu

au upinzani, ilikuwa ni *Federation des Patroneges* ambapo nilitoa pendekezo langu la kwanza kwa umma. Kwa wakati huo lilikuwa na wanachama wapatao elfu hamsini. Lilikuwa likihujumiwa mara kwa mara, lakini liliweza kudumu na kufanikiwa kupata fursa sawa bila yeyote kufahamu ni kwa namna gani. Mwishoni mwa sherehe za shirikisho wakati wa Majira ya Vuli ya mwaka 1906, nilimwandikia barua Katibu Mkuu wake, Charles Simon, ambaye alikuwa mtetezi shupavu na mratibu mkuu, baadaye barua hiyo ilichapishwa katika toleo la mwezi Julai la Jarida la Michezo ya Olimpiki. Ndani yake, nilipendekeza kuanzishwa kwa Kiapo cha Michezo ya Olimpiki. Wazo hilo lilipitishwa kwa haraka zaidi kuliko ilivyotarajiwa na haswa katika vikao ambavyo vilikuwa na upinzani kwa wakati huo.



# IX

## Michezo ya Nne ya Olimpiki (London, 1908)



**22.** *Uwanja wa Michezo ya Olimpiki jijini London mwaka 1908*

Mtu mwingine asingeona umuhimu katika idadi ileile ya Majarida ya Olimpiki yanayotoa taarifa yoyote ya kuhamisha Michezo ya Olimpiki kutoka Roma kwenda London. Changamoto hii mpya ilitukumbusha kuhusiana na mambo mengine yaliyotufanya tufikie uamuzi wa busara na kunyamaza kimya. Kwa hiyo, uamuzi ulifikiwa pindi Chama cha Olimpiki cha Uingereza kilipopata uhakika wa mafanikio ambayo hayakutangazwa rasmi kwenye gazeti lolote. Kwa busara hiyo, changamoto hizo tulizozipata huko Tiberia, zilikuja kutatuliwa mjini Thamesi. Maandalizi yote yalikuwa yamefanyika katika kipindi cha Michezo ya Athene, ingawa hii iliandaliwa vizuri zaidi kuliko ile ya mwanzo, licha ya kuwa iliacha wasiwasi na ghasia kwa sababu haikuwa na misingi mathubuti. Wasiwasi na vurugu hizi zilipenya hadi kwenye ngazi za uongozi wa Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki (IOC). Kati ya wajumbe wanane au tisa ambao walikuwa wamekwenda huko Athene, walipoteza nyadhifa zao kwa muda katika mikutano yao ya kwanza na Brunetta d'Usseaux hakuweza kuzuia jambo hilo lisitokee. Walikuwa wameazimia kutetea upangaji upya wa mwanzo wa IOC na tayari walikuwa wamempa mamlaka ya urais mwanamfalme. Kiongozi mpya alifedheheshwa na ofa hiyo. Jambo la kipuuzi walilolifanya kwa kuichafua kamati ya Kigiriki kwa njia hii, walikuwa wanainyima uhuru wote wa kimataifa. Zaidi ya hayo, isipokuwa kwa azimio la mwisho, yote haya yalitegemea idhini ya Rais. Kwa kawaida, Rais aliyapinga yote, ikiwa ni pamoja na cheo cha heshima alichokuwa amepewa Mwanamfalme. Muda mfupi baadaye, mimi na Mwanamfalme tulikuwa na maongezi marefu huko Paris kuhusiana na suala lenyewe.

Lilikuwa ni jambo ambalo halikukubalika kwetu sote, lakini maongezi yalikuwa na utani mwingi kiasi cha kuishia na vicheko tu. Niliamua kuzungumza kwa uwazi na uhuru wote na mazungumzo yetu yalikuwa ya namna hiyo tangu mwanzo hadi mwisho. Kwa hiyo "kikao" cha huko Athene ambacho si Laffan, Baillet-Latour, Blonay wala Sloane ambao walishiriki, hakikuchukuliwa kama sehemu ya kikao kilichojadili masuala ya Michezo ya Olimpiki.

Lakini kwenye mkutano huo kulikuwa na 'Mwangalizi' ambaye baadaye alionekana kutekeleza jukumu muhimu sana. Hapa ninamzungumzia W. H. Grefnffell, tangu alipoteuliwa kuwa kama Jaji Desborough, ambaye baada ya kuwa karibu na IOC kwa mwaka mzima, alifukuzwa kwa sababu ya ushabiki wa Michezo ya Olimpiki. Laffan (ambaye kwa muda mfupi alipokea madaraka ya Herbert aliyestaafu kutokana na maradhi), aliungana pamoja na Bwana Howard Vincent ambaye alikuwa na sifa tatu muhimu ambazo ni utendaji, upangaji wa malengo sahihi na shauku ya kuyafikia malengo hayo. Ikiwa imeachwa kwenye uangalizi wa hao viongozi, Michezo ya Nne ya Olimpiki ingekuwa na matokeo mazuri. Pia kulikuwa na Maonesho, lakini kazi yake kubwa ilikuwa ni kutoa fedha zinazohitajika. Lilikuwa badiliko zuri katika uzoefu wa michezo ya zamani.

Kiuhalisia, wakati Maonesho ya Ufaransa na Uingereza yalipozinduliwa jijini London tarehe 26 Novemba, 1906, Jaji Desborough alilitangaza wakati huohuo eneo lililokuwa zuri na linalovutia zaidi ambalo Michezo ya Olimpiki ingefanyikia hapo. Jaji Desborough ambaye ufahari wake kama kiongozi ulikuwa umebebwa na sifa yake ya uimara katika michezo hususani mchezo wa kuvuka Maporomoko ya Niagara, alitangaza kupitia vyombo vya habari vya Uingereza kuwa, "kuanzia sasa, Michezo ya Olimpiki itafanyika Uingereza, mahali ambapo michezo mbalimbali imeanzia, ni jambo la msingi ikafanyiwa maandalizi na kusherehekewa kwa ubora wa nchi ambayo imekuwa kama chimbuko la michezo."

Na hiki ndicho kilichotokea karibia katika kila sehemu. Inawezekanaje kudhani kuwa maelezo ya kijeuri kama haya hapa chini yaliandikwa na mwandishi wa habari wa Ufaransa, F. Frank-Puaux mara baada ya Michezo, au anayejulikana kwa ushabiki wake wa michezo na akitolewa maoni mengine mazuri ya kuungwa mkono kutoka nchi zingine? Frank-Puaux alisema "Michezo hiyo ilisababisha pigo la mwisho kwa nchi ya Uingereza yenye hadhi ya kimichezo; Uingereza ilikuwa imeonesha dhahiri kuwa, ilikuwa imekabiliwa na upinzani mkubwa kutoka nchi zingine zisizokuwa na fikra pana tena, upendeleo na uhuru, vitu ambavyo waliushawishi ulimwengu kuwa wanavyo". Na kama ningeangalia kwenye mafaili yangu, ningechukua nyaraka kadhaa za Kimarekani, barua za binafsi, majarida, vipeperushi na kadhalika… ambavyo vilikuwa na mashtaka makali sana.

Je, ni kitu gani kingeongeza machungu haya yote baadaye? Hakukuwa na msingi wowote imara; isipokuwa ukubwa wa tukio ndiyo ulioibua Michezo mipya ya Olimpiki katika uhalisia wake mithili ya michezo mizuri iliyoozoeleka katika jamii hadi watu waliposadiki katika usemi wa wahenga na hatimaye wakawa mashabiki wa michezo na hili lilikuwa jambo jipya kwa sababu liliipandisha na kuikuza hadi kwenye kiwango ambacho haijawahi kufikia hapo kabla. Tumeshuhudia matamasha makubwa na mazuri ya namna hiyo. Lakini kumbukumbu zetu hazijasahau kile kilichotokea katika uwanja wa michezo jijini London. Uwanja mkubwa wa mpira uliokuwa na safu za viti vilivyopangwa mithili ya nusuduara, wakati mwingine vyeusi vyenye mashabiki wenye shauku kubwa, walishangilia kiasi kwamba kwa upande wangu sijawahi kuona kabla iwe ni Ulaya au Bara la Amerika. Katika tukio hili, ilionekana kuna mgogoro wa moja kwa moja uliokuwa unatengenezwa kati ya mataifa mawili ya Ujerumani na Uingereza ndani ya Michuano mikali kati ya mabingwa wao. Hatimaye, muda mfupi baada ya uhakika wa ushindi wa Michezo kubainika, kulikuwa na msururu wa maandamano kutoka katika mashirikisho ya Ufaransa yakiwa na lengo la kuvuruga uongozi mzuri wa Michezo ya Olimpiki yakiishushia hadhi IOC na kupinga mamlaka yake. Hali hii ilisababisha mvurugano mkubwa ambao baadaye ulitulizwa lakini uliacha alama. Hata hivyo, Michezo haikuathirika. Kinyume chake, kuibuka kwa vurugu kulionekana kuipa nguvu Michezo hiyo.

Wakati wa Majira ya Vuli ya mwaka 1907, mkutano wa IOC huko the Hague, ulikuwa umeshapata taarifa za kuridhisha kutoka kwa waandaaji wa Uingereza. Kazi ambayo waliikamilisha ndani ya muda mfupi wa miezi sita, kwa hakika ilikuwa nzuri sana. Misingi ya maadili yote ilikuwa imewekwa kwenye sekta mbalimbali, hata zile ambazo zilikuwa hazijafanyiwa majaribio, yaani Sanaa na Fasihi. Programu ilikuwa imewasilishwa tayari kwa ajili ya uchunguzi na kamati tatu zilizokuwa zimeundwa na wajumbe wa IOC, ambazo ziliimaliza kazi kwa haraka. Hata hivyo, makubaliano fulani yalipaswa kufanyika. Ilikuwa ni kwa mara ya kwanza mafundisho ya mazoezi ya viungo (sarakasi) ya Uswisi na Ujerumani yalikuwa yameletwa mbashara kwenye maeneo yaleyale, na kwamba mashindano ya kimataifa ya mbio za kupiga makasia kwenye Mto Thames yalipaswa kuhusisha nchi zote… Jijini Athene, malalamiko yaliibuka kuhusiana na majopo ya kimataifa. Katika Michezo ya mwaka 1908, kila mtu alikuwa na mwelekeo wa kujaribu wazo la kuwatumia waamuzi wa Uingereza pekee, wakiwa na idadi ndogo ya "maofisa" wa kigeni walioteuliwa kuwasaidia pale inapobidi; suluhisho duni lisilofaa katika kurahisisha uendeshaji wa michezo. Kwa upande mwingine hakukuwa na zile changamoto za kidiplomasia na kijamii ambazo kwa mwaka unaofuata wa Michezo ya Olimpiki, zingejitokeza. Hata hivyo hali ya Utawala haikuwa sawa. Kuanzia mwanzoni mara tu baada ya Michezo ilipofufuliwa, Australasia (kama ilivyokuwa ikijulikana kwa kipindi kile) ilikuwa na mwakilishi kwenye IOC na kwa sababu ya kuhusishwa katika umbali mrefu, hakuna mtu aliyeshangaa miongoni mwa orodha ile. Nchi zote za Kanada na Afrika Kusini zilikuwa ni sehemu ya Himaya ya Uingereza, na ilikuwa ni kawaida

kwamba, timu zao zikiwa jijini London zingepewa kipaumbele japo wakati mwingine zilipaswa kuchukuliwa kama za mataifa mengine nje ya himaya hiyo kwa mujibu wa haki zake na timu zao. Kwa hiyo, mahitaji ya kuweka mipaka ya kisheria kwa ajili ya madhumuni ya Michezo ya Olimpiki – bila kujali sheria za kimataifa lakini bila ya kuathiri sana misingi yake na kuzingatia ukweli. Tatizo lilikuwa kubwa sana. Halikutatuliwa mara moja. Makubaliano ya haraka na yanayowezekana yalipaswa kufanyika. Baadhi ya mambo yaliyolifanya liwe tatizo gumu yalikuwa yafuatayo: Kwa mfano, je, Mkanada anaeishi Uingereza angekuwa na hadhi gani? Pengine angekuwa huru kuchagua kujiunga ama na timu ya Kanada au Uingereza kama alivyotaka? Kulikuwa na uamuzi gani uliopitishwa kuhusiana na kile kinachoitwa "wenyeji" ambao walikuwa ni raia katika moja ya koloni la Uingereza? Na pindi uongozi unapoanza kwa nchi ya Uingereza, ungeiathirije nchi ya Ujerumani, kwa mfano, endapo Bavaria au Saxon wangeamua kwa ghafla kudai timu zao wenyewe? Nilipoiunda IOC, nilizikaribisha jamhuri zote mbili za Hungaria na Cheki ili wawe wanachama katika mrengo wa kuzisaidia katika masuala ya michezo na kujitawala kwa nchi hizi.

Lakini wakati Hungaria ikiwa ni nchi yenye haki zake za kipekee, nchi ya Bohemia haikuwa hivyo. Ghasia zingejitokeza mwaka 1912. Mwaka 1908, kulikuwa na mapigano machache huko Viena. Kwa vile Ujerumani ilikuwa inahusika, bila kusita niliwasiliana na Jenerali Von der Asseburg. Ninaamini alizungumza na Mfalme kuhusiana na suala hilo katika kushughulikiwa kwa namna yoyote na Waziri Mkuu.

Mwitikio ulieleza kuwa, Reich alipendelea zaidi wazo la kuwa na timu moja, na timu ya pamoja kutokana na msimamo wa Michezo ya Olimpiki lakini walielewa kuwa katiba maalumu ya ufalme wa Uingereza, ilihitaji timu tofauti. Hata hivyo, hakukuwa na ugumu kutoka kwa Wajerumani. Pamoja na hayo, mtazamo wa Marekani ulikuwa tofauti kabisa: Sulvan na wenzake wenye nguvu walichukizwa sana na upendeleo wa Uingereza.

Tatizo jingine kubwa lilikuwa ni mfumo wa vipimo ambao ulikuwa wa muhimu sana. Ingawa mabadiliko ya mbio za yadi 100 hadi meta 100 (ambayo yalifanya kuwa yadi 109.3) hayakuwa na shida kwa wanariadha wa Uingereza kiufundi, wengi wao waliona kuwa ni aina fulani ya aibu ya kitaifa. Haya yote yalipitishwa na Chama cha Michezo ya Olimpiki cha Uingereza na IOC na hivyo kurahisisha na kuharakisha sana uchunguzi na majadiliano jijini the Hague. Kikao kilikuwa kizuri. Kikiwa kimewekwa chini ya uangalizi wa mme wa Malkia na kufunguliwa na Waziri wa Mambo ya Nje, kikao kilifanyika katika mazingira mazuri ya amani katika mojawapo ya Ukumbi wa "kihistoria" wa Treve, ulioko Binnenhof. Tulimuona kwa mara ya mwisho mwenzetu mmoja maarufu Bw. Howard Vincent, ambaye alifariki ghafla kabla ya Michezo kuanza. Kwa mara ya kwanza, rafiki yake wa Hungaria, Bw. Jules de Muzsa, ambaye aliaminiwa sana, ilibidi asubiri mwaka mzima kabla ya kukubaliwa kuwa mwanachama kwa sababu serikali yake ilikuwa imemtuma The Hague, "akiteuliwa" kama mrithi wa F. Kemeny ambaye alitaka

kustaafu. Lilikuwa jambo gumu kwetu kuamini. "Siku ambayo IOC ingekoma kuwa chombo cha kujiendesha", ingepoteza umahiri wake: uhuru kamili. Wenzangu wote sasa waliaminishwa katika jambo hili na wakaichukulia fursa hii ya uchaguzi huru kuwa ndiyo msingi wa katiba yetu.

Michezo ya 4 ya Olimpiki ilifunguliwa kwa ufahari na sherehe kubwa mnamo tarehe 13 Julai 1908. Mfalme Edward VII na Malkia wake, wana wa Mfalme na Binti wa Mfalme wa Uswidi na Ugiriki na wanadiplomasia wote walihudhuria sherehe hiyo, ambayo ilikuwa ya kuvutia sana. Kwa mara ya kwanza, msururu wa wanamichezo elfu moja na mia tano ulipita ambao waliwekwa nyuma ya bendera zao kumi na tisa zikiwatakia kila heri kama ilivyokuwa imeelezwa kwenye Mkutano katika Ukumbi wa Michezo wa Kitaifa wa Ufaransa: karibu wote (isipokuwa Wamarekani) walikubali kuvaa mavazi yao ya michezo na mwonekano wote wa gwaride ulibadilika. "Lakini" kama ilivyoelezwa katika Jarida la Michezo ya Olimpiki la mwezi Julai 1908, hali ingekuaje endapo zingetumika kwaya za Uingereza badala ya bendi za jeshi. Kwa isivyo bahati, hili lisingewezekana. Niliendelea kushangazwa na ukosefu wa utashi wa miaka mingi kwa kuunganisha michezo na sherehe za ufunguzi. Ieleweke kwamba, wachongaji na wachoraji walikuwa hawahusishwi lakini suala la umma kutoelewa muunganiko wa michezo na sherehe za ufunguzi lilikuwa ni jambo lisiloeleweka. Hata hivyo, kulikuwa na maelezo katika upotoshaji wa uzuri na kuongezeka kwa ujuzi mzuri ambao maana *eurthmic* ya ilikuwa inapotea na kwamba maendeleo mazuri yalitufanya tuzoee mgawanyiko wa hisia. Elimu ya sanaa kwa watu inapaswa kurekebishwa na kuanzishwa upya. Nitarejea katika hoja hii na juhudi zangu za Michezo ya Olimpiki katika suala hili.


Kutokana na mtazamo wa kisanaa, kulikuwa na kuvunjwa moyo kwingine huko London. Mashindano ya sanaa ambayo *Royal Academy* ilikubali kuyaandaa, hatimaye yalishindikana. Badala ya kuwaruhusu washindani kuchagua mada zao wenyewe, ilionekana ni vyema zaidi kuzingatia miongozo. Kwa hili, uliongezeka ugumu mwengine wa usafiri na maonesho ya uchongaji. Kwa mara ya kwanza, wachongaji walionekana zaidi kuitikia wito.

Changamoto nyingine ilikuwa ni ukosefu wa mbio za farasi. Hata hivyo, yote haya yalihitaji kufanyiwa maandalizi vizuri miaka minne baadaye huko Stockholm. Kwa upande mwingine, tuliridhishwa katika mambo mbalimbali. Upangaji wa michezo haukuwa wa wazi sana. Bwawa la kuogelea lilikuwa limejengwa ndani ya uwanja wenyewe na majukwaa ya mieleka yalijengwa humo pia. Bwawa la kuogelea likiwa limezungukwa na mawe yaliyotengenezwa vizuri mithili ya chemichemi za Versailles, yakiwa na kifaa chenye ufundi cha kuinua mashua ya chuma ya kupigia mbizi na kuishusha tena wakati wa mashindano ili kutozuia watazamaji kuona michezo inayoendelea.

Jijini London, wanasarakasi waliheshimika sana na walikuwa maarufu sana kwa watazamaji. Kwa walio wengi, walikuwa ni kivutio. Wanasarakasi wa nchi za Skandinavia walikuwa wakishangiliwa kwa shangwe kubwa, "hawa ni kama ndege", kila mtu alishangilia hivyo. Mchezo wa mapigano ya kutumia panga ulikuwa ukiendelea upande wa kulia wa uwanja, katika mazulia makubwa ambayo yalikuwa yamepambwa vizuri. Katika mashindano yote haya, matokeo yalihamasisha sifa ya Michezo ya kimataifa. Tuzo za washindi wa michezo ya sarakasi zilichukuliwa na Mwingereza, Mfaransa na Wajerumani wawili. Nchi nne za Skandinavia zilishinda tuzo ya pamoja ya michezo ya sarakasi. Ufaransa na Hungaria zilishinda pamoja kwa mapigano ya kutumia panga. Wanamieleka ambao walikuwa 68, waliwakilisha nchi kumi. Walioshinda tuzo ni Mhungaria, Mufini, Muswidi na Muitalia.

Mchuano kati ya timu za Uingereza na Marekani kwa upande wa riadha ulikuwa ni mkali na timu zote mbili zilionyesha ari ya kushinda na hata mtu angedhani kwamba uadui wao wa kale umerudi tena. Mwanamichezo wa Uingereza na Marekani walinyakua mataji yote isipokuwa taji la mchezo wa urushaji mkuki lililonyakuliwa na Uswidi. Hata hivyo, Afrika Kusini na Kanada kwa kuzitaja chache, zilikuwa ni miongoni mwa washindi wa medani. Mgawanyo wa medani ulikuwa ni wa usawa kiasi cha kuridhisha sifa za kitaifa, japo hili halikuwa hivyo katika uhalisia wake. Wakati shauku inapopanda juu kwa kiwango hicho, matukio huweza kutokea. Kila upande uliutuhumu upande mwingine kwa kutokuwa na uchezaji mzuri. Tukio dogo tu lilikuwa likizua gumzo uwanja mzima kutokana na hali ya kimtazamo iliyokuwapo. Wakati wa kurudi nyumbani, pindi washindi wa Marekani wakipokewa kwenye Ukumbi wa Jiji la New York, walipanga mstari huku wakiwakejeli Waingereza wakisema "Simba wa Uingereza tumefungwa minyororo"! Hili lilisababisha kashfa kubwa ya kidiplomasia.

Kuanzia siku ya kwanza, Mfalme Edward alikuwa amewachukulia wanamichezo wa Kimarekani kama watu wa kipekee kwa sababu ya tabia zao na kelele za kishenzi ambazo zilikuwa zikisikika mara kwa mara uwanja mzima. Sikuweza kuielewa nia ya Sullvan hapa. Alieleza kuhusiana na kuchanganyikiwa kwa timu yake na hakuweza kufanya lolote la kuwatuliza. Hili lilifuatiwa baada ya kuonekana kwa usaliti mpya; alikishawishi Chama cha Wanamichezo wa Ridhaa kuiteua tume kwa madhumuni ya kuunda IOC mpya na kutengeneza sheria kwa ajili ya Michezo inayokuja. Lakini kipindi hiki, hakuna mtu aliyemsikiliza wala kumfuata katika jaribio lake la kutofautisha kati ya "Michezo faafu ya Olimpiki" na "michezo mingine". Kategoria ya kwanza ilijumuisha michezo ya mbio za miguu pekee, kuruka juu na kurusha vitu.



**23.** *Katika mavazi ya wakati huo, Pierre de Coubertin akicheza tenisi kwenye lie de Puteaux karibu na mji wa Paris, mnamo 1889. Pierre de Coubertin alikuwa katikati akiwa ameshikilia reketi yake kwa usawa.*


IOC haikuwa na haja ya kuhofia tena udanganyifu huo. Katiba yake kwa wakati huo ilikuwa hairekebishiki. Katika sherehe iliyoandaliwa na Serikali ya Uingereza na kusimamiwa na Bw. Edward Grey, nilipewa fursa ya kutoa maelelezo kamili kuhusiana na sera, mipango yake na vikwazo vya ndani ambavyo vililenga kuzuia mamlaka na matakwa yetu wenyewe. Kila kitu kilikuwa wazi na kulikuwa na uhakikisho wa mafanikio ya michezo ijayo.

Kulikuwa na idadi kubwa ya timu huko London. Kwa wanariadha peke yake, kulikuwa na dhifa sita ambazo zilikuwa na wageni kati ya 250 na 300, wanamichezo wengi sana na kulikuwa na mapokezi ya wageni kila mahali. Kwenye ufunguzi wa Michezo, huduma ya kidini ilitangulia kufanyika katika kanisa la Mt. Paulo wakati ambao Kasisi wa Pennsylavania alitoa mahubiri ya kutafakarisha sana.

Kwa wakati huu Michezo ilikuwa na sifa ya kujulikana kwa jina la "Michezo ya Msimu wa Baridi". Waliifanya mwezi Oktoba na walijumuisha masumbwi, kuteleza kwenye uwanja wa bandia, mpira wa miguu, mchezo wa hoki..... Haikuwa suluhisho bora lakini hisia kali zilizokuwapo nchini Uingereza kuhusiana na misimu ya michezo, ilifanya hiyo michezo iwe ya lazima. Kuhusiana na Michezo ya Baharini (mashindano ya mashua na kupiga kasia), hii iliadhimishwa kwenye Kisiwa cha Wight na Henley. Mashindano ya mashua (ya kuendeshwa kwa makasia au matanga) huko Henley haukuwa na masilahi ya kiufundi kwa kiasi fulani lakini ulipendeza zaidi ya ulivyokuwa ukidhaniwa. Haijalishi "udhoofishaji" huu wa polepole wa mpango wa jumla ungepaswa kuepukwa katika siku zijazo.

# X

## IOC Jijini Berlin (1909)



*24. Athene 1896, Willbald K.A. Gerbhadt na Pierre de Coubertin*

Wakati sasa ulikuwa umefika kwa Kikao kilichokuwa kikisubiriwa kwa muda mrefu cha IOC kufanyika jijini Berlin. Muda mfupi baada ya Michezo ya London, ambapo Wajerumani walipokewa kwa shangwe sana na baada ya muda mwingine kabla ya Michezo ya Stockholm, ambayo walitamani kushinda kwa kufanya kila linalowezekana, mchezo huo haukuwa wa kufurahisha sana kwao. Ujumbe wa Ujerumani ukijumuisha Jenerali Count von der Asseburg, Count C. Wartensleben na Dkt. W. Gebhardt, ulikuwa wa "Kimichezo ya Olimpiki" zaidi kuliko ulivyokuwa hapo awali. Jenerali huyo ambaye alipendwa sana na wenzake kwenye IOC, alifurahia fursa huko Berlini; fursa ambayo ilimwezesha kuendelea kuwa na umaarufu katika mkutano huo. Idadi ya wajumbe wapya walikuwa wamejiunga na IOC mnamo Desemba 1908. Katika kura ileile

tuliyoipiga: tuliichagua Marekani - ikichukua nafasi ya Jems Hyde ambaye alikuwa ameitumikia kwa muda tu. Allison V. Armour, mwendesha mashua maarufu, ambaye alikuwa nyota kwenye michezo ya kupiga makasia ya mjini  Kiel na rafiki wa karibu wa Keizer William; kwa Romania, George A. Plangino na kwa Uturuki, Selim Sirry Bey ambaye ni mwanamichezo mzuri na shabiki wa Ufaransa, ambaye hata hivyo alifanya kazi chini ya maelekezo ya Wajerumani. Wageni hawa wote wangefurahi sana kuwa na mkutano wa 1909 uliofanyika katika mji mkuu wa Himaya ya Ujerumani. Mwishowe, kwa mara nyingine, vikao vyetu havikuwa na ajenda yoyote hata ndogo ya kisiasa. Mpango wa Michezo ya 1912 huko Stockholm, kwa upande mmoja na tathmini ya ridhaa kwa upande mwingine, uliipa mwonekano pekee wa kiufundi. Kila kitu kilikuwa sawa. Kufikia mwishoni mwa 1908, Kikao kilionekana kuwa na mafanikio zaidi na kulikuwa na ushiriki binafsi wa Mwanamfalme, uendeshaji wa mikutano katika Jengo la Bunge, ambapo kila kitu kilionekana kufanikiwa vizuri.

Hata hivyo, mafanikio haya yalikaribia kuathiriwa na kifo cha Jenerali Von der Asseburg, ambaye alifariki ghafla tarehe 31 Machi baada ya kuugua kwa siku mbili. Kifo chake cha ghafla na kisichotarajiwa kabisa kilichotokana na kiharusi kiliniacha katika bumbuwazi kwa siku kadhaa. Uvumilivu sana ulihitajika kwa upande wa Warternsleben, ambaye bado alikuwa ni kijana mdogo na hata hakuwa mzaliwa wa Berlin, hakuweza kutuambia tuahirishe mkutano. Lakini kwa ujasiri wake alichukua nafasi ya aliyekufa, jambo ambalo lilinifurahisha. Baada ya hayo yote, lilikuwa suluhisho bora. Alizisimamia taratibu zote hizo kwa ustadi. Kila kitu kiliachwa kana kwamba kilikuwa kimetayarishwa na Jenerali, Wartensleben akapokea kijiti kama mwenyeji. Kuanzia tarehe 27 Mei hadi 2 Juni, vikao vya kazi na mapokezi vilifuata kwa haraka. Mwanamfalme, Kansela Bethmana-Hollowerg na Waziri wa Mambo ya Nje Von Schen waliisikiliza kwa umakini Kamati ambayo hata wao walipokewa na Mfalme siku ya mwisho. Ukaaji huo wa Berlin katika mazingira maalumu, kulinipa fursa ya kuona mambo mazuri sana, lakini haitakuwa rahisi kwangu kuyaelezea katika simulizi hizi za "Michezo ya Olimpiki". Ingefaa zaidi niyahifadhi kwa kumbukumbu zangu "binafsi" na kujizuia hapahapa kuelezea uamuzi mkubwa wa kiufundi wa mkutano. Katika kipindi cha vikao sita mfululizo vyenye shughuli nyingi, tulipiga kura kwa kauli moja kuunga mkono michezo kufanyikia Stockholm na tukaanza kusoma programu ya Michezo ya 1912. Kiuhalisia, uchaguzi wa mji mkuu wa Uswidi ulikuwa umeamuriwa kwa kupiga kura huko London mwaka uliopita. Wenzetu wa Ujerumani walijiondoa kwenye kinyang'anyiro cha michezo ya Berlin kama tulivyowatarajia kufanya hivyo, wakiiahirisha kwa njia isiyo rasmi hadi 1916. Hata hivyo, Waswidi ambao hawakupenda kujipendekeza na kujiingiza kwenye mtego bila kujua, walikuwa wametayarisha na kuwasilisha rasimu kamili ya utangulizi, wakikaribisha mjadala kuhusiana na masuala mengi muhimu.

Pengine lingekuwa wazo zuri kuelezea ni kwa namna gani, muundo upi na njia zipi programu za Michezo ya Olimpiki zilikuwa zimeandaliwa kwa siku zile kwa sababu

wanamichezo wengi hawakuwa wanafahamu lolote na mitazamo mingi potofu imechapishwa kuhusu jambo hili.

Mkataba mkuu wa Michezo ya Olimpiki haukubainisha majukumu maalumu kwa waandaaji au IOC, isipokuwa kwa makundi ya lazima katika michezo. Mkataba huu ulikuwa umeandaliwa na IOC kulingana na maelekezo yaliyotolewa na Mkutano wa Sabbone mwaka 1894. Makundi yanayorejelewa hapo juu yalikuwa ni kama ifuatavyo; wanariadha, wanasarakasi, michezo ya mieleka, michezo ya kuendesha mashua na michezo ya kupanda farasi. Lakini hakuna kilichoachwa kutokana na umbali au migawanyiko zaidi ya makundi madogomadogo, ambayo niliyafikiria kuwa baadaye yangekuja kuwa na michezo iliyounganishwa, daima inayofanana ambayo taarifa zake zingeandaliwa na mkutano wa IOC ikiwa na mwakilishi. Lakini mnamo 1909 Kamati za Kitaifa zilikuwa kwenye mchakato wa kuundwa: hakuna nchi yoyote iliyokuwa na kamati. Hungaria, Uswidi, Ujerumani, Bohemia na Uingereza, kama nikikumbuka vizuri, ndizo nchi pekee zilizokuwa na kamati nzuri. Sehemu kubwa ya nchi zingine, Kamati za Olimpiki zilikuwapo, lakini ama kwa sababu kuwapo kwake bado kulikuwa na wasiwasi au kwa sababu hazikuwa na mamlaka ambayo zilipaswa kuwa nayo, hivyo zisingeweza kutegemewa. Kuhusiana na mashirikisho yale ya kimataifa bado yalikuwa machache sana, yote yakikabiliana na matatizo ya kifedha na kwa sehemu kubwa, yakiwa na matatizo makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake. Yale mengine ya kitaifa yalikuwa yakipinga Michezo ya Olimpiki, yakidhani kuwa, Kamati za Kitaifa za Olimpiki zilikuwa mashirika pinzani na yalitaka kushughulika moja kwa moja na Kamati ya Maandalizi ya Michezo bila kujua ni mvurugano gani ungetokea. Michezo ya Olimpiki ilijumuisha mkusanyiko wa michezo yote, na kama isingekuwa hivyo waandaaji wa Kamati za Kitaifa za Michezo ya Olimpiki wangelazimika kuwasiliana sio tu na kila nchi bali pia kila kikundi cha michezo katika kila nchi.

Suala la Kamati za Kitaifa lilikuwa na utata mwingi. Kila kamati walikuwa huru kujiunda wengi zaidi au kidogo kadiri walivyotaka. Wakati fulani, tulikuwa na Kamati ya Kimarekani yenye wajumbe mia moja na Kamati ya Japani yenye wajumbe wanne tu. Hatukuingilia mchakato wa uundaji wala uendeshaji wao. Hata hivyo, tulilazimika kujiandaa kukabiliana na kamati kadhaa zilizokuwa zinapingana au kuzozana ndani ya nchi moja. Hali hii ilikuwa tayari imetokea Amerika Kusini. Je, katika hali kama hizi, tungemtambuaje aliye sahihi? Ili kuepusha matukio ya aina hii, nilitoa mwongozo ambao sikutaka tuutumie, lakini ambao kama ingelazimu ungeutumiwa na waandaji wa Michezo ili uwasaidie kuondokana na hali ngumu iliyokuwapo. Kwa mujibu wa mwongozo huu "kutambuliwa" kwa Kamati ya Kitaifa lilikuwa ni suala linalomhusu mwanakamati wake au mjumbe wa IOC kwa nchi inayohusika. Uamuzi wao ulikuwa wa mwisho. Tukiwa ni mamlaka huru, tulikataa kadiri tulivyoweza kulazimishwa kuutumia mwongozo huo, tukiamini kwanza mazungumzo ya kidiplomasia. Mara nyingi hali hiyo ilionekana kuwa ngumu, lakini kadiri muda wa Michezo ulivyokaribia, ingebadilika

yenyewe kutokana na hamu ya washindani waliochaguliwa kuhudhuria Michezo na shinikizo walilolileta kwa viongozi wao kuwafanya waisikilize hoja.

Haya yote yanaeleza sababu kwa nini IOC ililazimika kuchukua jukumu kubwa katika maandalizi ya kiufundi ya Michezo, tofauti na mawazo yangu ya mwanzo. Katika kipindi chote hiki, kuanzia 1896 hadi 1914 tulizihimiza Kamati za Maandalizi kuwasilisha programu zao (tulizozihamasisha mwaka 1896 na 1900 na baadaye kuundwa na wao wenyewe mwaka 1904, 1908 na 1912) kwa majadiliano na marekebisho ya makubaliano ya pamoja. Kwa ujumla, jambo hili lilichukua miezi kumi na minane hadi miaka miwili na wala isifikiriwe kuwa tulipuuza maoni ya mashirikisho na vikundi vingine vyenye uwezo. Pamoja na kwamba, baadaye kwa namna isiyokuwa ya moja kwa moja walishirikishwa ipasavyo na walikuwa na fursa nyingi za kutufanya tufahamu maoni yao, ambayo mara zote yalizingatiwa kila ilipowezekana, ilimradi walitumia njia zinazofaa kutoa maoni yao na hawakujaribu kuleta mabadiliko kwenye misingi mizuri ya taasisi.

Hivi ndivyo ilivyokuwa huko Berlin mwaka 1909 na huko Luxemburg mwaka 1910, ambapo programu ya Michezo ya Tano ya Olimpiki ilikuwa imeandaliwa kwa utondoti. Programu hiyo tuliihitimisha huko Budapesti mnamo mwaka 1911. Hakukuwa na Michezo ya Olimpiki kwa hapo awali uliokuwa umepangwa kwa uthabiti, umakini na uangalifu zaidi,… Kwa ule wa London, ingawa muda ulikuwa mfupi, sifa hizi zinazofanana zilionekana katika maandalizi. Hata hivyo, kwa Michezo ya Stockholm, wanakamati wenyewe walikuja. Kwa kawaida, maafikiano fulani yalipaswa kufanywa hapa na pale. Ikumbukwe kuwa, bado tulikuwa katika nafasi nzuri ya kumwambia mtu mwingine, "Una vyumba vizuri vya mapokezi. Tafadhali hebu tuvitumie kwa sherehe nzuri, kwa gharama zako". Mtindo huu wa kuiweka katika namna ya ucheshi, ambayo mara nyingi ilinifanya nicheke, ilibaki na itaendelea kubaki kweli. Itakuja kuonekana zaidi kuwa bado ilikuwa kweli kwa miaka ya 1920 na 1924. Katika mwaka wa 5 wa Michezo ya Olimpiki, ilitulazimu kukubali kushindwa kwa muda katika mchezo wa masumbwi. Sio tu kwamba mtazamo wa umma wa Uswidi haukukubaliana na mchezo huu, bali hata mechi za masumbwi hazikuruhusiwa kwa mujibu wa sheria za nchini Uswidi. Ingawa mchezo wa masumbwi haukuwahi kujulikana kwa uhalisia wake, katika mpango wangu wa "kielimu", niliendelea kuupa umuhimu mkubwa licha ya upungufu wake uliopo kwa sasa. Lakini katika hali hii ilitubidi tukubaliane. Uswidi kwa upande wake ilikubali kupitisha idadi kubwa ya maazimio, hasusani katika uga wa michezo ya sarakasi. Nilipoitembelea nchi hiyo mwaka 1899 kwa mara ya kwanza, sikuwahi kuamini kuwa, wanamichezo wa Ling wangekubaliana na hali hiyo kwa miaka kumi na miwili baadaye kiasi cha kuvumilia kuchezwa kwa michezo yote katikati ya Stockholm na kujengwa kwa majukwaa yaliyokuwa yakichukiwa hapo kabla katikati ya uwanja. Kwa ilivyo bahati, katika miaka hiyo kumi na miwili ya mageuzi katika michezo ya Uswidi, ambayo ilianza kwa wakati fulani hapo kabla, ilianza kuungwa mkono, kwa

kuhamasishwa na Mfalme na Mwanamfalme na zaidi kwa mwenzetu aliyekuwa maarufu na mwenye shauku ndugu Balck.

Zaidi ya hayo, Kamati ya Uswidi ilitoa maombi ya mchezo wa kuendesha baiskeli uondolewe kama ilivyo kwa mchezo wa masumbwi; maombi ambayo yalikubaliwa kwa sehemu tu kwa vile mbio za farasi ziliruhusiwa jambo ambalo nilifurahia kuona limeachwa japo si kwa mbio za barabarani. Kanuni ya mbio za marathoni iliibuliwa kwa mara nyingine tena lakini kila mtu alitambua kutoweza kuiacha. Mashindano ya michezo na sanaa ya wapanda farasi yalifanyika na kuyabadilisha kwa itifaki lakini kwa isivyo bahati yalikuwa yamekataliwa huko London. Sehemu kubwa ya kikao hicho ilitawaliwa na mijadala ya michezo ya ridhaa ambayo nitaielezea kwa kina kwenye sura inayofuata.

Muda mfupi baada ya mkutano wa Berlin, Dkt. W. Gebhardt, ambaye alikuwa amengoja hadi mwisho wa muda wa kustaafu, alitoa barua yake ya kujiuzulu na badala yake tukamchagua Baron von Venningen, mwanamichezo mahiri ambaye ni mwanachama maarufu. Gebhardt, ambaye alikuwa amechaguliwa mwaka 1895 alikuwa nasi kwa miaka kumi na minne na alikuwa amefanya mambo mengi.

Mwanzilishi mkuu wa Kamati ya Michezo ya Olimpiki ya Ujerumani alikuwa ameshawahi kuwa ni mkuu wa timu za Ujerumani mnamo 1896 na 1900 na Padri Kemeny, alikuwa aliiwakilisha IOC huko St. Louis. Muda mfupi baadaye, mwanachama wa pili aliyechaguliwa kwa ajili ya Italia alikuwa ni; Diwani wa Jimbo hilo Attilio Brunialti, mbunge na Makamu wa Rais wa Taasisi ya Mafunzo ya Mazoezi ya Viungo. Huyu alikuwa ni



**25**. *1909 Wajumbe wa IOC jijini Berlin (katika hatimlazo) waliopo kwenye sherehe za ufunguzi: 1. Count Cesar de Wartenstenbert (GER), 2. Count Brunnetta d'Usseaux (ITA), 3. Baron R. de Willbrand (FN), 4 Bw. Theodora Cook (GBR), 5 Mchungaji R.S. de Courcy Laffan (GER), 6. Prof. Reihard, 7. Lord Desbrough wa Taplow (GER), 8. Jenerali Victor Balck (SWE), 9. Kansela Atzrott, 10. Selin Srry Hey (TUR), 11. Count Clarence de Rossen (SWE), 12. Bi. Victor Balck, 13. Dkt. Martin 14. Count Geza Andrassy (HUN), 15. Bw. Muller, 16. J. Sverre (NOR), 17. Seneta Jules de Muzsa (HUN), 18. Kamanda J. Sverre (NOR), 19. Bi. Von Rosen, 20. Baron Pierre de Coubartin (FRA), 21. Bw. Allison V. Armor (USA), 22. Prof. William M. Sloane (Marekani), 23. Baron FW de Tuyll (HOL), 24. Baron Godefroy de Bloney (SU), 25. Barcness Pierre de Coubertin, 26. Bw. Von Hunefeld, 27. Count Albert Bertor de Sauvgny, 28. Countess Albert Bertier de Sauvgny, 29. Count Bertier de Sauvgny (eon), 30. Barcness Godefroy de Blonay 31. Bw. George A. Plagino (ROM) 32. Bi. George A. Plagino.*

mbadala muhimu kwa safu zetu. Wageni hao wawili walifanya kikao chao cha kwanza kwenye mkutano uliofanyika wakati wa Majira ya Vuli mwaka 1910. Mkutano huo ulipaswa kufanyika huko Budapesti, lakini nilikubali maombi ya wenzetu wa Hungaria ya kuuahirisha hadi 1911 kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wao. Nilifahamu kuwa, mkutano wa Budapesti ungekuwa suala la aina yake likiambatana na matukio mengi ya kijamii na nilitaka kuingilia kikaokazi kati ya Berlin na Budapesti, katika mji usioegemea upande wowote. Mji wa Luxembourg ulikuwa umeteuliwa tayari. Serikali ya Grand Duchy na baraza la mji walitukubalia kufanyia mkutano humo. Malkia wa Grand Duchess, ambaye kwa isivyo bahati hakuweza kuhudhuria mwenyewe, alituandalia dhifa nzuri sana kwa jina lake. Katika sherehe hiyo, Malkia huyo aliyowakilishwa na Bw. na Bi. Pescatore wa huko Chateau de Septfontaines, ilikuwa fursa yetu ya kupata mwanachama mpya kwa kuwa baadaye tulimchagua Bw. Maurice Pescatore, kama mwanachama wa Luxembourg kwa kipindi hicho akiwa Mbunge na mwenye haiba ya kupenda michezo zaidi ya wenzake. Tulimpoteza miaka kumi na tisa baadaye wakati mpanda farasi na mwindaji huyu asiyechoka alipofariki kwa ghafla na kabla ya wakati baada ya kuhuisha safari zake kwa kuitembelea Afrika kuanzia Mashariki hadi Magharibi. Nilishangaa na kufurahi kumsikia Waziri wa Nchi Eyschen, kiongozi mkuu wa Serikali ya Luxembourg katika hotuba yake ya kukaribisha IOC na kuipongeza kwa katiba yake. Hadi wakati huo, hatukuwa tumesikia lolote zaidi ya kukosolewa na wakuu wa mashirikisho ambao walivuruga malengo ya Kamati hiyo. Lakini baada ya kupitia vifungu vichache vinavyounda Katiba, Bw. Eyschen, ambaye aliheshimika sana kwa utashi wake wa kisiasa huko Ulaya, aligundua na kuthamini uhalisi wa utaratibu wake, ulivyoundwa vizuri ili kuhakikisha uhuru kamili wa Kamati na utetezi wa Michezo ya Olimpiki ya kisasa dhidi ya kila mtu na kila kitu. Kwangu, hili lilinitia moyo sana kiasi cha kukataa mielekeo fulani ya woga isiyokuwa na sababu ambayo nyakati fulani ilionekana miongoni mwetu.

# XI

## Michezo ya Ridhaa (1909)



**26.** *W. M. Sloane*



**27**. *Jules de Muzsa*

Hapa historia inajirudia tena! Ni miaka kumi na sita sasa tangu tulipodhani kwa haraka kuwa tumetatua tatizo lote, baada ya tatizo lilelile kujirudia tena kwa namna inayosumbua mithili ya polomaji unaoteleza na kunyiririka kutoka mikononi mwako. Binafsi sikujali sana. Ndiyo: leo naweza kukiri kuwa tatizo halikunisumbua sana. Limekuwa likitumika kama dira ya Mkutano ya kupanga na kuhuisha Michezo ya Olimpiki. Baada ya kuutambua umuhimu unaohusishwa nalo katika duru za michezo, siku zote nilionesha uchangamfu

lakini uchangamfu usiokuwa na matumani ya kweli. Mtazamo wangu kuhusu michezo pengine ulikuwa tofauti na ule wa wanamichezo wengine. Kwa upande wangu, michezo ni kama imani ya madhehebu yake, mafundisho, ibada,... lakini zaidi ya yote hisia za kidini zilinifanya kuwa na utoto unaofanya hayo yote nikitegemea mwanamichezo atapokea sarafu za faranga tano kama shemasi wa kanisa asiyetarajia kupokea mshahara kwa ajili ya kulitunza kanisa. Kwa sasa nimekomaa kiasi cha kutomnyamazia mzushi anayejitangazia uhuru. Siwezi kuwa na mtazamo wa aina hiyo. Hata hivyo, kwa lengo la kutafuta suluhisho bora zaidi, nilikubali kuwa mtu fulani alipaswa kuzingatia sheria na kuweka vizuizi fulani zaidi na nilifanya kila niwezalo kusaidia. Hususani Waingereza ndiyo waliguswa sana na suala zima. Hii ilikuwa ishara ya uimara wa IOC hasa walipoigeukia kuiomba msaada.

Mwaka 1902 ilitumwa hojaji iliyokuwa katika lugha tatu kwenda kwenye vilabu vyote na ilikuwa na mwitiko mdogo ambao haukuwa na matumaini. Baada ya Michezo ya London, "Baadhi ya Wanamichezo ambao waliishi kwa kutegemea Michezo” wakifurahia maisha katika ulimwengu wa michezo, walilichukulia uzito suala hili. Walidai kuwa, IOC pekee kwa mamlaka yake, katiba yake na mfumo wake wa kuajiri, ilikuwa na uwezo wa kulitafutia ufumbuzi suala hilo, jarida la Kiingereza lilianza kukusanya taarifa na maoni kuhusiana na suala hilo.

Miezi michache baadaye, faili kubwa lilitufikia likiwa na nyaraka zaidi ya 150. Baada ya kuzisoma kwa umakini kwa matumaini ya kupata kitu kipya, yote yaliyokuwamo, yalikuwa yalishasemwa siku za nyuma. Nilihisi kuwa tatizo halisi lilitokana na muundo wake pamoja na njia zilizotumika kulitatua; kila mtu alitaka kulitatua kabla ya kulielewa vizuri.

Mmoja wa Wafaransa wenzangu, Count Albert de Berrier, ambaye alikuwa mtaalamu sana katika masuala yote ya michezo – zaidi ya yote, ningesema, alikuwa anaipenda sana michezo, alikubali kuiwasilisha ripoti kwenye mkutano huko Berlin, ripoti ambayo tulifanyia kazi pamoja nyumbani kwake huko Compiegne.

Dhana ya mwanaridhaa ambayo ilikuwa imetumika kama kielelezo cha fasili nyingi katika nchi za Ulaya (ng'ambo ya Atlantiki), tayari ilikuwa imepitwa na wakati. Ilikuwa imetoka Uingereza. Ilibainisha kuwa mwanamichezo angekoma kuwa mwanaridhaa ikiwa:

1. angepokea tuzo ya fedha taslimu;
2. angeshindana na mchezaji wa kulipwa;
3. angepokea mshahara kama mwalimu wa michezo au mkufunzi;
4. angeshiriki katika "mchezo wa wazi" yaani wazi kwa washiriki wote.

Kinachoshangaza zaidi kuhusiana na hoja hizi nne ni utofauti uliopo. Ya pili inaibua mjadala mkubwa. Ya tatu inamlinganisha mwalimu au mkufunzi na mwanamichezo wa kulipwa (jambo ambalo kwa upande wangu sikuwahi kulikubali) kwa namna ambayo mmoja angeweza kuizungumzia kwa juujuu. Ya nne imepoteza maana yake yote. Ni mchezo gani "wa wazi kwa washiriki wote"? Ili kuielewa, mtu anapaswa kuisoma historia ya desturi na maisha ya kimichezo nchini Uingereza kwa miaka hamsini iliyopita. Kiuhalisia, ulikuwa ni muundo wa ulinzi wa kijamii na historia ya mfumo wa michezo.

Pamoja na kwamba hojaji ilikuwa imeshapitwa na wakati, hata hivyo ingeweza kutumika kama msingi wa utafiti wa suala linalotafutiwa ufumbuzi. Ilikuwa ni muhimu kuifikiria tena: fedha – mawasiliano - utekelezaji au ufundishaji na uhusiano uliopo baina ya mtu binafsi na kikundi.

Siku nyingine baada ya miaka mingi kupita, niliisoma tena ripoti ya 1909 na sikuweza kujilaumu kwa wakati huo kutokana na ripoti hiyo kutofanikiwa kujikwamua kwenye vikwazo vyote. Hitimisho lake lilikuwa wazi na la moja kwa moja. Kama wangeipitisha ripoti hiyo, tusingekuwa na changamoto nyingi, migogoro isiyokuwa na maana pamoja na kupoteza muda. Zaidi ya yote tungeweza, endapo tusingezuiliwa hasa kuingia kwenye kiota, angalau kudhoofisha sana aina hatarishi za wanamichezo ambao kwa baadaye walianza kueneza uzushi kama ule wa kipindi cha waasi wa Byzantine ulioongezeka katika kipindi cha Tertullia mithili ya nge wakati wa Majira ya Kiangazi kwenye Mto Nile. Vyanzo vyote vya moja kwa moja vyenye faida na thamani kubwa vililalamikiwa; kuridhika kwao zaidi kulihitaji ukiukwaji mdogo wa taratibu.

Kanuni ya utoaji upya wa sifa iliruhusiwa mradi tu itolewe na mahakama moja huru yenye uwezo wa kutoa dhamana mbalimbali kadiri iwezekanayo; aina ya namna hiyo ni Mahakama ya michezo ya The Hague. Kiapo kilifanyika kutokana na shinikizo la desturi; kiapo cha kina kilichoandikwa kwa ajili ya michezo ya kawaida; kiapo cha mdomo kilichotolewa mbele ya bendera ya kitaifa ya mwanamichezo wa Michezo ya Olimpiki. Gharama ziliruhusiwa kurejeshwa katika mazingira yanayoridhisha, mradi marejesho hayo yaligharamia tu usafiri, chakula na malazi na si matumizi ya starehe.

Tulikataa rasmi kuruhusu mwanamichezo ya ridhaa kunyimwa hadhi yake kushindana na mwanamichezo wa kulipwa na kushindana na mwanamichezo aliyefungiwa na shirikisho lake au kwa kushiriki katika mashindano ambayo "hayajaidhinishwa" na

shirikisho: kanuni za kijinga na za kipuuzi ambazo zilikuwa zimewekwa na zaidi ya shirikisho moja.

Hadhi ya kocha au mwalimu ilitofautishwa wazi na hiyo ya mwanamichezo wa kulipwa. Kanuni zilipendekezwa kutumika kama msingi wa sheria kwenye mawazo haya yote ya kimapinduzi, ambayo yalikuwa ya muhimu sana na yanayofaa kwa mustakabali mpya wa kidemokrasia na wa ulimwengu wote wa siasa ambao ulikuwa umeanza kufahamika kwa wenzangu wa IOC. Walikuwa na uhitaji mdogo sana wa kukubaliana na masharti haya mapya kuliko vile ilivyotarajiwa na wale miongoni mwa tabaka la juu hawakupewa nafasi kwa namna yoyote ile.



***28.*** *Akiwa na umri wa miaka 72, Coubertin alikuwa bado akipiga makasia jijini Geneva. Mwanamichezo shabiki aliyechapisha kitini kilichoitwa "La Cure de Veyron" cha 1926.*



***29.*** *Wakati wote alikuwa akipenda kupata uzoefu mpya wa michezo. Coubertin ameoneshwa hapa akiendesha guta, uvumbuzi mpya kwa wakati huo.*

Kwa upande mwingine, watu wengi walikuwa na wasiwasi na wakijua vyema maoni ya duru za michezo katika nchi yao wenyewe, walihofia mvutano mkali wa ana kwa ana. Waliomba marekebisho yafanyike kuhusiana na muundo angalau wa sehemu kadhaa za Ripoti. Nakala ambayo ilichapishwa kwenye Jarida la Michezo ya Olimpiki la Agosti 1909, lilikuwa ni toleo lililorekebishwa. Ningependa sana kuiomba tena nakala asilia kama ilivyowasilishwa kwenye IOC huko Berlin. Lakini haipo kwenye makavazi na sikufanikiwa kuiona.

Hofu hiyo niliyoitaja iliifanya Kamati iamue kuchukua idadi ndogo ya maswali kutoka kwenye Ripoti na kuyawasilisha kwenye mashirikisho na vyama vinavyohusika. Hatimaye, ifuatayo ni hojaji tuliyoituma kwa muhtasari:

1. Je, unafikiri haiwezekani kuwa mwanamichezo wa kulipwa katika mchezo mmoja na kuwa mwanamichezo wa ridhaa katika mchezo mwingine?

2. Je, unafikiri kocha au mkufunzi anaweza kuwa mwanamichezo wa ridhaa katika mchezo ambao haufundishi?

3. Je, unafikiri mwanamichezo wa ridhaa ambaye amebadilika na kuwa mwanamichezo wa kulipwa, anaweza asiwe mwanamichezo wa ridhaa tena? Je, unaruhusu kuwapo kwa hali isiyokuwa ya kawaida katika sheria hii? Kama ni ndiyo, kwa namna ipi?

4. Je, unakubali kuwa mwanamichezo wa ridhaa anaweza kurejeshewa gharama zake za usafiri na hoteli? Hadi kwa kiwango gani?

5. Je, unakubali kuwa mwanamichezo anaweza kupoteza hadhi yake ya uanamichezo wa ridhaa kwa kuwasiliana tu na mwanamichezo wa kulipwa?

Majibu ya maswali haya yatarejeshwa Bara la Ulaya kwa mwenzetu wa Hungaria Bw. J. de Muzsa; kwa Bw. Th.A. Cook wa Himaya ya Uingereza, na kwa Profesa W. M. Sloane wa Bara la Amerika. Huu ulikuwa mgawanyo uleule ambao niliuzindua mnamo mwaka 1891 na ambao ulionekana kufanya kazi.

Muda mwingi ulitolewa kwa ajili ya kuyasoma na kuyajibu maswali kwa kina. Hakukuwa na chochote kilichouharakisha mchakato huo. Haukufanyika hadi mwaka uliofuata, kwenye Mkutano wetu huko Luxemburg (Juni 1910), ambapo wenzetu walizirejesha nyaraka walizozipokea. Kwa isivyo bahati, majibu yalikuwa yanatofautiana sana. Siyo tu katika nchi moja kutoka kwa mchezo mmoja hadi mwingine, au katika nchi tofauti kwa mchezo mmoja, bali hayakuonekana kuwa na mwafaka hata kidogo. Maelezo mafupi; hakukuwa na sababu yoyote. Mambo ya kusadikika: hayakuwa na uhalisia, hayakuwa yamepangiliwa vizuri. Kwa kuliona hili, nilizikumbuka hisia za wasiwasi kwa wenzetu ambao walikuwa wakihofia kuchukua nafasi. Hata hivyo, walituepusha na shida nyingi baadaye, japo tangu wakati huo nilipoteza kabisa nia ya

dhati niliyokuwa nayo katika suala la michezo ya ridhaa. Nilirudi kwenye msimamo wangu kuwa, kocha na mwanamichezo wa kulipwa hawapaswi kuwekwa kwenye hadhi moja, kwamba ni kiapo, siyo jambo la kujionesha hadharani, lakini kwa maelezo ya kina yaliyotiwa saini, ilikuwa ni namna pekee ya kuwa na uhakika kuhusiana na historia ya mwanamichezo kwa sababu kusema uongo katika jambo hili lingeweza kumfanya afungiwe moja kwa moja. Tofauti za madaraja hazikupaswa kuwa na nafasi katika mchezo, muda umepita wa kutarajia mwanamichezo ajilipie gharama za usafiri na malazi, ambapo hali hiyo kwa mwanamichezo wa ridhaa haikuwa na uhusiano wowote na kanuni za utawala wa chama cha michezo. n.k., nk., nk …, kwamba hakukuwa na wanamichezo mamluki wa ridhaa waliofuatiliwa na kulaumiwa lakini wanamichezo wengi wa kulipwa walihusishwa na uongo huo ambao posho zao lazima zilitolewa, n.k.. nk.. nk.

Nimeandika nini! Kufuru! Kama vile kasisi wa Alphonse Daudet, akiacha kwa muda katikati ya wimbo wake na kunywa kinywaji, nahisi ninapaswa kusema: “Nihurumie”! Kama wafuasi wangu wangenisikia sasa!

# XII

## Jijini Budapesti (1911)



**30**. *1. Count Geza Andrassy (IOC, HUN), 2. Count Eugene Brunnetta d'Usseaux IOC, ITA), 3. Victor Balck (IOC, SWE), 4 Baron Pierre de Coubertin (IOC) President FRA), 5. Bi. Maurice Pescatore (LUX), 6. Bi. Victor G. Balck (SWE), 7. Seneta Jules de Muzsa (IOC, HUN), 8 na 9 Rais wa Baraza la Hungaria na mkewe, 10. Countess Clerence de Rosen (SWE), 11. Bibi Balck 12. Baron von Venningen (IOC, GER), 13. Mch. R. S. de Courcy Laffan (IOC, GER), 14. Angolo G. Bolanaki (IOC, Misri), 15. Kansela Attilio Brunnet (IOC, ITA), 16. Kansela Jiri Guth-Jarkovsky (IOC, Bohemeia), 17. Count Albert Gaurieer Vignsi (IOC, MON) 18. Count Caesar von Warternsiebern (IOC, GER), 19. Profesa William M. Sloane (IOC, Marekani), 20. Lord Desbrough wa Taplow (IOC, GER), 21. Allison V. Amour (IOC, MArekani), 22. Wajumbe wa Kamati ya Maandalizi, 23. J. Sigfrid Edstron (SWE), mjumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Michezo ya Olimpiki ya 1912, Rais Mteule wa IOC, 24. Selim Sim Bey (IOC, TUR), 25. Johan Svere (IOC, NOR), 26. Maurice Pescatore (IOC, LUX), 27. Kristian Hellostron (SWE) mjumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Michezo ya Olimpiki ya mwaka 1912, 28 na wajumbe 29 wa Kamati ya Maandalizi.*

Mwaka 1905 na 1911 ilikuwa miongoni mwa miaka yetu ya mafanikio makubwa. Mkutano wa Budapesti ndiyo uliokuwa kiini cha mjadala, lakini kazi tuliyoikamilisha, iwe ilihusiana na masuala ya huko au maeneo mengine zilihusisha maeneo mengi. Kwa yote yaliyopita, ningependa kuipongeza nchi ya Hungaria kwa kufanya vizuri tangu mwanzo, ikijidhihirisha yenyewe kuwa imekuwa mdau mkubwa wa Michezo ya Olimpiki na ikibaki kuwa ni mwanachama mwaminifu hadi leo. Kwa upande wangu Hungaria ilikuwa ni nchi rafiki. Polandi pamoja na urafiki wa muda mrefu kwenye michezo, ilikuwa imegusa maisha yangu ya utotoni. Hungaria ilikuwa nchi yangu ya ujana kama vile Uingereza na Marekani nchi ambazo nilikulia huko na baadaye Ugiriki na Uswisi nchi ambazo niliendelea kuwa na uhusiano nazo kwa muda mrefu. Nina mambo mengi ya kuwafanyia marafiki zangu kutoka nchi mbalimbali. Hawakuwahi kunikengeusha kwa namna yoyote ile kuipenda nchi yangu. Lakini kama vile ninavyoelewa umuhimu wa aina hii ya mtangamano wa kiulimwengu, kwa akili ya kawaida ni lazima mtu awe

mwangalifu dhidi ya mambo hatarishi ya kutoka nchi mbalimbali yanayotokana na kusafiri tu na athari zake za kutofungamana nayo.

Tuliingia jijini Budapest mwezi Mei 1911, tukikaribishwa kwa ukarimu wa hali ya juu sana. Kumbi nzuri zilikuwa zimeandaliwa kwa ajili yetu kwenye Jengo la Chuo cha Sayansi. Lilikuwa ni eneo hili ambapo Archduke Joseph, alisimama kwa niaba ya mfalme ambaye hakuwapo, kutoa hotuba yake ya ukaribisho baada ya ile ya Waziri Mkuu, Count Khuen-Hedervary. Mapokezi ya Eneo la wazi na dhifa zote ziliandaliwa na serikali na jiji, na kwa kumbukumbu zangu, sherehe nyingi za namna hii ziliambatana na miziki yenye sauti nzuri aina ya okestra za gipsi ambayo ilisikika masikioni mwetu wakati wote wa kukaa humo.

Wakati huo Kamati ya wajumbe arobaini na watatu iliundwa kutoka mataifa tofauti thelathini na moja. Hatimaye uundaji wa kamati hiyo ya uhakika ulikamilika, baada ya kuchaguliwa kwa watu wengi mashuhuri kama vile Baron Von Venningen na Count Sierstorpff wa nchini Ujerumani, Wakili wa Serikali Bw. Brunialt (wa Italia), Profesa na ambaye baadaye alikuwa Seneta Jigoro Kano, mfufuaji wa Sanaa za Kale (wa Japani), Baron Willebrand (wa Ufini), Jenerali Sir Hunbury William (Kanada), Messrs, Svere (wa Norwei), Bolanaki (wa Misri) na Evert J. Wendell (wa Marekani) ambao kwa muda mfupi wangeungana na Mwanamfalme Otto von Windschgraetz na Count Rundoff Colloredo huko nchini Austria. Wote au karibu wote, walikuwa wanamichezo kwa maana halisi ya neno hilo, kwa kuzingatia wazo nililolianzisha tangu mwanzo, yaani wanaume wenye uwezo wa kuchambua undani wa swali lolote lile, lakini zaidi ya hayo walikuwa ni watu wenye utaalamu wa kipekee ambao hawakuutegemea kwa kila jambo, watu wa kimataifa ambao wasingepofushwa katika jambo lolote la kimataifa kutokana na uzalendo kwa nchi zao, wanaume ambao walikuwa na uwezo wa kujisimamia wenyewe na kundi la kiufundi ambalo lilijitegemea lenyewe kwa hatua zote. Miongoni mwa wajumbe hawa wote, ambao tayari walikuwa wamezoea kukutana wakiwa wenye furaha kubwa katika mikutano yao ya kila mwaka, muunganiko wao katika utendaji wa kazi ulizidi kuimarika. Kipindi chote kilichokuwa kimebakia kabla ya mwaka kuisha, nilikuwa nikiwasiliana nao mara kwa mara.

Iliaminika na kudaiwa kuwa, ilikuwa namna rahisi ya kutukashfu kwamba wajumbe wote walikuwa "wameteuliwa" na mimi. Hakukuwa na ukweli wowote katika jambo hilo. Ni mjumbe mmoja tu kati ya wale wote niliowataja alikuwa mgombea wangu binafsi. Uchaguzi ulikuwa ukifanyika mara kwa mara, lakini uchaguzi halisi ulitanguliwa na uchunguzi wa muda mrefu, wakati mwingine yalifanyika mahojiano ya ana kwa ana na mhusika, lakini mara nyingi kwa kutumia mdhamini au wadhamini wake.

Aidha, watu walihoji sana kuhusiana na bajeti ya IOC. Kimsingi ilikuwa bajeti tofauti kabisa na nyingine yoyote. Hata hivyo, hili halikuifanya iwe ya kushangaza zaidi. Wakati watu walipofahamishwa kuwa usajili wa mwaka kwa kila mwanachama hauzidi faranga

ishirini na tano, hawakuamini. Hata hivyo, huo ndio uliokuwa ukweli na uwazi. Na kiasi hicho hakikuongezwa hadi mivutano ilipotokea. Kati ya hizi faranga ishirini na tano, ishirini zilikwenda kwenye Jarida la Michezo ya Olimpiki na tano zilienda kwenye mfuko wa IOC. Tozo za usajili wa Jarida la Michezo ya Olimpiki zilizokuwa na jukumu dogo sana zilipelekwa kwenye vilabu au watu binafsi ambao uungaji wao mkono ulionekana kuwa wa muhimu na bajeti yake yote ilitokana na tozo za matangazo. Gharama za uendeshaji wa ofisi ya IOC "ulimwenguni kote", zilikuwa ndogo sana. Nilikuwa nimetekeleza wajibu wangu binafsi. Kila mjumbe alijilipa gharama zake mwenyewe za kila mwaka na gharama zingine za ziada zilizojitokeza wakati wowote ambapo Mkutano ungefanyikia nchini kwake. Maneno kama haya yalipunguza ari ya wagombea wengi zaidi au wasiohitajika. Hakuna hata senti moja ya ruzuku iliyowahi kuja kwetu. Ni mambo mengi kiasi gani mtu angeweza kufanya, akiwa na rasilimali chache wakati akikataa kwa makusudi urasimu na utaratibu mgumu wa kiutawala, nyaraka nyingi pamoja na usumbufu wa wapiga chapa.

Mkutano wa Budapest haukuwa mzuri tu kwa namna ulivyoendeshwa. Vikaokazi vyake vinane vilihudhuriwa na wajumbe wengi sana. Tulihitimisha na ajenda ya programu ya Stockholm na ikiwa kwa sababu ambazo tayari nimezitaja, ilibidi tuachane na wazo la kujumuisha mchezo wa masumbwi, mafanikio matatu ya kiufundi yalifikiwa ambayo hayakuwezekana hapo awali. Kwanza kabisa, yalihusiana na michezo ya wapanda farasi. Haya yalikuwa yamejumuishwa tangu mwanzo. Hali nzuri ya mazingira ilikuwa imewafanya waachwe wakati wa mwisho kwenye programu ya pili huko Athene kwa sababu ya kushindwa kupata farasi kwa wakati. Majiji ya Paris na la St. Louis hayakuwa tayari kuongeza michezo ya mbio za farasi kwenye michezo mingine. Huko London, licha ya nia njema ya waandaaji, muda uliopatikana ulikuwa mfupi sana na ubaguzi fulani uliibua vizuizi. Hakuna kitu cha aina hiyo kilichotokea katika michezo ya Stockholm. Hata hivyo, jitihada za dhati na za muda mrefu ilibidi zifanywe. Mwenzetu wa pili wa Uswidi, Count Clarence von Rosen, alifanya kila kilichohitajika kwa shauku na bidii ambayo haikuisha kwa wakati huo. Katika ziara ya uenezi kote Ulaya, alifanikiwa kushawishi serikali zote na majeshi. Matokeo yake, "Michezo hii ya kwanza ya Kupanda Farasi" ilikuwa na sifa za kijeshi kwao na hii ingebaki hivyo katika michezo yote ya Olimpiki ambayo ingefuata baadaye. Lakini hili halikuweza kusaidia kwa kiwango chochote mwanzoni.

Ubunifu mwingine ulikuwa ni kuanzisha "mashindano ya kisasa ya riadha ambayo kila mchezaji alishiriki katika michezo mitano". Tayari nilikuwa nimewasilisha wazo hilo kwenye IOC katika hafla mbili zilizopita na pendekezo langu lilikuwa likikabiliana muda wote na ukosefu wa uelewa na chuki binafsi. Sikuwa nimeifafanua vizuri. Hata hivyo, wakati huu uelewa wa kuifahamu Nguvu ya Michezo wenzangu waliupata na wakalikubali tukio ambalo nililipa umuhimu mkubwa, uandaaji thabiti wa wanamichezo mahiri, mashindano ya kisasa ya riadha yaliyohusisha mbio za miguu, mbio za farasi,

kuogelea kwa nadra, michezo ya majukwaani na hatimaye, mashindano ya kulenga shabaha ambayo nilitamani yabadilishwe na kuwa mashindano ya kupiga makasia, japo hili lingeongeza sana ugumu kwenye maandalizi ambayo tayari yalikuwa na changamoto nyingi. Mashindano ya kisasa ya riadha yalipata mafanikio makubwa tangu wakati huo, bila ya dhamira yangu ya dhati kuwahi kutekelezwa: mienendo isiyoridhisha kwa washindani, matukio yaliyofuatana kwa mfululizo na kwa haraka bila kusimama, farasi waliotolewa na nchi inayoandaa michezo na kisha kuangushwa kwa kura katika dakika ya mwisho - na hiki ndicho nilichodhani kingeipa mwenendo wa kielimu sifa ya kiwango cha kwanza kabisa. Upinzani uliohusu kwenye madaraja ulizushwa polepole dhidi ya dhana hii ya mchezo na ukaishia kuwafanya waandaaji waliokuwapo kusahau kabisa kanuni zilizowekwa na mwanzilishi wa mashindano ya Michezo Mitano ya kisasa.

Mafanikio ya tatu ambayo ningependa kuyataja ni kuanzishwa kwa tuzo za uwindaji na upandaji milima mahiri uliokamilika tangu sherehe zilizopita za Michezo ya Olimpiki. Wazo hilo lilitolewa katika mkutano wa kwanza wa mwaka 1894 na tuliletewa kwenye mkutano kama mapendekezo. Nilitarajia lingekamilika baadaye kwenye tuzo ya tatu ya Michezo ya Olimpiki ya aina hiyohiyo ya usafiri wa anga. Haya yote yalikuwa na kaulimbiu ya; "*michezo yote, kwa mataifa yote*." Zaidi ya hayo, ilikuwa rahisi kuandaa na gharama yake ilikuwa ndogo,... Hata hivyo, katika mambo yote matatu, tofauti za wazi kabisa na nia ovu vilidhihirika; dakika moja watu wangeunga mkono na dakika inayofuata wangepinga, wakifichua udhaifu ulio bayana bila ya kuwa na malengo maalumu. Naamini kuwa, siku moja tutarejea kwenye mjadala wa wazo lililotajwa hapo juu. Maana lilikuwa ni zuri sana.

Hatimaye, Mashindano ya Sanaa pia yalifanyika miaka mitano baada ya programu hiyo kuandaliwa kwenye Mkutano wa Paris. Sheria na kanuni rahisi sana zilichapishwa katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani (Jarida la Michezo ya Olimpiki la Septemba 1911), lakini bila ya kusita kwa upande wa Kamati ya Uswidi ambayo Bodi ya Utendaji ya IOC ililazimika kuahidi msaada wake wa moja kwa moja wa kutuma mialiko. Baadaye nilisikia kwamba Wasanii na waandishi wa Uswidi walikuwa wameonesha upinzani mkali dhidi ya wazo hilo na nilipata fursa baadaye ya kulielezea kwa namna ya kushangaza ambayo imetufikisha hapa.

Ili kuwahamasisha washindani wa baadaye na ikiwezekana kuanzisha vuguvugu la kuunga mkono wazo hilo, tulifanya juhudi kubwa kwenye IOC mwaka 1911. Ni lazima nikiri wazi kuwa, watendaji wenzangu walipata ugumu kidogo kufurahishwa na sehemu ya mpango huu. Nilijikuta nikifanya kazi nyingi na kubeba gharama zote. Kwanza kabisa, shindano maalumu la usanifu lilipangwa huko Paris na nilifanikiwa kumshawishi Rais Fallieres kuwa msimamizi. Mada ya shindano hilo ilikuwa ni uanzishaji wa mipango ya "Olimpia ya Kisasa". Washindani wote waliandikishwa bila ya ubaguzi wa utaifa au kitu kingine chochote.

Mada ilikuwa imefafanuliwa na kutolewa maoni hapo awali katika mfululizo wa makala za Jarida la Michezo la Olimpiki; kuanzia Mwezi Oktoba 1909 hadi Machi 1910. Kwa hakika ilikuwa na matatizo mengi ya kiufundi na matarajio mbalimbali ya kuvutia wasanifu wachanga. Hata hivyo, mwitiko ulishuhudia ukaidi na hali ya kutojali kwa upande mwingine. Mbali na makala hizi zilizokusanywa katika majarida kwa madhumuni ya uenezi, Jarida lilichapishwa kwa mara ya pili mfululizo likiwa na kichwa cha habari kinachosema "(Mapambo, Fashifashi, Nyimbo, Maandamano)." Jarida hilo lilipelekwa kwenye vilabu vya Sanaa, shule, vikundi pamoja na majukwaa madogo ya "wasomi" ambayo yalionekana kulihitaji.

Wakati baraza la wazee la mashindano ya "Olimpia ya Kisasa" likiongozwa na Bw. Th. Homolle, ambaye ni mkuu wa zamani wa Shule ya Athene na kwa sasa ni mkuu wa makumbusho ya kitaifa ya Ufaransa, alitoa tuzo kwa mradi mzuri wa wasanifu wawili wa Vaudois (Uswisi), Bw. Eugene Monod na Bw. A. Lavarriere na IOC iliandaa sherehe kwa heshima ya washindi wawili wa tuzo; na zaidi ya hapo ilikuwa ni sherehe ya asili, nzuri na ambayo haijawahi kutokea. Ilifanyika usiku, katika uwanja wa Sorbonne uliojaa, licha ya hali ya hewa kuwa mbaya watu takribani elfu mbili walihudhuria. Nyuma ya



**31** *Cubertin kati ya 1930 na 1937 katika maktaba yake akiwa na binti yake Pienee*

pazia la kijani kulikuwa na bendi za okestra na kwaya. Ua wa nje ulikuwa umeanza kuingia giza. Mianga ya taa nzuri iliendelea kuangaza kwenye nguzo zote, huku ikitofautiana kwa kila moja katika wingi wake, njia na rangi mbalimbali. Programu ya muziki, miondoko iliyofanywa na wanasarakasi mia moja waliobeba mienge na mitende, ambao walicheza kama Okestra wenyewe na efibi kumi na sita, ambao mazoezi yao ya kimya yalichukua eneo la mbele la Chapel ya Richelieu, wote hawa walisaidia kutengeneza muunganiko mzuri wa sauti, mwanga, ukimya na taswira halisi. Uzuri wa usanifu wa mpangilio ulisaidia sana. Mwingiliano wa majukwaa ya enzi za kati na za

kisasa, msafara mdogo wa wapiga vinanda na wapiga zumari ulioandamana na wimbo wa King John's Ceremonial March ulioimbwa na Saint-Saens', "Mgiriki", ngoma za wanawake wa Kigiriki na kufuatiwa na uigizaji wa mchezo wa kupendeza wa Maurice Pottecher, uliojulikana kwa jina la "Mwanafalsafa na Wanamichezo". Sherehe hiyo ilihusisha michezo halisi ya mieleka. Yote haya yalifuatana kwa haraka hadi wakati wa kufungua, ambapo fashifashi zilizimwa kuanzia juu ya mnara hadi chini ya kuba, nyimbo za kwaya za Rumeau na Palestrina zilisikika kwa sauti kuu mbele ya watazamaji makini na wenye hamasa. Haya yote yalihitaji tu ushiriki wa vilabu vya sarakasi, shule ya michezo ya kupigana mapanga na vyama vya muziki vya wilaya moja ya Paris. Kwangu haikuwa tu utimilifu wa ndoto yangu ya pekee, bali upatikanaji wa uhakika kuhusiana na sanaa maarufu. Katika suala hili, ustaarabu ulikuwa umetoka kwenye njia sahihi na "ufufuaji wa mapigo ya muziki" peke yake ndio ungeyarejesha tena katika mwelekeo sahihi: mapigo ya muziki, sanaa iliyopotea ambayo watu huizungumzia sana bila kujua uhalisia wa jinsi ilivyokuwa siku za nyuma!

Idadi ya Majarida ya Michezo ya Olimpiki ambayo yana maelezo ya sherehe zilizofanyika tarehe 16 Mei, 1911 na wakati huohuo ripoti ya Kikao cha Budapest (kilichoanza wiki moja baadaye), vilikuwa na programu ya mwanzo ya Mkutano wa Saikolojia ya Michezo, ambao ulifanyika huko Lausanne mwaka 1913 na kutangazwa sherehe kubwa zitakazofanyika huko Paris wakati wa Majira ya Vuli ya 1914 kwa madhumuni ya kuadhimisha kumbukumbu ya miaka ishirini ya kufufuliwa kwa Michezo ya Olimpiki, wakati huohuo Mkutano wa wajumbe wa Kamati za Kitaifa, ulikutana kwa ajili ya kuandaa masharti ya kiufundi yatakayosimamia Michezo ya siku zijazo. Kwa hivyo, Budapest inaashiria kwetu uthabiti wa misingi ambayo tulikuwa tumeijenga kwenye IOC na ukubwa wa matarajio tuliyokuwa nayo baada ya kukamilika kwa jengo hilo; yote hayo nilijaribu kuyaeleza kwa kuandika kwenye medali mpya kaulimbiu ambayo nilitarajia kuiona ikichukua nafasi ya "*Utimamu wa Akili, Uthabiti wa Mwili*" *(Mens sana in corpore sano)* ambayo kuwa "*bora kiafya*" ulibakia kuwa "utatibu uliopendekezwa kwa matarajio ya vijana "Akili Iliyochangamka kwenye Mwili wenye Mazoezi" *(Mens fervida in corpore lacertos)* ambao walianzia hapa. Gazeti liliandika kwa utani, "Wanamichezo" "watakuwa na wakati mgumu kujaribu kupata usawa kati ya bidii ya akili na uthabiti wa mwili. Itakuwa: kama vile kuruka kwa ndege: mtu anaweza kuanguka kutoka humo, mwingine anaweza hata kujiua, lakini mwisho wake ni ushindi na kwenye mabawa mawili ya ndege ambapo kila upande, kwa wale ambao hawataanguka walikuwa na fursa pengine ya kuifikia Olimpiki kamili.

Kabla ya kuumaliza mwaka 1911, lazima niizungumzie ziara yangu ya Uholanzi. Baada ya kuwasili Brussels na Antwerp na kukaa muda mrefu kidogo, huko the Hague na Chuo Kikuu cha Lyden, nilihudhuria mkutano wa Marais wa vyama vya michezo vya Uholanzi huko Amsterdam na mwisho wa chakula cha jioni kilichoandaliwa na mwenzetu van der Tuyll, nilikuwa nimefanya makubaliano naye kuhusiana na hatua za mwanzo za

majaribio kuelekea kwenye sherehe zijazo za Michezo ya Olimpiki nchini Uholanzi. Nilifikira kuwa, huu utakuwa ni uzoefu mzuri na wenye manufaa makubwa. Miji mikubwa ya ulimwengu haikufaa sana kwa matukio kama haya. Miji ya The Hague na Amsterdam yote ilifaa zaidi. Lakini Waholanzi walionekana kuwa na shauku ya kuiona miji yao ikichaguliwa wakati huohuo wakiwa na wasiwasi kuona miji yao ikibebeshwa majukumu. Jambo hilo lilijadiliwa katika makala fupi iliyochapishwa kwa Kiholanzi katika Jarida letu. Kuanzia hapo uwezekano ulibakia kwenye upeo wa macho na ili kuendelea kuwa pale tulibahatika kuwa na F. W. van der Tuyll bingwa aliyeaminika zaidi na mwenye ushawishi mkubwa wa mashindano. Miaka kumi na minane baadaye, hali ya uwezekano ilikuwa halisi. Kwa isivyo bahati, hakuwapo tena mahali hapo ili kuyafurahia mashindano.



# XIII

## Michezo ya Tano ya Olimpiki (Stockholm, 1912)



**32**. *Stockholm 1912, Mhe. Rais wa Kamati ya Maandalizi Mwanamfalme Guatay-Adoff, akitoa hotuba yake kwenye ufunguzi wa sherehe, nyuma yake wajumbe wa IOC ambao ni Pierre de Cubertin (akiwa na fimbo yake ya kutembelea), Victor G. Balck, Sigfrid Edastrorn, Jules de Muzsa, Attilio Brunalt, Miguel de Beistegul, Count Clerence de Rosen, Count Brunnertt d'Usseaux, Jiri Guth-Jaskovsky, Maurice Prescatore, Angelo C. Bolanaki na Mch. R.S. de Courcy Laffan.*

Ni mambo machache tu yaliyokuwa yamebakia ili kukamilisha majaribio ya kuchukua nafasi ya IOC kwa kuanzisha shirika jipya la kimataifa. Tarehe 27 Februari, 1911 Sloane aliandika kunitaarifu kwamba, Sullivan hakuja tu kuona ubatili wa kazi kama hiyo bali pia kwamba alipoalikwa kujiunga na mashabiki kindakindaki ambao bado walikuwa na ndoto kuhusiana na jambo hilo, alikataa na hata alijitahidi kuwakatisha tamaa. Kwa upande mwingine, mashirikisho yalikwepa zaidi kukabiliana na ukweli. Mnamo 1909, Chama cha Waendesha Baiskeli wa Kimataifa kilikuwa kimetangaza azimio lake la kukataa aina yoyote ya kushiriki katika "Kamati za Michezo ya Olimpiki ya Kimataifa" na kujiwekea uwezekano wa kushiriki katika "yale mashindano yaliyokuwa yamepangwa kufanyika Athene." Lakini kamati ya Ugiriki ambayo ilikuwa inatarajia kusherehekea Michezo ya kati chini ya mwamvuli wa Akropolisi mwaka 1910, tungeongeza msaada wetu wa uwajibikaji kwa mwaka 1906 ambapo tulilazimika kuliacha wazo hilo. Hii ilitokana na ukosefu wa pesa na mdororo wa kiuchumi. Kutoka Athene, tulipokea pendekezo lisilo rasimi la kuujumuisha mfululizo wa Waathene katika mzunguko wetu

wenyewe. Michezo ingeadhimishwa kila baada ya miaka minane nchini Ugiriki na kila baada ya miaka minane katika nchi nyingine. Haikuwezekana kukubaliana na pendekezo hili. Ingekuwa na maana ya kufanya kazi yetu wenyewe bila manufaa yoyote ya kweli. Hali ya siasa za kimataifa ilikuwa haijatengemaa kuchagua uwanja kwa muda mrefu ujao wa kufanyia Michezo. Ilikuwa muhimu kwa IOC kulinda uhuru kamili wa kuchukua hatua katika suala hili pia.

Baada ya waendesha baiskeli, ilikuwa zamu ya wapiga makasia kujaribu mbinu zao dhidi ya IOC kwenye Mkutano lililofanyika Lucerne kuelekea mwisho wa 1908. Aidha, hata hawa hawakuweza kushinda. Wakati mashirikisho yakilazimika kutambua kutofaulu kwa mashambulizi yao, Kamati za Kitaifa za Olimpiki zilikuwa zikiimarisha nguvu zake. M. Bolanaki na Count Gautier Vignal walikuwa wameunda kamati nchini Misri na Monako, huku Khedive na Mfalme wa Monegasque wakikubali kuwa kama Marais wa Heshima. Kamati za Uingereza na Ujerumani sasa zilikuwa zimeanzishwa. Hivyo ndivyo ilivyokuwa pia kwa nchi ya Hungaria. Kamati ya Marekani, chini ya uongozi wa Kanali Thompson na Sullivan kama Katibu wake, ilikuwa nayo imeanza kuimarika hatua kwa hatua. Kamati zote za Ubelgiji, Denmark na Uhispania (ya mwisho kati ya hizi tatu ilikuwa imeundwa hivi karibuni na wenzetu Marquees wa Villamejor, ambaye ni ndugu yake na Count wa Romannes), zilikuwa zikifanya kazi vizuri. Kanali S. W. Djoukitch alikuwa ametoka tu kuunda moja nchini Serbia. Kulikuwa na kamati huko Australia, Kanada, Uholanzi, Italia, Japani, Norwei, Ureno na Romania. Wafaransa na Waswisi pekee ndio walionekana kuwa na shida kidogo katika kujipanga. Hata hivyo, walifanikiwa kupata suluhu bila kuyabughudhi mashirikisho ya ndani kwa upande wa yale ya zamani na yale ya baadaye kwenye majimbo huru.

Pia kulikuwa na kamati za Cheki na Ufini. Kwa kweli, ya kwanza ilikuwa ni kongwe. Ilipangwa kuanzishwa mwaka 1899 na ikaundwa mwaka wa 1903. Daktari Jiri Guth-jarkovsky alikuwa ameingiza kwenye katiba ya kamati hii vipengele vya uvumilivu ambavyo kwa uzalendo wake wa Kicheki, angeweza kuvimudu. Alikuwa amefanikiwa kumshawishi si tu Bw. Srb, Meya wa Prague, ili awe Rais wa Heshima wa kamati hiyo, bali pia Mwanamfalme Lobkowitz kuwa msimamizi wake. Kwa upande wa Ufini, ingawa kamati yake haikuwa kongwe sana, ilikuwa imehusishwa na uhuru wa kitaifa na kufikia mnamo mwaka 1908 tulimchagua mjumbe wa Kifini, Baron von Willebrand. Sasa mambo yalikuwa yakienda kasi. Michezo ya Olimpiki ilianza kuhusishwa na masuala ya kiserikali. Familia za kifalme zilikuwa zikihusika na serikali pia.... kiasi kwamba katika mji wa St. Petersburg na huko Vienna, vishindo vya michezo hiyo vilikuwa vimeanza.

Kwa bahati nzuri, matatizo mengi yaliweza kutatuliwa bila ya ugumu wowote huko Austria. Badala ya kuwashambulia Wacheki pekee, Waustria waliwageukia Wahungaria pia. Jambo dogo tu la mpangilio wa alfabeti. Hivyo, ili wasilalamikiwe kwa kukipendelea Kiingereza au Kijerumani badala ya Kifaransa, Waswedeni waliamua kutumia lugha ya Kiswidi - ambayo hakuna mtu mwingine aliyeelewa isipokuwa wao wenyewe tofauti na

ilivyokuwa kawaida. Kwa hiyo, magazeti yalijadili mapema mpangilio wa alfabeti ambao wanamichezo wangeunda gwaride moja siku ya ufunguzi. Waziri wa Austria huko Stockholm, baada ya kufahamishwa mapema kuhusiana na jambo hili dogo, aliiambia Vienna kwamba ili kufanya mambo yawe sawa, wanamichezo wa Austria na Wahungaria walipaswa kuunda kikosi kimoja cha gwaride. Kansela wa Kifalme alikubaliana naye, na akayaarifu mamlaka ya Stockholm kwamba, hivi ndivyo ilivyopaswa kufanyika. Kwa wakati huo Wahungaria, walilichukulia tofauti jambo hili kwenye masuala yanayohusiana na haki zao kwenye Michezo ya Olimpiki na tarehe 19 Januari, 1912, Bw. von Muzsa aliiarifu Uswidi, kwa niaba ya Kamati ya Kitaifa kwamba, timu yao ingejiondoa kwenye Michezo ikiwa agizo hili lingeendelea kutekelezwa. Lilikuwa jambo la kushangaza sana kubadilishana taarifa nyingi za kidiplomasia. Hatimaye, Kansela aliamua kusalimu amri kimyakimya.

Kwa wakati huo, wanasoka wa Austria kwa miezi kadhaa walikuwa wakidai kutengwa kwa timu za Cheki na kujaribu kuwahusisha Wajerumani katika ugomvi wao. Kilichofanya hali kuwa ngumu zaidi ni kwamba ndugu yetu ambaye alikuwa mgeni, Prince von Windischgraetz, kwa kufunga ndoa yake na Bintimfalme Elisabeth, tayari alikuwa mjukuu wa Mfalme Franz-Joseph na kwamba kwa maoni yake mwenyewe na hulka za usuluhishi, kutokana na hali ile asingeweza kumpinga Kansela wake, ambaye alitaka kuondolewa kwa jina la Bohemia kutoka kwenye orodha ya nchi za Olimpiki. Zaidi ya hayo yote, nilipokea barua kutoka kwa Balozi wa Urusi mjini Paris, Bw. lswolsky, vilevile akitaka kuondolewa kwa Ufini kwa niaba ya "Wizara ya Mambo ya Nje".

Kulikuwa na pande tatu kwenye jambo hilo. Uundaji wa Kamati ya Michezo ya Olimpiki ya Kimataifa ulihusika kwa kiasi fulani, kisha uundaji na utaratibu wa maandamano ya vikosi vilivyoshiriki katika Michezo na hatimaye kuinuliwa bendera endapo ushindi utakuwa kwa mwanamichezo wa Cheki au Ufini. Wakati wa kuyapokea maandamano ya kwanza, kamati ya Uswidi ilikuwa imetoa tamko la wazi zaidi kuwa, lilikuwa ni jukumu la IOC kuamua na kwamba uamuzi wa mwisho ungeheshimiwa. Wenzangu kamwe wasingeruhusu wajumbe wawili kati ya waliokuwapo kulazimishwa kujiuzulu, japo suala lenyewe halikufikia hatua hiyo. Si Dkt. Jiri Guth, wala Baron von Willebrand aliyekuwa katika mazingira magumu ya kufikia uamuzi huo. Kilichokuwa kinatakiwa ni kwamba, kinyume na majina yao kwenye orodha ya IOC, neno Austria lilipaswa kuandikwa badala ya Bohemia na Urusi badala ya Ufini. Kwa hiyo, kila mtu alikuwa akingojea uamuzi wa IOC na wajumbe wa IOC walikuwa wakingojea ule wa Rais wao.

Nilikuwa katika hali ya sintofahamu kwa sababu, upande mmoja kulikuwa na ukweli wa kisiasa usiopingika na kwa upande mwingine, sababu ya haki na shukurani tulizokuwa nazo kwa nchi zilizotuunga mkono kwa dhati. Hata hivyo, hisia zangu zilipaswa kuegemea upande wa pili kwa vile nilijikuta nazitekeleza. Kama ningekuwa huru kufanya hivyo, ningelitoa eneo lao wenyewe si kwa Bohemia na Ufini tu bali pia kwa

Polandi na Irelandi. Bila ya shurti, kabla ya barua iliyotarajiwa kufika kutoka kwa Warusi, Ufini iliwekwa kwenye orodha baada ya Urusi na Bohemia kuwekwa kati ya Austria na Ubelgiji. Nilianza mjadala mrefu ambao niliuendesha kidiplomasia kwa kadiri nilivyoweza. Nilitahadharisha kuhusiana na makubaliano hayo, nikionesha kuwa Mfalme wa Urusi alibeba kati ya majina mengine ya Grand Duke wa Ufini, Mfalme wa Austria na yale ya Mfalme wa Bohemia na hii ndiyo sababu nchi hizi mbili zilikuwa zikifurahia mamlaka ambayo yalikuwa tofauti na yale ya nchi nyingine zilizokuwa na uhuru mdogo; zaidi ya yote, niliendelea kurejelea kwenye ukweli usiopingika wa "Mazingira ya Michezo", ambayo ilikuwa tofauti kabisa na mazingira ya kisiasa: nilibadilisha njia ambayo tuliitumia kuamua kuipendelea Bohemia na Ufini na kukataliwa kwa maombi ya Sokols la Krosha (Croatia) ambayo yalikuwa yametolewa mwaka jana na ambayo hatukuyazingatia kuwa yaliegemezwa kwenye misingi thabiti... Lengo langu kuu kwa wakati huu lilikuwa ni kucheza kwa muda na mwishowe kwa makusudi nililichanganya suala hilo kwa kuliandikia mara moja jimbo la St. Petersburg au moja kwa moja kwenda Vienna, wakati mwingine kwenda Stockholm na mara nyingine wakati wa matukio mengine kwenda kwenye kamati za kitaifa. Kwa haraka niligundua kuwa, jambo hili lilikuwa likisababisha kero kubwa siyo tu kwa Bw. lswolsky bali pia kwa Wizara ya Urusi na kwa kweli jimbo la St. Petersburg liliishia kwa kutuacha peke yetu. Kwa upande wa jiji la Vienna ambalo lilikuwa likisumbua zaidi, hatimaye tulilazimika kukukubali kwa makubaliano na kamati yenyewe ya Cheki, ambayo herufi zake za mwanzo (COT) ziliendelea kuonekana pekee kwenye orodha kama ukumbusho na matarajio. Suala la bendera lilitatuliwa kama ifuatavyo: endapo ushindi utapatikana, taa za rangi zingewashwa kuelekea bendera ya Cheki au Ufini na taa zingewashwa kuelekea kwenye bendera za Austria au Urusi. Na hivi ndivyo bendera ya Urusi ilivyopandishwa katika sherehe za ushindi! Hotuba niliyoitoa mwenyewe, ilinipa furaha ya kumwambia Jenerali Woyeikof mwishoni mwa Michezo. Kwani Jenerali huyu maarufu wa Uwanja, ambaye jukumu lake mwanzoni mwa mapinduzi lilikuwa la kujadiliwa sana, alikuwapo. Alikuwa amesafiri kwa meli ya kivita ili kuhudhuria Michezo hiyo, akiongozwa na ujumbe mkubwa au maofisa vijana na hata akiongozana na okestra ya balalaika - kwa furaha kubwa ya Grand Duchess Maria, mke (baadaye mtalaka) wa Mwanamfalme William wa Uswidi, ambaye alikuwa ni mzalendo wa Urusi.

Maelezo haya ambayo yalifupishwa, yalionesha kwa kiasi kikubwa kwamba Michezo ya Tano ya Olimpiki kama waridi la kupendeza zaidi, kwa upande mwingine lilikuwa na miiba! Kwa kweli ni mtandao tata ulioje wa changamoto za kidiplomasia, fitina ndogo za kibinafsi, kupaswa kuwa mvumilivu licha ya shuruba zilizopo na zenye hila za chinichini. Ilibidi mtu awe na tahadhari wakati wote ili aweze kuona matukio yanayokuja ili aweze kuyazuia kabla hayajatokea. Matukio haya yalikuwa miiba. Lakini ninawezaje kulielezea ua la waridi? Lina mwonekano mzuri kiasi gani! Kamwe haikuwahi kutokea wakati wa Majira ya Kiangazi ya Uswidi yakapendeza kiasi hiki. Kwa wiki tano mfululizo, uoto wa asili ulipendeza sana, jua lilikuwa likiangaza, kukiwa upepo mwanana wa bahari na

usiku wenye mbalamwezi, mitaa yenye mianga ya taa za kuvutia na maua kila mahali. Katika mazingira ya mazuri ya jiji, furaha ya jumla ya vijana haikuwa na kifani. Kulikuwa na muda mfupi wa kulala, lakini hata hivyo hakuna mtu aliyetaka kulala. Kulikuwa na mfululizo wa sherehe bila ya kuonekana kwa athari yoyote mbaya. Uwanja wa Kigothi, wenye matao na minara iliyochongoka, uzuri wake wa kiufundi, kanuni na taratibu zake zilizopangika vizuri, ulionekana kuwa wa kipekee. Kutegemeana na mahitaji yaliyokuwapo, ukumbi huo ulifanya kazi kama ukumbi wa sherehe, ukumbi wa tamasha, ukumbi wa michezo na ulikuwa tayari kila wakati asubuhi katika matukio mengine ya kimichezo. Wakati wa jioni moja tuliuona ukiwa umefunikwa na miraba ya nyasi zilizowekwa kando, zikiwa zimetandazwa vizuizi na kupambwa kwa ukingo wa maua kwenye michezo ya wapanda farasi. Kila kitu kilifanyika kimya, haraka na bila makosa. Ingawa huko London maisha ya jiji hilo kubwa hayakuwa yameathiriwa na kuingia kwa Michezo ya Olimpiki, jiji lote la Stockholm liliathiriwa nayo. Jiji zima lilishiriki katika juhudi hizo kwa heshima ya wageni na tuliona kidogo jinsi picha ya Mji wa Olimpia ulivyokuwa enzi hizo, ingawa kwa kiwango kikubwa, lilipambwa na kuimarishwa na uwapo wa huduma na vifaa vyote vya kisasa, bila ubaya wowote ambao ungewashtua, kiasi kwamba michezo ya kale ya Ugiriki na michezo ya kisasa vilionekana kuwa vimeungana kutenda kama wenyeji wa michezo kwa pamoja.

Mwanamfalme alikuwa akizunguka kila mahali, bila kuchoka, akiwa mwenye busara, mtendaji, akitabasamu kila wakati na kamati yake iliendana naye. Balck alitawala eneo hilo kwa mwonekano wake maalumu, ukamilishaji wa juhudi zake za hapo awali za kuishawishi nchi yake ijiunge na michezo ya kila aina bila kukataa kwa vyovyote vile michezo ya sarakasi asilia. Na hata kama bado kulikuwa na watetezi wachache wasiokata tamaa wa itikadi hii ya kipekee, ilisemekana wamekimbia Stockholm ili wasivione vifaa vya itikadi hii kubwa iliyoanzishwa hapo na maoni ya umma yalikuwa sawa na yale ya Balck.

Nikilisoma Jarida la Michezo ya Olimpiki la mwaka 1912 ambapo sasa lina mwaka wa saba tangu kuwapo kwake na zaidi likijita kuelimisha, niliona kuwa idadi yote ya majarida ya mwezi Juni ilitengwa maalumu kwa ajili ya Uswidi na kwa kuzingatia historia yake ya zamani na kutazama hali yake ya sasa, iliyokamilishwa na nukuu zilizochaguliwa vizuri kutoka kwenye kitabu kizuri kilichochapishwa hivi karibuni na Andre Bellesort. Idadi hiyohiyo pia ilikuwa na akaunti ya shirika la michezo la Uswidi. Uswidi haikutumia gharama au jitihada yoyote kuwapokea vijana wa ulimwengu wa pili. Na ilikuwa inafaa kwa vijana katika wakati wao kunufaika na somo walilojifunza nchini Uswidi… Mtazamo ulianzishwa katika toleo lililofuata la Kiingereza, lenye kichwa cha habari "*Pax Olimpica*"; hotuba yenye maadili mazuri iliyoandikwa na Laffan, ambayo ilikuwa ya muda kitambo uliopita na wakati huohuo ikihimiza uzingatiaji wa kanuni kuu za kuvumiliana na kuheshimiana tulizopewa na Michezo ya Olimpiki ya watu wa kale, hotuba ambayo mvuto wake ni wa siku za nyuma sana, kamwe haikuwapo hapo awali

hotuba ya namna hiyo ambayo ilivuta hisia za wanamichezo wengi. Hii ilifuatiwa na ripoti ya mashindano ya kisanii na kifasihi. Matokeo hayakuwa mazuri sana na yalidhoofishwa zaidi na msisitizo wa wasanii wa Uswidi wa kushughulikiwa tofauti na kufanya maandalizi ya shindano lao la pili, matakwa ambayo tulifanya makosa kuyakubali ingawa ubaya na kutofaa kwake kulipaswa kutufanya kukataa kwa njia sahihi. Hata hivyo, mashindano ya kwanza yalifanyika, tuzo zilitolewa na kazi za kushindania tuzo zilioneshwa. Ilikuwa ni hatua ya kwanza katika mwelekeo sahihi ambayo ilikuwa ni ya muhimu sana.

Toleo la mwezi Agosti lilihusisha kumbukumbu za Kikao cha lOC kilichoanza tarehe 4 Julai, katika Ukumbi wa Seneti wa Jengo la Riksdag, mbele ya Mwana na Bintimfalme, pamoja na wajumbe wengine wa familia ya kifalme: Kikao kilichokuwa na mahudhurio mazuri sana: wenzetu wote wa Uingereza, Marekani, Ujerumani, Italia na wale wa Australia na Hungaria walikuwapo. Mwenzetu wa Japani alishiriki kwa mara ya kwanza. Michezo ya 6 ya Olimpiki ilipaswa kusherehekewa huko Berlin: Kansela wa Reich ya Ujerumani alituma salamu za Kaiser. Kila kitu kilionekana kushawishi. Kufikia wakati huo Mkutano wa Paris ulikuwa umeandaa programu na kanuni za mwisho.

Toleo la mwezi Julai lilichapisha matokeo ya Michezo. Marekani walikuwa wameshinda tuzo 26 za kwanza, Swedeni 23, Uingereza 10, Ufini 9, Ufaransa 7 na Ujerumani 5. Na baadaye ikafuatia Italia, Hungaria Norwei, Afrika Kusini, Kanada, Ubelgiji, Ugiriki, Uholanzi, n.k.

Kulikuwa na mashindano mawili ya riadha ambayo kila mchezaji alipaswa kushiriki katika michezo mitano (pentathloni): ya kwangu yalikuwa ya "kisasa" ambayo yalikuwa na mwanzo mzuri sana, na mengine ya "zamani," ambayo mshindi alikimbia meta 200 kwa sekunde 22.9 na meta 1,500 kwa dakika 4, sekunde 44, aliruka meta 7.70, kurusha visahani meta 35.57 na mkuki dakika 46.71. Takwimu zilizowekwa na washindi wa michezo tofautitofauti zilikuwa: sekunde 21:7, dakika 3 sekunde 56, meta 7.60, meta 45 na meta 60. Kulikuwa na ulinganifu mzuri na wa ukweli wa pande zote pamoja na ule wa wataalamu.

Timu ya Marekani ililetwa kwenye jengo kubwa, ambalo lilijengwa ndani ya jiji la Stockholm, likitumika kama hoteli yao: jengo lilikuwa kama kituo cha mafunzo ya kudumu na nyimbo za kukimbia mchakamchaka zenye sitaha, baiskeli za hapohapo, bwawa la kuogelea ambamo waogeleaji waliunganishwa kwa kamba na kuvutwa nyuma baada ya kila pigo, visahani na mikuki vilifungwa kwa kamba ili viweze kutumbukia baharini na baadaye kuvutwa tena kwenye ubao! Mafanikio ya kiufundi ya aina hii, yaliambatana na masharti ya lazima, yalistahili na kuyapokea malipo yake. Sullivan ambaye alikuwa amejitolea kwa moyo wote kwa ajili ya kazi hiyo tena aliongoza timu yake vizuri na kuwa mfano wa kuigwa, wakati Kanali Thompson, ambaye aliiongoza

kutoka kwenye jahazi lake, aliongeza hisia za hamasa na ukarimu wa kikundi cha wanamichezo vijana wazalendo. Uingereza licha ya umakini wa maofisa wake, haikuwa na maandalizi mazuri na ilikaribia kukata tamaa kutokana na kushindwa. Lakini Ufini bila ya rasilimali za kifedha, bila uwanja mzuri wa michezo, iliyodhoofishwa na msimu wake wa baridi kali, ilichukua ushindi wa kushangaza, kwa sababu tu wanamichezo wake walikuwa wameazimia kuleta heshima kwa nchi yao.

Kumbukumbu. Mwanamke wa Uswidi, Bi. Wersall, alikuwa na wanawe sita wote wakishiriki katika Michezo kwa njia moja au nyingine, mdogo zaidi kama mvulana wa skauti aliyejiandikisha kusaidia katika kudumisha utulivu na kubeba ujumbe. Ni uhalisia kiasi gani uliokuwapo kwenye maadili ya zamani! IOC ilimtunuku medali ya Olimpiki.

Tulivumbua mambo mawili. Huko London, kulikuwa na kanisa la St. Paulo. Huko Stockholm, hakukuwa na kanisa kuu lililostahili jina hilo. Kwa hiyo ibada fupi ya kidini ilifanyika katika uwanja wa michezo mwanzoni mwa sherehe ya ufunguzi: zaburi fupi na sala vilitolewa kwa Kiswidi na Askofu Mkuu wa Uppsala, kisha nyingine zilifuata kwa Kiingereza na kusemwa na Mch. Laffan: zote zikitumia dakika kumi. Na katikati ya ukimya mkubwa wa maelfu ya watazamaji na wanamichezo hawa, hafla hiyo ilionekana kufikia kiwango cha juu. Lakini nilihisi kuwa tulivuka mipaka….

Ili kuepuka fitina zilizoambatana na tuzo ya mapambo, Mfalme alianzisha moja mpya maalumu kwa ajili ya hafla hiyo: medali ya fedha yenye utepe wa bluu na manjano iliyokoza, ambayo ingetolewa kwa uhuru. Lilikuwa suluhisho kamili, lakini wapinzani walifanya kazi nyuma ya pazia, ambapo mwishoni mwa Michezo, kulikuwa na hali mbaya tena, "kurushiana maneno" kati ya nchi mwenyeji na wageni, kutoheshimiana...


Vyombo vya habari?.... havikufanya kazi kama ilivyotarajiwa, hususani upande wa uwezo na kutopendelea. Hata hivyo, vilieleza sana maendeleo ya jiji la London kuliko mabaya yake. Tofauti na vyombo vya habari vya ndani, vile vya kigeni vilitangaza kwamba "nakisi ingekuwa takribani alama 400,000" na vikasema kwamba "itakuwa hivyo kwa wakati wote." Mara moja nilimwomba Balck anitumie akaunti haraka iwezekanavyo ili niweze kuzichapisha. Gharama zilifikia taji 776,000, risiti za taji 822.767. Ilikuwa ziada nzuri. Kuhusu ujenzi wa uwanja ambao katika hali yake ya kukamilika, ungegharimu takribani milioni moja, lilikuwa jengo la kudumu kujengwa kwa ruzuku kutoka kwenye Serikali na mamlaka za miji. Jiji la Stockholm liliendelea kufaidika kwa namna yoyote unayoweza kudhani.

Michezo mzuri wa Mbio za Farasi ulikuwa ni wa mwisho. Rosen aliwataka wawe na ubora unaotakiwa na alikuwa amefanya kila lililowezekana ili kuhakikisha kwamba wanakuwa jinsi walivyokuwa! Mashindano yaliisha. Ndipo saa za kuondoka zikafika. Wakati ulikuwa umefika wa kuondoka na wakati wa Majira ya Kiangazi ya Kaskazini

yalipokaribia kuisha na miale ya jua ikizidi kufifia, mgeni wa mwisho alienda akiwa amejawa na shukurani kuelekea kwa marafiki zake wa Skandinavia na akiwa amejawa na matumaini kwa mustakabali mzuri zaidi wa Michezo ya Olimpiki…

# XIV

## Mkutano wa Saikolojia ya Michezo (Lausanne, 1913)



**33**. *Dkt. Morax 1838 - 1913*

Kufikia mwishoni mwa karne ya 19, Uswisi haikuwa nchi ambayo mtu angeweza kuiita nchi ya kimichezo, ingawa baadhi ya michezo ilifanyika kule. Ilikuwa ikishiriki maonesho ya mitindo ya Toepffer, ambayo hayakuwa mabaya lakini hayakuwa ya kawaida na ya kimataifa. Uswisi ilikuwa na wanasarakasi na wanamieleka pekee. Haikuwa na uchu wa kupata mafanikio zaidi na ilitumia milima yake kwa ajili ya matembezi na si kwa michezo ya msimu wa baridi. Kisiasa ilikuwa na mfumo wa majimbo na kulikuwa na hali ya kutoaminiana kati ya majimbo hayo na Serikali kuu. Matokeo yake Uswisi haikujishughulisha ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki na hali hiyo haikunihangaisha, kwa kuwa sikuifahamu vizuri. Nilikata kauli kwamba jinsi ilivyoonekana kwa mbali ndivyo ilipaswa kuwa. Hakukuwa na wazo lolote kutoka kwangu au kutoka kwa watalii kwamba kutakuwa na mabadiliko ya ndani. Mwaka 1903, niliongoza bila kutarajia, utafiti wa taasisi na mfumo wa jeshi la Uswisi chini ya uongozi wa ofisa maarufu, Kanali de Loys. Niligundua haraka kwamba katikati ya Ulaya, Uswisi ilikuwa nchi ndogo ambayo imetoa mchango mkubwa kipindi kilichopita na ina wakati mzuri ujao. Kwa sasa, Uswisi ni mfano wa nchi ya kistaarabu ya kuigwa na nimevutiwa nayo sana.

Katika muktadha wa michezo, Uswisi ilionekana ikibebwa na mazingira ya asili na ilikuwa ngumu kuelewa ni namna gani ingeweza kuyatumia mazingira hayo. "Uswisi, malkia wa michezo" ni kichwa cha habari iliyochapishwa katika jarida la "Michezo ya Olimpiki" la Novemba 1906 ambalo lilikuwa likitabiri yajayo ambayo yalikuwa bado hayajatokea.

Nchi hii ilitabiriwa kutoa mchango mkubwa katika jukumu la Michezo ya Olimpiki lakini ilihitaji kuchukua hatua ya kufikia lengo. Wakazi walipaswa kukumbushwa kwamba hakuna chochote kinachoweza kupatikana kirahisi bila kuandaa akili zao kufanya mabadiliko. Mwenzetu wa Uswisi Godefroy de Blonay alikuja kutambua jambo hili, hasa alipojaribu (polepole na kwa uchungu) kuunda Kamati ya Taifa ya michezo ya Olimpiki licha ya kukabiliana na upinzani mkubwa katika baadhi ya maeneo wakati wa utekelezaji wa jambo hilo.

Si kwamba naandika makala kuhusu Uswizi hapa. Katika kitabu changu cha "Histoire Universelle" niliweza kueleza kwa unyoofu uzuri wa nchi hii. Nakumbuka namna nilivyotamani kutimiza lengo langu hapa Uswisi. Nilianza na Laussanne na ili kuishawishi, niliamua kutumia mkakati wa mkutano wa kisayansi.



**34.** *Mkutano wa Ufunguzi wa Michezo ya Olimpiki, uliofunguliwa na Baron Pierre de Courbetin ambaye yupo katikati ya wajumbe waliopo jukwaani.*

Jukumu la kimataifa la Lausanne, ambalo lilianza zamani, siku ambayo papa alikuja kuweka taji la ufalme juu ya kichwa cha Rudolph wa Habsburg, lilikuwa limepuuzwa kwa kiasi fulani mwanzoni mwa karne ya 20. Baadhi ya watu walikuja kwenye matibabu yaliyofanywa na madaktari maarufu, wengine walifurahi kusimama hapo kwa muda wakati wa safari, lakini haikuwa na jukumu lililo wazi la kutekeleza.

Chuo kikuu chake ambacho kilikuwa kimehamishiwa hivi karibuni katika majengo mapya makubwa ambayo usanifu wake wa kisasa ulikuwa na mng'ao mpya, ulichukua nafasi ya heshima sana katika ulimwengu wa taaluma bila kuchukua jukumu lolote la kuongoza. Kikiwa kimejengwa kwa kupendeza kando ya ziwa, kukiwa na misitu iliyoenea na kutoa kila fursa inayoweza kufikiriwa ya michezo, ilikuwa (ama ndani ya

chuo au maeneo jirani) mahali pazuri pa kuanzisha makao makuu ya Michezo ya Olimpiki. Ili jambo hili litimie, tulipaswa kukubaliwa.

Nilikuwa nahitaji kuona huduma za afya zikiambatana na tibasaikolojia, jambo ambalo lilikuwa linajirudiarudia akilini mwangu. Nikiwa na marafiki wengi madaktari, wa kwanza akiwa daktari mwanamichezo Fernand Langrange, mwandishi maarufu wa kitabu cha "Psychologie des Exercise du Corps", naweza kuzungumza bila kuficha.

Muda sio mrefu uliopita katika Praxis, jarida la lugha mbili la taaluma ya matibabu ya Uswisi, nilieleza mtazamo wangu kuhusu "hulka mbaya ambayo hutokea michezoni", ambapo, badala ya kuzingatiwa kama jambo muhimu, ilidhaniwa kama jambo la kawaida katika nyanja mbalimbali na hasa ile ya michezo. Hii si sehemu ya majaribio wala si ya kutoa muhtasari wa suala hilo gumu. Lakini jambo nililosema katika tukio lile lilikuwa linatosha kuanzishwa kwa mkutano wa Lausanne. Niliongea na wenzangu kuhusu tukio hilo mapema mwaka 1909 na miaka miwili baadaye, katika mkutano wa Budapest, niliwapa mwongozo ambao waliupokea vizuri na baadaye ulichapishwa katika lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani na Kiitaliano. Ni fupi na nafikiri ni muhimu kuichapisha tena hapa yote:

**Asili ya Shughuli za Michezo**
Uwezo binafsi wa mtu: uwezo wa jumla (uthabiti, ujuzi, uimara, uvumilivu); uwezo mahususi (kipaji cha kufanya mazoezi fulani) – jukumu na ushawishi wa michezo ya kale; uchunguzi na hitimisho linalotolewa – je, uwezo wa asili unatosha kumhamasisha mtu au anahitaji msukumo wa ndani wa michezo? Asili na matendo ya vichocheo hivi. – Je, inaweza kuzalishwa au kuwa mbadala kwa kuiga au matokeo ya utayari?

**Mwendelezo na Njia Zilizotumika**
Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba mwanamichezo halisi anapatikana pale uhitaji unapokuwapo.

Je, inawezekana kuwa mwanamichezo anapatikana kwa kushughulisha mwili kwa kufanya mazoezi makali ya viungo na pia kuwa na ari ya kupenda au matamanio ambayo yanatokana na ushawishi au analenga kupata umaarufu, kama vile kupata urembo, afya au madaraka?

Vipengele vya kisaikolojia vya kila kategoria ya mazoezi; sifa za kifikra na kimaadili zinazoendelezwa au kutumika kwa kila mchezo; masharti mbalimbali yanayosimamia michezo: upweke na urafiki; ari ya timu na upinzani; uanzishwaji na nidhamu; uundaji na maendeleo ya timu.

**Matokeo**
Ili kupata matokeo mazuri michezoni, mambo ya kuzingatiwa ni;


Mazoezi: Tofauti kutoka kwenye hali iliyozoeleka. - Mazoezi ya kawaida yanaweza kuwa ya mwili tu na kujenga uimara wa mwili, lakini pia yanaweza kuchangia maendeleo ya maadili; kwa maendeleo ya nia, ujasiri na kujiamini na bila shaka pia maendeleo ya kifikra kwa kuwa na utulivu na mpangilio wa mawazo. Ni katika mazingira yapi? Mwishowe, je, shughuli za michezo zinaendana na falsafa halisi ya maisha?

Mpango huu ulipaswa kutetewa mbele ya taaluma ya matibabu na kuwashawishi wanafalsafa na walimu kwa kuwaonesha kazi yetu; na wakati huohuo tulikuwa na kazi kuamsha ari ya wanamichezo wenyewe. Ilikuwa - kwa kushangaza sana - daktari ambaye alinisaidia, rafiki wa zamani wa wakwe zangu, Dk. Morax, wakati huo alikuwa mkuu wa Huduma za Afya katika Jimbo la Vaud. Watoto wake watatu walikuwa maarufu katika Sanaa, fasihi na sayansi. Huko Morges, mahali alikokuwa akiishi, alivutiwa na kila kitu kilichokuwa kikiendelea duniani. Hakuna jambo lililotokea Ulaya au maeneo ya mbali ambalo halikuamsha udadisi ndani ya huyu mzee ambaye muda wote alizungukwa na vijana na alikuwa jasiri sana.

Mara moja alipendezwa sana na mkutano huo, akielewa kwa haraka mawazo yangu kuhusu Michezo ya Olimpiki, na hata fursa za Uswizi. Kupitia kwake, nilipata ushirikiano wa profesa wa Chuo Kikuu, Bw. Millioud, ambaye kozi yake ilisomwa na Benito Mussolini, wakati huo akiwa mwanafunzi asiyejulikana, ushirikiano wa Mkuu wa Chuo de Felice na mkuu wa shule binafsi maarufu Bw. Auckenthaler. Hivi ndivyo kundi la kwanza lilivyoundwa. Nilimshawishi mwanafalsafa na mwanahistoria maarufu Gugliemo Ferrero, kufanya ufunguzi, na Theodore Roosevelt kuandika ujumbe wa kuhamasisha. Lakini nilikuwa na hofu kuhusu mjadala uliokuwa ukikaribia kuanza. Mada zilizoorodheshwa hazikuwa za kawaida sana na zilikuwa hazijazoeleka kwa wajumbe wengi wa mkutano. Lakini mpango huo ungedumu, heshima ya majina fulani na uhalisi wa jaribio hatimaye ungevutia umakini wa wahusika.

Mkutano ulifunguliwa Alhamisi asubuhi, tarehe 8 Mei, 1913. Siku mbili zilikuwa zimepita tangu kikao cha IOC kifanyike kwenye Baraza la Seneti la Chuo Kikuu, wanachama watatu wapya walijiunga; Kiongozi wa Somerset wa Uingereza, Count Penha-Garcia wa Ureno na Baron de Laveleye wa Ubelgiji. Kikao cha ufunguzi kilifanyika ukumbini. Mji ulikuwa umepambwa kwa bendera. Kundi la vijana wa skauti waliunda gwaride kwa kuachiana nafasi kwa ajili ya kutoa heshima.

Kwaya nzuri za Umoja wa waimbaji wa Michezo ya Ridhaa na kwaya ya Wanaume ya Lausanne zilishangiliwa kwa sauti kubwa na hadhara na kiongozi wa shirikisho Decoppet akatoa hotuba kwa niaba ya Baraza Kuu la Shirikisho.



**35.** *Courbetin kati ya mwaka 1930-1937*



36. *Courbetin alipotembelea kiwanda cha Ovamarttine huko Nyon (Uswisi), akiwa ameambatana na Dkt. Messrti na Waziri wa Ugiriki Canallopoulos*

Kwa upande wangu, nilikuwa na jukumu la kuhuzunisha la kutoa hotuba fupi ya kumkumbuka Dk. Morax, ambaye alifariki hivi karibuni, baadaye Ferrerro alitoa hotuba maalumu iliyosheheni umuhimu wa kifalsafa. Baada ya hapo mkutano uliniomba nisimamie kazi yake na ukachagua Makamu wa Rais, ambao ni wawakilishi wa serikali za Ubelgiji na Austria, pamoja na Profesa Millioud na Bw. Auckenthaler.

Baadaye, kitabu kilichokuwa na kumbukumbu mbalimbali zilizowasilishwa kilichapishwa: nyingi ni za kuvutia kama nilivyotaja hapo juu.

Wasifu wa Roosevelt ulikuwa mfano mzuri kwa wote, kama vile uchunguzi wa Louis Dedet, mwanamichezo wa zamani, wakati huo mkuu wa Chuo maarufu cha Nomandi.

Alikuwa mtaalamu wa masuala yanayohusiana na timu, uundaji wa timu, maisha ya wachezaji, kuwatenga na uraibu na kadhalika.

Halmashauri ya Manispaa ya Lausanne na Meya, Bw. P. Maillefer, walizindua mfululizo wa maadhimisho tarehe 7 mwezi Mei. Jioni iliyofuata, kandokando mwa mto maarufu wa "*Abbaye de l'Arc*", eneo lenye miti ya kupendeza iliyostawi kwa karne nyingi na karibu na Ziwa Geneva, ndio lilikuwa eneo la sherehe.

Kwenye eneo lenye nyasi, wanamieleka 22 bora zaidi walishangiliwa na wachungaji wa ng'ombe na kondoo wenzao katika mtindo wao wa kuvutia walipokuwa wakishindana kwa kutumia mwanga wa mienge. Kwa upande wa nyuma, kwenye vichaka na miti, kulisikika sauti za waimbaji wa kwaya. Mwishowe, bendi ya "*Ranz de Vaches*" ilianza kutumbuiza wakati mienge ilianza kutoweka mmoja baada ya mwingine na wanamieleka walihitimisha baada ya usiku kuingia. Jioni ya tatu, onesho la kufurahisha, lililoandaliwa mahususi kwa ajili ya mkutano, lilifanyika kwenye kasino. Kulikuwa na nyimbo na ngoma za kufurahisha zilizokuwa zikitoa mwangwi mkubwa. Pia kulikuwa na sherehe ya Venetian huko Ouchy, ukumbi uliotolewa na Baros na Baroness Godefroy de Blonay ambao tayari walikuwa wamewakaribisha wanachama wa IOC kwenye Grandson Castle, na hatimaye, katika kuhitimisha mkutano huo, uliandaliwa mlo maalumu na Baraza la Jimbo la Vaud katika ukumbi wa kihistoria wa Chillon Castle ambao ulipambwa vizuri.

IOC haikuathirika moja kwa moja kutokana na mkutano huu. Jukumu lake lilibaki kufadhili utaratibu mpya wa utafiti wa kisayansi na ilifurahi kuona jinsi uzinduzi ulivyofanyika. Katika kikao chake, baada ya kushughulikia "mambo ya sasa" - usemi unaotumika kuashiria mambo yaliyobaki - na baada ya kujadili na kuidhinisha programu na kanuni za mkutano wa Paris uliopangwa kwa mwaka uliofuata, IOC ilijikuta inakabiliwa na suala la Thorpe.

Kabla ya Michezo ya Olimpiki ya 5 kuisha, James Thorpe, mshindi wa michezo mitano (pentathlon) na michezo kumi (decathlon), alishutumiwa kwa vitendo ambavyo si vya kimichezo. Kamati za Sweden na Marekani, zilituma nyaraka kwenda IOC ambayo kwa mara ya kwanza ilipewa kazi ya kutatua kesi ya namna hii. Nyaraka hizi zilikuwa na sehemu nne (4) barua kutoka kwa James Thorpe kwenda kwa Sullivan, barua kutoka kwa mkuu wa chuo cha Carlisle cha Pennsylvania kwenda kwa Sullivan, taarifa kutoka kwa Sullivan kwenda kwa rais wa IOC na mwisho taarifa kutoka kwa Rais na Katibu wa umoja wa Chama cha Wanamichezo wa ridhaa wa Marekani na Kamati ya Michezo ya Olimpiki. Hawa wote baada ya uchunguzi wa kesi walitoa maoni yao yakiambatana na sababu zao. Baada ya miaka ishirini kupita, ninaposoma tena hizi nyaraka, ninahisi fahari niliyokuwa nayo awali, hisia ambazo wenzangu wanazo pia. Kwa hiyo, kutokana na mapendekezo ya wawakilishi wa Uingereza wa mwaka 1913, kiongozi wa Somerset na Mchungaji Laffan wa IOC, baada ya kufikia uamuzi wake, ilituma pongezi zake kwa

maofisa wa Marekani kwa mtazamo wao mzuri wa kimichezo kwenye hili tukio. Kuna baadhi ya watu waliosema kwamba Thorpe alikuwa Mmarekani mwenye asili ya Wahindi Wekundu, na hii ndio sababu alitolewa "kafara" kirahisi kama mbuzi wa azazeli. Hii haikuwa sahihi. "Kutolewa kafara" ilisababishwa na Marekani kuwa katika ngazi za chini mwaka 1912 na hili lilikuwa pigo kwa fahari ya nchi. Kuhusu ukweli wa shutuma zilizomkabili Thorpe, sina la kusema. Wakati huo, huko Marekani kulikuwa na wanafunzi wengi mahiri katika michezo kutoka familia duni, ambao wakati wa Majira wa Kiangazi walishiriki mashindano ya Mpira wa Magongo (Baseball) wa kulipwa, kwa kutumia majina ya kuazima. Mwaka 1909 na 1910, Thorpe alifanya jambo lilelile kwa jina lake, lakini bila kujua matokeo ya kitendo chake. Hakuna mtu aliyejua jambo lolote kuhusu kitu alichofanya na aliporudi chuoni Carlisle aliendelea kuchukuliwa kama mwanamichezo wa ridhaa. Baada ya kusoma barua yake iliyoandikwa kwa unyoofu kutoka kwa mkuu wa chuo chake, ningejizuia vipi kufikiri kuhusu wachezaji wa Tennis waliofanya makubwa zaidi bila kusumbuliwa? …. Pamoja na hayo, hakukuwa na sababu ya kusita na Thorpe alivuliwa ubingwa na alitakiwa kurudisha tuzo alizoshinda Stokholm.

# XV

## Maadhimisho ya 20 ya Ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki (Paris 1914)



**37**. *Pierre de Coubertin*

Siku moja mwaka 1910 nilioneshwa nyaraka kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, ambayo sikumbuki vizuri ilihusu nini, baada ya kusambazwa kwenye idara nyingine, ilirudishwa Quai d'Orsay ikiwa na maandishi: "Serikali ya Ufaransa Haitambui Michezo ya Olimpiki" isingekuwa vigumu kwangu kumtambua Ofisa mwenye hasira kiasi hiki aliyeandika maneno hayo. Maandishi yale yalinikera sana na nilijisemea moyoni, "subiri"! Kwa muda mfupi utaona ama Serikali ya Ufaransa inaitambua michezo ya Olimpiki au la". Tangu wakati huo nilidhamiria kufanya sherehe ya 20 ya ufufuaji wa michezo ya Olimpiki ya Juni 1914 kuwa makubwa kiasi cha kuifanya Paris itambulike katika uso wa Dunia.

Tangu mwanzoni kulikuwa na kikwazo kimoja. Tulipaswa kuilazimisha serikali idhamini sherehe badala ya kuiomba, jambo ambalo lingezua hoja na uchunguzi wa kina kwetu waandaaji na mashindano yenyewe. IOC ilipanga kukutana Budapest (Mei 1911). Rais wa baraza Bw. Monis ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani alikuwa amelazwa kutokana na kupata ajali. Nilikwenda mwenyewe Palace Beauvais na nikamkabidhi kadi yangu Katibu wake ambaye, jina lake lilifanana naye na nafikiri walikuwa ndugu. Nilipokewa na mwanamume mtanashati ambaye alielewa hali mara moja. Nikamwambia, "tazama, hiki ndicho kitakachotokea. Kamati yenye wajumbe wanne wa Ufaransa kati ya wageni arobaini kutoka nchi tofauti, thelethini watapiga kura. Bila shaka, kamati hii itapiga kura kuunga mkono kufanyika kwa maadhimisho ya 20 ya

ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki ya Juni 1914 huko Paris na itakuwa heshima kubwa kwa Jamuhuri ya Ufaransa. Kutakuwa na mwitikio mbaya endapo heshima hii haitakubaliwa mara moja au kama majibu yatachelewa kutolewa baada ya mjadala wa kina. Kwa upande mwingine ninafahamu kwamba, kuna urasimu kwenye utaratibu wetu wa kiutawala na kisiasa. Hii hapa ni barua nitakayoituma kwenda kwa Rais wa baraza mara baada ya uchaguzi kukamilika… Unadhani ni mwitiko wa aina gani ungefuata?... Nilisoma barua na majibu yake, taarifa ambayo ipo kwenye Jarida la Michezo ya Olimpiki la Julai 1911: "ulinionesha wema kunitaarifu kuhusu matokeo ya kura ambapo mkutano wa IOC wa Budapest na kadhalika (yakafuata maelezo muhimu)… Ninakushukuru kwa mawasiliano haya na ningependa upeleke shukurani za serikali ya Ufaransa kwa wajumbe wa IOC."

Hivi ndivyo mambo yalivyokuwa. Uamuzi huo uliungwa mkono kwa kauli moja tarehe 25 Mei. Ndani ya wiki nne, nilikuwa na barua ya Waziri iliyokubali maombi yetu. Niliamua kushirikisha maandalizi ya mkutano wa kamati ya kitaifa kwenye kamisheni maalumu, iliyochaguliwa na IOC nami nikabaki kwenye mipango ya sherehe, ambayo niligharamia mwenyewe. Nilikuwa Rais wa kamisheni iliyoundwa na Messrs, Brunetta d'Usseaux, de Blonay, Callot, Laffan, Sloane, van Tuyll na von Venningen. Lengo kuu lilikuwa ni kuandaa idadi za uwakilishi wa kamati za Michezo ya Olimpiki za kitaifa kwenye mkutano na baadaye, kutathimini misingi ya programu kwa ajili ya Michezo ya Olimpiki ijayo. Kamisheni ilikutana miezi 8 baadaye, tarehe 27 na 28 Machi 1912 huko Basle kupokea ripoti ya Profesa Sloane kuhusu suala la kwanza na ya Mch. Laffan, kuhusu suala la pili. Baadhi ya marais wa Kamati za Taifa, hususani Messrs, Duvignau de Lanneau (Ufaransa) na de Laveleye (Ubelgiji), walikuja kueleza kuhusu maoni ya wenzao.

Shirikisho la Sarakasi la Ulaya na Shirikisho la Kimataifa la Ulengaji Shabaha, Kuogelea na Kupiga Makasia yalialikwa kutoa maoni yao. Katika kikao cha Stockholm, miezi minne (4) baadaye, IOC iliidhinisha pamoja na marekebisho machache mapendekezo ya Kamisheni na kuipa uwezo wa kuendelea na kazi yake. Kwa kweli Kamisheni ilitumia fursa ya uwapo wa Marais nchini Uswisi au wawakilishi wa kamati za taifa za Ujerumani, Marekani, Ubelgiji, Urusi, Italia, Austria, Denmark, Australia, Ufaransa, Ugiriki, Uholanzi, Hungaria, Japan, Luxembourg, Norway na Finland kuongea nao pamoja na wanamichezo kutoka mataifa hayo. Hii ilisababisha kuwapo kwa nyaraka nyingi za malengo na maoni ya kiufundi. Wakati huohuo, nilitoa mwaliko kwa kamati zote kuhudhuria sherehe za Paris. Kamisheni ilikutana tena huko Lausanne siku moja kabla ya mkutano mwaka 1913.

Ikiwa ni matokeo ya idhini ya mwisho yaliyopendekezwa na IOC, programu na kanuni za mkutano wa Paris vilichapishwa katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani kwenye Jarida la Michezo ya Olimpiki ya mwezi Juni mwaka 1913.

Kamati zilizotambuliwa na IOC zilipaswa kuwa na idadi ya wajumbe wasiozidi 10 wa nchi zifuatazo; Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, Marekani, Italia, Urusi, wasiozidi 6 kutoka Austria, Ubelgiji, Hispania, Ugiriki, Uholanzi, Hangaria, Sweden ; na nchi zingine zote wajumbe 5 isipokuwa Ufini, Luxembourg, Monaco na Czechoslovakia ambazo zitabaki kuwa na wajumbe 2. Kwa kuwa wanachama wa IOC walikuwa na haki ya kupiga kura, hawakupaswa kuwa wajumbe wa kamati ya taifa. Nchi zisizokuwa na Kamati ya Taifa zingeweza kutuma wajumbe watatu walioteuliwa na Waziri wa Mambo ya Nje lakini kura yao itakuwa ni ya kushauri tu. Baadaye yakaja mapendekezo kuhusiana na uthibitishaji wa mamlaka, ukumbi wa mkutano, midahalo na majadiliano, lugha zilizoidhinishwa ni (Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani), na badaye masuala yaliyoibuliwa (sifa; jinsi, umri, utaifa,hali ya hadhi ya washindani wa Michezo ya ridhaa- idadi ya matukio ya Michezo kwa kila mchezo- orodha ya matukio ya lazima, michezo ya hiari -kanuni za kiufundi – waamuzi na tuzo). Ninanukuu vichwa vya habari tu vya sura. Kulikuwa na maelezo ya kina, kama tulivyoona, matokeo ya mjadala uliochukua miaka miwili na yaliyoungwa mkono na utafiti wa kina.

Kabla sijaanza kupanga programu za sherehe, nilisubiri hadi kipindi cha uongozi cha Rais Fallieres cha miaka saba kiishe, wakuu wa nchi wa Ufaransa tangu kujiuzulu kwa Jules Grevy, kulikuwa na matukio machache ya Michezo ya Olimpiki. Baada tu ya mrithi wake kuchaguliwa, nilimtaarifu nia yetu, lakini baadhi ya hatua za kijamii zilikuwa zimechukuliwa. Wakati wa Majira ya Vuli ya mwaka 1913, nilikwenda Paris na kupokewa na Rais mpya, Bw. Raymond Poincare, ambaye alinipokea kwa ukarimu mkubwa. Wakati huohuo nilimtembelea Waziri wa Mambo ya Nje, Bw. S. Pichon ambaye nilimfahamu alipokuwa Jenerali mkazi wa Tunisia na Rais wa Manispaa ya Paris. Kila kitu kilienda vizuri. Muda mfupi baada ya mkutano na kikao huko Lausanne, nilirudi Paris kwa Mkuu wa Nchi kumpelekea programu nzima ambayo ilikuwa na sherehe zisizopungua kumi na saba (17). Rais alipaswa kuwapo katika maeneo matatu; Sorbonne, Trocadero na Elysee. Rais alianza kucheka. Kulikuwa na mwaka mzima umebaki. 'Ndivyo ilivyo?' aliuliza. Nikajibu; 'ndiyo'. Basi, nitaandika' alisema kwa kifupi. Aliandika tarehe zote zinazomhusu kwenye shajara yake. Nilipoanza kuelezea tukio, alinikatiza na kusema kwamba ameelewa.

'Ufaransa yote!' tabasamu lake lilionesha uzalendo wake.

Katika programu ambayo Rais alikuwa ameidhinisha tu, hafla katika hoteli ya De la Rochefoucauld, iliyoandaliwa na Kiongozi wa Doudeauville, hafla kwenye bustani ya Chateau de Maintenon, iliyokuwa inamilikiwa na kiongozi wa Noailles. Pia, kulikuwa na onesho la wapanda farasi lililoandaliwa na Count Potocki lililofanyika kwenye mapokezi ya huko Elysee, Wizara ya Mambo ya Nje na ukumbi wa mji.

Aidha, kulitakiwa kuwa na mechi ya mapigano ya mapanga huko Cercle Hoche, iliyoandaliwa na Rais wao Duke Decazes, mechi iliyofanyika usiku eneo la Bois de

Boulogne na maonesho ya mashindano ya kupiga makasia yaliyofanyika kwenye Mto Seine, ambayo yaliandaliwa na wenzetu Wafaransa Count de Bertier na Bw. Albert Glandaz. Kulikuwa na tafrija iliyofanyika katika ubalozi wa Ujerumani...ambayo baadaye ilifuatiwa na tafrija nyingine ambayo iliandaliwa na Count Brunetta na muziki wa asili katika Mgahawa wa Ambassadeurs, mwenyeji akiwa Kanali Thompson, Rais wa Kamati ya Marekani.

Ufaransa yote….onesho lililofanyika huko Comedie Francaise, ambalo liliunda sehemu ya mapokezi niliyoyafanya pamoja na Bi. De Coubertin, yalikuwa na hatua tatu za igizo la kifaransa la tangu enzi za kati la Franc Archer de Bagnolet.

Utaratibu na mipango yote ya chakula iliandaliwa na Stern. Kulikuwa na maandalizi ya kutembelea vivutio vya utalii; makaburi ya zamani na wajumbe wangetembezwa maeneo mbalimbali; kutoka Bois de Boulogne hadi Sorbonne, ikijumuisha Sainte-Clotilde, Pantheon, Elysee, Trocadero, nyumba za kibinafsi, ukumbi wa jiji na kadhalika

Hatimaye, kila mjumbe wa mkutano alikabidhiwa kitabu kinachoitwa "*Notes on Contemporary France*" kilichoandikwa na Messrs. A Ribbot, Leon Bourgeois, Edmn. Perrier na watu wengine kadhaa. Watu walikuwa wakishangaa kuwa ninawaza nini, sikuhisi kwamba vita ilikuwa imekaribia wala sikuona kwamba inazuilika. Labda siku moja nitapata fursa ya kueleza mawazo yangu lakini niliona kwamba hakuna kitu cha kusababisha vita. Niliweza kupinga ushawishi huu kwa kuwa sikuona sababu yoyote ya msingi.

Miaka miwili iliyopita, nikiwa Stockholm niliongea na Ofisa wa ngazi ya juu wa Ujerumani. Nilimwambia, kwa maoni yangu, kuliko ilivyokuwa katika kipindi chochote cha historia, Ufaransa ilikuwa na utajiri mkubwa wa nguvu za kijeshi zilizotawanyika hivi kwamba isingekuwa rahisi kuishinda. Nakumbuka namna alivyokasirika aliposikia kauli yangu. Alielewa kwamba nilikuwa naongea kwa uhakika. Mwezi juni, 1914 haikuwa kazi ngumu kubadili matendo yangu yaendane na kile nilichokizungumza mwaka 1912.

Bila kutarajia, ulitokea mgogoro mbaya katika baraza la mawaziri mara mbili na kusababisha kukosekana kwa utulivu wa kisiasa. Baada ya kufika Paris, wajumbe wa mkutano walishuhudia kuvunjwa kwa baraza la mawaziri la Ribot's, ambapo Bw. Leon Bourgeois alishika nafasi ya Waziri wa Mambo ya Nje. Mapokezi katika Quai d'Orsay yalipangwa kufanyika siku mbili baadaye. "inamaanisha hakuna kitu kitakachoendelea?" niliuliza nikiwa na furaha huku nikiwa nimeificha. "kwa nini?" – "hakuna Waziri" – "hakutakuwa na Waziri yeyote". Bw. na Bi. Viviani ambao walikuwa wameteuliwa asubuhi ile walikuwa tayari kwenye chumba cha mapokezi, wakiwa watulivu kana kwamba wao ndio waliofanya maandalizi yote ya hafla hadi mwisho. Katika mkusanyiko huu wa kimataifa ulioundwa na wajumbe wa mkutano, (karibu watu mia moja arubaini), kulikuwa na watu wenye uzoefu mkubwa wa maisha, ambao walikuwa na

nafasi kubwa. Wengi wao walishangaa kuona jinsi Ufaransa ilivyobaki katika hali ya utulivu licha ya kuvunjika kwa Baraza la Mawaziri.

Dondoo za maadhimisho ya ukumbusho wa huko Sorbonne, ulioongozwa na wakuu wa nchi, walioambatana na mabalozi wote, wakati ambapo walitajwa washiriki zaidi ya mia moja waliojumuisha wana wa Mfalme, wakuu wa mashirika, serikali, vyuo vikuu na taasisi. Kulikuwa na nyimbo kutoka kwa waimbaji mashuhuri wa Uswidi waliokuja Paris kwa ajili ya Sherehe. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza ya kupeperusha bendera ya Michezo ya Olimpiki hadharani na yalikuwa mafanikio makubwa. Bendera ilikuwa nyeupe, huku kukiwa na rangi tano zilizoungana, zenye rangi ya buluu, manjano, nyeusi, kijani na nyekundu, zilizowakilisha sehemu tano za dunia zilizounganishwa na Michezo ya Olimpiki na kukiwa na rangi ya nchi zote.


Sherehe ya Trocadero haikuwa kama ilivyotarajiwa. Baada ya wimbo wa utangulizi wa "Echoes of the past", nyimbo kadhaa za kale na za Byzantine, zilikuwa zimeimbwa na kwaya ya kanisa la Ugiriki. Baada ya taa kuwashwa, kundi la *"Sauti za Kaskazini"* (*"Voices of the North"*) la waimbaji wa Uswidi likaamsha matumaini ya kufufuliwa kwa Michezo ya Olimpiki. Waliimba kwa kushirikiana na watumbuizaji wengine wakieleza maudhui ya Michezo ya Olimpiki. Mabinti, wakiwa wamevaa suti za kale, walikuja kuonesha heshima kwenye bendera za nchi tano za kwanza kuandaa Michezo ya Olimpiki: Ugiriki, Ufaransa, Marekani, Uingereza na Uswidi. Kulikuwa na shamrashamra mbalimbali zikiambatana na mlio wa kengele. Midundo ilioana vizuri lakini mwanga ulikuwa hafifu na hakukuwa na mpangilio mzuri.

Ili asivuruge sherehe na kupunguza taratibu za itifaki, Rais alikubali kuingia kimyakimya na gizani.

Sherehe hizi za mwaka 1914, zilizoishia Rheims katika burudani ya kupendeza iliyotolewa na Marquis de Polignac katika chuo cha Wanamichezo, hazikuingilia kazi ya mkutano. Mbali na siku ya safari ya Kwenda Maintenon, kulikuwa na vikao viwili kila siku, kimoja asubuhi na kingine mchana, kuanzia saa nane hadi saa kumi; kukiwa na jumla ya vikao kumi na vitano. Matokeo yake ni kwamba kiasi kikubwa cha kazi kilikamilika. Wajumbe walionesha nia njema ya wazi na walijitoa kuonesha juhudi zao. Niliongoza vikao vyote isipokuwa kimoja na hakukuwa na tatizo lolote. Hotuba zote ziliwekewa mipaka; kulikuwa na muhtasari wa Kiingereza au Kifaransa tofauti na tafsiri, jambo lililofanya wote waelewe haraka. Nilijitahidi kuhakikisha kwamba mijadala iwe shirikishi wakati huohuo nikihakikisha kwamba ni mifupi kadiri inavyowezekana. Pamoja na ukubwa wake, tulifanikiwa kufanya mjadala wa programu yote. Hakuna mtu aliyefikiri kwamba kumbukumbu za mkutano zisingechapwa. Ili kuhakikisha kwamba hakuna makosa yanayojitokeza, kamisheni iliundwa ili kulinganisha matini zilizotayarishwa katika lugha zote tatu. Kamisheni hii ilipaswa kukutana mwezi Agosti na uchapishaji kufanyika wakati wa Majira ya Vuli. Hata hivyo, haikuwezekana hadi mwezi

Novemba mwaka 1919, miaka mitano baadaye ndipo IOC iliweza kuchapisha uamuzi uliofikiwa kuhusu mabaraza, kanuni maalumu, washiriki na sifa bainifu na kadhalika.

Maandalizi haya yote yalifanyika kwa ajili ya Michezo ya 6 ya Olimpiki ambayo ilipaswa kuandaliwa Berlin. Ndiyo maana tiketi nyingi ziliandaliwa na karibu michezo yote ilijumuishwa katika




38. *Washiriki wa Mkutano wa Michezo ya Olimpiki wa mwaka 1914 wakiwa wamekusanyika kumzunguka Pierre de Courbetin. Picha yetu inaonesha Jenerali Victor Balck, Baron Godefrey de bronai, Anjello C. Boranak, Mch. R.S. de Courcy Laffan (CER), J. Sigfredy Edatron, Albert Grandez, Ernerst Clobus, Jullesy de Muzsa, Frentz Pechel, Count Von Sielotorpf, James E. Sullvan, Robert M. Thompson*




*39. Courbetin akiwa na mkewe huko Baselona mwaka 1928*

maandalizi ya jumla ya michezo ya mwaka 1916, ambayo ilikatizwa ghafla na vita vya kwanza vya Dunia.



# XVI

## Miaka Minne ya Vita



*40. Jalada la toleo la mwisho la jarida la Michezo ya Olimpiki (Olympic Review) kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia*

Vita vilipopamba moto kati ya Ujerumani, Uingereza, Dola ya Austria na Hungaria, Ubelgiji, Ufaransa, Urusi na Serbia vilizua hali ambayo ilitishia uwapo wa taasisi ya Michezo ya Olimpiki. Athari yake ya kwanza ilikuwa kusimamisha mchakato wa Rais wake kustaafu.

Kwa kweli yalikuwa ni matamanio yangu kuacha kazi niliyokuwa nikifanya kwa muda wa miaka ishirini na, ingawa hakuna uamuzi uliofikiwa, nilikuwa nimejadili uwezekano huo na baadhi ya watu wa karibu. Kwa hali ilivyokuwa, isingewezekana kustaafu kabla ya mwisho wa kipindi changu cha miaka kumi ya uongozi mwaka 1917. Nahodha haachi chombo chake wakati wa dhoruba.

Changamoto mbili ziliibuka mara moja, ya kwanza ilihusu michezo inayofuata na ya pili ilikuwa muundo halisi wa IOC.

Kuhusiana na hoja ya kwanza, wiki mbili tu zilikuwa zimepita tangu Ubelgiji ivamiwe, nilipokea mapendekezo ya "kuhamisha" michezo – mara ya kwanza haikuwa wazi lakini baada ya muda ilifahamika kwamba itahamia kwa Sullivan, ambaye alikuwa mhimili imara wa mkutano uliofanyika. Aliomba kupewa maelekezo na hatukusita kutoa. Inawezekana kusifanyike Michezo ya Olimpiki lakini idadi yake inabaki. Huu ni utaratibu wa tangu zamani. Ujerumani, ambayo wakati huo iliamini kwenye vita na ushindi wa haraka, haikuomba kutolewa kama muandaaji wa Michezo ya Olimpiki.

Kufanya uamuzi wa kuipa nafasi Marekani au Skandinavia ingekuwa hatua ambayo matokeo yake ni magumu kutabiri na kungehatarisha umoja wa Michezo ya Olimpiki. Kwa hiyo, nilikataa kufanya hivyo.

Suala la muundo wa kamati hiyo lisingeibuka ikiwa maoni ya umma ya Waingereza, ambayo kwa mara ya kwanza yalikosa mashiko, hayangeshinikiza baadhi ya vyama vya kimataifa vya kitaaluma au kisayansi kuwafukuza wanachama wao wa Ujerumani. Ufaransa, Ubelgiji na Urusi hazikuwa zimejiandaa kufanya hivi.

Kwa hali hii, hatua hiyo ingekuwa sawa na kupanda mbegu zilizoharibika katika udongo usiojulikana. Hali ingekuwa mbaya zaidi kama kungekuwa na wawakilishi kutoka Ujerumani au Austria katika bodi ya IOC lakini uzuri ni kwamba hawakuwapo. Kwa hiyo, bodi iliendelea kama ilivyokuwa na iliahirisha vikao vyake. Baadaye, tungeona jinsi mambo ambavyo yangekuwa. Kufanya uamuzi wowote wa haraka kungefanya hali kuwa mbaya zaidi. Kwa makubaliano kati yangu na wenzangu wa Ubelgiji na Ufaransa, nilikataa maombi ya Bw. Thomas A. Cook ambaye aliamua alijiuzulu.

Baada ya haya mambo mawili kukamilika, mambo mawili mengine yaliibuka ambayo yalihitaji hatua za haraka kuchukuliwa. Haikuwa wazi kuhusu yalipo makao makuu ya IOC. Baadhi ya watu walifikiri yalikuwa Paris kwa kuwa niliishi huko kipindi hicho. Kipindi hicho tulifuata utaratibu, ambao ulianzishwa mwanzoni mwa michezo ya kisasa. Katika utaratibu huo, ofisi iliyosajiliwa ilikuwa ikihamishwa kila baada ya miaka minne (4) Kwenda kwenye nchi ambapo Michezo ya Olimpiki itafanyika, fursa ambayo ilidaiwa mara chache lakini ingedaiwa na Berlin kama ingehitaji. Kwa hiyo, kwa hali ilivyokuwa Ulaya, utulivu wa kiutawala ulikuwa muhimu sana kwa Michezo ya Olimpiki.

Tukijadili jambo hili kwenye IOC, lakini wenzangu hawakuonekana kuvutiwa na malengo yangu. Kwa kuzingatia unyeti wa suala lenyewe, niliamua, baada ya kuwajulisha wale ambao walikuwa bado wanafikika, kubatilisha mapingamizi hayo, na tarehe 10 Aprili, 1915 katika Chumba cha mikutano cha ukumbi wa Lausanne Town, tulisaini hati ya kuidhinisha Lausanne kuwa kituo cha utawala duniani na hifadhi ya kumbukumbu (makavazi) ya Michezo ya Olimpiki ya kisasa. Bw. De Blonay, mjumbe wa

Uswisi alinisindikiza. Meya, Bw. Maillefer na wajumbe wa Halmashauri ya Mji walipokea taarifa kwa niaba ya Mji. Baraza la jimbo la Vaud pia lilikuwa sehemu muhimu ya jambo hili ambapo Bw. Motta, Rais wa Shirikisho, alishiriki kwa kutuma telegramu ya kutia moyo kutoka kwenye Baraza la Shirikisho.

Hatua yangu ya pili ilikuwa ni kuhusu sherehe zijazo za Michezo ya 7 ya Olimpiki ya mwaka (1920). Kikao cha IOC kilichokuwa kimefanywa Paris mnamo Juni 1914 kilikuwa tayari kimeitwa kuchunguza jambo hilo. Budapest na Antwerp waliomba kuandaa michezo hiyo. Antwerp iliwakilishwa na wajumbe ambao waliwasilisha maombi yaliyoandaliwa vizuri na kuchapwa. Ilikuwa mapema mno kufanya uamuzi. Duru ya kwanza ya upigaji kura iliisha kwa kura kukaribiana ingawa Budapest ilipata zaidi.

Wakati huohuo mnamo mwezi Oktoba 1914 wakati misheni ambayo nilikabidhiwa na serikali ya Ufaransa, mara tu ilipohamia Bordeaux, ilinifanya nisafiri kote Ufaransa. Nilipita Lyon mara kadhaa. Nikiwa huko Bw. Herriot alinionesha uwanja wa kuvutia alioanza kujenga. Aliponiomba ushauri kuhusu nafasi ya Lyon kugombea kuandaa michezo ya mwaka 1920 au 1924, nilikuwa mwangalifu nisimkatishe tamaa. Mwaka uliofuata, nilifanya mipango ya kutia saini hati muhimu ambayo, wakati Lyon akiomba kuandaa Michezo ya 7 ya Olimpiki mwaka (1920), aliweka kipengele ambacho kinaonesha kuwa yuko tayari kuahirisha maombi yake hadi mwaka 1924 ikiwa Antwerp ataonesha utayari. Hati hiyo ilisainiwa na Meya wa Lyon na Ubelgiji na Comte D’Assche. Baada ya muda mfupi, tulipokea barua iliyoandikwa vizuri kutoka kwa Comte de Baillet-Latour iliyoafiki makubaliano kwa niaba ya Kamati ya Michezo ya Olimpiki ya Ubelgiji.

Kwa hiyo kama nilivyokuwa nimeamua kuzuia uhamisho wa michezo ya mwaka 1916, niliona kwamba lilikuwa ni jambo jema ili kutoa fursa kwa michezo kufanyika mwaka 1920 na 1924, katika maeneo tofauti. Ndiyo maana, sikuridhika na kuzipa nafasi Antwerp na Lyons, nilisikiliza pia mapendekezo kutoka Marekani.

Lakini sio kutoka Marekani; Sullivan alikuwa amefariki ghafla; maombi yenye msisitizo yaliendelea kuletwa. Heshima ya IOC iliimarishwa huko na Siku ya Kimataifa ya Kamati ya Michezo ya Olimpiki, iliyotengwa na Maonesho ya San Francisco ili kuipa heshima maalumu. Maonesho ya Marekani yana kawaida ya kutenga siku maalumu kwa ajili ya nchi au taasisi. Mmoja wa waandaaji ambaye alikuwa Stockholm mwaka 1912, alivutiwa sana na Michezo ya Olimpiki huko.

Michezo Mitano ya kisasa iliamsha shauku yake. Ingawa haikuwezekana kuandaa Michezo ya Olimpiki huko San Francisco mnamo mwaka 1915, aliiomba IOC angalau kuunga mkono hafla ya michezo mitano. Mwenzetu Allison Armor alipewa jukumu la kutuwakilisha. Mnamo Machi 18, 1915, bendera ya Michezo ya Olimpiki ilipeperushwa kwenye maonesho na hotuba ya kuvutia ilitolewa na Rais wa maonesho, pamoja na utoaji medali kwa washiriki.

Muda mfupi baadaye, nchi ya Kuba (Cuba) ikajiunga. Kufikia kipindi hiki, tulianza kuzoea suala la Michezo ya 6 ya Olimpiki kufanyika bila shamrashamra lakini tuliendelea kuorodhesha kama ilivyokuwa zama za kale. Tulielekeza juhudi na matarajio yetu mwaka wa 1920. Maeneo yote matatu; Atlanta, Cleveland na Philadelphia yalikuwa yanafaa.

Kamati iliyoundwa mjini Havanna haikutoa ahadi nyingi, ikifahamu zaidi matatizo, lakini wakati huohuo ilihakikishiwa kuungwa mkono na serikali, akiwamo Mkuu wa Jamhuri, Rais Menocal.

Iwe mradi wetu ungekamilika au ungeshindikana, ilitusaidia kuingia Amerika ya Kusini, ambapo idara ya uenezi ambayo nilishirikiana nayo ilinipa msaada mkubwa. Katika eneo hili la Dunia, kulikuwa na mambo mengi ya kukatisha tamaa; wajumbe wengi wa Argentina ambao hawakuwa na msaada. Ama walikosa uelewa wa jambo lenyewe au walikuwa wakishiriki harakati za uhuru, kwa hali hiyo walituudhi sana. Wakati fulani, kilabu ya Chile ilimpa wakati mgumu mwenzetu, Profesa Garcia ingawa alichaguliwa kwa mapendekezo ya serikali yao. Kitu nachoweza kusema kuhusu ujumbe wa Kijeshi wa Chile katika michezo ya Stokholm ni kwamba hawakuitendea kwa usahihi IOC; baada ya hapo jaribio lilifanyika Buenos Aires la kufanya Michezo ya Olimpiki ya kujitegemea. Huko Brazili, michezo iliendelea polepole, lakini kwa kumtumia Bw. De Rio Branco, kapteni wa zamani wa mpira wa miguu na Waziri kwa sasa wa Bern, tulikuwa na mtu anayejituma na mwaminifu. Mwaka 1916, niliweza kuunda kamati ya muda huko Paris, ambayo kiongozi wake alikuwa Bw. De Matheu, balozi Jenerali wa Salvador, na tunamshukuru kwa kuweza kuendesha uenezi kwa mafanikio makubwa. Kijitabu chenye jina la Olimpiki ni nini? *(que es el olimpismo?)* kilisambazwa sana katika nchi za Amerika ya Kusini.

Kamati hii ilifanya kazi kama ile Kamati ya Uhispania, ambapo shauku na ukarimu wa Marquis de Villamejor uliimarisha azma yetu.

Mwaka 1916 huko Madrid, nilipata fursa ya kuongoza kikao cha Kamati hii, ambayo iliandaa kijitabu kizuri cha kuhamasisha Michezo ya Olimpiki.

Heshima kubwa ambayo IOC ilioneshwa huko San Francisco ilikuwa na matokeo ya moja kwa moja huko Ufilipino ambapo Wamarekani tangu mwanzo wa utawala wao walijitahidi kuhimiza michezo.

Kabla ya vita, niliwasiliana na Chama cha Michezo cha Mashariki ya Mbali, ambacho makao makuu yake yalikuwa ni Manila na Rais wake wa mwaka 1915 alikuwa Dkt. Wu Ting Fang wa Shanghai, akisaidiwa na washauri mahiri wa Marekani.

Kwa kusaidiwa na maofisa wa YMCA, walifanya kazi nzuri na kipindi hiki heshima ya IOC ilikuwa imewafikia, wakionesha kuwa na shauku ya kuruhusu "Michezo yao ya Mashariki ya Mbali" kuwa chini ya IOC. Walihitaji kuzijumuisha nchi za China, Japani na Siam na

walifurahia kuongeza takwimu za idadi ya watu. Bila kuzingatia usahihi wa hesabu za makadirio ya Marekani kwa siku zijazo, tulikuwa tayari tumewaamini.

Waliniandikia wakisema “walianzisha shule ya chekechea ya Michezo ya Olimpiki”. Hali hii ilikuwa inatia moyo. Kitu tulichokuwa tumepoteza kwenye upande mmoja, tulikipata kwenye upande mwingine. Nilikuwa sahihi nilipoandika katika moja ya Makala zangu kwamba ikitokea vita vikazuia michezo ya olimpiki kufanyika Ulaya, basi kuna bara jingine litaiandaa na kuifanya na kwamba, ikiwa vijana wa bara hili wangelazimishwa kwa muda kuacha kushiriki michezo hii, vijana wa bara jingine wangechukua nafasi hiyo.

Jarida la Michezo ya Olimpiki lilikuwa ndiyo mwathirika wa kwanza wa janga la vita. Mara ya mwisho kuonekana ilikuwa Julai 1914. Ilikuwa ni ngumu kuliendeleza, kwa kweli tayari niliamua kulisitisha baada ya Desemba na



41. *Tarehe 12 Machi, 1895 Courbetin alifunga ndoa na Marie Rothan katika Kanisa la Mt. Pierre de Challet huko Paris, binti wa Mprotestanti na Mwanadiplomasia kutoka familia ya kifahari ya Alzatani.*



*42.Pierre de Courbetin mwaka 1915. Hali ya kisiasa kwa wakati huo, ilimlazimisha Courbetin kuhamisha nyaraka za IOC kwenda Laussanne tarehe 10 Aprili, 1915. Alijitoa kuitumikia nchi yake na aliteuliwa na Serikali ya Ufaransa kufanya kazi ya Ukatibu Uenezi wa kitaifa.*

niliwaalika wenzangu ili kulibadilisha na kuanzisha jarida la kiufundi la lugha tatu.

Nilitarajia kukamilisha jukumu lake mapema ili nipate muda zaidi wa kufanya utafiti wa kihistoria. Kuanzia Julai hadi Desemba ingechapisha na kueleza nyaraka na kumbukumbu za mkutano. Kutokana na vita nyaraka hizo zilichapishwa huko Ghent na katika misukosuko ya vita, baadhi ya kumbukumbu ziliharibiwa.

Baadhi ya wajumbe walifariki wakati wa vita; Count Brunetta d'Usseaux, Baron de Venningen, aliyeuwawa kwenye mstari wa mbele katika wiki ya kwanza, na Evert Wendell. Pia, nafasi iliyoachwa na Bw A. Ballif ambaye alijiuzulu, ilichukuliwa na Marquis de Polignac. Mnamo 1918, muda mfupi kabla ya makubaliano ya kusitisha vita, wajumbe watatu wapya walichaguliwa kutoka Amerika ya Kaskazini na Kusini, ambao ni Messrs. Bartow Weeks, Dorn Y. de Alsua na P.J de Matheu.

Hatimaye, mwaka wa 1917, muda wangu wa kuwa madarakani ulikwisha na nafasi yangu kuchukuliwa na mpatanishi Bw. de Blonay, ambaye alikubali kuchukua majukumu yangu rasmi kuanzia tarehe 1 Januari 1916. Katika kipindi hicho hakuna mkutano wa mashauriano au sehemu ya mkutano ingeweza kufanyika hadi mkataba wa amani usainiwe.

Angalau kila kitu kilikuwa kimeandaliwa huku tukisubiri siku ya kuanza tena.



# XVII

## Michezo ya Saba ya Olimpiki (Antwerp 1920)



43. *Pierre de Coubertin na Henny de Ballet-Latour bembeni ya Mfalme H. M. Albert.*

Mara tu mkataba wa kusitisha mapigano ulipotiwa saini, nilianza kuwasiliana na wenzangu ambao walikuwa karibu. Ilikuwa muhimu kwa Kikao hiki kufanyika Lausanne, ambako kwa wakati huo ilikuwa ni makao makuu ya kudumu ya Michezo ya Olimpiki na ilihitaji ithibitishwe kuendelea na hadhi yake kama ilivyokuwa. Kufikia Majira ya Vuli ya mwaka 1919, ilikuwa imetimia miaka ishirini na mitano tangu Michezo hii ifufuliwe. Bila kuyapa mazingira umuhimu kama ilivyokusudiwa, hata hivyo, ulinganifu huu ulipaswa kuongeza ari na hamasa ya Kikao. Mamlaka za umma za Uswisi zilikuwa na maoni hayohayo. Bw. Gustave Ador, ambaye alikuwa amechaguliwa hivi karibuni kuwa Rais wa Shirikisho, wadhifa ambao alipewa kwa sababu ya heshima ya ulimwengu mzima na shukurani za wapiganaji kwa jitihada zake za kuwafunga majeraha yao, alikubali mara moja kuongoza sherehe ambayo ilifanyika kwa heshima zote na ilikuwa na mafanikio makubwa licha ya hali ngumu wakati wa Majira ya Kipupwe kikali ambacho kilidumu. Marafiki zetu wa Lausanne, wakiongozwa na Dkt. Messerli asiyechoka na aliyejitolea, waliandaa mazingira mazuri na tofauti kwa ajili ya Kikao chetu. Majadiliano yalikuwa ya amani kama ilivyotarajiwa tu kati ya marafiki waliofurahi kukutana tena na kushuhudia uzuri wa Michezo ya Olimpiki. Ilikuwa ni nje ya vyumba vya mkutano ambapo fadhaa zilikuwa nyingi. Paris ilikuwa kitovu cha migogoro. Bila kutegemewa, upinzani usio na

ukweli, usio na uaminifu ulikuwa umeibuka na ulielekezwa dhidi ya chaguo la Antwerp. Ikiwa hisia zingetakiwa kwa wakati kama huo, ni nini kingekuwa bora zaidi kuliko chaguo tulilokuwa tukifanya la Antwerp kama ukumbi wa mashindano ya Michezo ya 7 ya Olimpiki? Ni mji gani mwingine ambao ungekuwa sawa na huo? Nina hakika kwamba, kwa kuarifiwa ipasavyo, matakwa ya watu wengi yangedhihirika kwa shauku katika kuupendelea mji wa Antwerp. Kwa vyovyote vile, Ubelgiji ilivutiwa kwa kiasi kikubwa na mkutano wetu, na Serikali ikiwa inaelewa wajibu wake wa kuandaa tuzo za Michezo, ilithibitisha kuwa, iko tayari kuipokea michezo hiyo.

Count de Baillet- Latour hakuridhia kulijadili suala hilo na Mfalme Albert pamoja na mawaziri wake. Kwa mtazamo wake wa kuwa mkweli, alikuwa amechunguza uwezekano wote na aliazimia kuendelea na kuifanikisha Michezo. Ingawa majaribio mengi yalifanywa ili kumkatisha tamaa, alitoa ahadi kwa mji wa Antwerp – ikiwa na msisitizo wa uhakikisho ulioletwa kutoka Uingereza na Mch. Laffan kuwa kila kitu kingekuwa tayari kwa wakati uliokusudiwa. Na hivyo, ndivyo ilivyokuwa.

Kuba (Cuba) ilikuwa ikijiondoa taratibu kwenye mchakato wa kuandaa mashindano ya Michezo ya Olimpiki. Na kwa kuzingatia nafasi ya Ubelgiji, hakuna hata nchi moja nyingine ingetarajia kupata fursa ya kuandaa mashindano hayo. Lakini tatizo kubwa liliibuka: kulikuwa na ushiriki wa "himaya kubwa" kama zilivyokuwa zikijulikana. Ilikuwa ni miezi michache tu tangu mwanajeshi wa mwisho wa Ujerumani alipoondoka katika ardhi ya Ubelgiji na tangu pigo la mwisho la mizinga liliposikika kwenye uwanja wa vita. Akili ya kawaida ilipendekeza kwamba isingekuwa jambo la busara kwa timu ya Ujerumani kuonekana kwenye uwanja wa Michezo ya Olimpiki kabla ya 1924. Kwa upande mwingine, kuitenga nchi yoyote mwanachama, hata mara tu baada ya mzozo ulioigawa Ulaya; ingeleta mpasuko katika katiba ya Olimpiki ambayo ilikuwa na nguvu hadi wakati huo; na inaweza kuwa jambo la hatari. Hata hivyo, suluhisho lilikuwa rahisi sana. Katika kila Mashindano ya Michezo ya Olimpiki, kulingana na utaratibu ulioanzishwa mwaka 1896, ni Kamati ya Maandalizi iliyotuma mialiko. Kwa njia hiyo, Kamati ya Maandalizi ilisimamia usambazaji wa mialiko, bila kanuni ya msingi ya kiulimwengu kukabiliana na ukiukaji wowote wa moja kwa moja. Kwa hiyo, IOC haikuwa na uamuzi mpya wa kuchukua. Hata hivyo, licha ya maoni ya wengi wetu, njia ya kati ilichaguliwa ambayo ilijumuisha kuhesabu nchi ambazo zingealikwa, kwa kisingizio kwamba wengine hawakuwakilishwa kwenye IOC. Hilo lilikuwa kosa kubwa, kwani kwa wakati huo kujitoa kwa Ujerumani na kujiuzulu kwa nchi zingine kuliacha nafasi kadhaa tupu katika safu zetu, na hivyo kubaki kwa Wahangaria ambao hawakuwa ama wamejitoa au kujiuzulu.

Wakati wa Kikao cha 1919, ndege kumi na nne za kijeshi za Ufaransa zilitua Lausanne kutoka Nancy, kwa mwaliko wa Shule ya Lausanne ya Usafiri wa Anga. Barua kutoka

kwa Rais wa Baraza la Mawaziri, Waziri wa Vita, ilinijulisha kwamba kwa kutuma kikosi hiki, kwa idhini ya Serikali ya Shirikisho na "katika hafla ya kuadhimisha miaka 25 ya kufufuliwa kwa Michezo ya Olimpiki" Bw. Clemenceau alitaka kuweka alama ya "heshima kubwa" ambapo aliitisha IOC na shughuli zake. Kwa njia hii, wale wasioridhika walialikwa ili kuwanyamazisha lakini hata hivyo waliendelea kwa muda mrefu kunung'unika na kuonesha nia yao mbaya kwa namna nyingi. Walitaka nini hasa? Hakuna kitu sahihi sana. Baada ya kushinikizwa ili kueleza malalamiko yao, hatimaye magazeti yaliyowaunga mkono yalikaa kimya na ushiriki wa Ufaransa, kwa upande wake ulianza kuonekana.

Huko jijini Antwerp, miongozo iliyotolewa na mwenzetu, wakati mwingine ilikuwa ni ya kidikteta na ilifanya mambo mazuri. Kila kitu kilipaswa kuanzishwa tangu mwanzo, na kila kitu kilifanyika - bila shaka si kwa kiwango cha kifahari na kwa uzuri uliotarajiwa katika miradi ya awali iliyowasilishwa kwenye IOC kabla ya vita, wakati waraka wa kugombea wa jiji uliwasilishwa kwa mara ya kwanza, lakini kwa utaratibu mzuri, kwa kiasi, busara na umaridadi. Kuhusu idadi na ubora wa maingizo, tulihakikishiwa haraka. Moja ya wasiwasi mkubwa wa kawaida ulihusiana na mauaji ya kikatili kwa wanamichezo wengi na ukosefu wa mafunzo kwa wale waliobaki. Katika hali hii, Michezo ya Kirafiki, iliyofanyika Paris wakati wa Majira ya vuli ya mwaka 1919 chini ya usimamizi wa Jenerali Pershing, ambaye alikuwa na uwanja uliojengwa kwa ajili hiyo karibu na Vincennes ambao bado una jina lake. Michezo iliandaliwa kwa nia ya kuwaweka sawa kiafya na kuwafanya wafurahie kama njia ya kuchukua nafasi za askari wa majeshi tofautitofauti, ambao walirejeshwa nyumbani kutokana na sababu nyingi, jambo ambalo halikupewa kipaumbele kwa sababu idadi yao kubwa ilikuwa kwenye nchi ya Ufaransa wakiwa na shughuli chache sana za kufanya. Kwa kawaida, majaribio yalikuwa yamefanywa katika duru fulani ili kupotosha umma kwa kuzungumza kuhusu "Mashindano ya Michezo ya Olimpiki ya Kijeshi" na kupendekeza kwamba yanapaswa kufanyika wakati wa Mashindano ya Michezo ya Olimpiki ya kawaida mwaka mmoja kabla ya wakati. Kwa mara nyingine tena suala likawa ni idadi ya Michezo na muda wa kila baada ya miaka minne! Hapa nina barua kutoka kwa J.J. Jusserand, akinipa maelezo ya hatua alizokuwa akichukua (Rais Wilson alipokuwa Paris wakati huo) na kunihakikishia kwamba Wamarekani hawangeruhusu kamwe matumizi ya maneno "Olimpiki" au "Mashindano ya Olimpiki" kwa madhumuni kama hayo. Michezo ya Kirafiki, kama inavyotarajiwa, ilionesha vilevile kwamba matumizi ya nguvu na shauku ya michezo haikuwa ikipungua.

Michezo ya 7 ya Olimpiki ilifunguliwa kwa uzuri mnamo tarehe 14 Agosti, 1920, mbele ya Mfalme na Malkia wa Ubelgiji, akiambatana na kiongozi wa Brabant, Mwanamfalme Charles na Bintimfalme Marie-Jose. Gwaride, hotuba ya ufunguzi, kwaya, urushwaji wa njiwa, saluti ya bunduki, sherehe zote za kifalme, thamani yake ya kielimu ambayo ilikuwa imeanza kutimizwa huko Stockholm, ilionesha jinsi ambavyo Michezo ya Olimpiki

bado ilikuwa na nguvu, hata mara tu baada ya vita, na kwa namna ambavyo tuzo zake ziliendelea kuthaminiwa kuliko tuzo nyingine zote za michezo kwa vijana duniani. Wakati wa jioni, Mfalme na Malkia walifanya karamu huko Ikulu kwa heshima ya Kamati ya Kimataifa ya Michezo ya Olimpiki; hii ilifuatiwa na mapokezi makubwa sana, ambayo mwisho wake wafalme waliondoka kwenda Brussels. Kadinali Mercier, aliyekuwa hapo, alikuwa akiongoza ibada ya kidini asubuhi hiyo kwenye kanisa kuu, aliona wakati huu kulikuwa na mpango tofauti na ule uliofanyika mwaka 1912. Kuhusu jambo hili bado sijapata fursa ya kueleza. Kwa kutoa huduma kwa umma katika uwanja wenyewe, kama huko Stockholm, kabla ya kuanza kwa mashindano, tutakuwa tukiwalazimisha wanamichezo, ambao tayari ni watu wazima, washiriki katika sherehe ya kidini ambayo inaweza kuwachukiza wengine. Kwa kuwaalika, nje ya Michezo hiyo, kwenye sherehe kanisani, tulikuwa tu tukihusisha dini kama nguvu nyingine yoyote kubwa ya maadili ya wanadamu na sherehe ya Michezo ya Olimpiki, Kisha tena, ilikuwa muhimu kwamba sherehe hiyo isiwe ya upande wowote katika kuelezea tofauti zote za mafundisho. Hakuna misa, hakuna hotuba ya kikuhani madhabahuni, *De Prefunds*, wimbo wa kumbukizi ya wafu wa miaka minne iliyopita, na *Deum*, wimbo wa mafanikio na matumaini, *lay hymns*, tunaweza kuziita hivyo zinazofaa kwa tafsiri nzuri ya kimuzuki. Ambayo inaweza kuongezwa hotuba, mradi ilikuwa imefundishwa katika masharti huria. Programu hii isiyo ya kawaida ilimvutia Kadinali Mercier. Sherehe hiyo ilikuwa na ukubwa maalumu wakati huu kwa sababu ya ukweli wa kusikitisha kwamba orodha ya waliokufa kwenye Michezo ya Olimpiki ilikuwa ndefu sana. Na wote waliokuwapo wakatoka, ninaamini, nimevutiwa sana na maneno yaliyosemwa katika Kanisa Kuu na kasisi maarufu katika ibada ya kusisimua iliyoambatana na muziki mzuri wa kwaya na vyombo. Wakati wa Michezo hiyo, mamlaka zote za kisiasa, kiraia na kijeshi za jiji, jimbo na nchi zilionesha nia ya dhati ya mafanikio yao. Hakuna zaidi ya Gavana wa Antwerp, Baron Gaston de Schilde, ambaye alikuwa maarufu sana kwa wote waliokutana naye. Antwerp ilikuwa imepambwa vizuri. Kutoka katikati ya jiji hadi uwanja wa michezo. Njia hiyo ilikuwa na bendera za Michezo ya Olimpiki. Kila mahali pete tano za rangi nyingi na kaulimbiu: *Citius, Alitius, Fortius* zilioneshwa kwa uwazi. Sherehe zilikuwa nyingi na zenye mafanikio makubwa na wapiga zumari kutoka kwenye kikosi cha Scotland mara nyingi waliongeza vionjo vya kupendeza.

Wanachama wakongwe zaidi wa IOC, Jenerali Balck, Profesa Sloane, Mchungaji Laffan, Daktari Guth-Jarkovsky, Baron G. de Blonay, Baron van Tuyll na Count von Rosen walijikuta, kwa mara nyingine tena, wameungana katika fikira zilezile, na karibu nao, idadi kubwa ya wengine waliunda kikosi kilichokua cha wale ambao hatimaye wangechukua na ambao wangekabidhi mwenge. Wenzake wa mbali walikuwapo pia; Wajapani, Wahindi, Waafrika Kusini, Wabrazili, wenzao muhimu kutoka kwenye mataifa yaliyokombolewa hivi karibuni- Waayalandi, Poland ambao waliwasilisha ugombeaji wao, mwakilishi wa Jiji la Los Angels, aliyekabidhiwa jukumu la kuhakikisha mustakabali wa Michezo kwa jiji hili unapatikana, wawakilishi wa YMCA, sasa


wamevutiwa sana na nguvu ya Michezo ya Olimpiki, ambayo mara nyingi walikuwa wameipuuza hapo awali. Miongoni mwa wale wa mwisho - waliotajwa mkereketwa, Elwood Brown, ambaye angekuwa mtetezi wa Michezo ya Olimpiki kwa miaka inayofuata kote Mashariki ya Kati na ya Mbali. Je, Michezo ya mwaka 1924 ingefanyika wapi? Suala hili lilikuwa akilini mwa kila mtu. Kwa kweli kulikuwa na ukosefu mkubwa wa makubaliano kati ya maofisa wa michezo. Wote walitaka mpango mkubwa, lakini hawakujua ni upi kati ya mageuzi, ubunifu na mabadiliko. Katika hotuba niliyoitoa mbele ya Mfalme siku ambayo Mfalme alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Mkutano wa IOC, nilionesha kwamba matumaini yetu ya siku zijazo yalikuwa katika upanuzi wa kidemokrasia. Mfalme alikuwa mmoja wa wale ambao mbele yao mtu anahisi kuwa huru kutoa mawazo yake. Lakini hakuna mwelekeo wa uhakika ambao ungeweza kutambulika bado, lilikuwa jambo la busara zaidi kungoja na kuona. Nilishauri kuahirisha uamuzi huo na wakati huohuo nikapendekeza kuitishwa kwa kikao. Huko Lausanne mnamo mwaka 1921, mkutano ambao ungerekebisha, kwa kadiri hali mpya inavyohitajika, uamuzi wa kitaalamu uliofikiwa huko Paris mnamo mwaka 1914, na ambao wakati huu walialikwa Wajumbe wa Shirikisho la Kimataifa na pia yale ya Kamati ya Michezo ya Olimpiki ya Kitaifa.



44. Kuanza kwa mbio za kilometa 60 huko London mwaka 1908



45. Fainali za mbio za meta 100 huko Paris mwaka 1924



46. Sherehe za Ufunguzi, huko Antwerp mwaka 1920



47. Marta Adiertz: Stockholm mwaka 1912

Mbali na mkutano huu, nilipanga mwingine, wa masuala ya kielimu na kijamii, kwa madhumuni ya kutafiti hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuandaa michezo kwa ajili ya watu wengi. Hili ndilo vuguvugu ambalo nilitaka kulianzisha nchini Ufaransa mnamo mwaka 1906 na ambalo wakati huu lingekuwa katika kiwango cha ulimwengu chini ya mrengo wa IOC.

IOC ilitoa makubaliano yake. Mazingira ya mikutano yetu yalifichua hali ya kutokuwa na uhakika na kusitasita kuhusu mwelekeo utakaochukuliwa. Nilihisi hamu isiyoeleweka kwa upande wa wanachama kutokuwa na uamuzi wa kuchukua na kuniachia kila kitu. Ilikuwa dhahiri kwamba uchaguzi wa mahali pa Michezo inayofuata ungepaswa kuahirishwa, lakini kama hii ingekuwa hivyo, basi Paris isingetarajia kuona inakubaliwa kuwa mgombea. Huzuni ilitawala miongoni mwa Wafaransa, timu zao hazikuwa maarufu hata katika matukio ya wapanda farasi. Ndani ya IOC yenyewe, maoni ya "wasio na upande wowote" yalielekea kutawala na kwao Paris ilionekana kuwa chaguo ambalo lingeendeleza kumbukumbu za vita. Kwa upande mwingine, mashirikisho ya Ufaransa yalidai kutunukiwa Michezo hiyo, yakisema kwa sauti kubwa kwamba "basi tutaona jinsi Michezo ya Olimpiki inavyopaswa kupangwa" na Mashirikisho machache ya kigeni yalisikiliza kwa hiari maneno haya. Vyombo vya habari viliunga mkono madai haya kwa dhati. Sikushawishika hata kidogo kuhusu uwezekano wa mpango huo, lakini nilihisi kuwa haikuwa wazo baya kuwapa nafasi. Kwa hiyo nilifikiri akilini mwangu mbinu isiyo ya kawaida na kungoja kimyakimya kwa wakati unaofaa ili kuuweka katika utekelezaji.

# XVIII

## Mbinu za mwaka 1921



48. *Marais watatu wa IOC wakiwa mbele ya Casino de montherion huko Laussanne tarehe 7 Mei, 1921. Kutoka kushoko kwenda kulia: Sigfrid, Pierre de Courbetin na Count de Ballet- Latour pamoja na Baron de Blonai.*

Hali hiyo ilihitaji zaidi ya yote tamko la umoja, na ndiyo maana kiongozi aliyekuwa madarakani alihisi kwamba kila mtu alikuwa akimtazamia kuongoza njia thabiti. Hatari haikuwa sana kiasi kwamba chombo kingine kinaweza kufanikiwa kuichukua Michezo ya Olimpiki. Mwanasiasa wa Ufaransa na mwandishi wa habari wa Ufaransa walikuwa wakiendesha kampeni isiyozaa matunda ya kuikabidhi Michezo kwa Shirikisho la Mataifa *(League of Nations),* ambalo halikuwa na misingi thabiti. Mapendekezo kama haya yalikuwa na nafasi ndogo sana ya kukubaliwa na ilikuwa rahisi kuyapinga kama ilivyokuwa upinzani wa baadhi ya mashirikisho fulani, yakiwa na shauku ya kuona wajumbe wao wameketi kwenye meza ya IOC. Hatari kubwa ilikuwa katika kufifia kwa wazo la Michezo ya Olimpiki, ambalo lilihatarisha kuletwa na kuenea kwa michezo ya kikanda ambayo ilikuwa matokeo ya kukosa uvumilivu, hali iliyoonekana kutawala. Zilikuwa zinaundwa hapa, pale na kila mahali, au angalau tulikuwa tukishambuliwa kila mara na mipango, programu na matangazo ya uundaji wa kamati na kamati ndogo.

Wakati wa miaka miwili ya mwisho ya vita, tishio la kujitenga lilikuwa linaonekana katika Michezo ya Olimpiki. Kwa hatua zisizo za moja kwa moja na zisizo rasmi siku zote nilikuwa nimefaulu kuzuia majaribio yoyote kama hayo. "Shirikisho la Wasioegemea upande wowote", ambalo kwa muda lilitangazwa, halijawahi kuwa zaidi ya mradi bila

kitu chochote halisi. "Shirikiso la Belligenrent" la kikundi cha Wajerumani halikuwa chochote zaidi ya wazo lisiloeleweka na hata kama wangejaribu kulimaliza sasa, hakika lingekuwa la muda mfupi tu; Hungaria na Uturuki pengine zingesitasita sana kujiunga nalo. Kwa upande mwingine, ikiwa "Michezo" hii yote ambayo ingepangwa katika nchi ya Poland, Catalonia, Balkan, India na Mashariki ya Karibu ingeruhusiwa kukita mizizi, huenda ingesababisha nyufa katika muundo wa Michezo ya Olimpiki. Ni kweli kwamba shughuli zote hizi zilitazamia baraka zetu na zilitegemea ushiriki wetu. Lakini kwa kiasi kikubwa hawakujua mambo ya Michezo ya Olimpiki na kutofahamu misingi ya IOC, walioyatunga na kutaka kuyapanga nia ngumu ya utaifa au tabia ya kidini ambayo ingevuruga tu harakati nzima mwishowe.

Niliuacha mwaka 1920 ukaribie na mabishano madogomadogo yaliyoachwa katika Michezo ya Antwerp yanaisha, utatuzi wa migogoro ya kiufundi ya akaunti, n.k. Mtazamo wa jumla ulioachwa na Michezo hii haukuathiriwa. Katika kipindi hiki nilikuwa nimeanzisha maandalizi ya Mkutano wa Lausanne. Serikali ya Shirikisho la Uswisi ilikuwa imekubali kwamba mialiko hiyo itolewe katika kila nchi na mabalozi na balozi za Uswisi. Ilikuwa muhimu kwamba wangefika mapema, husasani katika wakati huu mgumu zaidi kuliko ilivyokuwa kipindi cha Juni 1914. Huko Paris ilitubidi tu kuwaalika wajumbe wa Kamati za Kitaifa kwa madhumuni ya kuandaa orodha ya matukio mbalimbali katika kila mchezo na hali ya kiufundi inayowaongoza. Mnamo mwaka 1921, tulikuwa na tatizo lilelile lakini mengine mengi yalikuwa yametokea wakati huohuo, jambo ambalo halikuwa la kufaa kuyaweka yote pamoja ili kujadiliwa kwenye kikao kimoja.

Ratiba za "Mikutano na Makongamano ya Michezo ya Olimpiki" zinatoa picha halisi ya ukubwa wa tatizo. Kwa kweli, kulikuwa na mfululizo mzima wa mikutano iliyopangwa kutoka tarehe 26 Mei hadi 12 Juni 1921: kwanza kabisa Mkutano wa Ushauri wa Michezo ya Majira ya Kipupwe (Mei 26 na 27), kisha Mkutano wa Upandaji Milima (Mei 28), ukifuatiwa na Mkutano wa Michezo ya Kupanda Farasi (Mei 29 na 30). Kilichofuata kilikuwa ni Mkutano wa Mashirikisho ya Kimataifa ulioandaliwa na Bw. Paul Rousseau ambaye alikuwa akipanga kuanzisha aina ya shirikisho kuu au baraza la mashirikisho; suluhisho ambalo lingekuwa msaada au kizuizi kulingana na mtazamo uliokuwapo wakati huo, lakini ambayo ni ya kimsingi. Sikupinga kwa vyovyote vile, kama ambavyo wengine walionekana kuamini. Mkutano wa Michezo ya Olimpiki ungefanyika kuanzia tarehe 2 hadi 7 Juni. Hatimaye mipango ilikuwa imefanywa ya kufanya Kongamano la Mashauriano la Fasihi na Sanaa, na Mkutano wa "Manispaa", uliokusudiwa tu kufanya maandalizi kwa mtazamo wa maandalizi ya michezo kwa umma na "kurejeshwa kwa michezo ya kale ya sarakasi" ambayo nilikuwa nimezungumzia kwa mara ya kwanza huko Paris, mnamo Novemba 1912 na ambayo ilibaki - kama ilivyo – tofauti na matarajio ya moyo wangu.

Mara programu hii kubwa ilipoidhinishwa na IOC, niliandika waraka kwa wenzangu, nikautuma kwao na wakati huohuo nikatoa taarifa kwa waandishi wa habari. Ilikuwa

tarehe 17 Machi 1921. Tangazo la uamuzi wangu wa kujiuzulu baada ya Michezo ya 1924 lilitanguliwa na vifungu vifuatavyo: *Uchaguzi wa jiji kwa ajili ya hatua zaidi (Michezo inayofuata) ni muhimu sana; wakati huu, kutokana na ukweli kwamba Michezo ya 8 ya Olimpiki itaambatana na kumbukumbu ya miaka thelathini ya ufufuaji wake. Wagombea wengi wa kuridhisha wamepokewa. Ikiwa tutazingatia sifa za miji pinzani, jina la Amsterdam linaonekana kutawala. Lakini, kwa upande mwingine, wakati mfufuaji wa Michezo ya Olimpiki atakapoamua kazi yake ya binafsi kuwa imekaribia mwisho, hakuna mtu atakayekataa kwamba tuna haki ya kuuliza kwamba ishara maalumu inapaswa kufanywa kwa niaba ya jiji lake la asili, Paris, ambapo ufufuaji wa kisasa wa Michezo ya Olimpiki ulitayarishwa na kutangazwa naye rasmi mnamo Juni 23, 1894. Kwa hiyo ninapenda kuwajulisha kwa dhati, washirika wangu wapenzi, kwamba katika mkutano wetu ujao nitawaomba nyote kuhusu tukio hili kuu la kutoa utashi wenu na masilahi yenu ya kitaifa na kukubali kupeleka Michezo ya 9 ya Olimpiki Amsterdam na kulitangaza jiji la Paris kuwa eneo la Michezo ya 8 ya Olimpiki*.

Yalikuwa ni mapinduzi ya kiufundi! Na kwa hakika ilikuwa ni mara mbili tangu uamuliwe mustakabali wa Michezo miwili ya Olimpiki, hakuna kilichoizuia IOC kuchukua uamuzi wowote lakini ambao haikuwahi kuchukua hapo awali. Kulikuwa na mkanganyiko na mshangao fulani huko Paris na mahali pengine pia. Hakuna mtu aliyetarajia uingiliaji kati huo mkubwa wa Rais. Kimaadili ilikuwa vigumu kukataa kile nilichokuwa nikikiomba. Ndiyo maana, mara tu hali ya kusitasita kwa mara ya kwanza ilipoisha, duru za michezo za Ufaransa ziliacha upinzani mkubwa uliokuwa ukijengeka dhidi yetu na ugumu uliokuwa unaendelea, vilitoweka na hali ikawa shwari.

Mfululizo wa "Makongamano na Mikutano ya Olimpiki" yalifunguliwa katika hali nzuri, yakiwa na matokeo yenye tija. Hali hiyo iliendelea katika mikutano hiyo, licha ya masuala magumu yaliyoulizwa na mijadala mikali ambayo ilipaswa kufuata. Kwanza kabisa kati ya hayo yalikuwa changamoto ya "Michezo wakati wa Majira ya Kipupwe". Waskandinavia hawakuitaka hata kidogo. Mnamo 1894, michezo ya kuteleza kwenye barafu ilijumuishwa katika orodha ya matukio yanayohitajika. Mnamo 1908, London ambayo ilikuwa na "jumba la barafu", iliweza kuandaa matukio ya kuridhisha. Lakini mnamo 1912, Stockholm iliweka msimamo kwamba haikuwa na eneo linalofaa, ili kuondoa mzigo wa kuandaa tukio hili. Hata hivyo katika miaka ishirini na mitano iliyopita, michezo ya wakati wa Majira ya Kipupwe haikuwa imeanzishwa katika nchi kadhaa na ilikuwa ya ridhaa, kiuhalisia hadhi ya michezo hii iliondolewa kutoka kwenye programu ya michezo ya Olimpiki na kuifanya kutokuwa na thamani. Kwa upande mwingine, walipaswa kupangwaje? Mbali na upinzani wa Skandinavia, kulikuwa na masuala mawili ambayo yasingeweza kufanyika kwa wakati mmoja au mahali pamoja na Michezo ya Majira ya Kiangazi. Ingewezekana kutengeneza barafu bandia, lakini sio theluji, na hata kilele kidogo cha mlima. Je, Waholanzi wangetarajiwa, katika mwaka 1928, kusimamisha safu za milima ya zamani au kufanywa mahususi kwa ajili ya tukio

hilo? Hata hivyo kuunda kwa safu hizo kulihusiana na nchi ya Skandinavia, ambayo ilikuwa ndio suluhisho la pekee, ingawa kulikuwa na vikwazo. Kwa sababu hii, nilikuwa nimejaribu kukatiza mjadala kwa mkutano wa kwanza kati ya wataalamu, ripoti ya Bw. A. Megroz, kwa niaba ya Mkutano wa Mshauri, kwa kiasi fulani ilipunguza mshtuko na mwishowe ulivunjwa nje ya nchi kwamba Ufaransa - ikiwa ingechaguliwa (ambayo haikuwa hivyo bado) - itakuwa na haki ya kupangwa, huko Chamonix mnamo 1924, wiki ya michezo ya Majira ya Kipupwe ambayo IOC ingeweza kutoa udhamini wake, lakini bila ya kuwa na " sehemu halisi ya Michezo". Kifungu hiki cha mwisho kilifutwa baadaye. "Michezo ya Majira ya Kipupwe" ilianzishwa mwisho licha ya Waskandinavia ambao walimaliza kwa kuacha pingamizi lao na kutambua kwamba kwa kuzingatia majukumu ya hasa Uswizi na Kanada hawakuweza tena kuwa na madai ya kutawaliwa ambayo walikuwa nayo kwa muda mrefu.

Ripoti ya Mkutano wa Upandaji Milima ilitayarishwa na mpanda milima maarufu, Dkt. Jacot-Guillarmod, anayejulikana sana kwa safari zake za Himalaya. Vilabu vichache vya Alpine viliwakilishwa ingawa kimsingi walikuwa wamekubali kushiriki bila shauku kubwa. Kwa kweli, ni ngumu sana kupima sifa za kulinganisha za ushujaa kama za aina hii, lakini, kwa kuwa hakuna kilichozuia kila Shindano la Olimpiki ama kutangaza kwamba hakukuwa na sababu za kutoa tuzo kwa washindi au kutangaza washindi wawili wa tuzo wa zamani wa Aequo, pendekezo la kualika kila kilabu cha Alpine kuweka mbele madai ya wagombea wake halikuwezekana hata kidogo. Huko Chamonix mnamo 1924 hakukuwa na shaka yoyote akilini mwa mtu yeyote kwani msafara wa Mlima Everest ulizidi kwa mbali uwanja wote kwa uvumilivu na ujasiri, lakini katika mwaka 1928 tulilazimika kuacha zawadi hii ya kupanda milima na, kama nilivyokwishasema, katika kufanya hivyo, kwa maoni yangu tulifanya makosa makubwa sana.

Mkutano wa Michezo ya Wapanda Farasi uliitishwa kwa mwaliko maalumu ulioelekezwa kwa Mawaziri wa Vita. Haipaswi kusahaulika kwamba mikutano hii yote ilikuwa ya mashauriano tu, yaliyoandaliwa kwa madhumuni ya kuwaandaa wajumbe ama wa IOC au wa Mkutano, kutegemea ni mkutano gani ulihusika na masuala yaliyoibuliwa. Tayari nimetaja jinsi Michezo ya Kupanda Farasi ilivyokuwa mizuri kwenye Mashindano ya 5 ya Olimpiki (Stocholm 1912), shukurani zimemwendee Count von Rosen kwa juhudi zake, lakini muktadha wote ulikuwa wa kijeshi pekee.

Bila shaka ilikuwa ni jambo lisiloepukika kwa sababu, mbali na uwindaji na michezo ya polo, michezo ambayo ni ghali sana kuchezwa na mtu mwingine isipokuwa mamilionea uliowekewa vikwazo- michezo ya upandaji farasi wa raia iko chini ya mwavuli wa jeshi. Mbali na nchi fulani zinazozalisha farasi, kwenye makoloni ambako farasi hutumika kama nyenzo ya usafiri au maeneo kama California ambako farasi huzalishwa kisasa, mbio za farasi zimekuwa zikikwamishwa na mipango duni ambayo ingeweza kuondolewa na mipango mizuri ya serikali. Lakini hatua kama hiyo haikutokea kwa mtindo na kwa kiwango kinachohitajika. Haiwezekani kwangu kujaribu kuchunguza

suala hili hapa; itachukua muda mrefu sana. Kwa zaidi ya miaka ishirini na mitano, sijawahi kuacha kuleta jambo hilo katika vifungu au mipango ya aina mbalimbali, lakini siku zote nikiwa na lengo moja, kueneza mchezo wa farasi miongoni mwa "wasiopanda", hii ikimaanisha wale ambao hawana uwezo wa kutunza farasi wao wenyewe. Nilipata uhakikisho mwingi wa idhini kutoka kwa watu mbalimbali kama vile "mwendeshaji mbaya" Theodore Roosevelt na mpanda farasi mashuhuri Count Maurice de Cosse'-Brissac, lakini ilipofika wakati wa kutekeleza hatua hizo, nilikumbwa na kizuizi kisichoweza kuzuilika, kana kwamba lilikuwa suala la utashi, au kujinyima haki ya msingi. Bado ninaweza kusikia mirindimo ya makofi ya kushangilia hotuba fulani zilizotolewa kwenye karamu ya Michezo ya Wapanda Farasi huko Stockholm mwaka 1912 ... na waliohudhuria walijumuisha kundi la Wafalme, Viongozi Wakubwa, wakuu wa misheni, na maofisa wote walioshiriki katika mashindano hayo. Kila mtu alionekana kukubaliana kwa moyo wote. Lakini hii haikuwa hivyo kwa kweli. Mashujaa wa Enzi za Kati hawakuwa wa kiungwana kabisa katika maoni yao ya kupanda farasi kuliko warithi wao leo. Katika Mkutano wa 1921, ambao ulihudhuriwa pamoja na watu wengine na Jenerali wa Italia Belloti na Jenerali wa Ubelgiji Joostens, ningeweza tu kukubali maoni yangu kama uwezekano wa mbali na sina budi kujitosheleza kwa kuambatisha muhtasari wake kwenye kumbukumbu za mkutano. Programu ya wapanda farasi wa michezo ya Olimpiki ilibaki kama ilivyokuwa angalau kwa muda, lakini masuluhisho ya muda ya aina hii yana njia ya kudumu kwa muda usiojulikana.

Paul Rousseau hakufanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuunda shirikisho lake kuu. Ilibidi aridhike na udumishaji wa "Ofisi ya Mashirikisho ya Kimataifa" ambayo ilitoa kwa kusitasita tu haki za chini za kuingilia kati na njia tupu za kuishi. Sijui kama chombo hiki kipya kingefikia matarajio ya mhamasishaji wake, lakini kwa mtazamo wa Olimpiki bila shaka kingeisaidia IOC kwa nafasi ya kiufundi ambayo ilikuwa kubwa sana na majukumu ambayo nilikuwa nikitarajia kila wakati ingekuwa na uwezo wa kutupa mbali siku moja. Kwa vyovyote vile, Mkutano wa Mashirikisho ya Kimataifa, katika mkutano wa kwanza ambao niliombwa kufungua na kwenye karamu ya mwisho, ilionesha kwamba enzi ya kutoelewana ilikuwa na mwisho kati yao na IOC.

Kongamano la Olimpiki lenyewe, ambalo nilimteua, kama ilivyokuwa haki yangu, mwenzetu wa Uswidi J.S Edstrom kama Rais, lilikuwa la kusisimua sana, na nyakati fulani lenye dhoruba. Edstron aliongoza kwa ujitoaji wake wa kawaida, kipaji cha werevu ... na onesho la mamlaka ambalo lilinifanya nitabasamu nilipofikiria ni mara ngapi nimekuwa nikishutumiwa kwa ubabe. Hali ilikuwa tofauti sana na ile ya Mkutano wa 1914, licha ya ushawishi wa utulivu wa mazingira ya mpangilio wa Vaudois. Madhara ya miaka ya vita ambayo yalikuwa yamepita tu yalikuwa yakiwafanya waendelee kuhisi.

Hisia za utaifa ziliamshwa kwa jambo dogo zaidi na, wakati mwaka wa 1914 tulikutana kwa madhumuni ya kutunga sheria ya kudumu ya Olimpiki, wakati huu kutokuwa na

utulivu na kutokuwa na uhakika kulitawala. Tangu mwanzo, wajumbe walizingatia uwezekano wa Mkutano mpya mwaka wa 1925, ambao ungeweza kuitishwa ili kurekebisha kile kilichoamuliwa mwaka wa 1921: ni wazi kwamba kulikuwa na hali ya kusikitisha, ambayo hata hivyo iliruhusu kuongezwa muda fulani. Kwa hiyo mara tu ilipokutana, Mkutano ulikubali, kama ilivyotarajiwa, kwenye ukumbi kwa ajili ya Michezo miwili ijayo. Katika kikao cha kwanza kabisa kilichofanyika tarehe 2 Juni jioni, IOC ilikubali maombi yangu ya kuandaa maadhimisho ya 8 na ya 9 ya Olimpiki huko Paris na Amsterdam.

Hoja hiyo ilikuwa imependekezwa na Bw. Guth-Jarkovsky, na kuungwa mkono na Messrs, de Baillet-Latour na de Polignac. Pingamizi liliibuliwa kwa sababu ya ukiukwaji wa taratibu, hoja hiyo ilipigiwa kura ya pili, ambayo ilitoa kura ya pili ya kura hiyohiyo kwa watu walio wengi kuunga mkono tuzo ya mara mbili ambayo nilikuwa nimejiepusha nayo, wakitaka chini ya hapo awali kuingilia uhuru wa kupiga kura lakini ingekuwa ya kusikitisha sana kuona Amsterdam- ambayo ilikuwa imeonesha moyo mkuu wa michezo na nia njema ya kimataifa kwa kujiondoa na kuipendelea Antwerp na ilikuwa ikifanya vivyo hivyo tena katika mwaka 1921 kwa kuipendelea Paris, chini ya masharti ambayo tayari yametajwa- kunyimwa kuridhika kwa muda mrefu kunasubiriwa na hivyo kudaiwa kihalali. Kuhusu Paris, kila mtu alikuwa katika makubaliano. Ingekuwa hivyo kwa Amsterdam isipokuwa kwa ukweli kwamba, kadiri Mkutano ulivyokaribia, hasira mbaya zilizuka nchini Italia na mashambulizi ya hasira huko Amerika. Roma ilikuwa imegundua ghafla kwamba ingeweza kupata Michezo ya 1924 au kwa vyovyote vile ile ya 1928, na Los Angeles, iliona nafasi yake imeahirishwa hadi 1932 mapema zaidi, ilizingatia kusubiri kwa muda mrefu sana kwa maoni ya Atlantiki, iliyozoea kama ilivyokuwa kwa haraka kuchukua hatua. Pande zote mbili za Atlantiki vyombo vya habari vilikuwa vimeitikia, kwa bahati bila madhara kuhisiwa hadi wakati fulani baada ya kuchapishwa kwa barua yangu tarehe 17 Machi. Furaha ya Waitaliano ilikuwa imefikia kiwango cha juu ndani ya siku chache ambapo Bw. Gaston Vidal, Katibu Mkuu wa Jimbo la Elimu ya Ufundi, aliona ni bora kuchukua nafasi yake wakati wa mwisho kama mwakilishi wa Kamati ya Olimpiki ya Ufaransa kwenye Mkutano wa Lausanne. Mwenzetu Montu alifadhaishwa na kuamua kujitoa baada ya kura. Kwa ujumbe wa Marekani, walionekana kuwa na kinyongo lakini hawakujua jinsi ya kujieleza kwani hapakuwa na sababu za msingi.

Tangu matukio ya 1901 na 1905 (kuhamishwa kwa Michezo ya 1904 na 1908 kutoka Chicago hadi St. Louis na kutoka Roma hadi London), IOC ilikuwa imeamua kuzingatia maombi tu ambayo yaliungwa mkono na shirika ambalo tayari limeandaliwa vizuri na kwa udhamini wa fedha nyingi. Ndivyo ilivyokuwa kwa Stockholm, Berlin na Antwerp; na itakuwa kwa Amsterdam pia. Roma, kinyume chake, haikutoa tena dhamana yoyote, hakuna kamati iliyokuwa imeundwa, wala hapakuwa na fedha za kugharimia. Katika nyakati hizi za taabu baada ya vita na kwa hakika nimeamua kustaafu, kulikuwa pia,

zaidi ya hoja zote zilizokwishatajwa, kwa upande wangu, nilikusudia kupanga mambo kwa siku zijazo ili hali ya utulivu iendelee kuwapo katika kipindi cha kiongozi ambaye angefuata baada yangu.

Kwa mtazamo huohuo na kwa kisingizio cha safari ndefu niliyoipanga wakati huo, niliishawishi IOC kuidhinisha kuundwa kwa Bodi ya Utendaji ambayo haikuwa nyingine bali ni “ofisi” iliyopanuliwa, ambayo ni kuweka masula ya sheria ya hali ya mambo ambayo tayari imeimarishwa. Bodi, ambayo ingeanza kazi rasmi tarehe 1 Oktoba 1921, ilijumuisha Messrs, de Blonay, Guth-Jarkovsky; de Baillet-Latour, Edstrom na de Polignatic.

Misingi mingi ilikuwa imewekwa huko Lausanne bila kuvuruga, lakini kwa njia isiyo sawa. Maandalizi yalikuwa mazuri sana, shukurani ziwaendee mamlaka zinazohusika na Kamishna Mkuu, rafiki yangu Eugene Monod, ambaye alikuwa ameshinda shindano la usanifu katika mwaka 1911. Sasa tulikuwa na miaka mitatu mbele yetu kufanya Michezo ya 8 ya Olimpiki iwe "bora zaidi na kamilifu kuliko ambavyo imewahi kushuhudiwa". Haya ndiyo yalikuwa matamanio ya waandaaji na walitarajia kwa nia njema kufanikiwa kabisa katika azma yao.

# XIX

## Idara Sita za Serikali kwenye Uwanja Mmoja (1922)






*Bw. Louis Faure - Duke na Uwanja wa Michezo ya Olimpiki wa Colombus ambao aliusanifu.*

Matumaini yao yalikatishwa tamaa mara ya kwanza. Kichwa cha hapo juu cha makala ya kuhuzunisha ya Bw. Robert de Jouvenel, iliyochapishwa katika *"EQeuvre",* kinatoa maelezo ya kile kilichotokea. Ndani ya muda mfupi sana kwa kweli Michezo ya Olimpiki iligeuka kuwa mawindo ya utawala wa joka kubwa na wakuu wa nchi sita. Mbali ya Baraza la Manispaa la Paris, Idara za Mambo ya Ndani, Mambo ya Nje, Vita na Elimu ya Umma zilihusika moja kwa moja katika jambo hilo. Makubaliano na Idara ya Kilimo kuhusu eneo ambalo Kamati ya Olimpiki ya Ufaransa ilitaka kujenga uwanja wake yalileta idadi ya Idara hadi sita. Tarehe 27 Juni 1921, muda mfupi baada ya Kongamano la Lausanne kumalizika, Count Jean de Castellance aliwasilisha ripoti kwenye Baraza la Manispaa, ambalo alikuwa mjumbe wake, pendekezo lililotanguliwa na ripoti fupi iliyo wazi kabisa. Ingewezekana kuanza kuanzia hapo bila ya nia yoyote ovu kuhusu manufaa ya kibinafsi au masilahi ya wilaya mbalimbali. Michezo hiyo ingeweza kutayarishwa kwa wakati uliotakiwa. Kwa isivyo bahati, haikuwa hivyo. Iwapo mtu alilinganisha waraka huu wa mwanzo ambao nimetoka kuunukuu na ripoti ya kikao cha Baraza cha tarehe 11 Machi 1922, kama ilivyochapishwa katika "*Taarifa Rasmi ya Manispaa"* ya tarehe 12 Machi, angetambua fujo mbaya iliyokua katika muda mfupi wa takribani miezi minane swali rahisi sana ambalo isivyo bahati lilikuwa gumu na lingine ambalo halikuwa la aina hiyo. Kama Bwana de Castellance alivyosema watalazimika kufanya maandalizi ya uwanja wenye uwezo wa kuchukua watazamaji wapatao 80,000, eneo la michezo ya baharini na moja kwa ajili ya michezo ya mapigano lenye viti takriban 15,000. Zaidi ya hayo wangelazimika kupanga upatikanaji wa usafiri unaofaa, na hatimaye kukadiria jumla ya mikopo inayohitajika. Baada ya hapo, wangelazimika

kuweka fedha tu kwa Kamati ya Olimpiki ya Ufaransa, chini ya udhibiti wa kamisheni ya usimamizi inayoiwakilisha serikali na Jiji linalohusishwa kwa sababu ya upigaji kura wa pamoja wa sifa zinazohitajika. Bunge la Ufaransa lilikuwa tayari kupiga kura kuhusu suala hilo. Baraza lisingekuwa na wasiwasi zaidi na kuchukua fursa ya hali hiyo kuunda kitu cha kudumu. Yeyote anayeijua Paris, miundo yake ya kiutawala, ari ya mamlaka yake na nafasi yake ataelewa kwa urahisi athari tofauti kabisa zinazoletwa na miradi yoyote ya ujenzi, ikiwa miradi hii ni ya muda au ya kudumu. Mwishowe, masilahi, bila kueleza mahitaji, migongano na vurugu vilitokea kiasi kwamba wale wote wanaohusika walipoteza hatua ya kuanzia au lengo la kufikiwa.

Hiki ndicho kinachotokea katika tukio la sasa. Kuanzia Desemba 1921 hadi Aprili 1922 hali ya kuchanganyikiwa ilizidi kuwa mbaya hatua kwa hatua, na kufikia mwezi Machi mambo yalikuwa mabaya sana kiasi kwamba Kamati ya Michezo ya Olimpiki ya Ufaransa ililazimika kwa muda kufikiria uwezekano wa kuacha mradi huo. Katika IOC, tulikuwa tumejiandaa kukumbana na hali kama hiyo: sio kwamba niliwahi kufikiria kwa muda kuwa mzozo huo ungefikia kiwango hicho, lakini nilijua vizuri jiji nililozaliwa, ambapo nilikuwa nimeishi kwa zaidi ya miaka sitini. Kwa hiyo, nilikuwa nimefikia makubaliano ya kimyakimya na Los Angeles, kama yalivyoendelea na mmoja wa Wenzake wapya wa Marekani, W.M Garland, aliyekuwa mwananchi mwenye ushawishi mkubwa. Huko, uwanja mkubwa, kazi ambayo ilikuwa imeanza mara tu matumaini yalipokuwa yametolewa kwamba Olimpiki inaweza siku moja kuoneshwa hapo, ulikuwa karibu kukamilika. Mkutano wa kabla ya Olimpiki ulikuwa tayari umepangwa huko mwaka 1923 na hakuna kitu ambacho kingekuwa rahisi, ikiwa kingethibitishwa, kuliko kuahirisha mkutano hadi 1924 na kuugeuza kuwa Michezo halisi ya Olimpiki badala yake. Kujua hili kunaniwezesha kutazama kile kilichokuwa kikiendelea huko Paris kwa utulivu na kuongea kwa ujasiri, kana kwamba sijali matukio haya, kwa waandishi wa habari na watu waliokuwa wanahojiwa ambao walikuwa wanazidi kuongezeka. Count Clary, Rais wa Kamati ya Olimpiki ya Ufaransa, na Frantz Reichel, ambaye alikuwa katibu Mkuu wake aliyejitolea, walinifahamisha kila mara katika mzozo huo wa matukio madogo. Barua zao zinafundisha. Siku moja kiongozi huyo wa Saine alisoma kwenye Baraza la Manispaa sehemu ya barua ya siri ambayo nilikuwa nimeituma kwa Mheshimiwa Poincare, wakati huo akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, barua ambayo safari yake kutoka Quai d'Orsay hadi Ikulu ya Jiji, haikujulikana kwa aliyeandikiwa, haijawahi kufafanuliwa kabisa. Baraza la Manispaa lilizidi kuchanganyikiwa. Mmoja wa madiwani hata alipendekeza kwamba waialike "Bendi ya Sokols kuja, hii itakuwa moja ya vivutio vikuu vya Michezo ya Olimpiki!" Ilikuwa ni serikali iliyozuia chombo hicho kuanzishwa. Rais wa Jamhuri, Bw. Millerand, alionesha kupendezwa sana na Michezo hiyo na alikataa kukabiliana na mwelekeo wowote wa mji mkuu wa Ufaransa kwa kukata tamaa baada ya yeye mwenyewe kuihimiza Kamati ya Olimpiki ya Ufaransa kuweka ugombeaji wake. Rais wa Baraza, Bw. Poincare, kwa isivyo bahati pia alipatwa na wasiwasi wa kisiasa ili kulipa kipaumbele suala hilo. Hata hivyo, neno kutoka kwake lingetosha

kuonesha umuhimu unaoambatanishwa na jambo lililosemwa. Kwa bahati, hatimaye ilianza, ingawa kwa kiasi fulani ilisimama, na uamuzi ukachukuliwa wa kujenga uwanja huko Colombes. Kama ingekuwa uamuzi wangu, hakuna hata mji mmoja kati ya miji iliyopendekezwa ambao ungepata idhini yangu. Kulikuwa na kigezo kimoja cha ziada kilichokuwa kinalibeba jiji la Paris. Mbele ya Chuo cha Kijeshi, kwenye Jumba la Sanaa," kupotea kwa "Galeri maarufu ya Mashine" iliyojengwa mnamo mwaka 1889 kulikuwa kumeacha eneo kubwa la uwanja ambalo hatima yake ilitatuliwa bila shaka na ambayo hakuna jengo la kudumu ambalo lingejengwa ili kutoharibu moja ya matarajio mazuri zaidi ya Paris. Lakini kuutumia kwa kipindi kifupi cha Michezo ya Olimpiki kusingeuathiri kabisa. Wakati huo Chuo cha Kijeshi, chenye majengo yake makubwa, maeneo yake ya wazi na ua wake, kilikuwa karibu kutokuwa na watu. Nilikuwa nikikiangalia tena ili kuangalia mpangilio na vipimo. Ni "majumba ya wanamichezo" ya ajabu kama nini! Matumizi yangepunguzwa kwa kiasi kikubwa, mbali kabisa na ukweli kwamba hakuna mahali pengine popote katika jiji la usafiri kungeleta shida kidogo; njia za treni ya umeme, "reli za chini ya ardhi", boti kila kitu kilikuwa kinafikika kirahisi. Kwa njia yoyote ambayo mtu aliitazama suluhisho hili lilikuwa bora zaidi kuliko mengine yoyote, lakini haikuwa wajibu wa IOC kuingilia kati au kujaribu na kushawishi maoni ya umma. Nilijaribu kuipendekeza kwa njia isiyo rasmi, lakini haikufaulu.

Wakati wa Majira ya Vuli ya 1922, IOC ilikutana huko Paris. Tulipokutana, mgogoro ulikuwa karibu kuisha. Ilikuwa imekubaliwa kuwa safari hii ingekuwa mkutano wa kikazi bila matukio ya kawaida ya kijamii. Kwa kweli kulikuwa na karamu moja tu ya chakula cha jioni kilichotolewa na Kamati ya Ufaransa, tafrija ndogo huko Elysee na chakula cha mchana cha asili kwa mwaliko wa mwenzetu Glandaz katika "mashua maarufu ya msimamizi wa sherehe" ambayo sasa iko karibu na Daraja la Concorde. Sehemu hii imekuwa mojawapo ya migahawa ya kisasa zaidi ya mji mkuu yenye sifa nzuri ya kupika vyakula vya kisasa. IOC ilikuwa imepokea tu idadi ya wajumbe wapya: Jenerali Sherrill nchini Marekani: Bw de Alvear katika Jamhuri ya Argentina, ambaye alikuwa Mkuu wa Nchi muda mfupi huku akitupa heshima adimu ya kubaki kwetu; Kanali Kentish wa Uingereza; Boran de Guell wa Uhispania; J.J Kenane wa Irelandi; Prince Lubomirski wa Polandi na Dkt. Ghigliani wa Uruguay. "IOC sasa ilikuwa na wajumbe 54 kutoka nchi arobaini na mbili.

Kazi kubwa iliyokamilishwa katika Kikao cha 1922 ilihusisha kurekebisha miundo mipya na kuongeza marekebisho machache kwenye maandishi muhimu. Bodi ya Utendaji ilikutana kabla ya vikao vya kamati na mamlaka na shughuli zake kuainishwa ipasavyo. Mbali na kuundwa kwa Bodi ya Utendaji katika makao makuu yaliyosajiliwa (Lausanne), marekebisho yalifanywa katika sheria za IOC zinazohusiana na lugha rasmi (Kifaransa) kwenye sekretarieti pamoja na yote muda wa madaraka ya rais ambao ulipunguzwa, kutoka miaka kumi hadi minane. Ninaamini kwamba bado sijataja njia ambayo, tangu mwaka 1901, mamlaka haya yalipangwa kufanyiwa marekebisho kamili. Kuanzia tarehe

1 Januari mwaka huo, yalipaswa kuwa yamepita mikononi mwa Mshirika wetu wa Marekani, W.M Sloane. Kanuni ambazo nilikuwa nimekubali mwaka wa 1894 zilitoa uhamishaji huu wa mamlaka wa kila mwaka wa nne, lakini hii ilidokeza kwamba ukumbi wa kuadhimisha Michezo ifuatayo ulikuwa tayari umewekwa wakati huo. Ilikubaliwa kwa wote wakati huo kwamba Olimpiki inayofuata ingefanyika Amerika, lakini mradi wa Chicago ulikuwa bado haujaainishwa. Hakuna maombi rasmi yaliyotumwa na, kwa hiyo, hakuna upigaji kura uliofanyika. Sloane hakuwa ameridhika kusisitiza hali hii ilivyo. Alikuwa amelijumlisha suala hilo na, bila hata kunitajia jambo hilo hapo awali, aliwasilisha pendekezo kwa IOC kwa ajili ya kurekebisha sheria, akisema kwamba kwa maoni yake urais imara na wa muda mrefu wa miaka kumi ndiyo njia pekee ya kufanya Olimpiki kuwa imara na kuzaa matunda na kwamba kwa sababu hiyo alikataa kuchukua nafasi kutoka kwangu. Makubaliano ya pamoja ya wenzetu yangenilazimu kujitoa hata kama, katika nyakati hizo ngumu, sikuhisi ukweli na nguvu ya hoja zilizotolewa. Hivi ndivyo "Ufalme wa Olimpiki" kama wengine walivyouita, ulivyoanzishwa. Inashangaza kwamba ilikuwa matokeo ya hatua ya raia wa kidemokrasia zaidi wa jamhuri zote. Kwa hiyo muhula wangu wa uongozi uliongezwa hadi 1907. Nilipochaguliwa tena wakati huo, na baadaye tena mwaka 1917, muda wangu wa uongozi haungefikia kikomo hadi 1927. Lakini kwa vile nilikuwa nimeamua kustaafu baada ya Michezo ya 1924, wenzangu waliamua kwamba mrithi wangu atachaguliwa kwa kipindi cha Olimpiki mbili, yaani kwa miaka minane, muda wake wa uongozi ulianzia tarehe ya kuchukua madaraka 1925 ilionekana kuwa tarehe nzuri, mwaka mmoja baada ya Michezo, na miaka mitatu kabla ya Michezo inayofuata; ndio maana nilikubali kubaki kwenye wadhifa wangu hadi mwaka huo.

# XX

## Ikulu ya Roma (1923)



60. *1923: Ufunguzi wa Kikao cha IOC*

Fursa iliyopotea jijini Roma mwaka 1906, ilipaswa kurejeshwa. Hali ya sintofahamu huko jijini Lausanne mwaka 1921, iliwakumba wote. Kwa hiyo, nilikuwa makini hasa kwenye kikao cha mwaka 1923 ili kiwe na mafanikio zaidi. Wenzetu, Kanali Muntu na Marchese di Guglielmi, hawakuonesha juhudi zozote katika jitihada zao za kutaka ushindi ingawa walifanikiwa kushinda vizuri. Kikao hiki kilifanyika chini ya usimamizi wa Mfalme na Malkia wa Italia, Kikao kilifunguliwa katika ukumbi wa Ikulu tarehe 7 Aprili 1923, mbele ya watawala, wakiongozwa na Rais wa Chemba na Seneti, Makatibu wa mambo ya nje na wa Sanaa, Mkuu wa Mkoa wa Roma na wageni wengine wakubwa. Kikao kiliahirishwa tarehe 12 Aprili. Wajumbe wa IOC walibaki na kumbukumbu zisizofutika za mapokezi mazuri waliyopewa Quirinal katika hafla iliyofanyika huko Palazzo Rospigliosi jijini Roma, ambavyo viliandaliwa na Bw. na Bi. di Guglielmi, vilevile walipata chakula cha jioni kilichoandaliwa na Kanali Montu katika hoteli ya Aventino ambapo wageni waliweza kufurahia mandhari nzuri ya magofu ya Kasri la Kaisari yaliyoandaliwa mahususi kwa ajili ya tukio hilo. Waliutembelea mji wa Vatikani ambako

walipata mapokezi mazuri ya mwanzo, Rais wao alipata uhakikisho kutoka kwa Papa Pius XI kwa namna anavyovutiwa na Michezo ya Olimpiki. Aidha, walifurahia mapokezi mazuri kutoka Ofisi ya Taifa ya Utalii na kamati ya Michezo ya Olimpiki ya Italia. Hatimaye, walifurahi kukamilisha kazi kwa kiwango cha kuridhisha katika mifululizo ya mikutano.

Mambo mengi yanayohusu michezo ijayo yalikamilika, ijapokuwa jambo muhimu lililojadiliwa lilikuwa ni ushiriki wa Ujerumani na Urusi, "michezo" ya kanda, uenezi wa huko Amerika na hatimaye Afrika iliweza kushinda vikwazo vya michezo. Suala la Ujerumani lingekuwa rahisi kutatuliwa kwa sababu, kwa upande mmoja, hakuna uhalifu uliokuwa umetokea na kwa upande mwingine, wajumbe wa IOC wa Ujerumani waliondoka. Katibu Mkuu aliyeteuliwa kuratibu mashindano ya sita ya Olimpiki (Berlin 1916), ambaye, kwa uwezo wake alifanya kazi kubwa katika majadiliano ya Juni 1914 mjini Paris, alialikwa kwenda Roma ili kufikia makubaliano na IOC yanayohusu uchaguzi wa wajumbe wapya lakini, sababu ya mitafaruku, alishindwa kufika na hakufika kabisa hadi awamu nyingine ambayo waziri wa mambo ya nje, Lewald na Bw. O. Ruperti walichaguliwa. Wenzetu Wabulgaria, Waturuki na Wahangaria walikuwa wamekwishachaguliwa: ambao walikuwa ni Messrs, Stancioff, Selim Sirry Bey, Count Geza Andrassy na J. de Muzsa. Kulikuwa bado kuna nafasi ya Waustria iliyotakiwa kujazwa na hakukuwa na mgombea aliyekuwa ameteuliwa. Wakati huu IOC walikubali kupitisha azimio kwamba walifanya kosa kuikataa Lausanne mwaka 1921 na ambalo lilijikita katika kanuni mbili za marekebisho muhimu na ya kudumu ya falsafa kwa upande mmoja na kwa upande mwingine kukosekana kwa kizuizi cha kutuma mialiko, jukumu lote likiachwa katika mamlaka za nchi zinazoratibu michezo.

Baada ya Ujerumani, Urusi ikafuata. Isingewezekana bila ya hamasa kuwa, tulipata taarifa kutoka kwa mwenzetu Leon Ouroussoff mwanadiplomasia mstaafu, akielezea udugu wetu uliogawanywa katika makundi mawili ambayo yana mitazamo huru, aliomba kuwapo kwa usawa katika michezo hiyo jijini Paris; kwa timu zote za Kisoviet na klabu za michezo za wahamiaji ambao walipaswa kusajiliwa kwa misingi sawa. Nilihuzunika sana kwa namna ambavyo maoni yake yalipokewa na kukataliwa kwa sababu za "kiutawala". Hakuna mtu aliyegundua vyema zaidi yangu, ugumu uliokuwapo na matatizo yasiyotatulika ambayo yangejitokeza, lakini ninadhani kwamba IOC ingejipatia heshima yenyewe kama ingepokea mapendekezo kwa njia tofauti na kuyapeleka kwa wakati mwafaka kwenye serikali ya Ufaransa, yakiungwa mkono na maoni mazuri.

Kwa upande wa Waarmenia ambao walikuwa na kilabu cha vijana wahamiaji waliohitaji kusajiliwa, hali ilikuwa tofauti. Kwa wakati huo, Armenia iliendelea kuwa tumaini pekee na kumbukumbu katika mioyo ya watu wake na vilevile ingekuwa vigumu kwa Bohemia au Ufini kabla yake, kudai kuwa na jukumu kuu katika "muktadha wa kimichezo". Matatizo ya mataifa mengine yalikuwa yametatuliwa. Kwa mara ya pili, taifa huru la

Irishi liliwakilishwa katika kikao hicho. Nyaraka zake zilizokuwa katika lugha ya Kiselitiki zilizoambatishwa na toleo la Kiingereza, zilikuwa na mwonekano mzuri ingawa wa kizamani. Uanzishaji wa himaya ya Yugoslavia, ulimaliza tatizo la Croatia na Serikali ya Amerika ilikubaliana na matakwa ya Ufilipino kuruhusiwa kujumuika katika kundi kwa kupitia bendera yao katika gwaride la Michezo ya Olimpiki. Katika usiku wa michezo jijini Paris, IOC ingepata wajumbe 62 na nchi 45. Nchi ndogo ya Laussen ilikuwa na idadi kubwa ya wajumbe kuliko taifa kubwa la Geneva.

Waandaaji wa mradi walitenda haki baada ya vita na walidhamiria kuanzisha michezo ya "kikanda", hakukuwa na nchi iliyosalia. Nilifurahi kwa sababu sikuyaona matarajio ya dhati ya mashindano hayo ingawa niliona ni vyema kuyaacha yaishe yenyewe. Ni michezo ya Mashariki ya Mbali tu iliyokuwa chini ya usimamizi wetu ndiyo iliyodumu. Walionesha hitaji thabiti. Malengo mengine yaliyonivutia ilikuwa ni kuhusu michezo ya Kiafrika, ambayo nitaiongelea baadaye kidogo na michezo ya Amerika Kaskazini ambapo Brazil ilitambuliwa kwa kuzindua michezo hiyo mwaka uliopita (1922) katika maadhimisho ya miaka mia moja ya uhuru wa nchi hiyo. Haikuwa tu imewekwa chini ya usimamizi wa IOC, lakini Serikali ya Brazil ilinitumia mwaliko kuja kuwasimamia. Isivyo bahati, mazingira hayakuniruhusu kuondoka kwa wakati, lakini Bw. Count de Baillet-Latour aliweza kuchukua nafasi yangu. Kwa jinsi mwenendo wa eneo kubwa la bara la Amerika ya Kusini ulivyokuwa, mjumbe wa IOC sio tu alipata mapokezi mazuri kwa kazi aliyokuwa akiwakilisha, bali alitumia muda wake vizuri "kutangaza michezo ya Olimpiki", kuanzisha mashindano mapya kwa nchi hizi mpya ambazo hazikuridhishwa na malengo ya kimichezo. Kwa wakati huohuo aliweza kuondoa vikwazo, kukomesha migogoro na utata. Hata kama michezo ya jijini Rio ingekuwa mizuri au vinginevyo, ilikuwa vyema kwani ilionekana kuzaliwa upya kwa manufaa ya baadaye ya majiji mengine mbali na yaliyopo sasa yenye uhaba wa usafiri ikilinganishwa na umbali halisi tofauti na ilivyokuwa Ulaya. Tulihitaji kuchagua miji kama vile Mexico, Havana, Santiago, Montevideo na Buenos Aires, ambako wanamichezo kutoka nchi jirani wangekuwa na fursa za kushindana ama Amerika ya Kati au Amerika ya Kaskazini. Hii ingekuwa ni Michezo mizuri ya Olimpiki kwa watoto kulingana na kanuni zilizotumika huko Manila. Bw. Count de Baillet alitoa sababu za safari yake ndefu na kazi zote alizozikamilisha; taarifa yake ilipokewa kwa shangwe sana. Alilazimika kufupisha safari yake, hakurudi tena kupitia California na Japani ambako alitakiwa kuongoza michezo ya Mashariki ya mbali ambayo ilifanyika Osaka. Huko Los Angeles, ambako ujenzi wa uwanja ulikuwa umekaribia kukamilika, kulikuwa na matarajio makubwa katika safari yake kwa matumaini ya kupata uhakika kutoka kwake kwa kuzingatia michezo ya 1932 tangu ile ya Olimpiki ya 8 na 9 iliyokuwa imekwishafanyika. Lakini nilibaini namna nilivyokuwa shupavu, kufufua mtazamo uliofanywa huko Lausanne miaka miwili kabla na kufikia matarajio hata kabla ya wakati. Katika kuongeza umakini na shauku kulikofanywa na mwenzetu W.M. Garland, Los Angeles ilifanya mambo makubwa matatu. Kwanza, hali ya maandalizi ya Michezo ya Olimpiki kitaifa, ambayo yalitarajia ushindi mkubwa ikiwa

michezo itafanikiwa; pili, hali ya upendeleo kwa mtazamo wa matukio ya kisiasa na kijamii, zaidi uliondoa chokochoko zote zilizokuwa zikivuma ambazo nilizizungumzia mwaka uleule 1923, katika mfululizo wa machapisho ya gazeti la Uswisi lenye kichwa cha habari "Ulaya Inakwenda Wapi?" Hatimaye muda ulikuwa umefika wa kuonesha heshima katika michezo ya vijana ya Marekani kwa jitihada zilizofanywa tangu michezo ya Athene na kwa wakati ilikuwa mizuri na ushiriki wake mkubwa katika michezo iliyopita.

Sababu hizi tatu ziliwafanya wajumbe wa IOC kuchagua kwa pamoja sherehe za tuzo za Michezo ya 10 ya Olimpiki huko Los Angeles.

Mkutano wetu ulikuwa na majadiliano mengi mazuri ambayo siwezi kuyaeleza hapa. Kwa kuwa uchapishaji wa Jarida la Michezo ya Olimpiki ulisitishwa, kumbukumbu za kikao cha mwaka zilichapishwa kwa ujumla katika kipeperushi kwa gharama za mwenzetu Albert Glandaz, hivyo nyaraka zipo kwa mtu anayezihitaji. Tatizo la "upotevu wa mapato" lilisababisha kuibuka kwa mivutano midogomidogo, ambayo ilikuwa ikijitokeza mara kwa mara na baadaye ikawa mikubwa ambayo ni vizuri kuitaja; na kwa faida ya wajumbe, ni vyema kuiorodhesha mivutano hii tangu kuanzishwa kwa IOC ambayo haikuwahi kupata machafuko yoyote kama haya ambayo hayakuwa na sababu lakini kamwe hayakuisababishia maumivu yoyote katika utendaji wake. Sitaelezea zaidi kuhusiana na kipengele hiki kipya cha changamoto ya michezo ya ridhaa. Nimelizungumzia hili kwa mapana katika sura iliyopita, "kupoteza mapato" mgogoro mbaya uliodumu kati ya kundi la wanausasa na kundi la wahafidhina wa michezo ya Uingereza. Hakuna mtu aliyekuwa anajihusisha na mafunzo ya mchezo "halisi" zaidi ya Mwingereza Mch. Laffan na ambaye alikuwa na historia ya ndani sana, alikuwa akiangalia nafasi yake kwa namna ya kutekeleza kanuni za mabadiliko ya kijamii ambazo aliziona hazifai kutekelezeka.

Kilichosalia ni mimi kuongelea suala la "ushindi wa Afrika" ambao ulikuwa mwanzo wa maisha yangu ya Michezo ya Olimpiki, nilikuwa makini sana kiasi cha kuibua moja ya hoja pendwa zilizokuwa zikihusiana na masuala ya kikoloni.

Hotuba iliyotolewa kwa Mfalme Victor Emmanuel katika mkutano wa ufunguzi wa kikao cha IOC kilichofanyika Ikulu, ilijumuisha maelezo haya: "labda inaweza kuwa haraka sana kutambulisha kanuni za mashindano ya kimichezo katika bara ambalo liko nyuma ya wakati na miongoni mwa watu ambao bado hawana utamaduni asilia hususani wenye kujiamini katika matarajio ya upanuzi wa kuharakisha maendeleo katika nchi hizo. Hata hivyo, ngoja tufikiri kidogo, kuna nini kinaisumbua Afrika. Uvivu binafsi na ushirikiano wa pamoja - chuki na wivu bila sababu kwa watu weupe na wakati huohuo bado tuna matamanio ya kuwaiga ili kunufaika nao - mgogoro wa kutaka kujinasibisha kinidhamu na kujiweka pembeni - na katika hali ya upole, yaani kwamba haiwezekani bila ucheshi wao, mashambulizi ya kushtukiza ya mababu zetu… hizi ni baadhi tu ya sifa

za mashindano haya ambazo kizazi kipya kiukweli kimeleta mafanikio mengi kutoka kwenye michezo inayoendelea kuvutia. Michezo iliwakomaza. Iliwajengea afya ya misuli na kuwajengea uwezo wa akili kupokea chochote kilichofundishwa uliowafanya kuwa viumbe wenye nguvu pale tu juhudi zao zilipokuwa zimekamilika. Lakini michezo iliposhamiri, mambo yalitulia. Kwa kuzingatia kuwa ilikuwa kitu cha ziada, ilisaidia kutengeneza utaratibu na kutimiza malengo. Hata hivyo, tusisite kuisaidia Afrika kujiunga. Wajumbe kutoka taasisi kubwa wamekuja hapa ili kujadiliana nasi kuhusiana na suala hili…"

Hakika zaidi ya Kikao cha IOC, kulikuwa na vikao vya kamisheni ya mashauriano vilivyojumuisha kwa pamoja uwakilishi wa Wizara za makoloni ya Italia, wajumbe kutoka Algeria, Morocco, Utawala wa Tunisia na Kanali See, waliobeba ujumbe kutoka kwa Jemedari Lyautey kwa wakati huo alikuwa Jenerali Mkazi. Mwenzetu kutoka Ureno, Count Penha-Garcia, alikuwa ameteuliwa kuwakilisha nchi yake. Sitaelezea kwa kina kuhusiana na majadiliano, lakini nitawaelezea yote kwa ufupi kama inavyotakiwa kuhusiana na mradi ili kutorudia tena jambo hilo; walau mambo yaliyotokea kwa wakati ule na nina uhakika suala hilo litajirudia tena. Suala hilo litahusisha kufanyika kwa "Michezo ya Kiafrika" kwa kila mwaka kwa kuanzia na programu rahisi na ambazo ni za kawaida zisizokuwa na sifa za kujumuishwa kwenye michezo ya kikanda. Ningetamani kuiona Michezo hii ikiachwa kwa wazawa pekee. Vilevile ilipendekezwa kuhusisha mashindano kwa wakoloni waliokuwa ndani ya nchi kwa angalau miaka miwili. Kwa hakika, mtazamo huu ulieleweka kabisa, lakini mwanzoni ulifanya mambo kuwa magumu. Majiji yaliyoonekana kuwa tayari kufanya michezo ya kwanza yalikuwa ni Tunisi, Rabat, Casablanca na Dakar kwa nchi za Afrika zilizotawaliwa na Ufaransa, Tripoli, Benghazi na Asmara kwa nchi za Afrika zilizotawaliwa na Italia, Libreville katika sehemu ya Kongo iliyotawaliwa na Ubelgiji, Luanda na Sumac katika sehemu ya Afrika iliyotawaliwa na Wareno, Cape Town na Nairobi kwa Afrika Kusini. Kosa nilililofanya lilikuwa ni kufikiri (kuweka wazi wazo hili kwa IOC) uwezekano wa uzinduzi wa sherehe muhimu na adhimu zaidi ulitakiwa kufanyika jijini Algiers mwaka 1925. Katika hatua za mwanzo, uamuzi wa michezo kufanyika nchini Algeria uliungwa mkono na Bw. Th. Steeg, ambaye alikuwa Gavana Mkuu na mwenye mapenzi ya michezo kwa wakati ule. Uamuzi huo ulikumbana na upinzani mkali sana kwa sababu ulikosa uelekeo na makao. Wale wapinzani wote walifanya wawezavyo ili kupoteza muda na kuharibu malengo. Ingawa lilikuwa ni suala binafsi lakini kwa kiwango fulani kulikuwa na mvutano wa kiutawala. Hatimaye sherehe ziliahirishwa hadi mwaka 1929 na Alexandria ikachukua nafasi ya Algiers.


Kwa wakati ule maandalizi yalikuwa mazuri; viwanja vilijengwa. Mwenzentu wa Misri, A.C. Bolanaki, aliingia katika mradi huo kwa umakini na ukarimu sana uliosaidiwa zaidi na umahiri wake ambao ulikubalika kwa wote… Katika tukio la mwisho, werevu wa kisiasa wa Uingereza ambao Ufaransa ilikuwa mshirika, haukuwa na ufanisi katika kazi

zote walizozifanya na Mfalme Fuad aliuzindua uwanja wa Alexandria kwa uangalifu kutokana na vigezo vilivyotakiwa. Siwezi kueleza suala hili lenye kuudhi kwa maana tangu liharibike, nilikuwa nimeshatoka katika Urais wa IOC. Kwa ujumla, kulikuwa na mgogoro mkubwa, ile ari ya mapambano ya wakoloni dhidi ya ukombozi wa wazawa, hali ilikuwa mbaya sana kwa vile viongozi wakubwa wa nchi ya wazawa ndiyo waliohusika. Hoja zilizotolewa awali hazikuonekana kuwa na mashiko, badala yake zilionekana kuwa za kizamani na zisizokuwa na tija. Ulipita muda mrefu tangu zilipoanza kutumika. Jarida la Michezo ya Olimpiki lilikuwa na mada kuu inayohusu "Mchango wa Michezo katika Makoloni" katika mwezi wa Januari 1912. Miaka ishirini baadaye, nilifikiri kwamba maoni yale yamehusika kikamilifu kuruhusu mawazo yote yawekwe katika vitendo! Ilionekana kwamba wakati ulikuwa bado haujafika. Inawezekana wakati unaelekea kufika sasa na ninashawishika kusema kwamba, michezo itaandaliwa Afrika nzima lakini kwa isivyo bahati, haitafana zaidi kama ile ya Ulaya ambayo wanatumia mbinu nyingi kufanya maandalizi katika wakati mwafaka. Kwa kiwango chochote bado imesalia "medali ya Afrika" inayowekwa kila mwaka kwenye mabango na kaulimbiu… kwa ajili ya kuhamasisha michezo. Ingefanyika kwa wakati, kwa kila mahitaji ya jambo lolote zuri. Kwa upande mwingine, ilionesha mtu mweusi akirusha mkuki na mchezo wa kurusha mianzi, ikiwa na maelekezo kwa lugha ya Kilatini, kwa vile Afrika ina lugha nyingi za kikoloni na za asili: ni jukumu la *mwanamichezo kujua, kujisimamia na kujimudu mwenyewe (Athletae proprium est se ipsum noscere ducere et vincere).* Kujua, kujisimamia na kujimudu mwenyewe – kuwa na uchezaji mzuri, jambo ambalo ni la msingi kwa mwanamichezo wa kweli na ni muhimu kwa mafanikio yake.



# XXI

## Michezo ya Nane ya Olimpiki (Paris – 1924)



**51.** *Paris 1924 – Pierre de Coubertin katikati akitoa tuzo za Michezo ya Olimpiki kwa viongozi wa ujumbe wa Ufini. Upande wa kulia, Court Clary, rais wa kamati ya michezo ya Olimpiki ya Ufaransa, na upande wake wa kushoto, Baron Godfrey de Blonsy (US), mjumbe wa IOC.*

Michezo ya 8 ya Olimpiki ilifunguliwa huko Chamonix mnano Februari 1924 na ufunguzi huu ulikuwa na mafanikio makubwa ya kila namna na kusaidia kuondoa hisia mbaya na kupunguza ubaguzi wa watu wa Skandinavia, ambao mabingwa wao walijitofautisha kwa asili zao. Myeyuko wa barafu (jambo ambalo mara zote litakuwa changamoto kubwa kwenye Michezo hii ya Majira ya Kipupwe, hadi kwenye mji wa St. Moritz ambao ulishiriki kwenye michezo ya Olimpiki mara moja baada ya miaka minne) kwa bahati siku moja kabla ya ufunguzi kulikuwa na hali ya baridi kali na hali ya hewa nzuri. Kulikuwa na matukio kadhaa ya kukumbukwa kama vile mechi ya kuteleza kwenye barafu kati ya timu za Kanada na Marekani. Pia kulikuwa na tukio la kusisimua ambapo chini ya Mont Blanc, medali ya kupanda mlima ilitolewa kwa mmoja wa viongozi wa safari maalumu za kupanda Mlima maarufu wa Everest, Mwingereza jasiri ambaye, alishindwa lakini hakukata tamaa, aliapa kuiweka kwa mara nyingine juu ya kilele cha Mlima wa Himalaya. Kwa ufupi, wiki hii ya kwanza iliashiria vyema hatima ya Michezo ya Majira ya Kipupwe pamoja na uwezo wa Ufaransa kuandaa Michezo ya Olimpiki.

Isivyo bahati huko Paris, miezi minne baadaye, mambo yalianza kuharibika. Matukio haya ya 1922 yalikuwa hayaepukiki na yangechukua muda mrefu kwenye baadhi ya mambo na kuwa na matokeo yasiyorekebishika. Urasimu katika mfumo wa kiutawala na ukosefu wa uelewa vilileta athari mbaya zaidi kuliko kawaida. Kwa bahati nzuri uvumilivu na ustahimilivu wa waandaaji ulishinda matatizo yote. Kwa ujumla mtu asingeacha kuwapongeza na wageni ambao walikuwa makini walionesha heshima na hisia zao kwa Ufaransa. Serikali ilisahau kabisa haya yote na ilishindwa kunufaika nayo. Mtumishi wa umma mdogo sana aliniambia kwa unyenyekevu: "Binafsi, ninaweza tu kuongea kama mtu wa kawaida, lakini hata hivyo siwezi kujizuia kuhisi kwamba serikali imeshindwa kutumia fursa zote zinazotolewa na Michezo hii ya Olimpiki." Kwa kweli alikuwa sahihi na ukosoaji wake ulijumuisha makosa yaliyokuwa yamefanyika! Hapa sio mahali pa kujadili kwa undani hali hiyo, kwa sababu ingehusisha uchunguzi wa kina wa mitazamo ya wajumbe wa serikali na maoni ya umma nchini Ufaransa baada ya kile ninachokiita "ushindi usio na kichwa" katika kitabu changu "kingine" ambacho sijakichapisha. Ni fursa ya pekee kuwahutubia vijana wa ulimwengu waliokusanyika pamoja huko Paris na kuwatangazia amani iliyozingirwa na ushindi wao wa hivi karibuni! Ni mwanzo ulioje wa enzi mpya iliyohusu watu wote! Hata hivyo, sasa hakuna maana kuwa na majuto yasiyo na sababu. Ni bora tu kueleza mambo mazuri ya kipindi hiki cha Michezo ya Olimpiki ya Paris.

Kwanza kabisa, kulikuwa na hisia za ucheshi za wanamichezo, ambazo zilionekana kusimamiwa na watu wawili mashuhuri: Rais Doumergue na Mwanamfalme wa Wales, ambao furaha zao kwa kweli zimekuwa hadithi. Kwa kuwa tunavutiwa na michezo ambayo tunahusika nayo, nitaanza na wanamichezo. Wale wanaoelezewa kila wakati kuwa ni vigumu kuwafurahisha, wanaonesha ujinga wao na ukosefu wa uelewa kuhusiana na hali ya furaha na msisimko wa wanamichezo unaotokana na tukio la kuwaleta pamoja katika eneo moja maelfu ya vijana ambao walipata tuzo za heshima ambazo zilikidhi matarajio yao. Kwa kuongezea, vikwazo vilivyosababishwa na mafunzo, kuvishinda vikwazo, hali ya kutepeta kwa mwili na tofauti mbaya kati ya matarajio na hali halisi, nuksi, wasiwasi uliotokana na tukio la karibu,..... Wewe ni mtu wa kiwango gani katika jamii, ambaye mawazo ya lazima na muhimu, yanatokana na taarifa ya maandishi ya haraka na mara zote isiyokuwa nzuri (kwa wanahabari wa michezo, ambao kazi zao pia zina ugumu wake ambao hauko vizuri), unafahamu nini kuhusiana na uamuzi wowote wa utu uzima, kujisimamia na kusaidiana katika kile kinachoitwa nyumba za wanamichezo? Angalau uwe na heshima ya kutoa shukrani kwa ajili ya ari ya kimichezo yenye uwezo wa kuhimili tabia za mihemko kwa watazamaji hao ambao inawezekana ulikuwa mmojawapo – ambao mara nyingi wanakuwa na uadui na wivu mkubwa badala ya ushindani wa kiungwana. Watazamaji wachache waliozubaa wakati wakitazama michezo ya sarakasi au michezo ya kuendesha mashua ambao walikuwa ni washamba; makundi ya watazamaji wenye shauku mara tu mpira wa miguu au mchezo wa masumbwi unapokuwa na matukio ya fujo.... Kwa kulinganisha namna wanamichezo

halisi wanavyoonekana kwenye usawa na uchangamfu katika utulivu wa falsafa yao ya vitendo. Ni wazi kwamba kuna hali tofauti ambazo ni nyingi! Lakini hali halisi inabaki kuwa: kutoka Stockholm hadi Antwerp, kutoka Antwerp hadi Paris, kazi zake za kutia moyo ziliendelea. Huko Paris, kuliko ilivyokuwa hapo kabla, michezo iliimarishwa zaidi.

Rais Doumergue alikuwa kwenye uwanja wa ikulu ya Elysee wiki moja alipowasindikiza kwa gari hadi Sorbonne kuhudhuria sherehe za maadhimisho ya miaka 30 ya kufufuliwa kwa Michezo ya Olimpiki. Alioneshwa kisanduku kilichokuwa na medali mbili, moja ikiwa ni ile iliyowekwa miaka thelathini iliyopita na ambayo iliandikwa: "Mkutano wa Kimataifa wa huko Paris unatangaza kufufuliwa kwa Michezo ya Olimpiki, Juni 23, 1894" – na kwa upande wa pili ikiwa na muundo unaofanana, ulioandikwa juu yake maneno yafuatayo: "Mataifa yaliyokusanyika hapa yanasherehekea ukumbusho wa miaka thelathini ya kufufuliwa kwa Michezo ya Olimpiki, Juni 23, 1924". Mimi na wenzangu tulipomkaribisha Mkuu wa Nchi, mawazo mengi yalijaa akilini mwangu na zaidi ya yote kumbukumbu ya sherehe iliyofanyika Juni 1914 mwanzoni mwa Vita vya Kwanza vya Dunia ambavyo vilidumu kwa muda wa miaka minne, maisha ya vijana wengi waliozaliwa kufurahia michezo yalitolewa sadaka kwenye madhabahu ya vita vya Amagedoni: sherehe inayofanana na ya sasa, pamoja na kwaya zake, tarumbeta, bendera na hotuba za Michezo ya Olimpiki… zinazofanana sana na bado mtu angefikiri kuwa, historia imebadilika na hali ya kukosekana kwa utulivu ilichukua nafasi ya utulivu wa kijamii ambao ulitoweka kabisa.

Wakati wa jioni, katika Ikulu ya Elysee, Rais aliandaa karamu yake ya kwanza kwa heshima ya wajumbe wa Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki (IOC) ambao walijiunga na Meya wa Lausanne, aliyekuwa amealikwa Sorbonne kuwakilisha makao makuu mapya ya Michezo ya Olimpiki. Siku iliyofuata, alasiri, tafrija kubwa ilifanyika katika ukumbi wa sherehe wa Hotel de Ville, ikiambatana na maonesho ya jukwaani. Kikao cha IOC kilifunguliwa tarehe 25 Juni katika Ikulu ya Palais du Louvre kwenye vyumba vya kifahari vya Wizara ya Fedha. Tulikutana hapo tarehe 25, 26, 27 na 28 Juni. Baada ya hapo, kikao kiliahirishwa kwa muda ili kuruhusu Bodi Tendaji kuandaa ripoti mbalimbali, ambayo kwa sasa ina ofisi zake. Kikao kilianza tena tarehe 7 Julai na kuendelea hadi tarehe 13 Julai, jumla ya mikutano kumi ilihudhuriwa na wajumbe kadhaa wapya: Lord Cadogan (Uingereza) Dkt. Kishi (Japan), Bw. Benavides (Peru) na Bw. Aldao (Argentina).

Mnamo tarehe 5 Julai, Michezo ilifunguliwa kwa heshima uwanjani ikiambatana na shamrashamra za kawaida. Mbali na Rais wa Jamhuri, wageni mashuhuri waliokuwapo ni pamoja na Mwanamfalme wa Wales, Mwanamfalme na bintimfalme wa Romania, Mwanamfalme Mkuu wa Ethiopia, Mwanamfalme Henry wa Uingereza, Mwanamfalme Gustav-Adolf wa Uswidi, wajumbe wa serikali na wawakilishi wa jiji la Paris. Njiwa walirushwa, mizinga ilipigwa, na nyimbo zikaimbwa wakati bendera kubwa ya Olimpiki ilipokuwa ikipandishwa juu uwanjani hadi mwisho wa Michezo hiyo. Asubuhi, sherehe

sawa na ile ya Antwerp ilifanyika huko Notre Dame, na hali yake ya "kutoegemea upande wowote" katika mandhari haya ya kipekee, iliifanya ivutie sana.

Ras Taffari, akiwa amevaa koti lenye umbo la koni na kofia kubwa, hakuweza kuwatembelea wanamichezo katika vyumba vya kubadilishia nguo vya uwanjani, lakini mwanamfalme kijana alitumia fursa hiyo kujumuika nao. Mwanamfalme wa Wales alifurahi kuzungumza na mashujaa hao na muda si mrefu kila mmoja alijihisi huru. Alasiri moja, akiwa amesimama akizungumza nami kwenye nyasi za uwanja, aliangalia saa yake na kuuliza kwa raghba; "Je, kuna Muingereza anayeshindana katika mchezo wowote kati ya michezo inayofuata? Ningependa sana kwenda kucheza mchezo wa Polo katika uwanja wa Bois Boulogne. Nimeahidi kufanya hivyo, lakini kama kuna Mwingereza anayetakiwa kushindana, siwezi kwenda. Nilimjibu kwa kusema; "Ndio, Mkuu, yupo mmoja", na mwanamfalme akaacha mpango wake wa kwenda kucheza Polo bila kusita hata kidogo au kuonesha ishara ya kukasirika. Katika karamu kubwa ya wageni mia mbili iliyoandaliwa na Chama cha Olimpiki cha Uingereza, ambayo aliiongoza, alionekana mbele ya mabalozi, mawaziri na kiongozi wa kijeshi Foch… akisimama na kumpa kila mmoja wa wapiga filimbi kumi na wawili glasi ya shampeni, waliokuwa wamekaa kwenye safu nyuma yake baada ya kutembea mara mbili kuzunguka ukumbi wakipiga filimbi zao. Wakati ulipofika wa 'kugonga glasi', alianza na baba yake, na baadaye kwa mkuu wa Nchi ya Ufaransa na wakuu wa nchi zingine zilizoshiriki. Alipokuwa akikaa chini, aliniambia: "Lahaula! Kweli, hicho ndicho kikwazo cha kwanza kinachonikabili….' Na muda mfupi baadaye, aliinuka tena na kutoa hotuba ya kusisimua ya kuisifu Michezo ya Olimpiki.

Uungwana uliooneshwa na mwanamfalme Carol wa Romania ulikuwa nadra kuonekana. Aliendesha gari mwenyewe hadi uwanjani kila siku akiwa kwenye gari la wazi, kwa kawaida akiambatana na mtu. Siku moja mchana, alikuja peke yake. Sajenti wa polisi alikuja huku akikimbia kwenye jukwaa la Rais kunitafuta: "Bwana", akasema, "kuna mtu ambaye anasema yeye ni mwanamfalme wa Romania, lakini lazima awe mlaghai. Yuko peke yake kwenye gari lake na anaendesha mwenyewe. Amepelekwa katika kituo cha polisi kwa kukiuka utaratibu. Nilikwenda haraka. Mwanamfalme alifurahi sana. "Kwa nini umekuja?" aliniuliza. "Wangenipeleka kituo cha polisi, ingekuwa kituko kikubwa!" Wanaume waliokuwa kazini hawakuhisi hivyo na walionekana kujisikia aibu sana!

Wakati mechi za kupigana kwa mapanga, masumbwi, na mieleka zilipokuwa zikiendelea kwa nyakati tofauti, na katika uwanja, fainali za mbio za miguu, michezo ya kurusha ilifanyika huku watazamaji wakishangilia, na katika sehemu nyingine waogeleaji, waendeshaji wa farasi na wanamichezo wa kisasa wa michezo mitano wakishindana kutafuta ushindi, timu iliyomakinika katika ofisi za Rue de Grammont ilikuwa ikifanya kazi kwa bidii kuhakikisha kila kitu kiko sawa. Kwa wale wote ambao waliunda timu hii, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kazi yao kubwa ya kuratibu mashindano. Wakati huo huo ningependa kupongeza shughuli muhimu iliyofanywa na Count Clary,

Rais wa Kamati, ambaye alikuwa jasiri katika kazi zake za uratibu, hasa akiwa msingi imara wa suala zima, Franz Reichel, asiyechoka na mwenye nguvu za ujana, ambaye wanachama wa IOC walimtumia salamu za pongezi kwenye hati iliyosainiwa na kila mmoja wao.

Marquis de Polignac alikuwa mbobevu katika uandaaji wa mashindano ya sanaa ambayo, kutokana na jitihada zake, hatimaye yalistahili kuingizwa kwenye Michezo ya Olimpiki. Lakini sio kwa jambo hili tu, pia alifanikiwa kuandaa "Msimu wa VIII wa Sanaa wa Michezo ya Olimpiki" katika ukumbi wa Champs Elysees Theatre. Iliwapa wakazi wa Parisi fursa hasa ya kusikia muziki wa Simfoni ya Tisa – ule ambao kwangu ulikuwa muziki bora wa Simfoni wa wakati wote wa Michezo ya Olimpiki, simphoni bora ya Olimpiki - uliochezwa na Okestra ya Uholanzi na kwaya ya Kampuni maarufu ya Mengelberg ya Amsterdam. Hii haikuwa kumbukumbu pekee kwa Michezo ya Olimpiki iliyofuata, ambayo ingefanyika jijini Amsterdam. Balozi wa Uholanzi, alitupa mapokezi mazuri katika Ubalozi, alitoa dokezo la ustadi la "kuendeleza mwenge" kama ilivyoelezwa katika maneno yaliyotamkwa wakati wa kufunga Michezo. Wakati ulipowadia wa kuzitaja, bendera tatu zilipandishwa uwanjani: zile za Ugiriki, Ufaransa na Uholanzi, na nyimbo tatu za taifa zilipigwa kwa heshima yao. Sherehe hizi zitaendelea ili kuenzi kudumu kwa michezo ya Olimpiki ya Kale ya Ugiriki na vile vile michezo ambayo imekaribia mwisho na kwa ile itakayofuata. Zaidi ya hayo, itifaki ya sherehe za Olimpiki hatimaye ilikamilika; Nilikuwa nimeijenga kidogo kidogo na kwa hatua, ili nisiwashtue watazamaji na watendaji ambao wanaweza kuwa hawajajiandaa vizuri au wasipokee mabadiliko haya ya kufunga. Hata hivi sasa, watu wengi bado hawaelewi thamani yake ya kielimu na wanachukulia kuwa imepitwa na wakati. Lakini wamezoea sherehe hiyo, na hakuna uwezekano mkubwa sana kwamba mabadiliko yoyote yatafanywa.

Hivyo maandalizi yangu ya kustaafu yalikuwa yanakamilika hatua kwa hatua. Hata hivyo, kulikuwa bado kuna mambo muhimu mawili yaliyokuwa yamebaki. Jambo la kwanza, mara kadhaa, nilikuwa nimeishawishi IOC kuidhinisha uamuzi wa kuandika majina ya washindi, baada ya sherehe ya kila Olimpiki, kwenye mabamba ya marumaru yaliyowekwa kwenye kuta za uwanja ili kuendeleza kazi zao nzuri. Kungekuwa na upinzani kwamba viwanja vya Olimpiki havina uhakika wa kudumu kwa muda mrefu lakini, ikitokea vikabomolewa, je itawezekana kuhamishia mabamba kwenye ukumbi wa jiji? Kwa kuwa tamaa ya kushinda katika mashindano haya ya kila baada ya miaka minne ndiyo kubwa zaidi inayoshuhudiwa na vijana wanamichezo duniani, niliona kwamba ni muhimu kuwahakikishia zawadi ya kiraia ambayo ilikuwa imehifadhiwa na kutunukiwa katika nyakati za kale. Ahadi za nyuma nilizopewa kuhusu hatua hii ya Michezo ya Stockholm na Antwerp hazikuwa zimetimizwa. Hawakuonesha nia ya kufanya jambo lolote kuhusu hilo si kwenye Michezo ya Olimpiki ya Paris wala

Amsterdam. Hili lilikuwa kosa kubwa, ingawa ilikuwa rahisi kulirekebisha kwa nia njema, uvumilivu na fedha.

Jambo la pili, wakati ulikuwa umefika wa kuyapa Mashirikisho ya Kimataifa, ambayo sasa yalikuwa yameunganishwa na yana uhusiano mzuri zaidi na michezo ya Olimpiki, nafasi kubwa zaidi ya mipango ya kiufundi ya Michezo. Lakini nilidhani bora niache jukumu la kukamilisha mradi huu kwa mrithi wangu, ambaye hajajulikana bado. Bodi tendaji ilikutana Lausanne kila wakati wa Majira ya Vuli, kwa muda wa siku tatu, ili kutathimini masuala ya sasa na kufanya maandalizi ya kikao kijacho cha IOC. Katika mkutano wa tarehe 15 Novemba niliwasilisha kwa wenzangu, kufanya wapendavyo, mradi ambao baadaye nafasi yake ilichukuliwa na mipango mingine na ambao, haujawahi kuwekwa hadharani. Ulitoa nafasi ya kuundwa kwa Kamati ya Kiufundi ya wajumbe kumi na watano, ambao nafasi zao za uongozi zingedumu kwa muda wa miaka mitatu, kuanzia tarehe 1 Januari mwaka wa II kwa kila kipindi cha michezo ya Olimpiki hadi tarehe 31 Disemba ya mwaka wa IV. Kamati hiyo ingeundwa na wajumbe watatu wa IOC, wawakilishi sita kutoka Kamati ya Kitaifa ya Michezo ya Olimpiki na wajumbe sita kutoka Mashirikisho ya Kimataifa. Wakati wa maandalizi ya Michezo, kamati hii ingekuwa na jukumu la kusimamia maandalizi ya kiufundi, kupokea na kutoa taarifa kuhusu mapendekezo ya Mashirikisho na Kamati, kusimamia tafsiri sahihi na matumizi ya kanuni, na wakati wa sherehe, kutathimini malalamiko, kuamua hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa na kuendesha uchunguzi wa uhalali wa washiriki, utendaji kazi wa majopo na mengineyo.

Madhumuni ya kuunda kamati hii, ambayo kwa kweli uundaji wake ulikwama, yalikuwa ni kurejesha jukumu kamili la kiseneti la IOC na wakati huo huo kushirikisha vyombo vya kiufundi kwa karibu zaidi katika utendaji kazi wa pamoja kwa kuzipa mamlaka na majukumu zaidi.

# XXII

## Jiji la Prague (1925)



***52.** Baron Coubertin akiwa na Baroness, katika safari yake ya mwisho ya kikazi akiwa Rais wa IOC jijini Prague, 1925)*

Mwaliko wa kuitisha mkutano pamoja na kikao cha IOC mjini Prague mwaka 1925 ulikuwa umetufikia mjini Roma miaka miwili kabla na ulikuwa umekubaliwa mara moja. Ulitiwa saini na Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Bw. Benes. Mwaka huo nilimtembelea Rais Masaryk wakati alipokuwa Montreux na nilifurahi kuona shauku aliyoonesha katika michezo ya Olimpiki ya kisasa. Hata hivyo, ilikuwa sawa tu kuonesha heshima kwa mji mzuri wa Prague, ambao hakika ni mojawapo ya miji mizuri zaidi duniani, mojawapo ya vivutio vizuri zaidi katika historia na wenye mkusanyiko mkubwa na heka heka za kibinadamu. Kwa upande wangu, ambaye tangu mwanzo alikuwa amehusisha jiji la Bohemia na harakati za Olimpiki na hakuwahi kuacha kutetea haki zake, ilipendeza sana kumaliza kazi yangu huko. Pia ilikuwa njia ya kuonesha shukrani zangu na upendo wangu kwa mshirika wangu mwaminifu na rafiki Guth-Jarkovsky, mwakilishi pekee aliyesalia wa timu ya awali.

Kikao cha IOC kilifunguliwa katika Ukumbi wa Mji mnamo tarehe 26 Mei 1925. Wageni waliojumuika miongoni mwa wengine ni pamoja na Count Bonacossa (Italia), Baron Schimmelpenninck (Uholanzi), Katibu wa Jimbo Lewald (Ujerumani), Bw. Ivan Nyholm (Denmark) na Dkt. Haudeck (Australia). Katika mkutano wa kwanza, Kapteni Scharroo alitangaza habari za kuridhisha kutoka Amsterdam. Kwa kweli, tunampongeza na

wasaidizi wake, kila kitu kilikwenda sawa ingawa kwa muda mfupi Olimpiki ya 9 ilikuwa katika hatari kubwa kwa sababu "wanauamsho", ambao walikuwa wameanzisha mapigano dhidi ya "wapagani", walikuwa wamefanikiwa kuzuia upigaji kura. Ilionekana wakati mmoja kana kwamba michezo hii ya Olimpiki ingevunja rekodi pamoja na maandalizi yake kutokuwa mazuri. Lakini mtazamo wa umma ulikuwa kinyume na wenye mamlaka na baadaye maelezo ya umma yalionesha hawakuwa sahihi. Na utaratibu ulirejeshwa. Hata hivyo, sikufikiri kwamba mambo kama hayo yangeweza kutokea katika karne ya 20! Ni somo lililoje kwa wale wanaoamini kuwa wameona mambo mengi ya mwisho ya upuuzi na "wameweka chini mambo ya ujinga."

Kile ambacho kinyume chake hakikuacha kunitia wasiwasi kwa kweli ni ongezeko la mdororo wa fikra. Kwa sababu ujuzi sio kitu bila ufahamu: na ujuzi maalumu, ambao siku hizi mtu anafikiria kuwa unaweza kumwezesha mwanadamu kufahamu matatizo kwa ukamilifu wake, kinyume chake unatumika tu kwa ajili ya kuharibu. Baada ya kufanya uchunguzi wa tatizo hili kwa robo karne, tulibaini matokeo na utatuzi wake. Sikujipa muda wa kutafakari, badala yake niliamua kujishughulisha nayo kabisa na ndiyo maana labda mara kwa mara sikuwa makini na sikujali kutokuwapo wakati wa majadiliano ya Michezo ya Olimpiki huko Prague. Katika suala hili nilihisi kwamba jukumu langu lilikuwa limekwisha, nilikuwa na ufahamu wa kumwacha mrithi wangu katika hali nzuri.

Baada ya mambo kuhusu Uholanzi, tulichunguza kuhusu California, ambayo bado ilikuwa mbali lakini ilikuwa ya hali ya juu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Mustakabali wa ushindi wetu wa Afrika, ulioathiriwa na uasi wa Algeria, ulikuwa wa kufurahisha zaidi kwa kuwa Alexandria ilipokubali kuchukua nafasi na kwa kuwa A.C. Bolanaki alikuwa akijitolea kwa kazi hiyo kwa moyo wa dhati. Michezo ya Majira ya Kipupwe haikuwa na upinzani. Wenzetu wa Scandinavia, ambao sasa walikuwa wameamini na kushawishika, walikuwa wamejiunga na wazo bila kutoridhishwa na yoyote. Nilifurahishwa sana, siku zote nilitaka kuona kibali cha Michezo ya Kipupwe kinahalalishwa ipasavyo, lakini ninajilaumu kwa kuruhusu maandishi, ambayo yanaweza kusababisha matatizo baadaye, kuwa sehemu ya Sheria na Kanuni zetu chini ya Kichwa cha habari "Mkataba wa Michezo ya Majira ya Baridi." Kinyume chake, tulitakiwa kuzuia utoaji namba tofauti na kuyapa mashindano haya idadi sawa na Olimpiki ya sasa.

Hatimaye, tulifungua mjadala mgumu wa mambo ya siri na ya michezo ya ridhaa na kuyachunguza upya: upotevu wa mapato, fedha za matumizi, tofauti kati ya walimu na wanamichezo wa kulipwa, matokeo ya kuwaweka pamoja wanamichezo ya ridhaa na wa kulipwa na wengineo. Yote haya yalipaswa kujadiliwa tena kwenye mkutano usiokuwa na mivutano kwa sababu ya ajenda zake bali kuwajibika kwa matukio yaliyosababishwa na wasiofuata utaratibu fulani. Kwa upande mwingine, mwingiliano usiotarajiwa kutoka nje uliharibu uchaguzi wa Rais mpya wa IOC. Ilikuwa na lengo la kuzuia urais kupitia katika mikono mingine zaidi ya Wafaransa na kujaribu kunishawishi

nikubali hadi mwaka uliofuata, jambo ambalo lingenipa muda wa kufanya ujanja ili kufanikiwa. Ingekuwa ni makosa kabisa kwangu kukubaliana na suala hilo. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ambao walishauriana pamoja na Mch. Laffan - walikuwa na ubaguzi katika mapingamizi yao. Katika karamu iliyofuatiwa na tafrija iliyofanyika katika vyumba maarufu vya ikulu vya Kasri ya Hradschin na Bw. na Bi. Benes mnamo tarehe 27 mwezi Mei, Waziri aliniambia kwamba aliombwa kuwashawishi IOC lakini alikataa, kwa kuzingatia kwamba isingekuwa sahihi kwa upande wake kuingilia kwa namna yoyote ile uhuru wa IOC.

Uchaguzi ulifanyika siku iliyofuata, tarehe 28 Mei. Pamoja na kwamba idadi ya wapiga kura ilikuwa watu 40, waliokuwa wanahitajika walikuwa 21. Katika awamu ya kwanza ya upigaji kura, baadhi ya wapiga kura walinipigia mimi, kinyume na matakwa yangu, kama ishara ya heshima: katika awamu ya pili, Count de Baillet-Latour alichaguliwa. Utulivu na kuridhika vilitawala katika uchaguzi huu ambao ulishuhudia nguvu ya taasisi ya Michezo ya Olimpiki na kumpa kila mtu usalama wake. Kikao halisi kilimalizika kwa maelezo haya siku moja kabla ya kuanza kwa mkutano. Karamu nzuri sana zilikuwa zikifanyika karibu kila siku: karamu ya bustani ya Rais, maonesho ya Gala kwenye Opera, kifungua kinywa katika Kasri maarufu ya Wallenstein, chakula cha jioni kilichotolewa na Kansela na Bi. Guth-Jarkovsky, Waziri wa Afya, Meya wa Prague, Klabu ya Magari, Kamati ya Olimpiki ya Czechoslovak na wengineo. Kwa ajili ya ufunguzi wa mkutano huo, nyimbo nyingi nzuri za kwaya zilisikika, ambazo sauti zao nzito katika eneo hili la kihistoria ziliamsha kumbukumbu za Jean Huss na Mfalme George wa Podiebrad.

Ilikuwa imeamuliwa kwamba nikabidhi mamlaka yangu huko Lausanne na kwamba mamlaka ya mrithi wangu yanapaswa kuanza tarehe 1 Septemba. Kwa hiyo, nilikuwa bado Rais na nilipewa mamlaka ya kufanya hivyo wakati wa kongamano. Kwa pendekezo la Jenerali Sherrill, wenzangu walikuwa wameniteua "Rais wa Heshima wa Michezo ya Olimpiki" kubainisha kwamba heshima hii haipaswi kamwe kutolewa kwa mtu mwingine baada yangu. Lakini kama nilivyofanya katika mwaka 1921, nilimchagua J.S.Edstrom kuwa mwenyekiti wa mkutano huo. Chaguo hili lilikuwa maarufu kwa mashirikisho pia, Edstrom akiwa mwanachama wa IOC na Rais wa Shirikisho la Wanamichezo wa Kimataifa. Kwa jukumu hili muhimu alijitolea kwa bidii na uangalifu, unyoofu na hisia za haki na fadhili na waliridhika naye.  Hata hivyo, wakati huu, alipata shida kusimamia mkusanyiko huo na, katika siku za kwanza, alivunjika moyo kidogo. Kwa maoni yangu, hii ilitokana na tatizo ambalo halijatatuliwa tena ambalo liko akilini mwa wajumbe wengi wa mkutano. Walitamani kwa dhati kutaka kuendeleza manufaa ya taasisi za michezo, lakini walijiona wamewekeza katika majukumu ambayo mara nyingi yanakinzana kulingana na utaifa wao na mchezo fulani waliouwakilisha. Tamaa za utaifa zilikuwa zimezidishwa sana na vita hivi kwamba maoni mengi yalipotoshwa, wakati, kwa upande mwingine, kulikuwa na mwelekeo unaokua, uliochochewa na hali

ya jumla na pia kwa aina ya tabia ya uhifadhi wa siri wa kijamii, kulipa huduma ya kimataifa katika nyanja mbalimbali: mkanganyiko wa ajabu wa siku hiyo, ambayo watu wengi wa zama zetu tayari wamepata fursa ya kuziangazia.

Mkutano mwingine ulifanyika Prague pamoja na mkutano wa kiufundi. Ilikuwa ya kielimu na tulikuwa tumeiandaa kwa kushirikiana na Serikali ya Chekslovakia, kwa uangalifu kutaja kwamba "kanuni au mbinu za elimu ya maumbile ya mwili hazikuwa na shaka" na kwamba mkutano huo "hautakuwa na kazi ya kutafuta au kurekebisha mbinu bora", lakini tu "kujifunza kozi itakayofuatwa ili kuboresha vipengele mbalimbali vya shirika la michezo bila kudhoofisha au kubadilisha sifa yake ya msingi". Vipengele hivi maalum vilikuwa kama ifuatavyo: ziada ya maonesho; mechi za ndondi; vizuizi vya kuwashirikisha vijana rikabalehe; ushiriki wa wanawake; ufufuaji wa ukumbi wa mazoezi ya viungo wa kale; kukuza mchezo wa haki na uungwana; ushirikiano wa vyuo vikuu; tiba ya michezo na mapambano dhidi ya wanamichezo wa uongo. Ilikuwa, kama mtu anaweza kuona, mfululizo wa maswali ambayo, yanaonekana kuwa hayana uhusiano wowote, yote yaliunganishwa pamoja na kuwa na nguvu lakini yenye wasiwasi wa hali ya kawaida ya kisaikolojia. Kila swali liliambatana na aya yenye ufafanuzi iliyowekwa katika masharti yaliyoundwa na kuzuia uwezekano wa kuachana na mada kama ilivyofafanuliwa. Hata hivyo, Kongamano la kielimu lilikwenda kwa haraka sana katika mojawapo ya taratibu za kawaida za utoaji hotuba za kisasa, yaani, kukosa uwezo wa kushughulikia mada yenye lengo na inayotumika bila kupotoshwa na matakwa ya kusisitiza maoni au kukuza maslahi maalum. Kama kanuni ya jumla, hii inaongoza kwa ufasaha bila kitu na bila athari kubwa. Hata hivyo masomo yaliyoingizwa kwenye ajenda yalikuwa muhimu sana kwangu na ilikuwa ni matakwa yangu kwamba wangejumuishwa; kwa bahati nzuri nilipata fursa ya kurudi kwao baadaye chini ya hali nzuri zaidi.

Kwa mujibu wa uamuzi uliofikiwa, Count de Baillet-Latour alianza kazi tarehe 1 Septemba. Muda mfupi baadaye alifanya ziara yake rasmi katika Baraza Kuu la Voudois na Manispaa ya Lausanne. Rais wa Baraza Kuu na Meya wa mji aliandaa chakula cha jioni kwa heshima yake. Baadaye tulikwenda Berne, ambapo Rais wa Shirikisho, Bw. Musy, alitukaribisha kwa chakula cha mchana baada ya kutembelea Ikulu ya Shirikisho na kubadilishana mawazo ya kawaida.

# XXIII

## Mji wa Olimpia (1927)



53. *Pierre de Coubertin akiwa na binti yake Renee huko Olimpia*

Mnamo tarehe 16 Aprili, 1927, treni maalum iliondoka Athene kwenda Olimpia ikiwa imebeba msafara wa uzinduzi ulioongozwa na Waziri wa Elimu ya Umma, Bw. Argyros, pamoja na Mkuu wa Chuo, Rais wa Shule ya Akiolojia ya Ufaransa, idadi kubwa ya wanamichezo, na idadi ya Maprofesa pamoja na wageni mbalimbali. Safari bado ni ndefu. Reli inapita Ghuba ya Eleusis, ikifuata ufukwe unaoelekea Salamine, kuvuka Mfereji wa Korintho na kufuata Ghuba hadi Patras, kisha inageuka Kusini hadi Pyrgos na mwisho kufika Olimpia, katika bonde ambalo Mto Cladeos unapita. Magofu yapo karibu kabisa, chini ya Mlima Kronion, karibu na makutano ya Alfayo na Cladeos.

Kijiji na kituo kidogo cha treni kilichokuwa karibu na mji huo vilikuwa vimebaki na haiba yake ya ukale kana kwamba hakuna kitu chochote kilichoathiri eneo hilo takatifu na linaloheshimiwa na mahujaji wanaozuru. Katika hali inayofaa ya utulivu, nilikuwa nimefanya hija ile ile kwa miaka thelathini na mitatu hapo awali, nikifuatana na mwanachama wa Jumuiya ya Panachaic ya Patras ambaye alikuwa ameteuliwa kwa lengo hilo. Jioni moja Novemba 1894, nilikuwa nimewasili kutoka Athene, nikielekea

Ufaransa kupitia Italia, nikitambua matokeo ambayo yaliyokwisha kupatikana na matatizo mabaya sana ambayo yalikuwa yakiningoja. Nakumbuka njia iliyoelekea kwenye kilima kidogo ambacho kina jumba la makumbusho na hoteli. Upepo mwanana ulivuma kutoka kwenye kingo za Mto Alphaeus. Kwa muda mfupi, mwezi uliangaza mandhari yenye giza, na kisha usiku wenye nyota zinazong'aa ukaangukia juu ya miaka elfu mbili ambayo nilikuwa nimekuja kuiona tena. Siku iliyofuata niliamka mapema na kuketi dirishani nikisubiri jua kuchomoza, na mara tu mwanga wa jua ulipoangaza bondeni, nilifanya haraka kwenda kwenye magofu. Sikushangazwa wala kukatishwa tamaa kwa udogo wake, ambao unasababishwa kwa upande mmoja na idadi ndogo ya majengo na kwa upande mwingine, kuwa na msongamano wa watu kwa karibu sana (kutokuwapo kwa maeneo ya wazi ambayo ni tabia ya ustaarabu wa Wagiriki na Warumi ambao ni tofauti kabisa na upangaji wa usanifu wa Kiajemi).

Usanifu wa Kigiriki, ambao sijaufahamu bado, ni mtindo wa usanifu ambao unaonesha vipimo vyote. Tafakuri yangu iliendelea asubuhi yote na ukimya ulivunjwa na sauti tu ya kengele za mifugo waliokuwa wakielekea Arcadia.

Kumbukumbu za tukio la awali zilinijia jioni ile ya tarehe 16 Aprili, 1927. Nyumba nyingi zilikuwa zimejengwa karibu na kituo hicho, lakini katika sehemu ya hoteli na jumba la makumbusho hakuna kilichobadilika. Tulipita karibu na jiwe lililofunikwa kwa turubai. Ulikuwa mnara mweupe wa marumaru uliojengwa na Serikali ya Ugiriki ambapo nilikuta kwamba jina langu liliandikwa kwa herufi za Kigiriki na Kifaransa. Kulikuwa na karamu kubwa katika hoteli hiyo, aina ya karamu ya watu maarufu na vyakula vya asili ambavyo vililiwa sana nyakati za kale. Na kwa mara nyingine tena nilirudia ziara na matembezi niliyofanya awali; nilikesha nikichungulia dirishani huku nikitazama mbalamwezi inayoangaza nyanda za mto Alphaeus, wakati wa mapambazuko, nikizunguka katika magofu kutafuta mandhari ya zama nyingine.

Sherehe ya ufunguzi ilifanyika saa nne asubuhi mnamo tarehe 17 Aprili. Tulikusanyika pamoja, tukizungukwa na watazamaji wengi waliomiminika kutoka vijiji vyilivyo jirani, chini ya mnara huo uliokuwa umepambwa kwa bendera za Ugiriki na Ufaransa. Makasisi watatu, walijipamba kwa mavazi yao, waliimba zaburi na sala kwa sauti zao kubwa ambazo zilisikika kwa mahadhi ya Byzantine, mrithi wa Ugiriki ya kale ya Kikristo. Kisha Mheshimiwa Waziri, akatoa hotuba, ambayo niliijibu kwa kifupi. Kisha, kamanda wa Uswisi aliunganisha nchi yake na mji wa Lausanne katika sherehe iliyofanyika hivi punde tu: Sherehe iliyojaa utulivu kulingana na ukuu wa mahali hapo. Treni maalum iliondoka tena saa 12.45 ili kuturudisha Athene wakati usiku ulipoingia.

Ningependa kuandika hapa ujumbe wa maandishi uliotumwa kwa simu ya upepo siku hiyohiyo kwa "*Vijana wa michezo wa mataifa yote*". Maandishi haya hayakutolewa tena kwa uaminifu na baadhi ya tafsiri hazikuwa sahihi.

Mji wa Olimpia, tarehe 17 Aprili 1927 (Mwaka wa Nne wa michezo ya nane ya Olimpiki)

*"Leo, katikati ya magofu maarufu ya mji wa Olimpia, Mnara wa ukumbusho wa kufufua Michezo ya Olimpiki iliyotangazwa miaka thelathini na tatu iliyopita ulizinduliwa. Kwa ishara hii kwa upande wa Serikali ya Ugiriki, tukio la kijasiri lililofanywa liliupa heshima mji huu. Ni juu yako kuiweka hapo. Katika kufufua Michezo ya Olimpiki kwa ajili yako, jambo la mwisho ambalo mimi na marafiki zangu tulitaka lilikuwa ni kuifanya iwe sehemu ya makumbusho au somo kwa ajili ya sinema, au kwa ajili ya biashara au maslahi ya uchaguzi ili kuzitumia kwa madhumuni yao wenyewe. Tulichotaka, tulipofufua taasisi iliyoanzia karne ya ishirini na tano, ilikuwa ni kwa ajili ya ninyi kuwa tena wafuasi wa michezo kama ilivyobuniwa na mababu zetu wa kale. Katika ulimwengu wa kisasa, uliojaa uwezekano mkubwa lakini unaotishwa wakati huo huo na udhaifu mkubwa. Michezo ya Olimpiki inaweza kujumuisha shule yenye maadili mengi ya heshima na usafi kama ya uvumilivu wa mwili na nguvu, lakini hii itatokea tu ikiwa utaendelea kuinua dhana yako ya heshima ya michezo na uchezaji wa haki hadi kilele cha mafanikio yako. Wakati ujao unajengwa na wewe".*

Matukio mbalimbali yalikuwa yameandaliwa huko Athene hasa kutokana na jitihada za J.E Chryssafis, Mkurugenzi wa Elimu ya Viungo. Kwa miaka mingi alikuwa amejitolea bila kuchoka, kwa bidii na ufanisi mkubwa, kwa ajili ya utumishi wa manufaa ya umma. Yeye na mjumbe mpya wa IOC kwa Ugiriki. Bw. George Averof, ambaye alikufa mapema miaka miwili iliyopita, nilimuona akifanya kila alichoweza ili kufuta kumbukumbu zangu zote za matukio yasiyotarajiwa ya Michezo ya kwanza. Lakini kwa kweli hakuna kilichobaki. Kwamba mawazo yangu yalipaswa kukutana na pingamizi wakati huo, hata kuamsha hisia za utaifa kupita kiasi, lilikuwa ni jambo la kawaida tu. Kila mtu alielewa hilo sasa kwa kutayarisha michezo hiyo mipya katika kiwango cha kimataifa kabisa na kwa kutaka kuiweka katika kiwango cha dunia. Sikuwa nimechagua tu njia pekee zinazofaa za kuhakikisha kwamba wanaendelea kuishi lakini wakati huo huo nilikuwa nimetumikia maslahi bora ya Ugiriki ya kale. Kamwe sikuacha kuitumikia kwa namna nyingine pia, daima kwa kutafuta kuiboresha, si kuiwasilisha kama masalio ya wakati uliopita yanayostahili heshima na tafakari, bali kama jambo la wakati ujao linalostahili imani na ibada. Kwenye changamoto ambayo hatma ya jamii ya siku zijazo, inategemewa kuondoa migogoro kati ya misingi ya serikali ya Kirumi na ile ya jiji la Ugiriki.

Watu wenye mtazamo wa mafanikio wanajitahidi kutengeneza jambo jipya bila mafanikio. Tumekubaliana kushirikiana katika moja ya misingi hiyo miwili. Inaonekana kupendelea serikali ya Kirumi. Mimi ninaamini katika jiji la Ugiriki.

Natumaini wasomaji wangu watanisamehe kwa mawazo haya ambayo yanaweza kuonekana hayahusiani na michezo ya Olimpiki. Lakini wakati wa kukaa kwangu kwa muda katika nchi ya Ugiriki, nilifurahi sana kuona kwamba imani yangu ya kifalsafa sasa ilieleweka na kuthaminiwa na marafiki zangu wote wazuri wa Kigiriki. Kwa hivyo, kati ya sifa walizonipa, labda hakuna hata moja ambayo niliguswa nayo zaidi ya kufufua desturi

ambayo ilikuwa imepuuzwa tangu nyakati za zamani: kuwekwa wakfu kwa kiti cha marumaru katika uwanja na jina la mfadhili aliyeandikwa kwa herufi za dhahabu mgongoni. Niliwahi kushika nafasi hiyo mara moja tu. Ilikuwa kuangalia mkutano wa riadha uliofanyika wakati wa ziara ya timu ya Chuo Kikuu cha Uingereza; njia za kukimbilia, viatu vya njumu, viwanja vilirejeshwa. Lakini wanamichezo wa leo waliingia uwanjani kupitia njia za zamani za chini ya ardhi zilizotumiwa na watangulizi wao karne ishirini kabla: na roho zao zilikuwa zile zile na ujana wao uliogubikwa na msukumo uleule wa ujana wa furaha ya mwili.

Wakati, baada ya mashindano ya riadha, tulipata fursa ya kuzungumza pamoja, ilikuwa ni kujadili suala la uwanja na njia zake. Kila mtu anafahamu ugumu wa tatizo. Njia zake ni fupi sana kwa kasi ya sasa na wakimbiaji wanakinzwa na kunakuwa na hatari ya kujiumiza wenyewe. Mwelekeo wa kisasa wa kurahisisha majaribio ya mwanamichezo wa kuweka rekodi za juu zaidi na nzuri zaidi kwa kumpa kila msaada wa nyenzo unaowezekana, ni kinyume kabisa cha dhana ya zamani ambayo ililenga kufanya juhudi zake na kusifiwa zaidi kwa kuvizunguka vizuizi na kuvishinda. Kwa hiyo wimbo laini na wimbo wa Cinder wa chemchemi unawakilisha wazo la michezo. Lakini je, ni kweli kuwa tatizo hili haliwezi kutatulika? Nilikosea.

Wataalamu kadhaa wa kisasa waliokuwa nje na ndani walikuwa wamepata suluhisho. Ilijumuisha katika kupanua uwanja kwa theluthi moja kwa kuondoa safu mbili za viti, hivyo kuongeza eneo linaloweza kutumika. Wazo la kuukata uwanja wa michezo wa Pericles kwa njia hii!..... Lazima ilikuwa ni "msomi" aliyependekeza wazo kama hilo la kisomi. Mwanafunzi kutoka Kaskazini, aliyeletwa katika mila safi ya juu ya historia, alipinga kwa hasira dhidi ya ufanisi kama huo, ambao tayari ulikuwa umekataliwa, inapaswa kuongezwa, na watu wa Ugiriki. Kwa wakati mmoja, nilimwona mmoja wao akiinua macho yake kwa Acropolis ya kimungu ambayo bado ilikuwa imeoga kwenye miale ya mwisho ya jua huku vivuli vikienea kwa haraka pande zote. Watu walianza kupungua taratibu. Weupe wa marumaru uliibuka tena. Mwanafunzi huyo, akiwa amejaa furaha isiyo kifani, mwili wake ulikuwa unavutia kwa mng'ao wa ngozi kutokana na msisimko wa mwili unaosababishwa na michezo, uliojaa tumaini la ujana na tamaa, alionekana, kwa macho yake kama anaomba, kumchezea Minerva na heshima yake. Alikuwa kama sanamu inayowakilisha michezo mipya ya Olimpiki, alama za ushindi wa siku zijazo zinazongojea Ugiriki ya kale - ilikua hai sana, na iliyobadilishwa milele na mazingira ya wanadamu.

# XXIV

## Wanamichezo Nguli



**54.** *1919 – Pierre de Coubertin akiongozana na mrithi wake wa nafasi ya Urais wa IOC, J.Sigfrid Edstrum*

Idadi ya wanamichezo nguli ilikuwa ikiongezeka katika tasnia ya Michezo ya Olimpiki. Wale wa mwanzo walikuwa wakiwakilisha upotoshaji wa uhalisia. Wanamichezo nguli wa sasa wanarudia upotoshaji huo bila kufikiri, ambapo hakuna mtu anayetafakari kabla ya kuongea...... hata baada ya muda kupita. Kwa mara ya kwanza, maneno yale yalitamkwa kwa lengo la kukosoa au kuridhisha baadhi ya watu wenye lengo la kulipiza kisasi; mara kadhaa kwa sababu, ya kuwakilisha uamuzi rahisi na wa haraka ambao ulionekana utaleta manufaa kwa maendeleo ya michezo ya wakati ujao. Katika kategoria hizi, mwanamichezo maarufu aliyetoka kwenye aina fulani ya mchezo na kuingia kwenye aina nyingine, alijumuishwa. Ni mara ngapi sijaona kwa namna moja ama nyingine mambo yenye "kusikitisha yanayokatisha tamaa", kwenye malengo yangu ya msingi ambayo hayakuendana na matarajio yangu ya mwanzo!

Hivyo mambo yote haya ni ya kufikirika. Zaidi ya hayo, ni makosa kabisa kuitukuza Michezo ya Olimpiki ya kale kwa kuzingatia uzuri na baadaye kuikosoa kwa namna ya kuibua wanamichezo wa kulipwa. Vilevile Michezo ya Olimpiki ya sasa imekuwa ikichochea ushindani wa kimataifa na wa kibiashara ambao ndio umekuwa chanzo pekee cha mapato. Maneno "mwanamichezo wa kulipwa" na "mwanamichezo wa ridhaa" yaliyotumika kwenye michezo ya kale hayana maana yoyote kwa wakati huu.

Jambo linalofanana kwa vipindi hivi viwili kwa mtazamo wa Michezo ya Olimpiki ni sawa na mtazamo wa kidini unaofanana ambao uliibuka tena kwa muda mfupi miongoni mwa wanamichezo chipukizi kipindi cha zama za kati. "*Religio athleteae*"; wanamichezo wa kale walielewa maana ya maneno haya ambapo wanamichezo wa sasa bado hawajayaelewa. Nadhani wameanza kuelewa. Waandishi wa riwaya kama vile Montherlant na Kessel, kwa kuwataja waandishi wa Kifaransa wananifanya nifikiri hivyo.

Kwa akili ya kawaida tunaweza kutambua jinsi michezo ya kale ilivyofanyika bila kuwa na matukio ya kutatanisha kama vile kupatwa kwa jua na vikwazo kutoka kwa wapinzani. Michezo ya Olimpiki ilipitia changamoto mbalimbali. Licha ya changamoto hizo, Michezo ya Olimpiki iliweza kuendelea. Hata Michezo ya Olimpiki ya sasa itapitia mabadiliko kama ilivyokuwa awali. Michezo iliyofufuliwa ina faida mbili za ziada, kuwa na sifa zinazofanana katika mataifa yote na kutazamwa katika kila kona ya Dunia. Hivyo itakuwa rahisi kunyumbulika na wakati huohuo kuwa thabiti. Katika siku za awali za ufufuaji wa Michezo ya Olimpiki, ilipitia changamoto kubwa; kwa kipindi hiki imeimarika na haiwezi kusitishwa tena. Vita vya mwaka 1914-1918 havikuitikisa: hata mabadiliko ya kijamii hayakuiathiri. Ni vizuri kufahamu kwamba, pamoja na kuwa na kundi la "matajiri", kuna kundi la "watu wa kipato cha chini". Wafanyakazi ambao pia ni wanamichezo wamekuwa wakishiriki michezo kwa mafanikio. Wakati wa uandishi huu, nimeambiwa kwamba, huko Moscow uwanja mkubwa unajengwa kwa ajili ya Michezo ijayo ya Olimpiki. Inasemekana kwamba watatumia fursa hii kubadili jina la mashindano haya. Kama itakuwa hivi, litakuwa ni jambo la kitoto litakaloonesha mabadiliko mengi ambayo hayakufanikiwa kwa kiasi kikubwa duniani kote. Wakati ambapo taasisi nyingi zinahitaji mabadiliko, zimekuwa zikibadili majina pekee; wakati kinachohitajika ni vitendo na si maneno.

Kuongezeka kwa umaarufu wa michezo baina ya wafanyakazi wa kawaida ni kigezo cha maendeleo ya Michezo ya Olimpiki - bila kujali tofauti za kipato kati ya makundi mawili yanayokinzana ulimwenguni. Aidha, inaamanisha kwamba, michezo si anasa, shughuli ya watu wachache waliostarehe wala si aina ya kitu cha kuchangamsha mwili baada ya kazi za ofisini kama ilivyokuwa ikichukuliwa zamani. Kwa kila mtu inatoa fursa ya maendeleo binafsi ya kitaaluma au nafasi katika maisha. Ni fursa kwa wote na kila mmoja ana haki ya kushiriki.

Hakuna tofauti katika mtazamo wa kijamii kwamba, michezo ni mali ya makundi yote ya kijamii. Kipindi kifupi kilichopita wakazi wa bara la Asia walikuwa wanatengwa. Mwaka uliopita huko Geneva mmoja wa wawakilishi wa Japani katika Mkutano wa Shirikisho la Mataifa aliniambia "ni ngumu kuamini kwa kiasi gani kufufuliwa kwa Michezo ya Olimpiki kumeibadili nchi yangu. Tangu tulipoanza kushiriki kwenye michezo vijana wetu wamekuwa na mwamko mpya". Nilipata maelezo kama haya kutoka kwa wawakilishi wa India na China.

Ni jambo la kushangaza kwamba taasisi inaweza kueneza jambo hili kijamii na kimataifa. Kuna umuhimu gani kwangu kutoa mifano midogo ambayo haina mwelekeo ya utekelezaji ndani yake? Kwenye kila mashindano ya Michezo ya Olimpiki nilipata taarifa kuwa, mwandishi wa habari hakuwa anapata malazi mazuri, huduma nafuu ya chakula au huduma bora ya mawasiliano kama ilivyotarajiwa. Hili ni jambo la kibinadamu. Kwa hiyo waandaaji wanapaswa kuzingatia haya mambo matatu ingawa uhusiano wao na hatma ya mwisho ya mashindano ya Michezo ya Olimpiki haijulikani! Mashindano ya Michezo ya Olimpiki yataendelea kubaki juu ya misingi imara. Hii ndio sababu mwenge utakaozimwa hapa utawashwa sehemu nyingine; upepo unaovuma sasa utatosha kusambaza mwanga Dunia nzima.

Inaweza kudhaniwa kwamba mawazo haya yanachochewa na majivuno. Ingawa nina mawazo mazuri ambayo yananipa ufahari kwa kazi niliyokamilisha, sihitaji kupewa sifa: sifa inastahili pale ambapo mtu aliyepambana mwenyewe au dhidi ya mtazamo mbaya na kufanikiwa kwa bahati. Kupendelewa kwa heshima nyingi na majaliwa, nikiendelea na kazi iliyoko mbele yangu kutokana na msukumo wa ndani ambao wakati mwingine nilijaribu kuukwepa, sina mambo ya kujivunia.

Hii ndiyo sababu nimeandika kumbukumbu hizi ambazo sasa zimekaribia ukingoni. Nilikuwa na uchaguzi wa aina mbili: ama kutumia lugha ya kificho, kwa kutumia misemo mbalimbali na masimulizi yenye kuvutia au kuzingatia ukweli, huku nikifuata mtiririko wake wa asili. Namna hii ya pili ilikuwa ina udhaifu wa kunifanya nitumie nafsi ya kwanza lakini ilikuwa njia sahihi ya unyoofu zaidi. Katika kuitumia njia hii niliamua kutoacha jambo lolote la muhimu hasa kutowasahau wenzangu walionipa kwa ukarimu muda na huduma zao zilizonisaidia sana. Ningependa kutumia muda huu kuwashukuru wote ambao sikuwataja hapo awali.

Nikisema kwamba nimeridhishwa na mabadiliko ya mfumo mpya wa michezo ya Olimpiki, Je, jambo hili linanifanya nisione udhaifu wake? Njia sahihi ni kuweka matini ambayo kwa mawazo yangu ni muhimu. Ni "katiba ya mageuzi ya michezo" (charter of sports reform) ambayo ilitangazwa tarehe 13/9/1930 Geneva katika mkutano ulioongozwa na Kansela wa Uswisi Motta. Katiba hii ilitafsiriwa katika lugha nyingi, nakala zilichapwa kwenye mabango kwenye lugha za kifaransa na kijerumani na kulikuwa na mafanikio makubwa katika maonesho ya Berne. Katiba imekubaliwa katika maeneo mengi lakini vifungu vyake vinahitaji watu kujitoa sana ili kuvitekeleza. Jambo hili litatekelezwa hatua kwa hatua.

Ifuatayo ni matini yenye mapendekezo:

Hoja zinazotajwa kupinga michezo zinaweza kuandikwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

- *Maumivu makali ya viungo*
- *Kushuka kwa uwezo wa kitaaluma*

- *Ukuaji wa ushindani wa kibiashara uliopitiliza*

Haiwezekani kupuuza uwapo wa hatari hizi ingawa si wajibu wa wanamichezo. Watu wa kulaumiwa ni wazazi, walimu, mamlaka za umma, na kwa kiwango kidogo, wakuu wa mashirikisho na vyombo vya habari.

Marekebisho yanayotakiwa ni haya yafuatayo:

- *Kubainisha utofauti uliopo baina ya mazoezi ya viungo na elimu ya michezo kwa upande mmoja na elimu ya michezo na mashindano kwa upande mwingine.*

- *Kuanzisha mtindo wa Uswidi wa elimu ya stashahada ya michezo yenye majaribio ya aina mbalimbali yanayoendana na umri na jinsi, mashindano ya kimataifa ya kila mwaka wa kwanza, wa pili na wa tatu wa kila kipindi cha michezo ya Olimpiki.*

- *Kuondoa mashindano yote yanayoendeshwa kwenye kumbi za starehe, hoteli, kwenye maonesho na sherehe za kitaifa.*

- *Kuondoa michezo yote ambayo inaingiliana na michezo ya Olimpiki na yenye mrengo wa kikabila, kisiasa au kidini.*

- *Kuondoa mashindano ya ngumi yanayohusisha zawadi za fedha, kuingizwa kwa vifaa vya michezo kwenye michezo ya sarakasi kwa usawa kabisa na michezo mingine ya mtu binafsi: ari ya kuunganishwa kwa vilabu vya michezo ya sarakasi; kuwapo kwa utofauti baina ya mwalimu na mwanamichezo wa kulipwa, mwanzilishi ana haki ya kuzingatiwa kuwa mwanaridhaa katika michezo yote isipokuwa ile ambayo amefundisha; kuhifadhi kiapo cha mtu binafsi alichoapa kwa maandishi, pamoja na orodha ya vyanzo mbalimbali vya mapato; ukandamizaji wa ushiriki wa wanawake kwenye mashindano yote ambayo wanaume hushiriki; kutelekezwa na manispaa wakati wa ujenzi wa uwanja mkubwa uliokusudiwa kwa "maonesho" makubwa ya michezo tu na uingizwaji wa majengo haya na majengo yaliyojengwa kulingana na mpango wa kisasa wa michezo ya sarakasi ya Ugiriki ya zamani; kupiga marufuku uhudhuriaji wa vijana chini ya miaka 16 kuwa watazamaji katika mashindano yoyote.*

- *Uundaji wa vyama vya michezo shuleni ambavyo wanafunzi wenye asili tofauti na wazawa wataruhusiwa kushiriki kwenye mashindano. Kuondoa zuio la usajili wa vijana wa kiume wa skauti kwa kuzingatia umri.*

- *Uimarishaji wa tiba ya kimichezo ambayo inazingatia afya kuliko majeruhi na ambayo inazingatia afya ya akili ya wanamichezo.*

- *Kuhimiza ushiriki wa watu wazima kwenye michezo tofauti na baadhi ya vijana ambapo hatua zinapaswa kuchukuliwa ili kupunguza kasi.*

- *Kuongeza uelewa kwa wanamichezo wa kiume kwa kutoa mafunzo ya elimu ya anga, historia na jiografia.*

- *Kufanya mikutano ya waandishi wa habari za michezo ya kisasa kwa kuongeza Makala zinazohusu sera za nje na matukio ya dunia.*

Kama inavyooneka katiba hii haipendekezi mabadiliko kwenye mashindano ya michezo ya Olimpiki. Badala yake inaonesha msisitizo wa kuboresha mashindano ya Olimpiki ili kuyapa mwamko zaidi. Mashindano haya yatakuza ushindani na yataongeza ushiriki wa timu na yatakuza ushiriki wa nchi kwenye michezo. Watu mia moja wakijiunga na elimu ya michezo, hamsini kati yao watashiriki michezo. Watu hamsini wakishiriki kwenye michezo, ishirini kati yao watakuwa mahiri. Watu ishirini wakiwa mahiri watano kati yao wataweza kuwa weledi wa hali ya juu. Huwezi kuacha kutaja ukweli huu. Kila kitu kinategemea kuwapo kwa kitu kingine. Kwa hiyo rekodi ya riadha inasimama bila kuepukika kwenye kilele cha jumba la michezo, kama ule mshikamano wa milele unaorejelewa na mwandishi Mfaransa Taine kuhusu sheria ya Newton "huwezi kutumaini bila kuharibu kila kitu". Kwa hiyo, jiondoeni wenyewe, jiuzuluni, ninyi washiriki wa Utopia isiyo ya kweli ya uratibu ambao ni kinyume kabisa cha asili; kwa maana mlituona tukiendelea kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ambayo padre Didon alikuwa akiitoa kwa wanafunzi wake na ambayo tangu wakati huo imekuwa ikitumika katika Michezo ya Olimpiki.

"**JUU ZAIDI, NYEPESI ZAIDI NA IMARA ZAIDI** (*CITIUS - ALTIUS - FORTIUS*)"